

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

19 APRILI, 2012

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 19 Aprili, 2012**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI:** Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU):** Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. VITA R. KAWAWA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE):** Taarifa ya Kamati ya

Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

### **MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni tena siku ya Maswali kwa Waziri Mkuu. Walioomba ni 12. Naona wengine waliwahi sana kuamka, lakini nitajitahidi Wabunge wa vyama vyote amba majina yako hapa wapate nafasi. Kawaida yetu tunaanza na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI:**  
Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Katiba ya nchi yetu pamoja na sheria zake inaeleza kinagaubaga kuwa umri wa kupiga kura ama haki ya kupiga kura ni miaka 18 na kuendelea; na kwa sababu katika chaguzi ndogo za Igunga, Uzini kule Zanzibar na hata Arumeru pamoja na Kata kadhaa nchini ambazo zimekuwa zinafanya uchaguzi baada ya uchaguzi mkuu wa 2010, wananchi wamekuwa wanapiga kura bila kuandikishwa upya; na kwa kuwa imedhihirika kabisa kabisa kwamba idadi kubwa ya wananchi wenyе haki ya kupiga kura wanashindwa kupiga kura aidha kwa sababu ya kutokuandikishwa ama kwa sababu ya kupoteza shahada zao za kupiga kura; na kwa kuwa sheria inayosimamia utekelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura inatambua uwepo wa mpigakura kwenye daftari na siyo kiparata cha kupigia kura.

Je, ili kuwezesha wananchi wetu kushiriki katika chaguzi mbalimbali zinazofuata, Serikali inatoa tamko gani? Ni nini haki ya kupiga kura, ni kuwa na kiparata cha kupiga kura ama ni kuwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura?

Mheshimiwa Spika, pili; kwa sababu watu hawaandikishwi na hivyo tunawanyima haki Watanzania wengi sana wenyе haki ya kupiga kura; na huku tukijua kwamba wakazi wetu wengi wana makazi duni kiasi kwamba uwezo wa wao kutunza shahada za kupigia kura kwa zaidi ya miaka mitatu/minne ni mgumu sana na kwa hiyo wengi wanakosa hivyo viparata na wanakosa haki ya kupiga kura. Waziri Mkuu, unaliambia nini Taifa kuhusu haki hiyo ya msingi inayopotezwa aidha kwa makusudi ama kwa kufanya bila kujua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba jibu swali hilo!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbewe – Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa swali lake ambalo kwa kweli ni la msingi sana. Jambo hili na sisi tulilipata kuititia njia nyingine; na hivi sasa tunajaribu kulitazama tuone namna bora zaidi ya kuimarisha ule mfumo. Na limekuja kujitokeza hasa tulipoanza kwenye chaguzi ndogo, ndipo nalionna linajitokeza waziwazi. Kwa sababu ni kweli kwa mujibu wa utaratibu ulivyo sasa, lile Daftari la Kudumu ambalo ndilo tumelitumia, baadaye likaja kuwa *updated*, tukalitumia kwenye uchaguzi mkuu, kwa sehemu kubwa ndilo limebaki kama ndiyo dira yetu ya kutusaidia katika chaguzi hizi.

Lakini, hapo katikati yako mambo mengi yanatokea. Kwa hiyo, kati ya kiparata na lile daftari, ni dhahiri lazima tufika mahali tuone namna gani tunaweza tukawajumuisha wale wote ambao wanastahili hilo jambo. Kwa hiyo, matumaini yetu ni kwamba tutafikiria sasa kwa pamoja na Tume ya Uchaguzi, halafu tuone namna ya kuboresha huo mfumo kwa ajili ya kuwezesha chaguzi zijazo ziweze kutilia maanani jambo hilo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri Mkuu kutambua hili ni tatizo, na napenda kumhakikishia zaidi kwamba ni tatizo kubwa na ni tatizo kubwa kweli kweli. Na kwa sababu ameishatupa ahadi ya Serikali kulitafuta jambo hili, anaweza kutoa ahadi kwa Watanzania kwamba hakuna uchaguzi mwingine wowote mdogo utakaofanyika bila kuwa zoezi hili limekamilika ili kuwapa haki Watanzania wote kujiandirisha na kupiga kura?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mimi ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, lakini siwezi kuilazimisha Serikali kwa kiwango hicho ambacho unataka. Sana sana ninachowea kusema ni kwamba tutajitahidi katika muda mfupi iwezekanavyo tuweze kufanya kazi kwa karibu sana na Tume, tuone kama tunaweza tukafanya nini ili ikiwezekana hata hilo nalo unalolisema pengine likawa limeteklezwa.

Lakini kujilingiza moja kwa moja, inaweza ikaniwia vigumu kidogo kwa sababu nitakuwa pengine sikutenda haki kwa vyombo vinavyohusika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa tunaingia kwa Wabunge wengine. Naomba, mkiwa makini katika kuuliza maswali yenu, mnaweza kufikiwa wengi. Lakini mkianza kutuhutubia basi mtashindwa kufika huko.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa sehemu ya ushuru wa mazao ni 2% ya mauzo ya tumbaku

yalielekezwa kwamba 2% ya mwaka 2009/2010 iende Halmashauri za Wilaya, na 2% ya mwaka 2010/2011 ziende kwa wakulima walioathirika na kushuka kwa bei ya tumbaku katika msimu uliopita.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpaka sasa hivi fedha hizi hazijawafikia wakulima wala Halmashauri za Wilaya.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unatoa tamko gani juu ya fedha hizi ambalo litarudisha imani ya wakulima ambao kwa kweli waliathirika na kwa sasa wanazihitaji hizi fedha ili waweze kuendelea na mambo mengine ya maendeleo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Nkumba. Kwa mujibu wa taratibu tulizonazo, ushuru kwa mazao ambao unapaswa kutozwa na kuchukuliwa katika ngazi ya Wilaya tulisema usizidi 5%. Lakini kwa mazao haya ambayo ni mazao ambayo yanatuingizia kiasi kikubwa cha fedha kama Taifa, ndiyo maana uamuzi wa 2% kwamba ziende kwenye Serikali za Mitaa kwa maana ya kuwawezesha kuwarejeshea wakulima likawa ni la msingi sana kwamba si asilimia yote iende kwenye Serikali za Mitaa, tuigawe kidogo ili na mkulima imsaide katika kuboresha uwezo wake wa kuendelea kuzalisha.

Sasa limekuwa na mvutano na ndiyo maana zile 2% kwa msimu ule uliotangulia na huu, bado limekuwa likileta mvutano. Lakini, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Nkumba kwamba kwa sababu jambo hili tunalo, tunalifanya kazi, matumaini yangu ni kwamba haitachukua muda mrefu kabla hatujafikia uamuzi. Na mimi naamini uamuzi halali utakuwa ni kuwawezesha wakulima wapate ile 2%. Lakini kwa vile tunalizungumza, tutafikia mahali tutatoa kauli ya moja kwa moja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2011 vijana waliofanya mitihani wa Kidato cha Nne wapatao 3,303 walifutiwa mitihani yao wakiwapo vijana 31 wa shule ambayo ipo Jimboni kwangu inaitwa Ng'amba Sekondari.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, vijana hawa ni wengi, kadri ya maelezo ya Serikali ni kwamba vijana hawa hawataruhusiwa kufanya mitihani mpaka miaka mitatu ipite. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa ni vijana wadogo, ni Watanzania, wameishapewa adhabu ya kufutiwa mitihani yao tayari, kwa nini Serikali inawapa adhabu nydingine ya kukaa miaka mitatu ndipo wafanye mitihani? Hatuoni kwamba kwa kufanya hivyo tutadumaza elimu ya vijana hawa, na sasa kuna sababu ya Serikali kuwaonea vijana hawa huruma wafutiwe mitihani lakini baada ya mwaka huo mmoja waliofutiwa wafanye tena mitihani hiyo? (Makof)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, suala hili ni gumu kidogo. Lakini, wacha nijaribu tu kulitolea maelezo kidogo. Ni kweli kwamba Serikali ilichukua uamuzi huo, lakini ni kweli vile vile kwamba hata Waheshimiwa Wabunge mmekuwa wakali sana kwenye jambo hili la mitihani ama kugushisha au wanafunzi kutumia njia ambazo si halali kutaka kujishindisha mitihani wakati hawana sifa hizo. Ninyi mmekuwa mstari wa mbele sana kuishauri Serikali kujaribu kuchukua hatua kali dhidi ya vitendo vya namna hiyo.

Kwa hiyo, katika matokeo ya safari hii hilo lilijidhihirisha wazi wazi. Na pengine mfano mzuri ni pale ambapo walijaribu kutueleza watu wa Wizara ya Elimu, walipokuta wanafunzi katika baadhi ya madarasa katika mtihani ule ambao unataka useme “a, b, c, d”, wote wameandika “o”. “o” ambayo kwenye “a, b, c, d” haipo. Maana yake ni kwamba kuna mtu aliwaandikia “d” lakini ikaonekana ni “o”, kwa hiyo darasa zima wameandika “o”. Sasa unaelezaje kitu cha namna hiyo, kwa sababu ni ushahidi tosha kwamba hawa wanafunzi walionyeshwa kitu ambacho si cha kweli kwa maana kwamba walidanganyika “d” wakaifanya “o”.

Mheshimiwa Spika, yako mengi ya namna hiyo katika matokeo ya safari hii, ndiyo maana kidogo Serikali ikaamua kwamba katika jambo hili kama mnataka tusaidie, kama mnataka tuboreshe elimu, ni vizuri watoto wa Kidato cha Nne, wanaofika Kidato cha Nne wawe kweli ni wato ambao wamekidhi vigezo vya kufika Kidato cha Nne. (Makof)

Sasa, rai ya Mheshimiwa Zambi ni ya msingi. Lakini nataka niombe vile vile Waheshimiwa Wabunge, na sisi tujue kwamba tukiendelea kulichukulia jambo hili kimzaha mzaha, kiulegevu legevu hivi, tutafika huko mwisho, mtu hata kujieleza kwa lugha hata ya Kiswahili tu anashindwa, kitu ambacho kitakuwa ni hatari sana.

Kwa hiyo, ninachoweza kumwahidi Mheshimiwa Zambi ni kwamba kwa sababu jambo hili limetokana na maamuzi ya Baraza la Mitihani, chombo chetu ambacho kipo kwa mujibu wa sheria mliyoitunga, sana sana naweza nikawasilisha rai hii kama Wabunge wengi mnafikiria ni ya msingi sana, basi tuwaombe walegeze masharti.

Lakini mimi nasema kulegeza masharti inaweza ikawa kweli pengine ni ya manufaa, lakini *tahadhari* yangu ni kwamba ni vizuri tukaendelea kuliona kama ni jambo lisilokubalika. Lakini nitawasilisha na tutawashauri, tuone namna ya kuweza kuchukua hatua stahiki pengine kwa kulinganisha uzito wa jambo lenyewe au kosa lenyewe au kuona uwezekano pengine badala ya miaka mitatu, basi ibaki labda miaka

miwili. Lakini ni vizuri bado tukaendelea kulisimamia hili kwa pamoja ili kuhakikisha tunapata vijana ambao wana sifa. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi naelewa wewe ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ukitujibu kama ulivyojibu Mheshimiwa Waziri Mkuu maana yake unatuacha njia panda.

Kwa nini Serikali isitamke tu kwamba vijana walikosa, na mimi kama nilivyosema kwenye swalii langu la msingi kwamba vijana hawa wameishapewa adhabu tayari ya kufutiwa mtihani wao, hiyo ni adhabu tosha na kwamba hawatafanya mtihani vyovyote vile kwa mwaka huu wameshachelewa. Kwa nini Serikali isiwasamehe na kwa sababu wengi wanaomba ili kuanzia mwaka kesho wajiandikishe kufanya mitihani? Serikali inaona kuna ugumu gani Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ukiwa mzazi, mara nydingi hufanyi hivyo. Kama toto limekukosea kosea, limekuja limeombia radhi, husemi hapo hapo, hapana! Unamwambia tu nimekusikia, lakini angalia! Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema tupe tu nafasi kidogo, jambo hili wacha tukalitete vizuri.

Naelewa unachojaribu kusema na mimi ni mzazi nina watoto wanasoma vile vile, lakini nataka bado niendelee kuwaonyesha watoto hawa pamoja na Walimu ambao bado tuna-deal nao sasa hivi kwamba ni vizuri tabia hiyo ikakoma. Nadhani hilo ndilo jambo la msingi kabisa. (*Makofi*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama unavyojuu hali ya amani imevunjika kabisa Wilayani Tandahimba na moja ya sababu ni kwamba wananchi wamekata tamaa na Serikali yao kutokana na kutowalipa malipo ya awamu ya pili ya korosho zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wiki iliyopita hapa Bungeni uliliambia Taifa kwamba nyaraka zote zilikuwa ziko tayari kwa ajili ya kipeleka Benki Kuu kwa malipo. Ni lini sasa Mheshimiwa Waziri malipo hayo yatakuwa tayari? Aidha, huoni kwamba kuna funzo la Serikali kwamba kwa awamu ya pili kwa msimu ujao, malipo yasiwe kwa awamu awamu, walipwe mara moja, labda malipo ya nyongeza tu ndiyo ya awamu ya ziada?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nilikuja nikaeleza hapa kwamba tulikuwa tumepiga hatua nzuri kwa maana ya kwamba karatasi zote sitahiki zilikuwa sasa zimeshafikishwa kwenye vyombo vinavyohusika,

na nikasema ni matarajio yangu kwmaba tunadhani wiki inayokuja mapema hivi jambo hili linaweza kuwa lipo katika hatua nzuri zaidi.

Kwa hiyo nataka tu kumhakikishia Mheshimiwa Njwayo pamoja na Watanzania na hasa wakulima wa korosho, kwamba Jumanne Benki Kuu pamoja na Benki ya NMB wamewekeana saini mkataba ambao umetoa dhamana kwa mkopo wa bilioni hamsini na nne (bil. 54). Kwa hiyo fedha hizo sasa zipo tayari kwa ajili ya kuwa dispersed kwenda kwenye matawi ya benki ambako vyama vya ushirika ndiko vitatakiwa kupitisha maelezo yao ya ziada.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji jana usiku katika kufuatilia jambo hili akanithibitishia kwamba ni kweli jambo hilo limeshafikia hatua hiyo na akaniambia kwamba sasa kinachofuata ni mikataba kati ya vyama vya ushirika na benki kwa maana sasa ya mkataba wa mkopo wenyewe na ule utafanyika sasa katika kila tawi, lakini kila itakapokamilika ule mkataba fedha zitatoka na kulipa wale wote ambao sasa wanahusika na hilo jambo.

Mheshimiwa Spika, mtatuwia radhi jambo hili mnaona linachukua muda kidogo kwa sababu masuala ya fedha na hasa inapokuwa ni mkopo kwenye mabenki wakati mwengine hatuna njia ya mkato kwa sababu ni vyombo vinasimamia fedha, vinapenda kuwa na uhakika kuwa fedha zitalipwa, lakini hapa hatua iliyofikiwa Mheshimiwa Njwayo nadhani ni nzuri tuwasih sana Watanzania huko wawe watulivu kwa sababu fedha mkataba wake kwa maana ya dhamana umeshakamilika na vyama sasa vichukue jukumu lake kuhakikisha kwamba jambo hili sasa wanaliharakisha kwenye matawi ya *NMB*.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali imejifunza nini kutokana na zoezi hili kwenda polepole, Aidha mara nyingi tumekuwa tukikuona Wabunge wa korosho pamoja na jambo lililopo sasa lakini lipo jambo la asilimia 65 ya ushuru wa kusafirisha nje kupelekwa kwenye Halmashauri zetu za Wilaya ili zikaendelee kusaidia kuendeleza korosho, una kauli gani kwa wakulima wa korosho katika hili?

**SPIKA:** Ili mradi ni korosho basi maswali mengine yanakuwa korosho

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, swali lilikuwa ni Serikali imejifunza nini.

**SPIKA:** Na ndiyo hilo naomba ujibu.

**WAZIRI MKUU:** Lakini sasa naona likahama tena likaenda kwenye asilimia 25. Sasa Serikali tumejifunza nini, mimi nadhani kubwa ambalo mtaona linajitokeza litajitokeza kwenye zao la pamba na mazao mengine ya aina hiyo, ni kwamba kuna mambo mawili kwangu moja, huu utaratibu wa kuwa na kitu kinaitwa Bei dira ni utaratibu ambao utatuletea migogoro siku zote, kwa hiyo ni lazima tufike mahali Watanzania tukubaliane tuelewane kwamba suala la bei dira halina tija katika mazingira tuliyonayo kwa sababu bei hizi hazitawaliwi kutoka ndani.

Kama tunataka tuendelee na utaratibu huo ni lazima tukubaliane kuwa na mfumo mwingine wa ziada wa kuwa na mfuko ambayo ndiyo utakuwa unasaidia. Kupunguza hiyo kasi ya tofauti inapotokea vinginevyo tunajidanganya, si korosho, siyo pamba, siyo tumbamku siyo mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni hili ambalo ni la msingi sana, na jana katika majadiliano hapa Wabunge baadhi wamelieleza kwamba inabidi Serikali tukazane sana kwa kutumia sekta binafsi na sisi wenye kwa njia nyingine ama za *Public Private Sector Partnership (PPP)* kufufua viwanda vya korosho, maana tukiwa na uzalishaji wa ndani tunaweza vile vile tukawa sasa na uwezo wa kuwa na soko la uhakika hapa ndani badala ya kutegemea soko la nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi makubwa niliyojifunza ni hayo mawili.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya swali lake ya kiwango cha fedha ambacho kinatakiwa kurejeshwa kwenye Halmashauri, Mheshimiwa Njwayo anajua kwa sababu jambo hili tumekuwa nalo kwa muda mrefu lakini nataka nimhakikishie tu kwamba kanuni ambazo tulikuwa tunafikiria zitachukua muda mrefu zilishakamilika, nadhani kazi tuliyonayonayo sasa ni kuhakikisha kwamba fedha zile zipatikane.

Lakini kwa sababu ya matatizo yaliyojitekeza ndiyo maana umeona tumechelewa kidogo kwa sababu imebidi tumwombe *Controller and Auditor General (CAG)* atutafutie fedha hata hizo zilizotangulia, zilitumika vizuri kwa malengo yaliyokubaliwa au hapana ndiyo maana umeona kidogo kuna kuchelewa kidogo lakini tutakapomaliza tunahakika nalo hili litakuwa limekwisha.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika ahsante, Mkoa wa Lindi wenye Wilaya sita Nachingwea, Lindi Vijijini, Lindi Mjini, Kilwa, Ruangwa pamoja na Liwale. Wilaya tano kati ya hizo zina umeme, aidha wa kutoka Songas au kutoka *Mnazi bay* isipokuwa Wilaya ya Liwale peke

yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Wilaya hii imekuwa na matatizo ya umeme kwa muda mrefu kwa sababu ya ukoo kuu wa jenereta iliyopo pale, Serikali haionti kama kuna sababu za wazi za kutoa sasa umeme kutoka Somangafungu kuitia Nangurukuru, kuitia Njinjo na kijiji cha Zinga na Kijiji cha Kimambi, kuitia Miguruwe na Kichonda ili tuweze kumaliza tatizo hili la umeme liliopo katika Wilaya hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili swali lingefaa sana kwa Waziri wa Nishati na Madini, maana ukimwambia Waziri Mkuu Vijiji vyote ulivyoitaja. Mimi naomba Waziri wa Nishati na Madini uandae majibu hayo. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipatia nafasi kumwuliza Waziri Mkuu swali moja.

Waziri Mkuu, mimi ningependa kukuuliza kuhusiana na utaratibu wa namna tunavyoendesha kampeni, wakati wa kampeni kunatokea maneno machafu, maneno yasiyofaa.

**SPIKA:** Kampeni za Uchaguzi.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Maneno yanayokatisha tamaa, kunatokea vitisho, kunatokea utaratibu wa kumwondoa mtu katika utu wake na kumwacha haheshimiki tena katika jamii.

Waziri Mkuu unasema nini katika utaratibu wa kutuelekeza namna gani tuweze kutafuta kura za amani pasipokuwepo matusi wala vitisho kama vile hakutatawalika, damu itamwagika, haiwezekani tusiposhinda na kuvua watu nguo, mimi naomba unisaidie utaratibu.

**SPIKA:** Ahsante, nadhani ni kampeni za uchaguzi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naona swali limevuta hisia za wengi maana hata sikusikia mwishoni unasema nini maana yake nilisikia makofi tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini angalau kwa yale maelezo ya utangulizi nimepata maudhui ya nini unajaribu kutafuta. Tunayo sheria inayotawala Uchaguzi na ndiyo inayotuongoza kwa mambo yote. Vipo vitendo mle vimekatwazwa visifanyike wakati wa kampeni za Uchaguzi na ndiyo maana mara nyingi inapokuwa yametendeka kwa kiwango ambacho kinaathiri matokeo ya Uchaguzi mtu ambaye alikuwa katika kinyang'anyiro hicho anayo fursa ya kwenda mahakamani na kufungua

kesi kwa kutumia misingi hiyo aliyoiona dhahiri kwamba imeathiri sana matokeo ya Uchaguzi wake. Kwa hiyo, hilo ndiyo jambo la msingi ambalo mimi nalionna katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kubwa na hili nataka niwaombe Watanzania wote kwa ujumla kwamba ni vizuri kama Watanzania jitihada zetu za kujenga mfumo wa demokrasia na hasa demokrasia ya vyama vingi, ni lazima wote tujifunze kutokujilingiza katika mambo ambayo unaona dhahiri kabisa kwamba yanamdhalilisha mgombea mwenzako. Hata kama ndiyo mbinu ya kujaribu kumwondoa katika safu ya uongozi, kwa sababu vitendo hivi havijengi demokrasia vinadhalilisha mfumo mzima. Kwa hiyo mimi nadhani ni juu yetu sisi wote Watanzania kuliona hilo na ni jambo ambalo kwa kweli lina-cut across vyama vyote, iwe CCM, iwe CHADEMA, CUF wote ni lazima tuone kwamba halifai, tujenge *democracy* ambayo inatuwezesha watu kuweza kufanya hilo jukumu bila kujilingiza nchi katika matatizo ya kukashifiana kitu ambacho hakina misingi mizuri. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante, una swali la nyongeza maana yake ni kuvunja tu sheria.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, kitu ambacho naongolea, habari ya kusema kwamba damu itamwagika, watu wanatishika. Pia katika habari ya kutukanana wanawake wengi wanashindwa kwenda kupiga kura kwa sababu hawana uhakika kama kutatokea amani au nini.

**MBUNGE FULANI:** Hongo!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Wanawake wanaonyonyesha, wenye mimba, hawaawezi kwenda kupiga kura kutokana na vitisho hivyo.

**MBUNGE FULANI:** Wananunua shahada.

**SPIKA:** Tafadhali Waheshimiwa Wabunge mtatolewa nje hamwezi kusema namna hiyo!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi naelewa anachosema Mheshimiwa Mshama. Lakini usifikiri kwamba jambo hilo linawagusa wagombea wanawake tu, inaweza kuwa tu ni kiwango. Lakini haya mnayoyasema hata kati yetu wanaume kwa wanaume yapo ya kukashifiana, kutukanana. Ndiyo maana rai yangu kwa ujumla ni kwamba wote tujaribu kutokujilingiza nchi katika mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapokuwa kwenye nyakati za mapambano yale, wakati mwengine tunajisahau. Kwa hiyo kila mmoja anajaribu kutumia kila mbinu hata za msituni anatumia tu. Lakini kwa kweli ni vizuri kuwa na chaguzi ambazo zina staha.

**SPIKA:** Ahsante sana, hii inawahu watu wote wa Tanzania siyo vyama fulani fulani tu. Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nimwulize Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu Taifa lina kauli mbiu inasema Maisha Bora kwa Kila Mtanzania. Lakini mimi hainiingii akilini inapofika wakati njia kuu za mawasiliano zingine zinasuasua sana katika suala nzima la kuijenga kauli mbiu hii. Kwa mfano barabara, reli na kadhalika, nitazungumzia kwa kifupi tu reli ya kati ambayo ni Kigoma mpaka Dar es Salaam, Mpanda mpaka Dar es Salaam, Mwanza mpaka Dar es Salaam.

Tunahitaji kauli ambayo itatoka rasmi kwa Serikali kupunguza ukali wa maisha wanaosafirisha mizigo abiria wanaosafiri.

Je, ni kweli kwamba sasa Serikali inataka kubeba yote mawili kwamba ijenje reli mpya wakati kuna reli ambayo inahitaji tu ukarabati ili kusudi wananchi waweze kuwa wanaosafirisha mizigo yao kwa urahisi na watu kusafiri kutoka Dar es Salaam na kwenda pande zote nilizozisema kwa urahisi zaidi? Naomba majibu Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, yapo mambo mawili ambayo Mheshimiwa Hewa amejaribu kuyasema, moja ni ukarabati wa reli ili kuongeza ufanisi wa reli yetu lakini amegusa vile vile kwamba kuna ujenzi wa reli mpya. Nataka nielewe kwamba bila shaka reli mpya anayozungumza pengine ni lile wazo la reli ya Tanga, Arusha, Musoma ili tuweze kuunganika na Uganda kuititia majini na kwamba hii reli ya kati ndiyo anaizungumza kwa maana ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, reli ya Kati imekuwa ikikumbana na matatizo mengi na hasa yanayotokana na mafuriko ya maji imekuwa ni tatizo kubwa sana. Lakini kwa upande wa pili reli hii kwa mazingira ya sasa nayo vile vile imepitwa na wakati kwa sababu ni reli ambayo geji yake inaruhusu ubebaji wa mizigo kidogo sana ukilinganisha na *standard* geji ambazo zinahitajika.

Kwa hiyo Serikali inachofanya kwa sasa tunahangaika na ukarabati kwanza wa reli yenewe katika sehemu mbalimbali kujaribu kuiboresha, pili kujaribu kuona namna ya kuongeza idadi ya mabehewa na injini na kadhalika kitu ambacho kusema kweli kitatusaidia lakini si cha tija sana. Kwa hiyo jibu safi ni kuona uwezekano wa ujenzi wa reli mpya ya kati ambayo itaweza kuwa na viwango vya uzito wa kubeba injini kubwa, na hiyo ndiyo dhamira hasa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati huo huo tuna hilo wazo la pili la kujaribu kuunganisha ile reli ya Tanga kwenda hadi Musoma vyote kwetu ni muhimu wa wakati mmoja. Tunachofanya sasa ni kwamba wenzetu wa China wamekubali kufanya uchunguzi kwa maana ya upembuzi yakinifu kwa reli ya Tanga Arusha hadi Musoma jambo ambalo tayari limeshaanza na linaendelea, wakati ule ule wameamua.

Vile vile kufanya uchunguzi kwa reli ya kati kwa maana ya Dar es Salaam mpaka Kigoma Tabora kwenda Mwanza na tawi la Kaliua kwenda Mpanda, kwa nini wamefanya hivyo wamefanya kwa sababu uchunguzi wa ya kwanza ilifanyika miaka mingi kidogo inaonekana ni vizuri kuuangalia upya baada ya hapo ndiyo tunazungumza sasa tuone namna ya kuingia katika miradi yote miwili kwa sababu yote tunaihitaji ya kujenga reli kwa kiwango ambacho tunafikiri ni stahiki. Lakini wakati huo huo tusije tukasahau kwamba tuna Isaka kwenda nchi jirani ambaeo nao tunaendelea nao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Hewa kwangu mimi yote ni muhimu kwa sababu ni lazima tujaribu kulitazama hili kwa upana zaidi, ni gumu, zito lakini nadhani ni vizuri tukalitazama kwa njia hiyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika nashukuru, Waziri Mkuu ni katika Bunge hili wakati tukipitia hotuba ya bajeti ya mwaka 2011/2012 Bunge hili uliliahidi kwa dhati kabisa kwamba sasa umefikia wakati wa kuboresha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani wote, Wenyeviti wa Vijiji, na Wenyeviti wa Vitongoji, ukaliahidi Bunge hili kuwa ndani ya bajeti hii katika utekelezaji wake utahakikisha kuwa maslahi haya yameboreshwa na Waheshimiwa hawa sasa wataanza kulipwa vizuri.

Kwa kuwa, sasa hivi tunakaribia mwisho wa bajeti na Madiwani wanaendelea kulipwa laki na ishirini, Wenyeviti wa Vijiji wanaendelea kulipwa shilingi elfu kumi na sehemu nyingine hawalipwi kabisa, Bunge hili unaliambia nini sasa kuhusiana na maslahi ya Waheshimiwa hawa? (Makof)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ni dhamira ya Serikali na tulisema hilo kwa nia njema tu, lakini baada ya kuingia katika mchakato wa bajeti ule kulionekana kwa kweli kulikuwa na mkwamo mkubwa sana kwenye eneo la upatikanaji wa fedha kwa hiyo tukaona pengine zoezi hili tulisitishe kwa muda.

Lakini tumekubaliana na wenzetu wa TAMISEMI kwamba safari hii piga geuza tuhakikishe tunaingiza jambo hili kwenye bajeti tena mapema ingawa inawezekana isiwe kwa viwango tulivyokuwa tumefikiria hapo awali kwa sababu ya ugumu wenyewe wa bajeti hata ya safari hii mtaiona itakuwa *tight* kidogo, lakini tuna uhakika kabisa kwamba tutaongeza kidogo siyo kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani tunachoweza kuahidi ni hicho tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina swali fupi kabisa maana yake muda unaisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa umeahidi kwa dhati kabisa kwamba maslahi haya yataboresha piga geuza, kwa hiyo na Bunge hili kama hayataboreshwa basi piga geuza bajeti haitapita (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Mtapiga geuza sasa, Waziri Mkuu

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tulipokee tu kwa nia njema kwa sababu ni jambo jema tu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika ahsante, kwa kuwa suala la vitambulisho vya Taifa limezungumzwa na Serikali kwa muda mrefu na wananchi wamesubiri kwa matumaini makubwa, Je unawaeleza nini Watanzania kuhusu maendeleo ya zoezi hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Betty Machangu kwamba jambo hili tumekuwa nalo kwa muda mrefu lakini naomba tu sasa niseme nafurahi sana angalau sasa tumefikia hatua ya utekelezaji, Wakati wa Bunge hili mtakuwa bila shaka mliwaona wenzetu wa NIDA wako hapa na nadhani tayari hatua za awali kwa baadhi viongozi zimeanza kuchukuliwa kuanza kuchukua picha, vidole na kadhalika kama hatua ya mwanzo sasa kuanza mchakato wa mchakato wa uandaaji wa hivyo vitambulisho.

19 APRIL, 2012

Sasa tutakwenda kwa awamu lakini tumekubaliana kwamba ni vizuri katika kila awamu basi NIDA wawe wanatoa taarifa za mara kwa mara kuonyesha ni watu kiasi gani safari hii wataweza kuingia katika utaratibu huo ili tujue sasa ni wakati gani tujue sasa ni wakati gani zoezi hilo litakamilika faraja tu ni kwamba angalau tumeanza.

Nataka niwaombe sasa Watanzania wenzangu kwamba zoezi hili maadam limeanza mtakapokuwa mmefikiwa kwenye hatua zile za mwanzo za usajiri tujitokeze kwa wingi tuweze kusajiliwa kupata zile data za msingi na hatimaye kuchukuliwa picha za vidole pamoja na picha ya uso.

Nataka niwaombe sana vile vile kwa sababu nimepata fununu kwamba kuna sehemu nyingine wanataka kutumia mwanya huu kuanza kurubuni watu, vitambulisho hivi havinunuliwi hakuna Mtanzania atakayetozwa hata senti tano kwa sababu yoyote. Zoezi lote litaendeshwa kwa gharama ya Serikali.

Kwa hiyo, mtu ye yeyote atakayekuambia kwamba unahitajika sijui 50,000, 60,000 ujue ni mwongo. Huyu anataka tu kukuibia na dawa ni kumripoti tu kwenye vyombo vinavyohusika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, muda umekwisha, maswali yamebaki nimeogopa kuchanganya kwa sababu wengine waliamka saa tisa naambiwa sasa ukimrusha mtu hata nitakuwa simtendei haki. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru kwa majibu ya maswali hayo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema maswali kwa Waziri Mkuu yanakuwa yale ya kisera. Yakiwa yanahu tu jambo fulani kweli itakuwa siyo kumtendea haki Mheshimiwa Waziri Mkuu. Inatakiwa Mawaziri wanaohusika ndio waweze kuulizwa maswali hayo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Naomba tutumie muda vizuri nitakupa nafasi baadaye.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 97

### **Kupanua Kituo cha Afya Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Hospitali ya Tumbi ambayo inaendelea na upanuzi imepandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa kupanua Kituo cha Afya cha Kibaha ili kiwe Hospitali ya Wilaya na kukidhi huduma za afya kwa kazi kwa wakazi wa Kibaha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvester Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama lifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kibaha ina Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ina Kituo cha Afya cha Mlandizi ambacho kipo nje kidogo ya Mji na kinahudumia wagonjwa wapatao 72,000 kwa Wilaya ya Bagamoyo. Kituo hiki kinatoa huduma za upasuaji na kulaza wagonjwa na tayari maombi yalishawasilishwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupandisha kituo hiki kuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mkoani (Kibaha) ambacho kiko karibu na hospitali Teule ya Tumbi ya Mkoani wa Pwani kitaendelea kutoa huduma za ngazi ya kituo cha afya. Mkoaa wa Pwani unaboresha vituo vyote vya afya kwa kuvijengea uwezo wa kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa kuviwezesha kutoa huduma za dharura za upasuaji kwa mama wajawazito.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Halmashauri kupitia vyanzo vyake vya ndani imetenga shilingi milioni 20.0 kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya akina Mama Wajawazito ikiwa ni sehemu ya mpango wa upanuzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, tathimini iliyofanyika imeonesha kuwa shilingi bilioni 13.0 zinahitajika ili kujenga miundombinu yote inayohitajika. Katika Bajeti ijayo ya mwaka 2012/2013, Halmashauri imeomba maombi maalum ya shilingi bilioni 4.0 kwa ajili ya upanuzi wa kituo hicho. Aidha, Halmashauri imeandaa andiko la mradi write up ambalo limewasilishwwa katika ubalozi wa Ireland kupitia kitengo chake cha afya pamoja na Ubalozi wa Korea Kusini kupitia kitengo chake cha misaada, lengo likiwa ni kupata shilingi bilioni 2.0 kuendeleza ujenzi huo. (Makofi)

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a)Kwa kuwa maandalizi ya kukifanya kituo hiki kuwa Hospitali ya Wilaya yalikwishafanyika ikiwa ni pamoja na hata eneo la kiwanja cha Chama cha Mapinduzi kutwaliwa na kupanua eneo zaidi la kituo hiki cha afya ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Rais kuja kuweka jiwe la msingi kwa ajili ya kupanua kituo hiki kuwa Hospitali ya Wilaya. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Kibaha kuhusu upanuzi wa Kituo hiki kuwa Hospitali ya Wilaya?

(b) Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kutoa fedha hizi zilizoombwa ili kukamilisha ujenzi huu na kukifanya kituo hiki kuwa hospitali ya Wilaya? (Makof)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) :** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Silvestry F. Koka Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Labda niliweke vizuri kwa sababu moja ya maeneo ambayo yamekuwa yanatusumbua lilikuwa ni hili ambalo anauliza la kwanza hapa. Nimejaribu kuzungumza na viongozi wote wa Halmashauri na nimezungumza na *RMO* jana jioni Dkt. Beatrice Deligaba na nataka nim-quote hapa maamuzi yaliyofanywa na *Regional Consultative Committee* baada ya kufuatilia maoni yaliyokuwa yametolewa yalisema kwamba Hospitali ya Wilaya itajengwa Mlandizi na siyo Kibaha Mjini, hii nataka ikae vizuri na watu wa *Hansard* waiweke hivyo. Wala sina ugomvi na hili analolizungumza hapa. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Rais amekwenda pale na kuna mambo amefanya pale. Kuna viongozi wengine wamekwenda pale wamefanya mambo makubwa. Hii haiondoi ukweli kwamba Kituo hiki kitajengwa kwa kiwango hicho kinachozungumzwa lakini si kuifanya hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ukisema Hospitali ya Wilaya hapa unazungumzia *Establishment*, unazungumzia ikama yaani kuna *DMO* na Wakuu wa Idara na wale wengine wanaozungumzwa hapa. Kwa hiyo, nataka niiweke vizuri na rekodi zimeonyesha hivyo na vikao vyote vilivyofanyika vinaonyesha hospitali ya Wilaya haitajengwa Kibaha Mjini, Hospitali ya Wilaya itajengwa pale Mlandizi. Natumai kujibu swalii lake hapa.

Kuhusu hiki kiasi kinachotakiwa kwa ajili ya hiki kituo kwa sababu nacho tutakiendeleza na hii naangalia pia kwamba Tumbi nayo

19 APRIL, 2012

tunaongeza pale, Tumbi itakuwa ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, hili la bilioni 13 hela hizi zimeingia katika utaratibu wa maombi maalum na tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri, walau wapate hizo bilioni 2 kwa maana ya maombi maalum.

Ukisema unaingiza kwenye Bajeti ita-bust haitawezekana. Kwa hiyo, tutasaidiana naye kuhakikisha kwamba zinapatikana.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma inafanyiwa upanuzi kwa sasa na kwa kuwa ujenzi huo umesimama kwa sasa kutokana na ufinyu wa Bajeti na Bunge liliopita la Saba niliuliza swali hilo kuomba shilingi milioni 800 tulizoomba kwenye Bajeti mwaka 2011/2012 na Mheshimiwa Naibu Waziri akaniahidi kwamba katika mapitio ya Bajeti ya safari hii angemwona Mheshimiwa Mkullo ili tufikiriwe kupewa hizo shilingi milioni 800 ili ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma uendelee.

Je, Mheshimiwa Waziri unasemaje kuhusu hiyo ahadi uliyolahidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkullo ndio nani kwa mujibu wa taratibu za Serikali?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, aliyeniahidi ni Waziri wa TAMISEMI kwamba angemwona Mheshimiwa Waziri wa Fedha na maombi hayo yakafkishwa Wizara ya Fedha.

**SPIKA:** Sasa wewe unasema mambo ya watu binafsi haya Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

Hiki anachosema ni kweli hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoka hapa sasa hivi kuzungumza na ameeleza mambo ambayo kwa kweli tulifikiri katika Bajeti hii tungeyafanya lakini tulipokwenda kwenye uhalisi wenyewe tukajikuta kwamba hatukuweza kutekeleza yale yote ambayo tulikuwa tumeyazungumza hapa. Ametoka kujibu sasa hivi hapa.

Sasa mimni nakaa kwenye vikao hivi tunavyozungumza wakati mwingine ukisikia haya yanayoelezwa pale kwamba tuna-cut bajeti tunapunguza matumizi tunaangalia nini na mimi nasikiliza. Sasa ukitaka sasa lakini kuna Hospitali ya Mkoa wa Dodoma tulisema milioni 800 huyu bwana hatuelewi tunachozungumza hapa. Mimi nataka niseme hivi anachozungumza ni kweli hivi tunavyozungumza Wabunge hapa wanapata huduma katika hii hospitali tunayozungumza hapa.

Kwa hiyo, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Felister Bura, kwamba kuna haja ya kusaidia kwa hiyo, tutaendelea kufuatilia jambo hili kwa karibu zaidi ili tuweze kuona kwamba tunafanya nini tuweze kuwasaidia.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Longido iliomba kwa muda mrefu Bajeti maalum kwa ajili ya kujenga hospitali ya Wilaya. Je, inatuambia nini katika Bajeti hii ili na sisi Wilaya ya Longido iliyoko pembezoni ipate Hospitali ya Wilaya? (Makof)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado jibu linabakia lile lile ambalo nimelisema hapa, Mheshimiwa Lakule Laizer hasira zake zilipanda, hizi zikaenda na mimi wananchi wangu wa Siha wananzaika hapo hapo. Kwa hiyo, *declare interest* kabisa hapa na nalionna kaka yangu huu anafahamu kabisa kwamba mimi kila wakati akizungumza habari ya Longido hapa huwezi kuangalia Longido kama unavyoangalia Tanzania kwa maeneo mengine ni maeneo haya ambayo sisi tumeona kwamba ni maeneo yenye matatizo.

Lakini nataka niseme hapa bado tutaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer ili kuweza kuona kwamba huduma hizi zinapatikana hapa na kuweza ku-promote hii Hospitali ya Wilaya ili iweze kufanya kazi kama inavyotegemewa.

**SPIKA:** Swali linalofuata nadhani limefanyika na Ofisi yangu kutokutoa maelekezo kwa Waheshimiwa Wabunge walipoleta ombi la kutaka swali lake ijibiwe. Kwa mujibu wa Kanuni ya 39 (4) ambayo inasema taarifa ya swali itatolewa kwa maandishi na itapelekwa na kumfikia Katibu si chini ya siku 21 kabla ya tarehe ambayo jibu linahitajika kutolewa.

19 APRIL, 2012

Sasa kwa hiyo, Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, alipaswa kuambiwa na Ofisi yangu kwamba swali lake halikufikia siku 21. Kwa hiyo, kwa sababu kosa moja haliwezi kusahihishwa na kosa la pili naomba hili swali litajibowi siku nyingine. (Makof)

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na maswali tutapata baadaye taarifa.  
*Order Please.*

Na. 99

### **Ajira za Mkataba kwa Walimu na Watalaam wa Afya**

**MHE. SALOME D. MWAMBU** aliuliza:-

Serikali imeazimia kujenga Vituo vya Afya kwa kila kijiji na shule za sekondari kwa kila Kata, hata hivyo shule za Kata hazina walimu wala vifaa vya kufundishia na pia zahanati zetu hazina watumishi wa kutosha na kwamba miaka ya nyuma Serikali iliazimia kuwaajiri kwa mkataba maalum watumishi wa Elimu na Afya waliostaafu lakini zoezi hilo likasitishwa.

Je, Serikali itarudisha lini ajira hizo za mkataba kwa kada hizo zenyenye upungufu mkubwa wa watumishi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwaajiri watumishi kwa mikataba umeanisha katika Kanuni D. 28 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma toleo la 2009 na waraka wa Rais, Na. 1 wa mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, kutopteka na maelezo haya ajira za mikataba hasa katika maeneo yenye mahitaji makubwa kama vile Afya na Elimu zitaendelea kutolewa kwa mujibu wa Kanuni nilizozitaja. (Makof)

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Serikali haioni kuwa inawavunja nguvu wananchi wanaojitolea na kusimamia hii miradi inapofika mwishoni inakuwa haina utekelezaji wa haraka?

(b) Pale kwenye tatizo kubwa anapokuwa mtumishi mmoja mmoja hasa tukiangalia zahanati akiwepo mama wajawazito wanapata shida mno, mtumishi anapopata dharura na ikatokea hayuko kituoni.

Je, kwa nini Serikali isipeleke hata watumishi watatu watatu kwenye kila kituo cha Afya. Mfano Mwangeza, Mpambala, Matongo, Niganga huko kote yuko mtumishi mmoja mmoja anapokwenda kwenye mshahara ndio hivyo zahanati inafungwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Salome Mwambu, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyotangulia kusema katika jibu langu la msingi ni kwamba hatujakataa kuajiri watumishi kwa mkataba katika maeneo yenye upungufu mkubwa wa watumishi. Mfano katika sekta ya Afya na Elimu. Kinachotakiwa ni mwajiri mwenyewe, kama kuna mtumishi wake ambaye anamwona anafaa na anakaribia kustaafu eneo hilo hakuna mtu wa kuweza kushika nafasi, basi yeye ndiye anayemwombea ajira ya mkataba. (*Makofi*)

Kuhusu suala la watumishi wa Afya katika maeneo ambayo Mheshimiwa ameyataja Wizara ya Afya tunawapa kibali kila mwaka cha kuwapangia watumishi wote wanaomaliza katika kada ya afya na wanapofika katika Wilaya husika, Wilaya zenyewe ndio zinaweka kipaumbele watumishi hao waende katika eneo gani. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyoainishwa katika swalii la msingi yanahusiana na swalii langu la nyongeza. Shule ya Sekondari ya Dabu iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ina vitabu vyatia mbili tu Sayansi na *Mathematics*. Shule hii haina vitabu vyatia *Jiografia, Civics, Kiswahili, Historia na kadhalika*.

Je, Serikali itapeleka lini vitabu katika shule hii ili wanafunzi wasiendelee kupoteza muda kuhudhuria shule bila kujifunza.

**SPIKA:** Ina uhusiana na hili swali la msingi? Mbona pale ilikuwa ni watumishi kupelekwa, hapa vitabu? Sijui nani ajibu hapa Serikali ni hiyo hiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba swali limekwenda tofauti kama ulivoyozungumza napenda nijibu kwa sababu niko kwenye Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna upungufu mkubwa wa vitabu katika shule nyingi hapa nchini, lakini tumeambiwa kwamba Serikali sasa hivi iko katika mchakato kutumia fedha yetu ile ya *change*, maarufu kama *change* ya Rada kuhakikisha kwamba tunaongeza upatikanaji wa vitabu katika shule zetu. (*Makof*)

Na. 100

### **Ujenzi wa Barabara za Nyamwaga**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Miundombinu ya barabara Wilayani Tarime si ya kuridhisha:-

- (a)Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Nyamwaga inayotoka Mto Mara – Nyamongo – Nyamwaga – Tarime Mjini yenye urefu wa km. 53?
- (b)Je, Serikali inasema nini juu ya barabara ya Mkoa wa *Security Road* inayotoka Rarya – Susuni – Kubiterere – Sirari – Remagwe - Nyabisaga- Borega – Kimusi- Ntantira - Muriba- Itivyo - Mangucha hadi Kegonga?
- (c)Je, ni lini ahadi ya Waziri Mkuu ya kupandisha hadhi barabara ya Mangucha – Masanga – Ketawasi – Gibaso hadi Mrito kuwa barabara ya Mkoa itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime Mjini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi ina mpango wa kuijenga barabara ya Tarime Mjini – Nyamwaga – Nyamongo hadi mto Mara yenye urefu wa km 53 kwa kiwango cha lami

nyepesi (*Otta Seal*) kwa awamu ili iendelee kupitika majira yote. Katika mwaka 2011/2012 Serikali imetenga shilingi milioni 330 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami nyepesi. Aidha mchakato wa kumtafuta mkandarasi upo kwenye hatua ya uchambuzi wa zabuni *evaluation*.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 369.611 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida muda maalum na ukarabati wa *security road* inayotoka Rarya – Susuni – Sirari – Barega – Nyantira – Muriba hadi Kegonga. Kazi za matengenezo zinafanya katika maeneo mbalimbali ya barabara hii kulingana na mikataba. Tayari mkandarasi ameshaanza kazi na anategemewa kumaliza kazi ifikapo mwezi Juni mwaka huu 2012.

(c) Mheshimiwa Spika, maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu kuipandisha hadhi barabara ya Mangucha – Masanga – Ketawasi – Gibaso – Mrito (Km 24) kuwa ya Mkoa yamewasilishwa Wizarani na Mkuu wa Mkoa wa Mara na yanafanyiwa kazi.

Aidha, kwa vile kwa sasa barabara hiyo bado ni ya Wilaya tunaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Tarime iendelee kuitengea fedha za kuifanya matengenezo na ukarabati ili ipitike kiurahisi wakati ombi la kuipandisha hadhi likiendelea kushughulikia kwa kuzingatia sheria Namba 13 ya Mwaka 2007.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kwa kiasi fulani yanatia matumaini kidogo, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Ni kwa nini Serikali isiwashirikishe wadau mbalimbali . Kwa mfano Wawekezaji wa mgodi wa *North Mara* katika kuhakikisha kwamba hii barabara inajengwa kwa kiwango cha lami na si kuwekewa lami nyepesi nyepesi?

(b) Ni lini ahadi hii ya Waziri Mkuu itatekelezwa ili kuwaondolea adha wananchi wa Tarime wanaotumia hii barabara ya kutoka Mangucha, Masanga, Kitawasi, Kibaso hadi Murito kwa kuwa Waziri Mkuu mwenyewe alipita akaangalia hii barabara jinsi ilivyo na uwezo wa Halmashauri ni mdogo kabisa katika kuijenga hii barabara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, kama ifuatavyo:-

(a)Kwanza kuhusu suala la Serikali kwa nini haliongei na mgodi kuweza kujenga barabara yenye lami nzito nzito zaidi. Ningependa tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango ya Serikali haiwezi kutegemea ufadhili wa mgodi, mpango wa Serikali ni kuijenga hiyo barabara kwa *otasil*, kwa lami nyepesi na sio kwamba tunajenga lami nyepesi kwa kufikiria tu haraka haraka lakini kwa kuzingatia ushauri wa wataalam kwa sababu barabara hiyo haina magari mengi kiasi ambacho tungeweza kujenga barabara ya lami nzito *concrete asphalt* kwa mfano.

(b)Lini ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itatekelezwa. Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea agizo hilo la Waziri Mkuu na tumesema tumepokea hiyo barua kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara na tunalifanyia kazi. Lakini kwa kuzingatia Sheria Na. 13 ya mwaka 2007, lakini tumesema kabla hatujatoa majibu kwa sababu hili ni mchakato wa wataalam, tungeomba Halmashauri husika iendelee kuihudumia hiyo barabara katika kipindi hiki kifupi.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ningependa kumwuliza kwa mara nyingine Naibu Waziri, katika Bunge lilitopita, niliuliza swali kwamba Mheshimiwa Rais akiwa ziarani Mkoani Kigoma pamoja na Balozi wa Abu Dhabi walitua ahadi kwa pamoja ya kujenga kilometra 50 za barabara ya lami kwa ajili ya kuunganisha barabara mbili za lami kati ya ile ya Uvinza- Kidawe kilometra 76 na ile ya Malagarasi-Nguruka kilometra 48. Naomba kujua mpaka sasa ule mpango wa kilometra 50 kuunganisha barabara hizi mbili umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kafulila, kama ifuatavyo:-

Huo mpango wa kuonganisha hizo barabara mbili bado upo, suala ni utekelezaji. Lazima twende kwa awamu kwa sababu ni mpango mpana zaidi unahusu ujenzi wa daraja na *joining roads*. Kwa hiyo, bado uko pale pale suala tu ni mpangilio wa kazi.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Mbeya-Chunya-Makongorosi toka imeanza mwaka 2008 imesuasua sana ujenzi wake kwa kiwango cha lami na kwa kuwa pamoja na kuwepo wakandarasi wawilli, mmoja wa kuanzia Mbeya- Lwanjio, mwininge Lwanjio -Chunya, lakini wananchi wa Chunya wameshtuka sana kumwona Mkandarasi wa kipande cha

19 APRIL, 2012

Lwanjiro -Chunya akianza kuondoa vifaa vyake ina maana kwamba labda ujenzi wa barabara hiyo umesitishwa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, unajua kwamba wananchi wa Chunya ni wa kwako unawaambiaje kuhusu ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Victor Kilasila Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kujenga barabara kutoka Mbeya- Chunya hadi Makongorosi uko pale pale. Hapo kati kati napenda kukiri kwamba kulitokea na matatizo katika hiyo barabara ambayo Bunge lilielezwa Mkandarasi aliyekuwepo ilibidi tumwondoe tumweke Mkandarasi mwingine ambaye ndiye yuko pale kwa sasa. Lakini hivi katika kipindi kifupi, kulitokea vile vile tatizo la malipo ambalo tumeshalirekebisha . Sasa, wananchi wa Chunya napenda tu kuwahakikisha tu kwamba ujenzi wa barabara hiyo bado uko pale pale na Serikali sasa inalifuatilia hilo suala kwa makini. (Makofi)

Na. 101

### **Vurugu za Mashabiki wa Mpira Nchini Misri**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Je, Tanzania inajifunza nini kutohana na vurugu za mashabiki wa mpira wa miguu huko nchini Misri ambazo zilisababisha watu 74 kupoteza maisha na wengine wengi kujeruhwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kujifunza kuwa mahali popote penye mikusanyiko ya watu wengi, yanaweza yakatokea maafa endapo taratibu za msingi za kuwepo mikusanyiko hiyo hazikuzingatiwa. Taratibu hizo za msingi ni pamoja na mamlaka zinazohusika na mikusanyiko kutofanya maandalizi ya kina kama vile usalama wa watu na mali zao, mazingira yanayolingana na ukubwa wa mikusanyiko, kubashiri

matukio yanayoweza kujitokeza kabla, lakini pia wakati na baada ya tukio la msingi na kuchukua hatua muafaka.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa bado mamlaka nchini Misri zinaendelea kutafakari sababu za msingi za kutokea kwa vurugu zile. Bado kuna fununu za kuhusishwa tukio hilo na sababu za kisiasa na huku wengine wakidai ni ushabiki tu uliopitiliza.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyyote iwavyo, Wizara yangu inaendelea kuchukua hatua za tahadhari kwa ushirikiano na mamlaka nyine zilizopo.

Hatua hizo ni pamoja na kuwaelimisha na kuwahamasisha Watanzania umuhimu wa kushabikia na kushangilia timu zetu kwa amani na utulivu. Kazi hii inafanywa kwa ushirikiano mkubwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama, Vyombo vya Habari, Viongozi wa Vilabu na TFF. (Makofii)

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Wengi wa wahanga wa vurugu wa soko nchini Misri, ukiacha wale waliopoteza maisha kwa msongamano na kukosa hewa, lakini wengi wengine wameonekana na majeraha ya silaha za kienyeji.

Je, Serikali ina mikakati gani ya ulinzi wa viwanja vyetu hapa nchini?

(b) Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri nanukuu kidogo, anasema kwamba wanahamasisha na kutoa elimu kwa Watanzania umuhimu wa kushabikia na kushangilia soka, lakini inaonekana elimu hii either ndogo au wanaoelimishwa hawafahamu kwa sababu dalili za uvunjifu wa amani zimekuwa zikijitokeza hasa katika uwanja wetu wa Taifa, viti vinavunjwa na kutupwatupwa, mashabiki wanatupa chupa katika uwanja na kadhalika.

Lakini hasa ushabiki wa kati ya Simba na Yanga umekuwa mkubwa sana. Ikiwa tu mtu amevaa fulana ya njano au nyekundu hata asiwe shabiki, lakini akipotelea upande wa timu mojawapo basi anaweza akapigwa na fulana ile ikachanwachanwa haya yote yanapelekea kuwa na uvunjifu wa amani.

Lakini pia sasa marefa wanapigwa kama watoto wadogo katika viwanja. Katika mchezo wa Azam na Yanga, refa kapigwa uwanjani pale na juzi hapa Dodoma kati ya mchezo na Polisi.

Je, kuna mikakati gani ya kutoa elimu zaidi kwa mashabiki pamoja na vilabu ili tusije tukafikia mahali walipofikia wenzetu wa Misri? (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana , sasa Waziri usije ukapata tabu ya kujibu kirefu, naomba ujibu kwa kifupi tafadhali, ni swali lile lile tu amelizungusha.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, kama ifuatavyo:-

Kwanza hili swali lake ambalo linasema Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha vitendo vinavyoashiria uvunjifu wa amani vinakomeshwa na havirudiwi, mimi napenda tu niseme kwamba Serikali ina mikakati, kwanza nikiri kweli kabisa kuna viashiria vya uvunjifu wa amani upon a baadhi ya mechi kama alivyozitaja baina ya Simba na Yanga, Simba na Kiyovu lakini pia hata huko kupigwa kwa marefa kumejitokeza na ninataka niseme tu kabisa kwamba kama Serikali tunataka tuchukue ombi rasmi na ambalo nimelizungumza pia katika jibu lang la msingi kwamba washabiki pamoja na wale ambao ni wapenzi wa soka tujitahidi kujizuiya kufanya fujo wakati tunapokwenda katika michezo yet hiyo ya mipira.

Tujitahidi kabisa kuhakikisha kwamba vitendo vyovyote vinavyoleta usababisho wa vurugu tunaviepuka. Tujengee utamaduni mzuri wa mashindano na hasa mashindano ya mchezo wa soka ni masuala ya burudani basi na sisi tunapokwenda pale, tujifunze kabisa kwamba tumekwenda pale kuburudika, lakini pia kuweza kushangilia timu zetu vizuri.

Sasa katika lile suala lingine la mikakati gani ambayo tunaichukua kuhakikisha vitendo hivi vya uvunjifu wa amani haviendelei au ukosefu wa amani hauendelei katika viwanja vyetu ni kwamba hatua nyingi za tahadhari tunazichukua kama Wizara na kama Serikali lakini tukishirikiana na *TFF* pamoja na Polisi na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama pamoja na vyombo vya habari na kama ni mfuatiliaji wa karibu wakati wa timu kubwa kubwa zikianza kucheza mara nyingi Kamada Kova anazungumza mtamsikia mara nyingi katika vyombo vya habari atazungumza kwa bidii kabisa lakini siku moja au mbili kabla ya hizo teams kukutana kunakuwa

19 APRIL, 2012

na mukutano ambao unawavuta wadau mbalimbali ambao wanaweza wakashughulikia kuhakikisha kwamba vurugu mbalimbali hazitokei.

Na. 102

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE)**  
aliuliza:-

Kuna Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) ambayo yaliingia nchini kwa lengo la kusaidia kutoa utaalami wa afya na kujenga uwezo wa kupambana na UKIMWI chini ya mradi wa PEPFAR sasa yameanza kubadili majina na kujisajili nchini huku yakichukua fedha za wafadhili kwa vigezo kuwa ni *NGOs* za kizalendo:-

- (a) Je, Serikali imeliona tatizo hili?
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani ili *NGOs* za Kitanzania ziweze kuwa walengwa wa ruzuku hizi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Faustine Englebert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna *NGOs* za Kimataifa zilizojaza na kuwasilisha Fomu Na. 9 kwa Msajili wa *NGOs* kwa lengo la kufanya mabadiliko ya kuwa *NGOs* za ndani; na kwa kuwa Mashirika ya ndani huanzishwa na Watanzania pekee, ni vigumu kwa sasa Wizara kusema kama kuna tatizo la *NGOs* za nje kubadili majina na kufanya kazi kama *NGOs* za kizalendo.

(b) Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Serikali kwa *NGOs* ni kuweka mazingira wezeshi si katika kufikia ruzuku za wafadhili wa nje pekee bali pia katika kupata rasilimali za ndani.

Baadhi ya hatua ambazo Serikali kupitia Wizara yangu imechukua ni pamoja na kutunga Sera ya Taifa ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2011 na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 iliyorekebishwa mwaka 2005 ambapo pamoja na mambo mengine zimelenga kuondoa migongano baina ya *NGOs* za ndani za zile za Kimataifa ikiwemo katika kufikia rasilimali kutoka kwa wafadhili wa nje.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Asasi nyingi zisizokuwa za Kiserikali, zimekuwa zikisaidiana na Serikali katika kutoa elimu katika jamii na kusaidia shughuli za kimaendeleo. Lakini baadhi ya asasi zisizo za Kierikali zimekuwa zikishindwa kufanya hivyo na matokeo yake kujihusisha kwenye masuala ya kisiasa na kujenga chuki kati Serikali na wananchi kwa ajili ya kutimiza azma za kisiasa kwa baadhi ya vyama fulani fulani:-

(a) Mheshimiwa Spika, huku tunakoelekea, tunaenda katika mchakato wa Katiba mpya na tuna habari kwamba kuna baadhi ya vyama vimejipanga kuhakikisha kuleta asasi zisizo za Kiserikali kwa ajili ya kushinikiza wananchi kutimiza malengo yao ya kisiasa na agenda zingine katika Katiba mpya.

Je, Serikali wanalijua hilo na wamejipanga vipi?

(b) Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko katika ada ya usajili na kama tunavyojuua vijana wengi ambao wanamaliza elimu ya juu mbali ya kwamba kuna tatizo ya ajira, lakini wengi wamekuwa wakipenda kuanzisha NGOs zao, lakini wanakwama kwenye ada ya usajili.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kupunguza ada hiyo ili vijana wengi waweze kuanzisha NGOs zao?

**SPIKA:** Ada yenewe shilingi ngapi?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ada yenewe ni shilingi laki mbili.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Ester Bulaya, maswali yake mawili ya nyongeza:-

Kwanza ningependa niwafahamishe wananchi kwamba kila NGO imeanzishwa ikiwa na majukumu ambayo yamo katika Katiba yake. Kwa hiyo NGO ambazo zinaacha majukumu yake na kufanya majukumu mengine ni uvunjaji wa sheria ambayo imeunda ile NGO.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la NGO iliandaa Kanuni za madili za NGO ambayo ilipitishwa 2008. Kwa hiyo, hizo NGOs zikiwemo pia na NGO za *briefcase* zinatakiwa kuchukuliwa hatua:-

(a) Mheshimiwa Spika, tuna Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao ni wasajili wa NGOs katika kila Wilaya. Kwa hiyo, kwa kupitia Bunge hili

nawahamasisha na kuwaagiza wale Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika Wilaya waangalie kwamba NGOs ambazo zinafika katika maeneo yao na kufanya majukumu mbali na yale ambayo yameandikwa watufahamishe ili hatua stahiki zichukuliwe.

(b)Swali la pili linazungumzia kuhusu ada ya usajili kuwa ni ya juu. Naona hili pengine tulichukue na tulifanyie kazi. Lakini nadhani ada iliyopo si kubwa kiasi hicho, lakini bado mimi nalichukua tuliangalie pengine inawezekana ni kweli kwa vijana ambao wanaanzisha asasi zao wanashindwa kufanya hivyo. Ahsante sana.(Makofi)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Katika kujibu swali la nyongeza kuhusiana na NGOs kwenda kinyume na majukumu yake na pengine kutumiwa kisasa. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali iko tayari kuchukua hatua kwa NGOs ambazo zimekwenda kinyume na majukumu yake. Sasa ningependa kuuliza swali tu.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuanzia NGO ya Mke wa Rais, Mama Kikwete ya WAMA ambayo wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwka 2010 ilitumika wazi wazi kisasa? (Makofi)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete, katika shughuli zake alizofanya wakati wa kampeni hakwenda kufanya kampeni kama WAMA. Alikwenda kufanya kampeni kama Mke wa Rais, ambaye anagombea nafasi. Ninaamini kwamba, hata wewe wakati ukigombea mke wako atakuwa bega na bega na wewe. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Bahati nzuri Mheshimiwa Mnyika hana mke, labda *girl friend* tu. (Kicheko/Makofi)

Haya tunaendelea, tutamtafutia mmoja humu humu. Tunakwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Hokororo atauliza swali hilo.

Na. 103

### ***Wafanyakazi Wanaokatwa Malipo ya Bima bila Kujiunga***

**MHE. AGNESS E. HOKORORO** aliuliza:-

Wapo wafanyakazi ambao hawajajiunga wala kujaza fomu za kujiunga na Bima ya Afya lakini wanakatwa kwenye mishahara yao,

ambapo wengine hutumia Bima zingine za familia zao kama vile AAR na kadhalika:-

- (a) Je, kwa nini wafanyakazi hao wanakatwa malipo ya Bima wakati siyo wanachama wa Mfuko wa Bima (NHIF)?
- (b) Je, makato hayo wanayokatwa yanakwenda wapi?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 8 ya Mwaka 1999, Watumishi wote wa Umma ni Wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hivyo, wanapaswa kuchangia asilimia tatu ya mishahara yao na mwajiri wao ambaye ni Serikali, kuchangia asilimia tatu ya mishahara yao kila mwezi na hivyo kufanya jumla ya asilimia kuwa sita ya mchango. Wapo baadhi ya watumishi ambao kwa kutokuelewa vyema Sheria, wanadhani kuwa uanachama unaanza baada ya kuanza kuchangia, kitu ambacho siyo sahihi kwani uanachama katika Mfuko ni suala la kisheria linalotoa wajibu kwa mtumishi kujaza fomu ili apatiwe kitambulisho. Hivyo, uanachama unakamilika mfanyakazi anapojaza fomu, anapowasilisha michango na anapopatiwa kitambulisho.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kila mwanachama anao wajibu wa kuhakikisha anajaza fomu ili apatiwe kitambulisho. Vile vile kila mwajiri ni vyema ahakikishe watumishi wote wanaokatwa fedha za Mfuko wanajaza fomu na kupata vitambulisho vitakavyowahakikishia upatikanaji wa huduma za tiba wakati wote. Pia Mfuko katika taratibu zake za utendaji kazi huwatemebelea wanachama na kuwashimiza kujaza fomu ili wapate vitambulisho.

(b) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni Mfuko unoendeshwa kwa mfumo wa kuchangia, ambao michango inayotolewa na wachama huwekwa pamoja bila kujali nani kachangia kiasi gani. Hivyo, michango hiyo ndiyo inayoujengea Mfuko uwezo wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali kama vile kulipa malipo ya huduma zitolewazo kwa wanachama, uwekezaji unaolenga kuboresha Sekta ya Afya kwa mfano ujenzi wa hospitali na kadhalika. Kukopesha vifaa tiba kwa hospitali, zahanati na vituo vya afya. Hata hivyo ni muhimu kutambua dhana hii ya makato kuweka kwenye vifaa vya Mfuko ili kuwezesha kufanya yafuatayo:-

(i) Kufanikisha dhana ya kusaidiana na mshikamano (*mutual solidarity*), pale wanachama wenye uwezo mkubwa wa kuchangia wanapomsaidia mwenye uwezo mdogo na asiyemwa anapomsaidia anaeumwa;

(ii) Kujiwekea kinga na uhakika wa kupata matibabu ya afya pale mwanachama utakapougu; na

(iii) Kutoa mafao ya Mfuko wakati wote wa uhai wa wanachama, ambapo huduma hutolewa kuitia vituo vya huduma za afya vya umma, watoa huduma bila faida na watoa huduma binafsi.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kimsingi Mfuko wa Bima ya Afya huduma zinazotolewa haziridhishi kabisa na hii inatokana na ukosefu wa dawa na vitendea kazi katika hospitali ambazo zimeteuliwa kutoa huduma hii. Je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki wafanyakazi ambao inawalazimisha kujiunga kwa kuwa hata waliokuwepo bado hawapati huduma bora za afya? (*Makofii*)

(b) Katika majibu ya msingi imeainishwa wazi kuwa Watumishi wote wa Umma ni Wanachama wa Mfuko huo. Je, kwa nini zipo baadhi ya Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ambayo hawahudumiwi na Mfuko huu badala yake wanatumia utaratibu mwingine wa kupata huduma za kiafya kama vile *TRA* na Benki Kuu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba ni kweli huduma za afya tunazotoa katika vituo vyetu vya umma bado hazikidhi kabisa haja au mahitaji ya wananchi. Nimekuwa nikitolea maelezo mara kwa mara suala hili na Serikali tumejipanga namna gani tunakabiliana na tatizo hili. Tatizo kubwa pale linalojitokeza katika vituo vyetu ni vifaa tiba, vitendanishi na dawa. Hii inatokana na mambo matatu ambayo Serikali tumejipanga namna ya kukabiliana na mambo haya.

Mosi, ni suala la bajeti finyu na ndiyo maana tumbeni toka mwaka 1999 Mifuko hii miwili ya Bima ambayo tumeeleza katika jibu la msingi na ule Mfuko wa Afya ya Jamii ambao unawaunganisha wananchi ambao hawapo katika ajira ya sekta rasmi wakiwemo wananchi wa kawaida, wakulima, wafugaji, mama lishe na kadhalika. Sasa hii kama tutakuwa

na coverage ya kutosha, tutaweza kujazia uhaba huu wa Serikali wa kupeleka fedha zisizoweza kukidhi mahitaji ya dawa na vifaa.

Lingine ni suala la mfumo wetu wa usambazaji wa hizi dawa, kuanzia manunuzi, kuhifadhi na kusambaza. Tumesema tunauboresha, ambapo sasa hivi tumeanza nalo, hali inaonesha tunakwenda vyema, badala ya kuishia Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya dawa hizi na vifaa hivi sasa vinapelekwa moja kwa moja kwenye kituo husika. Lingine kubwa ambalo ninawaomba Wabunge mara kadhaa ndani ya Bunge, mtusaidie katika kusimamia. Hapa tuna upungufu katika usimamizi wa huduma zetu na dawa ambazo tunapeleka kule. Kila kituo au kila zahanati kuna Kamati au kuna Bodi; Bodi zile zikiwa hai zitatusaidia sana katika kudhibiti uvujaji wa dawa. Lingine ni kwamba, Serikali tumeliona hili, baadaye tutaziwekea dawa *label* maalum ili wenzetu wa kwenye sekta binafsi wasituibie hizo dawa ambazo tunawapelekea.

Swali la pili, Taasisi ambazo anasema zingine, hizo alizozitaja ni taasisi ambazo zinajitegemea hazipo moja kwa moja Serikalini. Kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya Mwaka 1999, watumishi walio katika Serikali Kuu hao wote kwa mujibu wa Sheria hii ni wanachama na ndiyo maana wanakatwa na hata kama hawatapata huduma hizi lakini tunawashauri waende kwenye vituo vyetu ambavyo tunaviboresha siku hadi siku wapate huduma hizo.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Licha ya wafanyakazi katika baadhi ya maeneo hususan Jimbo la Rombo wakulima wamekuwa wakihamasishwa kuchangia Bima ya Afya kati ya shilingi elfu tano na elfu kumi kwa mwaka na kama ilivyo ada hakuna dawa zozote wanazopata. Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuhamasisha huduma hii ya bima kwa wakulima wakati haiwasaidii chochote ni dhuluma kwa hiyo ni afadhali kusitisha zoezi hili mpaka hapo itakapojipanga?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo ni kwamba, tunaamini Mifuko hii miwili ya Bima ya Afya kama ikiwa na wanachama wa kutosha tunaweza tukamaliza tatizo la uhaba wa fedha katika kuhudumia Sekta yetu ya Afya. Changamoto hizi ambazo zinajitokeza za kukosa dawa na vifaa katika vituo vyetu, wananchi naomba watuvumilie, watuelewe, yatafikia mwisho na tumejipanga vizuri sana kama nilivyoeleza kwenye jibu la nyongeza kwa Mheshimiwa Hokororo kwamba, mtupe muda haya baadaye haitakuwa hadithi, mtaona kwa vitendo.

19 APRIL, 2012

**SPIKA:** Jamani muda umekwisha, tunaenda Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Kabwe Zitto atauliza swali hilo.

Na. 104

**Uwekezaji wa Kampuni ya China Sonangol Nchini**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Mwaka 2006/2007, Serikali iliingia makubaliano na Kampuni ya China Sonangol kuhusu uwekezaji kwenye ATCL, Terminal III – J.K. Nyerere Airport na VIP Lounge J.K. Nyerere Airport:-

- (a) Je, makubaliano hayo yamefikia wapi mpaka sasa?
- (b) Je, katika makubaliano hayo Serikali ya Tanzania ilitoa nini (*offer*)?
- (c) Je, ni nini hatma ya ujenzi wa Terminal III?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mwaka 2007 Serikali ilifanya mazungumzo na Kampuni ya *China Sonangol International Limited (CSIL)* ya Jamhuri ya Watu wa China kuhusu uwekezaji katika Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) na uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha *Julius Nyerere International Airport (JNIA)*, kwa kuingia makubaliano ya awali (*Memorandum of Understanding*) katika maeneo hayo mawili.

- (a) Mheshimiwa Spika, baada ya kusainiwa kwa MoU ilitarajiwa kuwa majadiliano ya kina yangefanyika kati ya Serikali na Kampuni hiyo kwa matarajio ya kusaini Mkataba. Kampuni ya CSIL ilitarajiwa kununua asilimia 49 ya hisa za ATCL na hivyo kuwekeza katika ununuzi wa ndege mpya, uboreshaji wa huduma na uendelezaji wa JNIA. Majadiliano ya kina na CSIL hayakukamilika na hivyo utekelezaji wa makubaliano ya awali kutoanza. Kilichofanyika, kama hatua ya kwanza ni uboreshaji wa huduma za ATCL ambapo CSIL iliwezesha ATCL kukodisha ndege kubwa aina ya *Airbus*, 320 kutoa msaada wa kununua ndege mbili aina ya *Dash 8* na ujenzi wa Ukumbi wa watu mashuhuri (VIP Lounge) pale JNIA.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya CSIL kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, ilijenga Ukumbi wa Watu Mashuhuri kwa gharama ya Dola za Marekani milioni nane (sawa na shilingi bilioni 12). Kati ya hizo, Serikali ilitoa Dola za Marekani milioni mbili (sawa na shilingi bilioni tatu) na CSIL ilitoa msaada wa Dola za Marekani milioni sita (sawa na shilingi bilioni tisa).

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imechukua hatua za kuanza kufanikisha ujenzi wa jengo la tatu la abiria (*Terminal III*) katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere International Airport (JNIA). Hatua hizo ni pamoja na kulipa fidia za mali kiasi cha shilingi bilioni 28.5 na kuwatafutia maeneo mbadala Wakazi wa Kipawa, Kigilagila na Kipunguni, ambao maeneo yao yalikuwa ndani ya eneo la Mradi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kiasi cha shilingi bilioni 15.5 ili kulipa fidia Wakazi wa Kipunguni. Hatua nyingine ni kutafuta fedha za mkopo wa ujenzi au kutumia utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership – PPP*). Hadi sasa, kampuni 19 ikiwemo CSIL zimeonesha nia ya kuwekeza ATCL kwani muda wa uhai wa MoU kati ya Serikali na CSIL ulikwisha tarehe 30 Novemba, 2011.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Kampuni hii ya CSIL iliingia Mikataba miwili na Serikali yetu (*Memorandum of Understanding*). Mkataba wa kwanza ni huu ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumza na wa pili ulikuwa wa kupewa *block* mbili za kutafuta mafuta katika Mkoa wa Rukwa, *Lake Rukwa Basin*. Kwa kuwa kupewa huko kwa *block* ya mafuta na TPDC hakukufuata Kanuni na Sheria ya Manunuzi, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, illiagiza TPDC kufuta *block* zile kwa CSIL na kutangaza upya na wakafanya hivyo:-

(i) Serikali haioni kwamba hawa CSIL waligoma kuendelea kuwekeza ATCL kwa sababu wamenyang'anywa *block* hizo za mafuta?

(ii) Waziri amesema kwamba Kampuni hii iliiwezesha Tanzania kukodisha ndege ya Airbus na ndege hii ndiyo ambayo taarifa tulioisoma jana inaonesha kwamba imeliingizila hasara Taifa. Hivi sasa tunadaiwa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 200 kutohana na Hesabu za CAG, Taarifa kwa PAC na bado Serikali inaita ni msaada. Waziri anatoa kauli gani kuhusu jambo hili?

**SPIKA:** Ahsante. Swali la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini halafu baadaye utajibowi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na makubaliano ya kufanya *barter exchange* baina ya hawa CSIL na TPDC kuwapa haki za kutafuta kwenye *Lake Rukwa Basin* kwa mujibu wa (*Memorandum of Understanding*) hiyo. Hata hivyo, baada ya muda TPDC waliendelea kufuutilia suala hilo kwa misingi hiyo lakini kwa sababu majibu yalikuwa hayapatikani wakaiondoa ile na kwa ushauri wa Kamati ile, maeneo ya *Lake Rukwa Basin* yakatangazwa upya. Sasa hivi leseni hiyo inayo Kampuni ya *Heritage* ya Uingereza ambayo ndiyo imegundua mafuta Uganda. Kwa hiyo, kwa sababu jiolojia ya pale *Lake Rukwa* tumewapa wao, wao wanao uzoefu wa maeneo hayo; sasa hivi wapo kwenye hatua ya *Environmental Impact Assessment* kwenda kwenye *site studies*. Kwa hiyo, wanaendelea vizuri na kwa maana hii nataka kusema kwamba, *block* hizi zipo kwa mwekezaji mwingine ambaye ni *Heritage* wa Uingereza. Kwa hiyo, kwa sasa hivi Mkataba huo wa *Memorandum of Understanding* haupo tena katika misingi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu msaada ambao China Sinangol waliutoa kwa Serikali ya Tanzania, kwanza, walinunua hizo ndege mbili, *Dash 8* na kwenye *Memorandum* yetu sisi hakukuwa na masharti yoyote.

La pili, kwa sababu utendaji kazi wa *Air Tanzania* ulikuwa unasuasua na hawa waliona kuwa wangeweza kusaidia kwa kupatikana ndege za kukodisha kabla hatujaingia katika mchakato mzima wa kupata ndege za uhakika kwa shirika hilo, walisaidia kiwango cha fedha. Nani alikuwa aingie katika mchakato wa kuangalia ni ndege gani tupate na kwa mfumo gani? Hiyo ilikuwa ni dhima yetu sisi ambayo ilikuwa imekabidhiwa *Management* na Bodi ya *Air Tanzania*. Kwa bahati sana Serikali hatukuingilia na tungeingilia tungesemwa mambo mengi sana kuwa tunaingilia jikoni. Tungeingilia tusingefika hapa tulipo. Kwa bahati mimi ni mtaalam wa mambo ya anga, ningekuwa ni Waziri wakati ule hilo ningeliingilia. Kwa sababu kama ilivyosema Kamati ya Mashirika ya Umma jana, matatizo ni mengi, nitajaribu kuyaeleza kutokana na Mkataba huo, ambayo sisi tuliyaona na sisi tunayashughulikia pale ambapo nitachangia hotuba ile.

Kwa hiyo, kwa ufupi hawa siyo kuwa wameachana kule kwa kuzila, tunavyosema Kitanga hapana; waliona kuwa hawakuwa na uaminifu wao wenyewe na *Management* iliyokuwepo ndiyo wakaona hawawezi

kuendelea kuweka pesa zao zaidi pale. Kwa hiyo, *Terminal III*, tuna wawekezaji 19. Sasa hivi tuna mfumo tumeuanzisha, kuna watu wanaleta *proposals* zao zinakuwa zimekaakaa tu, tunazichambua mpaka tunafika tunaingia *Memorandum of Understanding*. Ninasema hivyo kwa sababu hapa itasemekana kuwa nimeingia *Memorandum of Undesrstanding* na *China Merchant*, tutalieleza hilo. Hiyo mliyopewa kwenye daftari siyo na ninasikitika kuwa Kamati inaweza kwenda kutoa document ambazo sizo.

Mheshimiwa Spika, nitasambaza *Memorandum of Understanding* ambayo tulikwenda na *China Merchant*, ambayo ni mfumo ambao tunasambaza na wote wengine kuwepo fomu moja ya kuweza kushindania. Kwa *Terminal III* tunao 19, tunafanya kazi ya kuwapelekea mfumo huu wa *Memorandum of Understanding*. *Proposal* watakazoleta sasa ndiyo tutakozifanyia kazi, kuzichambua mpaka kufikia kile ambacho sisi Watanzania tunakitaka. Tunajichanganya hapa, saa nydingine tunasema tusiingilie mashirika tunaingia jikoni, saa nydingine tunasema tuyaacie mashirika, wengine hatuwezi kuyaachia mashirika tunapoona kuna matatizo, tutaingia jikoni na tutaingia chooni ikibidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza, tumekula muda wote. Mimi napenda hili suala ulilosema, liletwe katika Kauli ya Mawaziri, tafadhilli; kwa sababu, hapa sasa wala sisi hatuelewi ni kitu gani, maana swali la msingi halifanani. Ninaomba, yaani nina tatizo la muda kabisa.

Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kama ni hili nimeagiza tulete Kauli ya Serikali. Kama ni hili, naomba iingie Kauli ya Serikali kwanza kwa sababu, sisi sote wametuchanganya hapo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI**  
**BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, swali langu halihusiani ni suala tofauti lakini linachimbuka kutoka kwenye swali la msingi la Mheshimwia Zitto, lakini siyo hilo aliliojibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo linafedhehesha Taifa hili ni Mikataba ambayo aidha Mashirika au Serikali inaingia na Wabia mbalimbali, ambayo inafanya tunaonekana kama Watanzania hatuna akili timamu. Katika Majibu ya msingi ya Waziri kutoka kwa swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe, tumeambiwa kwamba, Kampuni hii ya *China Sonangol* ilishirikiana na Serikali ya Tanzania kujenga Jengo la VIP Dar es Salaam kwa gharama ya dola milioni nane.

Mheshimiwa Spika, dola milioni nane ambayo ni sawasawa na shilingi bilioni 12 ni pesa za kutisha. Nina hakika ardhi iliyotumika kujenga Jengo hili ni ardhi ya Serikali. Nina hakika pia kwa vyovyyote waliofanya ujenzi huu walikuwa wamepata *tax exemption*. Kwa hiyo, mali yote iliyointingia kwenye ujenzi huu haikulipiwa kodi. Ujenzi uliofanyika pale *VIP Airport* Dar es Salaam ambao tumeuona, wote tunatumia ile *VIP*; ni ujenzi wa kawaida sana wala hakuna *construction* yoyote ambayo ni *expensive*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni moja; Serikali ya Tanzania ya Tanzania ilichanga billioni tatu katika ujenzi huu. Mimi nataka kuamini kabisa kwamba, fedha hizi zilitosha kujenga lile Jengo, lakini tunaambiya mwekezaji aliingiza dola milioni sita ambazo ni sawasawa na bilioni tisa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu na swali; ni kwa nini Serikali isitoe kauli hapa kwamba ipo tayari kumruhusu *Controller and Auditor General* afanye *Special Audit* katika ujenzi ule wa *VIP* pale *Airport*; ukweli uweze kujulikana kuhusu hali halisi ya ujenzi ule?

**SPIKA:** Ahsante. Serikali hebu fanyeni hivyo alivyoomba, kwa sababu muda umekwisha fanyeni *Special Audit*. (*Makofii*)

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji. Tupo nje ya muda na sipendi tabia ya kuzidisha maswali na hatupendi tabia pia ya kuacha maswali yaliyoulizwa kwa wakati. Mheshimiwa Zabein Mhita.

Na. 105

### **Udanganyifu Katika Mitihani**

**MHE. ZABEIN M. MHITA** aliuliza:-

Udanganyifu katika mitihani unaongezeka mwaka hadi mwaka katika mitihani ya ngazi mbalimbali kielimu:-

- (a) Je, Serikali imebaini kuwa ni nini chanzo cha tatizo hilo?
- (b) Je, Serikali imechukua hatua gani kumaliza tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, chanzo cha tatizo la udanganyifu katika mitihani ni kushuka kwa maadili ndani ya jamii yetu, ambapo baadhi ya walimu na wazazi, hushirikiana kuwarubuni wasimamizi ili watoe mianya ya kufanya udanganyifu kadiri ya mitihani inavyokuwa, kwa lengo la kuwafanya watahiniwa wapate alama za juu.

Mheshimiwa Spika, pili, baadhi ya wasimamizi kutokuwa makini katika kusimamia ipasavyo zile Taratibu za Kanuni za Mitihani, wakati wa ufanyakaji mitihani. Ukosefu wa umakini na kutodhibiti ipasavyo usimamizi katika vyumba vya mitihani wanavyosimamia, hiyo hutoa mwanya kwa watahiniwa kufanya udanganyifu wakati wa ufanyakaji wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, chanzo kingine cha tatizo ni kwa baadhi ya watahiniwa kutojiandaa ipasavyo kwa ajili ya mitihani hiyo na hivyo kukiuka Taratibu na Kanuni za Mitihani, ambapo watahiniwa wengine huingia ndani ya chumba cha mtihani na vitu visivyoruhusiwa (*unauthorized materials*), kuandikiwa majibu ya mtihani na watu wengine na baadhi hupeana majibu ndani ya chumba cha mtihani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kukabiliana na udanganyifu katika mitihani:-

(i) Serikali imefuta matokeo ya wale wote waliothibitika kujihuisha na udanganyifu katika mitihani.

(ii) Kuwashusha vyeo Walimu Wakuu wa Shule za Msingi za Serikali waliobainika kusababisha udanganyifu katika mitihani.

(iii) Serikali imewaandikia barua ya kusudio la kuwafutia usajili wa shule wamiliki, mameneja na wakuu wa shule zote 32 wa shule zisizo za Serikali zilizobainika kufanya udanganyifu katika mitihani hiyo na hata hivyo bado uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tushirikiane kukemea maovu yanayohusika na udanganyifu katika mitihani ya nchi yetu.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyanzo vya tatizo la udanganyifu ambavyo vimemelezwa na Waziri vimekuwa ni hivyo hivyo vinavyoelezwa mara kwa mara. Je, hakuna vyanzo vingine kwa mfano, mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara bila ya kuwa na matayarisho ya kutosha, kutokuwa na vitabu vya kiada na ziada kwa wanafunzi na walimu kwa wakati, kutoendeshwa mafunzo kwa walimu kwa mada mpya kwa wakati, navyo husababisha kwa kiwango kikubwa kabisa vyanzo vya udanganyifu katika mitihani? (Makof)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kadiri ya Mheshimiwa Mbunge alivyouliza swali hili la nyongeza, limekuwa tofauti kabisa na chanzo cha tatizo lenyewe; maana sasa amekwenda kugusa mambo ya mabadiliko ya mitaala na ni jambo ambalo kidogo haliendani na hapa.

Mheshimiwa Spika, hapa tunachokisema ni kwamba, chanzo cha tatizo la udanganyifu wa mitihani ni sisi wenyewe wazazi, wanafunzi na walimu, kushuka kwa maadili kwa ajili ya kuwasingizia watoto. Masuala ya mabadiliko ya mitaala mara kwa mara, hili nilishalisema kwamba hapa inahitajika elimu maalum. Tumesema kwamba, Serikali haibadilishi Mitaala ya Wizara ya Elimu mara kwa mara, kinachobadilika pale ni muundo mzima wa *sub-topics*. Nilishatoa mfano siku moja nikasema, Nchi ya Sudan ilikuwa ni nchi miaka mitatu iliyopita, lakini leo kuna *South Sudan* na *North Sudan*; sasa ile huwezi kusema pale ni mabadiliko ya mitaala, ni mfumo mwingine tu unauingiza kwenye *syllabus*. Somo la *computer* linapokuwa linaingia, mabadiliko haya ya sayansi na teknolojia, yanafanya tuingize vitu vingine ambavyo ni masomo, lakini siyo kwamba mtaala ndiyo unabadijika. Suala la mtaala ni zito linaendana na Sera. Mabadiliko ya masomo yanaingia kadiri ya mfumo wa Dunia yenyewe unavyoendelea, tunavyoingiza masomo. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Tunapenda kuweka vizuri kwamba, haitakuwa tabia yetu kuzidisha muda wa kipndi cha maswali. Pamoja na kukopa muda, kurudisha muda wa kuwasilisha Taarifa ambao Wenyeviti walifanya ilikuwa ni dakika kumi, lakini hizi dakika nyingine tulizofanya, zipo nje ya utaratibu na sababu zenyewe majibu marefu na maswali marefu. Kwa hiyo, tutakuwa tunawagongea kengele na kuzima hapa. Tutakuwa tunazima, kuna utaratibu wa kuzima hapa. Lazima Bunge liende kwa utaratibu, bila utaratibu litakuwa soko lingine lisilokuwa la kawaida.

Tunao Wageni wetu hapa; kwanza kabisa tunao Wajumbe wa Chama cha EAAPAC. Hiki ni Chama cha Umoja wa *Public Accounts Committee* katika maeneo ya *East Africa* na vitu kama hivyo, ambao wamekuja kuhudhuria Kikao cha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na Waziri wa Fedha. Wageni hao ni Mheshimiwa Nkusi Juvenal, huyu ni Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC - Rwanda*; usimame ulipo; ahsante sana. (*Makofi*)

Yupo Mheshimiwa Komkom Deng, yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC - Sudan* ya Kusini. Hongera sana kwa kupata nchi yenu na Serikali yenu.

Tunaye Mheshimiwa Bon Kwalwale, Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC - Kenya*; tafadhalii simama, ahsante.

Tunaye Mr. George Gazemba, Katibu wa Kamati ya *PAC - Kenya*. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye Mr. Ayaga Garang, Katibu wa Kamati ya *PAC - Sudan* ya Kusini; ahsante.

Tunaye Mr. Munyantore Jean de Dieu, Katibu wa Kamati ya *PAC - Rwanda*; ahsante sana.

Vilevile yupo Ndugu Athanas Pius, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (*Makofi*)

Ahsante ni wageni wetu, karibuni sana. Tunayo Taarifa ya kuja kwenu, nadhani mtashirikiana vizuri na wenzeni wa hapa na pengine tutapata nafasi ya kuonana.

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, wakiongozwa na Ndugu Mbogo Athuman. Wako wapi hawa wageni 12, hawakusema wanatoka wapi; ahsanteni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni 29 wa Mheshimiwa Said Juma Nkumba, ambao ni wanafunzi wa kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM*. Ninaomba hawa wageni wasimame; ni wageni wetu hawa ninyi mnakaa hapa hebu simameni mliko wanafunzi wa *UDOM*. Haya, ahsante sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wengine wanane wanatoka Chuo Kikuu cha *Saint John's* wakiongozwa na Ndugu Athanas Tano. Wale wa *Saint John's* pia

nao wasimame, ahsante. Huyo Ndugu Atanas Tano ndiyo nani, sasa mimi sijui hapo; hawa wameletwa na Mheshimiwa Omar Badwel. Ahsanteni, karibuni, ninyi wanafunzi wote tunawaomba mfanye kazi ya bidii sana ya kusoma ndiyo kinachotakiwa. (*Makofi*)

Yupo Ndugu Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge Mstaafu; yuko wapi Mheshimiwa Mudhihir? Tulikuwa naye hapa kipindi kirefu; ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye Ndugu James Patrick kutoka Ireland. Halafu tuna Ndugu Mark Marrone kutoka USA. Tuna Ndugu Widmel Mushi kutoka Tanzania. Sasa hiki kikundi chote hiki ni wageni wa Mheshimiwa Anna Abdallah na anajua sababu zake, nadhani kuna shughuli ambayo wanafanya pamoja. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Stephen Masele, ambaao ni wanafunzi 70 wa Chuo cha Uuguzi Kolandoto, Shinyanga. Hawa wauguzi wetu wako wapi? Wasimame walipo kama wamepata nafasi. Ninafikiri hawajapata nafasi asubuhi hii. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 27 ambaao ni Wachezaji na Viongozi wa Timu ya Mpira ya *Coastal Union* ya Tanga. Hawa wanatoka Jimboni kwa Mheshimiwa Nundu. Wako wapi Wachezaji wa *Coastal Union*? Wao wapo hapa juu; karibuni sana na ahsanteni kwa ku-promote michezo. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa Mariam Faki, ambaao ni walimu 16 kutoka Jumuiya ya Madrasa Dodoma. Hawa nao wako wapi? Ahsanteni sana, karibuni sana. Tunashukuru kwa kuja. (*Makofi*)

Wageni wengine waliopo kwa ajili ya mafunzo na hawa waliokuja nimewataja wanafunzi na makundi, pia mtapata nafasi ya kutembezwa na Maafisa wetu wa Bunge katika maeneo yetu ya Bunge.

Tunao pia wanafunzi 40 na walimu watano kutoka Shule ya Wasichana Huruma Dodoma. Wasichana wa Huruma? Mnafahamika kwa *uniform* yenu; nashukuru sana, mlifanya vizuri sana mtihani wa mwaka jana wa *Form Four*. Endeleeni kufanya hivyo hivyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, sijui ndiyo wale wale? Kama wapo wanafunzi wa *UDOM* ambaao sikuwataja naomba wasimame pia; ahsante sana. Kama nilivyosema, wanafunzi wote jukumu

Ienu la kwanza ni kusoma kwa bidii kwa sababu maisha ni safari na mkikosea tu mnapotea njia. Karibuni sana. (*Makofii*)

Shughuli za kazi; Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Momose Cheyo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, watakuwa na Kikao leo saa saba mchana ambacho kitafanyika katika Ukumbi wa *Basement*.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Kamati zote tunapenda zikae saa saba katika Ukumbi wa Pius Msekwa B. Wote mtakaa saa saba Pius Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana watakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 231.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa, leo saa saba mchana watakuwa na Kikao cha Kamati cha Chama, Ukumbi wa Pius Msekwa. Mkigongana huko mtajua wenyewe mimi sijui.

Mheshimiwa Mariam Kisangi, naomba ukutane na Mheshimiwa Jenista Mhagama, maana huyu alisema niwatangazie Wabunge Wanawake wa CCM watakuwa na Kikao saa saba mchana Ukumbi huo huo wa Msekwa, kwa hiyo, mtakutana huko.

Waheshimiwa Wabunge, toka jana tumeendelea kujadili Taarifa mbalimbali za *Watchdog Committees*, sasa tutaendelea na mjadala huo mpaka leo jioni. Hapa katikati Mawaziri wengine watakuwa wanapata nafasi ya kuweza kueleza yale ambayo pengine yamezigusa Wizara zao. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aweze kuendelea na shughuli hii kwa sababu yeye ndiyo alikuwa ameanza na shughuli hii.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika?

**NAIBU SPIKA:** Kuna Taarifa eeh?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika?

**NAIBU SPIKA:** Miongozo, mko wangapi? Basi, simameni hivyo hivyo. Tuanze na Taarifa; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Wengine wote kaeni nimeshawaona.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni mwongozo, Kanuni ya 68(7); mwongozo mlioutoa hapa ni kwamba, kutakuwa na Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu na watu watajiorodhesha saa moja na nusu na mtajitahidi kuangalia makundi mbalimbali maeneo ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Vyama. Leo mimi nilikuwa mtu wa 11 kutoka Kambi ya Upinzani ukiacha Kiongozi wa Upinzani, nilikuwa mimi peke yangu na kutoka kundi la Zanzibar na nimefika alfajiri vilevile kama ilivyotakiwa lakini sikupata nafasi. Je, mmebadilisha utaratibu? Ninaomba mwongozo wako. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Barwany.

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa mujibu wa kifungu Namba 47(1), baada ya kipindi cha maswali kumalizika, Mbunge yeьте anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama inavyooneshwa katika shughuli zinaweza kusitishwa na kujadili dharura muhimu ya umma ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya amani na utulivu katika nchi yetu sasa hivi ni tete. Katika maeneo mengi ya nchi yetu hususan maeneo ya Kusini, wananchi wanaishi katika mashaka hasa Wakulima wa Zao la Korosho. Taarifa tulizonazo sasa hivi katika Wilaya ya Tandahimba, maduka kadhaa yamechomwa moto, ambayo wakulima wanadai malipo ya pili. Hali kadhalika, miti ya umeme imeng'olewa na katika maeneo mengine magogo yanawekwa barabarani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi wanawapiga raia, tunaomba Bunge lako sasa lijadili hoja hii mbele ya Bunge kama inavyoonekana katika maeneo mengi ndani ya nchi yetu.

19 APRIL, 2012

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Kicheko*)

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako katika kifungu cha 68(7) kinachosema, hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadiri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *Order Paper* ya leo limetolewa swali la Mbunge ambaye amekuja juzi, wakati kuna maswali ya Wabunge zaidi ya miezi mitatu sasa. (*Makofi*)

Sasa nauliza ofisi yako hajui Kanuni zinazoongoza Bunge au wanapigia debe chama fulani au wanahisani wanayopata kutoka kwenye chama hicho au wanakula rushwa? Ninaomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7) juu ya tafsiri sahihi ya Kanuni ya 39(4). Wakati kipindi cha maswali na majibu kinaendelea leo, swali namba 98 la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso aliliondoa na mionganini mwa sababu alizozitoa ni kwamba, swali hilo lilikuwa halijatimiza vigezo vya siku 21 kabla. Taratibu zinaeleweka wazi kabisa kwamba, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, alipata barua ya kuteuliwa na Tume tarehe 14 Februari, 2012...

**WABUNGE FULANI:** Kaapishwa?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Kwa hiyo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, naomba ukae.

Mheshimiwa Silinde, unachofanya ni kujadili maamuzi ya Mheshimiwa Spika; Mheshimiwa amekwishakufanya maamuzi na amelitoa hilo swali, sasa kama kuhoji kuhusiana na maamuzi ambayo ndiyo busara ya Kiti, kitu ambacho ni kinyume kidogo na utaratibu. (*Makofi*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Naomba kumalizia Mheshimiwa Naibu Spika. Naomba kumalizia hoja yangu, nilitaka niulize Mbunge anapaswa

19 APRIL, 2012

aleta maswali mara baada ya kupata barua ya Tume ama kuchaguliwa au mara baada ya kuapishwa; ndiyo hoja ambayo inatakiwa iwepo?

(*Hapa Wabunge fulani walizomea*)

**NAIBU SPIKA:** Swali ni kwamba, Mbunge anakuwa Mbunge baada ya kupewa barua ya Tume au baada ya kuapishwa; ndiyo swali unakuwa Mbunge lini, siyo swali unapokuwa Mbunge tayari ndiyo unaweza ukauliza swali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninasimama kuomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), wakati Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto akijibu Swali Namba 102, lililoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, ameeleza kitu kimoja ambacho kidogo mimi binafsi kimenishtua. Inaonekana Wizara yake na yeye mwenyewe wanatambua uwepo wa *Briefcase NGOs* na kwamba, wana kanuni zao jinsi gani ya kuweza kushughulika na *Briefcase NGOs*. Sasa tafsiri niliyoipata kichwani kwangu, inaonekana *NGOs* zipo na zina utaratibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kupitia Bunge, kwa sababu wamezungumza hapa Bungeni; kuna *Briefcase NGOs* ambazo yeye anazitambua labda inawezekana tafsiri niliyonayo mimi ikawa siyo sahihi. Kwa kuwa jambo hili limeleta *contradiction* katika *mind* yangu, nilikuwa naomba mwongozo wako Serikali inavezaje kutambua uwepo wa *Briefcase NGOs* halafu inashindwa kuchukua hatua. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Natumaini wote wamekuwa covered.

**WABUNGE FULANI:** Bado Mheshimiwa Tizeba.

**NAIBU SPIKA:** Samahani, sana endelea Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninasimama kuomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Jana wakati shughuli zinaanza hapa Bungeni, Mheshimiwa Serukamba aliomba muda wa uchangiaji upunguzwe ili Wabunge wengi zaidi waweze kupata fursa ya kuchangia. Katiba yetu chimbuko lake ni Wananchi na Serikali itasimamiwa na Bunge. Katiba yetu pia katika Ibara ya 68, sehemu ya pili, ikisomwa pamoja na Ibara ya 99, vifungu vyake vyote 135, 136 na 137, vinalitaka Bunge hili litimizie wajibu wake kwa Wananchi. (*Makofii*)

Nilipata shida sana jana kuona idadi ya Wabunge waliokuwa wameomba kuchangia ilikuwa kubwa, lakini kwa muda uliopangwa wa majadiliano ya hoja hii, huenda Wabunge 30 tu ndiyo watapata fursa ya kuchangia kati ya Wabunge takriban 300 walioko hapa ndani. (*Makofi*)

Kinachoongoza utaratibu wa Wabunge kutekeleza wajibu wao wa Kikatiba siyo saa, nadhani ni matakwa yenyewe ya Katiba hii. (*Makofi*)

Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika; kwa nini basi ili kuhakikisha kwamba Bunge linatimiza wajibu wake wa Kikatiba muda wa kujadili hoja iliyoko mbele yetu sasa hivi kwa maana kwamba Ripoti za Kamati mbalimbali za Bunge usiongezwe; na kama tatizo ni gharama za kuendesha Vikao vya Bunge, basi niwaombe Wabunge tukubaliane kuendesha siku mbili au tatu bila posho lakin tutekelze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. IDDI MOHAMED AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa hoja mbalimbali ambazo zimetolewa, sijawahi kuona hoja iliyoungwa mkono kwa kiwango kikubwa kama hii ya mwisho. (*Makofi*)

Kwa ajili ya suala hilo hilo la muda ili tuweze kuendelea, Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Dkt. Tizeba, inahitaji ushauri wa Spika kutokana na Kamati ya Uongozi. Vilevile hoja ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ya kuangalia vizuri zaidi maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na utaratibu wake kwa Wabunge, nayo tutaiangalia vizuri tuone utaratibu wetu kama kwa jinsi tulivyokwenda tunahitaji kuweka vizuri zaidi.

Hoja ya Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, tunaichukua. Hoja ya Mheshimiwa Silinde na ya Mheshimiwa Machali, tunazichukua kwa maana ya kutolea ufanuzi kwa wakati mwafaka.

Hoja pekee ambayo siiafiki ni ya Mheshimiwa Barway na sababu yake ni kwamba; ni kweli kabisa tatizo hili la malipo ya pili ya wakulima wa korosho ni tatizo kubwa sana, ni kero kwa wananchi wote wanaohusika kule. Ninafahamu pia kwamba, hata Chama cha CUF walishafanya maandamano kule Tandahimba na baadhi ya sehemu za Kusini na kuna sokomoko linaloendelea hivi sasa, lakini Serikali inazo taarifa za kutosha kabisa za jambo hili. Nina hakika kabisa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mara kadhaa amejibu kuhusiana na jambo hili Serikali inalishughulikia.

Mimi naomba sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa bado tupo hapa Dodoma, tuendelee kuwa sambamba na Serikali yetu katika kuona namna gani jambo hili linafikia tamati. Hilo nisikubaliane naye kwa maana ya kuhitimisha shughuli nyingine zote tukaanza kujadili hilo peke yake. Tuwe na subira, mengine haya tuuachie Uongozi uendelee kuyatazama na tutayatolea ufanuzi kadiri muda unavyokwenda.

Sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee na utaratibu wetu; Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA KAMATI

### Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC)

### Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

### Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC)

(Majadiliano yanaendelea)

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea na kama tulivyokuwa na utaratibu wa jana, tutaendelea vilevile. Dakika ni kumi; ni dakika chache, ninaomba tujielekeze moja kwa moja nitafuata orodha ilivyo bila kuibadilisha chochote.

Kwa hiyo, msiniletee viji-note, ninaangalia kwenye orodha. Mheshimiwa Amina Mwidau, ilikuwa tuanze na Kiongozi wa Upinzani ametoka kidogo ataendelea wakati mwafaka. Mheshimiwa Amina Mwidau, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia siku hii ya leo. Kwanza kabisa, nazipongeza Kamati zote tatu kwa Taarifa ambazo ni nzuri kabisa, zinazogusa nchi yetu moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni-declare *interest*; mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC). Naomba niende moja kwa moja katika yale ambayo nimepanga kuyachangia kwa sababu muda wenyewe ni mdachu sana. Nitaanza moja kwa moja na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mashirika ambayo tumeyapitia, Shirika ambalo lilitifanya nikaumwa kichwa na kusikia kizunguzungu na nikalala na homa ni Shirika la ATCL. (*Makofii*)

Nilimwuliza Mbunge ambaye alikaa karibu yangu, Mheshimiwa Esther Matiko, wakati Mkaguzi anatupitisha kwenye mahesabu kuwa umeyaolewa yanayoelezwa humu, akaniambia yeye pia anasikia kizunguzungu ...

**MBUNGE FULANI:** Si mngeanguka?

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Menejimenti ya ATCL imenisikitisha sana kwa sababu iliingia Mkataba na Shirika la *Wallis Trading* la Lebanon Oktoba, 2007. Mkataba wa kukodisha Ndege ya *Airbus*, A320214, ulikuwa na kiburi cha hali ya juu nilijiuliza mara mbilimbili, hivi hawa wana mashiko kutoka wapi? Kilichonifanya nikaamini kuwa wana kiburi ni pale ambapo waliweza kuingia mkataba bila ya ridhaa. Waliingia mkataba kwa miezi takriban saba bila ya dhamana ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hilo, lakini pia ilinisikitisha sana kwa sababu kulikuwa na timu ya wataalam ambayo ilitoa taarifa kuwa, siyo jambo la busara kukodi ndege ile kwa sababu baada ya miezi takriban sita itakwenda tena matengenezo makubwa, kwa kitaalam ni *12 years checks* ambayo najua Mheshimiwa Nundu pale anafahamu. Ni matengenezo makubwa ambayo ndege hiyo inatakiwa ibadilishwe vitu vingi, lakini wao walidharau ushauri wa wataalam wale ambao wapo kwa ajili ya kushauri shirika na wanalipwa, wakaweza kusaini mkataba ule ambao ni wa miaka sita ni takriban miezi 72.

Pia kilichonisikitisha zaidi ni pale walipokubaliana katika mkataba ule, *rate* ya kukodisha ndege ile itakuwa ni dola 370,000 kwa mwezi, kama imeruka au haijaruka na ndege ile ilikaa miezi takriban 48 katika mikono ya ATCL. Katika miezi hiyo 48 ni miezi saba tu ambapo ndege ile iliweza kuruka lakini miezi 41 ilikuwa chini. Kwa ujumla mpaka kufikia tarehe 30 Januari, 2010 Shirika la *Wallis Trading* liliteta hesabu yake kwa ATCL inaonesha kuwa deni lile ilikuwa limesimama kwenye takriban pesa za Kitanzania bilioni 322,671,841,580, ambayo ni sawasawa na dola milioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hiyo ina uwezo wa kununua ndege mbili ambazo ni aina hiyo hiyo ya *Airbus 320*. Ukiangalia kwenye website ya *Airbus* utakuta bei ya ndege moja mpya a *brand new aircraft* ya aina hiyo imesimama kwenye dola milioni 88.3. Kwa hiyo, tungeweza kupata

ndege mbili mpya na chenji ikabakia, lakini *Management* hii imeonesha dharau kwa sababu timu ya wataalamu *ime-prove* ni kweli ndege ile imeruka miezi saba na ikaenda matengenezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imenisikitisha sana sana kwa sababu watendaji wale walionesha dharau na inaonesha kuwa hawapo peke yao, lazima wana mashiko sehemu wanayoyategemea na ndiyo maana wakafanya kiburi kile cha hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, Kamati katika hili imetoa mapendekezo lakini mapendekezo yale naona ni mepesi. Ninaomba Bunge lako hili liazimie kuwe na Kamati Teule ambayo itachunguza wingu la makubaliano yale ya kuingia mkataba na Ndege ya *Airbus* kwa sababu imefunikwa sana na mambo mengi, kuna mengi ya kujiuliza pale, tunaomba pachunguzwe na wale wote ambao watakuwa wamehusika wachukuliwe hatua. Ndugu zangu, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hakuna haja tena ya kulifufua Shirika hili.

### **MBUNGE FULANI:** Acha *life, life* kabisa!

**MHE. AMINA MWIDAU:** Hapo lilipofikia sasa hivi linatosha, tunaomba Serikali itumie hekima na busara waweze kuunda Shirika lingine jipya waachane na jinamizi hili la ATCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigosie kwenye ubinafsishaji. Kamati ilifanya ukaguzi katika Viwanda vya Korosho Lindi na Mtwara lakini vilevile katika Mashamba ya Mkonge Tanga. Mimi nitaongelea Tanga kwa sababu linanigusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mashamba ya Mkonge kuna migogoro katika mashamba matatu ambayo nitayaongelea kama muda utatosha. Migogoro hii ya ardhi imetokana na wawekezaji waliochukua maeneo yale wakasema wao ni wawekezaji, lakini mashamba yale ni mapori, wawekezaji walichukua kwa ajili ya kupata mikopo benki tu na siyo uwekezaji. (*Makofi*)

Nikianza na Shamba la *Mkembe Estate*, lenye hekta takriban 820, kwa kweli wanakijiji wale wanapata shida sana kwa sababu mwekezaji yule alilitelekeza Shamba lile akachukua mkopo akaondoka tangu mwaka 1990. Cha kushangaza, kuna watu wengine wanaojiita wawekezaji, wamejitokeza wanadai kuwa wamenunua Shamba lile kutoka Benki wakati wananchi wale wapo pale miaka nenda rudi,

wamechukua maeneo yao wanaishi wamejenga, wana mazao ya kudumu na mazao ya chakula. Leo mwekezaji huyo ambaye kwa Shamba la Mkembe anaitwa Sykes, amekwenda kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na Mwenyekiti wa Baraza lile akatoa maamuzi kuwa watu wale waondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana, wananchi wale watakwenda wapi? Wamekuja pale kwenye mashamba ya *settlers* miaka kibao tangu wakiwa wavulana, wameoa, wamezaa lakini leo wanaambiwa waondoke. Migogoro hii ya ardhi, Serikali itawafikisha pabaya, Wananchi wamechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mheshimiwa Amina Mwidau. Mheshimiwa Jerome Bwanausi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi. Pia niungane na wenzangu kuwapongeza Wenyevitit wa Kamati, kwa jinsi walivyowasilisha hoja kwa umahiri na kwa Taarifa ambazo zimeandaliwa kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze tu kuchangia kwenye eneo lilirozungumziwa na moja ya Kamati ambayo ni ya Hesabu za Mashirika ya Umma hasa kwenye sehemu ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imezungumzia sana suala la Viwanda vya Korosho. Kwa hakika, ukiangalia jinsi viwanda vile vilivyogawiwa kwa waliojiita wawekezaji katika Sekta ya Viwanda, inasikitisha sana. Kwenye Ripoti iliyotolewa na Kamati imeainisha kwamba, karibu viwanda vyote hakuna hata kiwanda kimoja kilichozidi milioni 100, ni milioni 30, milioni 40, milioni 45 hadi milioni 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo viwanda vinane; kipo cha Tunduru, Masasi, Newala visto viwili; *Newala One and Newala Two*, Mtware - Kiwanda cha Makonde, Masasi, Lindi na Nachingwea na Mtama. Kiwanda cha Mtama pekee ndiyo kimeonesha dalili walau za kuweza kubangua. Ninaomba kusisitiza kwamba, Serikali ifanye kila linalowezekana viwanda hivi virejeshwe kwa sababu wawekezaji wameshakiuka mikataba ili uwezekano uwepo ndani ya miaka miwili tubangue Korosho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tumkomboe mkulima ni lazima tuongeze thamani ya Zao la Korosho na uongezaji thamani wa zao hilo ni kwa kubangua. Kwa sasa inasikitisha kuona korosho ghafi tunazipeleka hasa India ambapo kule Wananchi wa India wanapata ajira, maganda yake yanakamuliwa yanapatikana mafuta, lakini pia maganda ya korosho yana kazi maalum ambayo inafanyika kule. Tungeweza kubangua hapa tungezalisha ajira, mafuta yangepatikana na maganda. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali tuwe makini kwenye hili ili ndani ya miaka miwili tuweze kubangua korosho. Uwezo wa viwanda hivi vinane vikiweza kuzalisha tani 10,000 kila mwaka tunaweza kubangua korosho tani 80,000 hadi 100,000 na uzalishaji kwa nchi kwa sasa ni tani 160,000. Kwa hiyo, kama viwanda hivi vingefanya kazi tungeweza kubangua Korosho zote. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilitaka kuongelea kuhusu masikitiko yangu kwa Serikali. Tangu Rais Jakaya Mrisho Kikwete, atangaze kwa wananchi juu ya azma ya Serikali kununua korosho na kuwalipa wakulima, ni zaidi ya miezi miwili. Hapa katikati nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivyosema kwamba, upo mchakato wa kibenki na mambo ya kipesa lakini niseme tu kwamba, pamoja na hayo lakini kumekuwa na ucheleweshaji wa makusudi katika zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baya kabisa ambalo limewafanya wananchi wa mikoa inayolima Korosho wakasirike sana ni juu ya tamko la mtendaji mmoja wa Wizara ya Kilimo alipoita waandishi wa habari na kuwatangazia wananchi kwamba tarehe 31 Machi waende wakachukue fedha zao katika mabenki. Nilitegemea Serikali baada ya yule mtendaji kutamka lile na kutowezekana, angetakiwa awaombe radhi wananchi kwamba alichotamka siyo sahihi lakini amekaa kimya *as if* hakuna kitu kilichofanyika.

Ninaomba Serikali wakati inapotoa matamko yake iwe makini kwa wananchi wetu kwa sababu inawaleta chuki kwa Serikali yao hasa pale ambapo matamko yanatolewa lakini utekelezaji haufanyiki. Pia ningewomba Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni, ndani ya siku mbili hizi apate taarifa sahihi na atoe tamko juu ya lini wananchi wale watapata fedha zao. Pamoja na ule mchakato aliousema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, tayari mabenki yameshatoa taarifa kuhusu Vyama vya Ushirika waende lakini ni lazima kuwe na ratiba ambayo itafuatwa ili wananchi wapate uhakika wa suala lao. (Makof)

Nikija upande wa Serikali za Mitaa, Taarifa ambayo imeletwa na Mheshimiwa Daktari Augustine Mrema; kwanza, naipongeza Taarifa ile kwani imeeleza kwa undani sana juu ya matatizo yalioyopo kwenye

Halmashauri zetu na mimi nina-*declare* kwamba, nimewahi kuwa Kiongozi kwenye ngazi ya Mtaa; Diwani na Meya, kwa hiyo, nimekuwa humo kwa muda mrefu sana.

Mimi ningekuwa na mapendekezo yafuatayo: Kwanza, kwa zile Halmashauri ambazo Watendaji wake Wakuu wamekuwa na tuhuma nzito sana za ubadhirifu wa fedha, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wanaohusika washughulikiwe kwa kusimamishwa kwa tuhuma hizo zilizotolewa na CAG halafu mambo mengine yataendelea baadaye baada ya uchunguzi kufanyika.

La pili, mfumo uliopo sasa wa Waheshimiwa Madiwani kuwa wasimamizi wa shughuli za Serikali za Mitaa siyo nzuri kwa sababu ni lazima tutenganishe Waheshimiwa Madiwani na Mkurugenzi. Kwa sasa Mkurugenzi ndiye anayewahudumia kila kitu Madiwani. Lazima tuwahamishe Waheshimiwa Madiwani wawe kwenye eneo lingine, aidha Wilayani kwa Afisa Tawala wa Wilaya na staili zao zielekezwe kule ili wahudumiwe na wao, lakini kitendo cha kuendelea kuhudumiwa na Mkurugenzi na Wakuu wa Idara hatutegemei kwamba tunaweza tukapata ufanisi mzuri katika shughuli hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni lile ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelieleza kwamba hatuwezi kupata ufanisi kama hatuwezi kuwajali viongozi wa ngazi za chini; Wenyeviti wa Mitaa, Vitongozi na Vijiji, wana mazingira magumu sana. Waswahili wanasema aisifiae mvua imenyea, maana na mimi nimekuwepo kwa takriban miaka mitano, najua kwamba kama hatukupeleka msisitizo kule hatuwezi kufanikiwa lolote. Pia Waheshimiwa Madiwani ni lazima waongezewe posho zao ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na Wenyeviti na Mameya waliopo kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu mafunzo; namshukuru sana Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mkuchika, ameshazindua rasmi suala la mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani. Tumechelewa, jambo hili lilipaswa lifanywe mapema kwa sababu Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji kama hawawezi kupata mafunzo haiwezekani kabisa wakafanya kazi yao kwa ufanisi unaostahili.

Lingine, ningeshauri Wakurugenzi na Wakuu wa Idara waajiriwe kwa mikataba kama ni miaka mitano au kumi ili wasipoweza kuonesha ufanisi wao basi huyo Mkurugenzi atakuwa hawezikufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni vikao vinavyoendeshwa kwenye Halmashauri kuhusiana na Vikao vya Bunge. Tulishawahi kutoa

ushauri kwamba ni lazima kuwe na ratiba iliyoandaliwa kwa pamoja kati ya ratiba za Vikao vya Bunge na Vikao vya Halmashauri. Waheshimiwa Wabunge, hawapati nafasi ya kushiriki kwenye Halmashauri zao, hawajui kinachofanyika, kwa hiyo, lazima kuwe na ratiba inayooana, wakati wa Bunge vikao visiwe vinafanyika hasa Kamati ya Fedha na Baraza. Sasa jambo hili tumelizungumza na ningeomba Serikali mkae pamoja ili Waheshimiwa Wabunge wahudhurie vikao hasa vya bajeti, wengi hawawezi kuhudhuria vikao vya bajeti kwani vinafanyika wakati wa Vikao vya Bunge. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerome Bwanausi. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Maselle.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza na mimi niwapongeze Kamati zote tatu na niungane mkono na maamuzi yao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningeomba nianze na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali juu ya suala zima la Bajeti. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anasema bajeti yetu siyo *realistic* na akatoa uthibitisho *PPRA* wamepata asilimia 34 tu ya bajeti yao. Ukitazama mapato ya Serikali ni asilimia 98.4, ndiyo makusanyo ya Serikali. Mpaka jana tulikuwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tumeambisha makusanyo ni asilimia 98.4. Sasa unajiuliza kama makusanyo ni asilimia 98.4; hizi fedha za matumizi ya Serikali zimekwenda wapi kama Wizara, Idara na Halmashauri hazipewi fedha?

Kwa hiyo, narudia kauli ambayo nimeitoa sana hapa Bungeni kwamba, mfumo wetu wa bajeti bado ni dhaifu, unahitaji kuangaliwa upya. Nami ningemwomba *Auditor General* na CAG atusaidie namna gani ya kutengeneza bajeti nzuri itakayohakikisha mfumo wa bajeti utakaohakikisha kwamba fedha zinakwenda katika Halmashauri na Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu hata Bunge lako Tukufu tumekatwa mara hii shilingi bilioni tano, sasa mnakwenda kila siku mnaomba pamoja na kwamba tuna Mfuko, lakini mnakwenda kila siku kupiga magoti Hazina. Sasa ukiangalia katika mfumo wa mihimili na wewe kila siku unakwenda kupiga magoti; hivi huu mhimili unaonekana kweli kama unasimama sawasawa? Kwa hiyo, la kwanza ambalo

ningewaomba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, mara hii tujitahidi katika bajeti hii ili Mfuko wa Bunge upewe percent yake na siyo kwenda Wizarani kila siku kupiga magoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hilo kwa sababu Kamati hizi zingeweza kufanya kazi zaidi kama zingekuwa na fedha za kutosha za kufanya kazi. Wananchi wanayaona haya ni mambo madogo sana kama kweli Bunge hili lingepata fursa ya Kamati zake kufanya kazi za *oversight* kwa nafasi zaidi. Mimi nina *experience* kidogo katika Kamati hizi za *PAC*, kama hamuwezi kufanya kazi kwa muda mrefu basi ni matatizo. PPRA leo wana Taasisi 172, wameweza kufanya ukaguzi asilimia 28 tu, bajeti waliyoomba ni shilingi bilioni 14 wamepewa shilingi bilioni nne, hawawezi kufanya kazi. Hivyo hivyo na Bunge haliwezi kufanya kazi kama halipati fedha za kutosha na kama linakwenda Hazina kila siku kupiga magoti kuomba fedha. Hii habari iishe katika bajeti hii ili tuzungumze vizuri na Serikali. Kwanza, Bunge lipate fedha yake ya kutosha ya kufanya kazi ili wananchi waone rasilimali zao tunavyozisimamia kwa mujibu wa Katiba. Naomba Waheshimiwa Wabunge, hilo tuungane pamoja ili *Commision* yenu iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la uwajibikaji wa Serikali. Inaelekea uwajibikaji ndani ya Serikali bado umekuwa kitendawili kikubwa. Ukitisoma Taarifa zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, miaka na miaka hoja zinarudiwa palepale. Sasa yale maagizo ya Rais kukaa na Watendaji Wakuu wa Serikali akawaagiza kwamba wajibu hoja za Serikali na hoja hazijibowi na hatimaye hakuna hatua zinazochukuliwa maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi natoa ushauri kwa Wabunge wenzangu kwamba, Ibara ya 62 ya Katiba inatupa mamlaka makubwa sana. Niliwasikia Wabunge wenzangu wakisema kwamba, tuache kulalamika na mimi nasema Bunge hili lifanye kazi asilimia 70 ya kuidhibiti Serikali na kuisimamia na asilimia 30 tuendelee kutoa ushauri, maana ushauri tumeshautoa kwa muda mrefu sasa kazi iliyobaki ni kusimamia maamuzi yetu. Katiba inaturuhusu, tufanyie kazi Ibara ya 62, tuhakikishe kwamba kama wenzetu hawataki kuwajibika basi hapa tuna uwezo wa kuwawayibisha tuwawayibishe. (*Makof!*)

Dharau na kejeli za watendaji zimekuwa kubwa, hawajali maisha ya Watanzania na sisi kama Wabunge tuliochaguliwa na Umma huu wa Watanzania, kwa niaba yao tunao wajibu wa Kikatiba kabisa wa kuisaidia Serikali pale inaposhindwa kutimiza wajibu wake. Kwa hiyo, ombi langu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni kwamba, asilimia 70 ya muda wetu tumeshasema miaka mingi, taarifa zimeshatoka nyingi, hali

bado inakuwa mbaya zaidi kila siku, sasa tutumie wajibu wetu wa Kikatiba wa kuweza kudhibiti yale madhambi ambayo yanafanyika na hayapati ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, Bunge hili linapitisha bajeti na ukisoma taarifa zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kuna mambo mawili yanayotokeza; ama kuna fedha imekusanywa hailetwi; kwa mfano, katika Ubalozi huko nje, kuna Shilingi bilioni 3.1 over collections haijarudishwa hapa nchini, na kuna mahali pengine wametumia zaidi. Sasa maana ya bajeti ni nini kama revenues zinakusanywa haziletwi kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina au wanatumia watu viwango vya ziada vya bajeti zao? Kwanza, wanavitoa wapi? Lakini kuna *reallocation* inayofanywa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa mfano hapa, Bunge lako hili, Shilingi bilioni tano zilizochukuliwa, tumekaa jana kwenye Kamati yako hapa tunazungumzia namna gani ya kuendesha Shughuli za Bunge, hakuna fedha! Sasa katika Taasisi kubwa kama hii inayowakilisha Watanzania wote, haina fedha za kufanya kazi: Je, Idara ya Maji, hadhi yake itakuwaje? Kwa hiyo, nasema hilo ni tatizo moja la msingi, ni lazima tulifanyiwe kazi na mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusioneane haya, tuwaambie. Kama makusanyo ni asilimia 98.4, fedha hii ya revenue imekwenda wapi ambapo Bunge hili halikuidhinisha? Kwa hiyo, nasema *role* kubwa bado irudi kwetu Wabunge. Turudi Wabunge kwa kupitia Kamati zetu hizi na taarifa zilizopo ili tuhakikishe mapato ya Serikali na matumizi yake yanakwenda kwa mujibu wa Sheria ya Fedha tulioipitisha ndani ya Bunge hili. Vinginevyo, tutaendelea na hadithi hizi kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, tumeshuhudia manunuzi mabovu sana. Ukitumba Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kila mahali penye manunuzi pana matatizo makubwa, na asilimia kubwa ya bajeti yetu hasa ya maendeleo ni manunuzi. Mikataba bado ni ya matatizo. Tumeona Mikataba wa ATCL hapa, Naibu Waziri alikuwa anajibu maswali akasema tumeingia *MoU*, halafu huku anasema ni msaada. Sasa kama ni msaada, kwa kweli tusingekuwa na matatizo yoyote, lakini wakati mwingine tunasema aah, huyu ni *PPPP*, sasa *which is which?* Hapa hapa ndani ya Bunge hili! Chukua Hansard ya leo tu, kuna kauli mbili tofauti katika jambo hili hili moja. Moja, wanazungumzia msaada jambo hilo hilo, na jambo hilo hilo linazungumzia *PPPP*. Lakini ukisoma yale majibu yenyewe yanasesma bado Mikataba hasa haujaingiwa. Hivi mlifanya kazi kwa *Memorandum of Understanding (MOU)? (Makofi)*

Kwa hiyo, nasema bado kuna *problem*, na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amesema tatizo la mikataba bado lipo. TBC hapa kuna matatizo ya mikataba vilevile, ukisoma taarifa hapa. Hebu Mwanasheria Mkuu wa Serikali naye atusaidie tumalize hili tatizo la Mikataba ya hovyo hovyo. Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani alisema atapitia mikataba hii ya madini na kadhalika, nayo bado ilishia njiani. Sasa hii mikataba mipyä inayokuja, Mwanasheria Mkuu wa Serikali tengeneza Kitengo kitakachosaidia kupatikana kwa mikataba ambayo ndani yake Watanzania watafaidika “*a win win situation.*” Hali tuliyonayo ni mbaya, wizi wa fedha ni mkubwa na ninarudia kusema kauli nilioisema hapa, kwamba bajeti ya Shilingi trillioni 13.5 asilimia 35 na Mheshimiwa Rais mwenyewe amesema, haiendi kwenye matumizi ya Serikali. Asilimia 30 ya Shilingi trillioni 13.5 ni fedha nyingi sana. Tunawaongezea umasikini Watanzania kwa sababu ya kutokuchukuliana hatua tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana.

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia ripoti ya Kamati hizi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwanza kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote hizi kwa kuwasilisha ripoti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kuzungumzia hoja za Mkaguzi pamoja na ripoti ya Kamati. Inasikitisha sana kuona kwamba ripoti za Mkaguzi kwa miaka karibu mitano mfululizo zinazungumzia habari ileile ya ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri. Kwa mfano, halmashauri za Kishapu, Misungwi, Rombo, na nyingine, haihitaji tochi kwenda kuchukua hatua kule. Pesa za Watanzania zinatafunwa kule!

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana kabisa na Wabunge wenzangu wote waliota mapendeleko yao kwamba, hatua zichukuliwe mara moja kwa wale wote wanaohusika na ubadhirifu wa fedha za umma katika Halmashauri hizo zilizotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya PAC ilitembelea miradi mbalimba ya Maji. Kwa bahati tulitembelea Mradi wa Ziwa Victoria ambao unaleta maji Shinyanga na Kahama. Mradi ule ni mkubwa sana na asili yake ni mradi wa kitaifa, umetumia zaidi ya Shilingi billioni 250 kutengeneza mradi ule. Lakini leo mradi ule wote wameachiwa wakazi wa Shinyanga Mjini wasiozidi 12,000 ambao wameunganishwa kwenye

mradi ule, na Mji wa Kahama ambao pia una wakazi wasiozidi 13,000 kuendesha mradi mzima wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikubalikil Nimejaribu kuleta malalamiko, maelezo, vielelezo Wizara ya Maji, lakini majibu hakuna. Utakachoelezwa ni kwamba *EWURA* imepanga. *EWURA* iko kwa ajili ya nani? *EWURA* iko kwa ajili ya kuhudumia Watanzania na lengo ni kupunguza għarama za maisha kwa Watanzania. Sasa mzazi ambaye unampenda mtoto wako unakwenda kumnunulia gari kwa mfano V8 lakini usimpe fedha ya kulihudumia, atalipaki tu. Wakazi wa Shinyanga hawana uwezo wa kulipa *bill* ya Sh. 300,000/= kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, *bill*s zinakuja Sh. 300,000/= sasa hivi kwa matumizi ya nyumbani, hawawez! Mimi naomba kauli ya Serikali. Ningombha Mheshimiwa Waziri Mkuu angenisikiliza kweli katika hili kwa sababu naona Waziri wa Maji hayupo na Mawaziri wengine hawapo, tupate majibu. Mwaka mzima nimefuatilia hili, kama haliwezekani mniambie leo na mimi nirudi kule niwaambie wananchi kwamba, lile limeshindikana, basi mtu-*disconnect* mtoe huo mradi wa Mwanza na turudi kule kule kwa maji ya Ning'wa tuliyyoyazoea ambayo tulikuwa tunalipa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamezungumzia suala la Bodi za Pamba za Korosho. Ni ukweli usiopingika kwamba Bodi ya Pamba imeshindwa kuwasaidia Wakulima, *ginners*, na haiko kwa ajili ya kuendeleza zao la Pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iko mifano hai, Bodi ya Pamba inatoa orodha ya Makampuni ambayo hayatakiwi kuingia sokoni. Nilitegħemea ingetoa orodha ya Makampuni ambayo inataka kuyasaidia yaingie sokoni. Lakini leo Bodi inasema kwamba, kama *ginners* hawatalipa Shilingi milioni 50 kwa kituo cha kununulia pamba, kwa mfano, kama *ginner* mmoja ana vituo vitano anatakiwa kulipa Shilingi milioni 250 ili apate leseni ya kununua Pamba. Hiyo haiwezekani! Naomba Waziri wa Kilimo atakapojibu hoja atuweke wazi kabisa kipengele hicho ama maelekezo hayo ya Bodi kwamba ma-*ginners* walipe Shilingi milioni 50 kama ni kigezo cha kupata leseni ya kununua Pamba. Hicho kipengele kifutwe. Kwa kweli naungana na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotaka Bodi ile ibadilishwe, Mnejementi iondolewe, iwekwe nytingine na ikiwezekana, basi na yenyewe ifumuliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya tumeyaleta muda mrefu, lakini hatua hazichukuliwi. Inafika mahali sasa tunashindwa kuelewa kwamba, tunachezewa kwenye Pamba. Sisi kwa kweli hatuwezi

kukubali kuchezewa kwenye Pamba. Kwenye madini tulishasema Kanda ya Ziwa; Shinyanga, Mwanza, tuna madini mengi lakini tumeiachia Serikali kuu kama pato la Taifa. Lakini kwenye Pamba, sisi tuna uhusiano wa moja kwa moja na Pamba. Ukichezea pamba umechezea maisha yetu. Tunaomba majibu ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *TBS* kweli limekuja. Kama Kamati ya *PAC* zimeagiza mara tatu hoja hazijajibwa na Kamati imetoa kabisa mapendekezo, wote wanaohusika na hasara ya zaidi ya Shilingi bilioni 18 wachukuliwe hatua. Ukisoma ripoti maalum ya *CAG* inasikitisha. Najua Wabunge wengine hawajapata fursa ya kuiona ripoti ile. Mkiisoma ndugu zangu hakuna tofauti na mtu anayekwenda kwenye mto ama kisima usiku na kutia sumu ili wanaokuja kuteka maji kesho yake wafe. (*Makofi*)

Sote tunatumia bidhaa nyingi kutoka nje, lakini orodha inayoonyesha bidhaa ambazo ni feki zilizoingizwa nchini ni kubwa mno na sehemu kubwa ya bidhaa zile ni zile ambazo ni za matumizi ya majumbani. Sehemu kubwa ni chakula na hasa chakula kwa watoto wachanga (maziwa).

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana unaona sasa hivi vijana wadogo, unakuta kavulana kana miaka tisa, kanaota ndevu. Yote hii inatokana na kutozingatia viwango vya vyakula ambavyo vinaingizwa nchini. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Na akina mama.

**MHE. STEPHEN J. MASILLE:** Akina mama sijasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBS* kwa kweli kama na penyewe panahitaji tochi nyingine ya kwenda kumulika pale, basi tutakuwa tumeshindwa kazi. Nashindwa kuelewa ni kwanini hatua hazichukuliwi? Kamati zimeagiza kila mara, hatua hazichukuliwi na watu wako kazini wanadunda mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba majibu yenyе kueleweka, ripoti ya *CAG* imetoka na kila mtu anayo na imeeleza bayana kabisa wala haihitaji kuunda Tume, lakini ikibidi tutaomba Kiti chako kiunde Tume Maalum ya Spika ikachunguze pamoja na zile Halmashauri nyingine zote zilizotuhumiwa na ubadhirifu wa fedha ili maamuzi yaletwe hapa Bungeni na Wabunge waweze kuchukua hatua kama ambavyo wengine wamependekeza kwa mujibu wa mamlaka tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunawalaumu Wakurugenzi ama baadhi ya Mawaziri, lakini siyo wote. Wako Mawaziri wanaofanya kazi vizuri sana, wako Wakurugenzi wanafanya kazi vizuri sana. Kwa mfano, kwenye suala hili la korosho, mahindi, Wizara ya Kilimo iliomba Shilingi bilioni 135, imepewa Shilingi bilioni 35 tu ambayo ni sawa na asilimia 24 ya fedha ilizoomba. Wengine wameeleza hapa jana kwamba Wizara ya Ujenzi iliomba zaidi ya Shilingi trillioni moja na pointi, lakini imepewa Shilingi bilioni 400. Ukiangalia tatizo kubwa liko Wizara ya Fedha, kwa sababu Wizara nyingine zinategemea Wizara ya Fedha itoe fedha. Sasa kwenye Kilimo fedha hazijakwenda, kwenye korosho fedha hazijakwenda. Mtu mmoja ananiambia fedha ndiyo zimeingia jana tu. Sasa miezi miwili tangu Waziri amepeleka timu kule, Waziri Mkuu ametoa tamko benki zitoe fedha, *guarantee* Serikali haijatoa, fedha ndiyo zimepatikana jana. Kwenye mahindi mpaka Wizara inabidi iuze mahindi tani zaidi ya 90,000 ili iweze kulipa madeni ya mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Keissy jana akasema kwamba, Wizara inaingiza mbolea feki, lakini ukirudi tena ambaye anatakiwa kuangalia viwango vya ubora wa mbolea inayoingizwa ni *TBS*. *TBS* ndiyo ina jukumu la kuangalia viwango vya bidhaa zote zinazoingizwa nchini. Kwa hiyo, naomba sana Wabunge wenzangu wale ambao wanafanya vizuri tuwapongeze, wale wanaaboronga tuwaadhibu. (*Makofi*)

Pale Kenya wenzetu wana *performance audit*, hata sisi tunayo. Wale wanaofanya vizuri kama ni Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, wanapewe zawadi (*reward*). Labda na sisi tuweke utaratibu huo wa Wakurugenzi wa Halmashauri wanaofanya vizuri wapewe *reward*. Mawaziri wanaofanya vizuri tuje hapa hata tuwapigie makofi. Lakini wale wanaaboronga kweli tuchukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia machache. Kwanza, nianze kwa kuunga mkono mapendekezo ya Kamati zote tatu yaliyotolewa na hivyo inabidi sasa Serikali ifanye kazi ya kuyafanyia kazi mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye kipengele kimoja, kinachohusu ubadirifupi na matumizi mabaya ya fedha za Umma, halafu kama nitapata nafasi nitaendelea na vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji walitangulia wameeleza masikitiko yao makubwa jinsi ambavyo fedha za Umma zinaliwa na ambavyo hazifanyi kazi yake sawasawa. Mimi katika kipengele hiki nitazungumzia mishahara hewa ambayo inatolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na mifano ambayo imetolewa na ripoti ya CAG ya mwaka 2010/2011, Vyuo kadhaa vimeonyeshwa kwamba vinapelekewa fedha kulipa Watumishi ambaa aidha wamehama, au wamekufa au wameacha kazi. Nitolee mfano Vyuo vichache; Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa. Ripoti inasema kwamba, jumla ya wafanyakazi 42 wamekuwa wakilipwa mishahara bila stahiki, bila kuwepo kutoka Oktoba, 2009 mpaka Juni, 2010. Kiasi ambacho kimelipwa mpaka muda huo ni Shilingi milioni 612. Huyu *Bursar* wa MUCE anapeleka wapi hiyo mishahara hewa? Ni kwanini hizo fedha zinapelekwa na hazirudishwi? Hicho ni Chuo kimoja (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni Chuo Kikuu cha Mzumbe. Ripoti inasema kwamba Hazina imekuwa ikipeleka fedha kwa miezi kadhaa na zimefika jumla ya Shilingi milioni 194.4 mishahara hewa. Wafanyakazi hawapo.

Kama vile haitoshi *DUCE*, Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam kimepelekewa jumla ya Shilingi milioni 778.7 mishahara hewa. Vilevile, *Mwalimu Nyerere Memorial Academy* nayo imelipwa jumla ya Shilingi milioni 134.7. Taasisi ya Ustawi wa Jamii Shilingi milioni 181. Jumla ya mishahara hewa yote ambayo imelipwa kwa kipindi hicho wakati ripoti inatoka ni Shilingi bilioni 1.9. Tunaomba Serikali itoe maelezo fedha hizi za Umma zinalipwa nani? Nani wanazipokea? Mishahara hii inakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwininge unanihusu mimi mwenyewe. Katika kuitia *Annual Reports* za Vyuo mbalimbali nilikuta katika *Annual Report* ya Chuo Kikuu Huria (*OUT*) ya mwaka 2009/2010 ikionyesha kwamba, mimi ni mtumishi pale. Jina langu Christowaja Mtinda, ni jina la peke yangu, hakuna mtu mwininge. Christowaja Mtinda ni yupi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sijawahi kuomba kazi *Open University*, sijawahi kufanya kazi pale. Yule *Bursar* anapeleka wapi huo mshahara? Naomba maelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu mwininge unatoka Hazina ambapo ripoti inasema wazi kwamba, Hazina inaonyesha kwamba

imekuwa ikipeleka mishahara hiyo hiyo katika vyuo lakini vitabu vya Vyuo vikioneshaa tofauti kabisa na fedha ambazo zimetolewa. Kwa mfano, Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hazina inaonyesha kwamba ilipeleka jumla ya Shilingi milioni 443.2 lakini Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi kinaonyesha kimepokea jumla ya Shilingi milioni 360.93 tofauti ya Shilingi milioni 82. Hizi hazina maelezo na ripoti inasema kwamba, baada ya kufuatilia kwa *cheque No.CQ114326* na pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwa *warrant fund No. 00258329* na kuonyesha wazi kwamba, Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi kilipokea Shilingi milioni 360.93 na kikaonyesha kwamba hizo fedha zilizosemwa zimetolewa na Hazina Shilingi milioni 443.2 sizo. Tunataka kujua Hazina imipeleka wapi hizo Shilingi milioni 82? Nani amekula? Tunahitaji maelezo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio katika Chuo hicho tu, pia *Muhimbili University*, vitabu vya Hazina vinaonyesha kwamba fedha zilizopelekwa kwa ajili ya mishahara ni Shilingi bilioni 1.2. Lakini *Muhimbili University* imepokea Shilingi milioni 781 peke yake. Tofauti ya Sh. 372.92 hazina maelezo Hazina, nani amechukua hizo fedha? Tunataka maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa kilipelekewa zaidi ya shilingi milioni 277.5 ambazo zilikuwa fedha zaidi ya mwezi mzima ambazo zinapokewa. Hiyo ni ziada kwa ajili ya mishahara. Fedha hizo hazikurudishwa Hazina na Mhasibu au *Bursar* hajatoa maelezo amefanya nini fedha hizo. Tunaomba maelezo ya kina na ni kwa nini Hazina haina kumbukumbu sahihi ya watumishi wa taasisi zake, inafanya uzembe mkubwa namna hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nitajikita kwenye eneo la ubadhirifu wa fedha na matumizi mabaya ya fedha za Serikali au fedha za umma. Sasa nizungumzie ubadhirifu mwagine, labda wengine hawajauona au wanauona ila hatujui. Kuna nyumba za Makatibu Wakuu wa Wizara ambazo Makatibu Wakuu wa Wizara wanapewa hapa Dodoma.

Hizi nyumba zinalipiwa na Serikali, lakini Makatibu Wakuu wa Wizara wanakuja wakati wa kipindi cha Bunge peke yake, wakimaliza wanaacha ma-housekeeper na walinsi zikiwa *full furnished*. Wabunge tunahangaika na majumba, tunapanga nyumba kuanzia Sh. 400,000/= mpaka Sh. 600,000/=, ni kwa nini Serikali isiwape Wabunge nyumba hizo wakapangisha wakalipa kodi na hao Makatibu Wakuu za Wizara wakalipiwa fedha hotelini wakati wakiwa kwenye kazi za Bunge? Hayo ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Naomba Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri. Jana Mheshimiwa Zambi alipokuwa anachangia hapa alisema kwamba katika kaguzi zao mbalimbali kwenye Halmashauri wamegundua kuna ubadhirifu mkubwa sana wa fedha. Naunga mkono hoja yake kwa mfano ufuatao:-

Halmashauri ya Wilaya ya Singida imekuwa ikipokea asilimia 20 ya ruzuku kama fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa kupelekwa vijiji. Halmashauri hii imepokea kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2008, 2009 na 2010. Lakini fedha hizo hazijawahi kupelekwa vijiji hata kijji kimoja. Baada ya kelele ya sisi Wabunge, Mkurugenzi alituambia kwamba fedha hizo zimetumika kwa matumizi mbalimbali na akaandaa akaunti hewa. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Christowaja Mtinda, tunakushukuru sana. Waheshimwa Wabunge, kama mnavyojua, hoja hizi ni za Kamati na kwa utaratibu wetu wa Wabunge katika hoja za namna hii zinachangiwa pamoja na Waheshimiwa Mawaziri pia kama wachangiaji wa kawaida. Kwa hiyo, baada ya muda kama sio mrefu nitaanza kuchukua pande zote na tutaendelea na uchangiaji wa namna hiyo jioni pia.

Sasa anayefuata ni Mheshimiwa Susan Kiwanga na atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Waziri Silima ajiandae.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ratiba imezingatiwa. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema baada ya kutoka India naendelea vizuri na afya na nitaendelea kuwatumikia Watanzania kadri nitakavyoweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmojawapo katika Kamati ya Serikali za Mitaa (LAAC) na nimejionea mwenyewe mambo mengi ya maajabu yanayotokea katika Halmashauri ambazo kwa uchache tumezifikia. Ingawa naungana kabisa na Kamati yetu, kwa kuwa muda ulikuwa siyo mwangi sana na tungejaza hata vitabu kumi, lakini kwa ufupisho tu tumewasilisha yaliyojiri tuliyoyaona kwa uchache, lakini yapo mengi zaidi yaliyostajabisha kuliko haya tuliyoyawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naungana na mawasilisho ya Kamati zote zilizowasilishwa. Kwa kweli ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge kuisimamia Serikali. Katika kipindi cha mwaka mmoja nilichokaa

Bungeni na katika kukagua Halmashauri mbalimbali kwa kushirikiana na CAG nimegundua kwamba pamoja na jitihada tunazofanya, lakini imeonekana kwamba tumeshindwa kuzifikia Halmashauri nyingi kutokana na uwezo mdogo wa bajeti ambao sisi Wabunge tufike katika Halmashauri na inapelekea Wakurugenzi wengine wana-relax. Wengine sijui wanakwenda kusali au kwa Waganga wa Kienyeji kwamba Kamati ya Serikali isifike maeneo yao! (Makofii/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri chache tunazozifikia katika kutembelea miradi kwa kweli zinatisha. Unaona kabisa, kwa mfano, tulikwenda kwenye Halmashauri moja wanasema kabisa daktari anasema amenunua kifaa fulani cha hospitali, tunamkamata mtu wa *store*, kifaa kiko wapi? Hakioneckani kwenye kitabu, kinaonekana kimenunuliwa, kimeingia *store*. Tunamkamata Mkurugenzi, anababaika, yule wa *store* anababaika, daktari anababaika. Sasa vitu kama hivyo vinajitokeza kwenye Halmashauri nyingi, lakini tumeshindwa kuzifikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kweli kama Serikali iliyopo madarakani ina nia ya sisi Wabunge kuisimamia hiyo Serikali, ni vyema bajeti ikaongezwa ili Wabunge twende kwa wakati kukagua miradi, siyo kuishia kwenye vitabu. Kwa mfano, miradi ya barabara. Sisi tunakwenda kukagua miradi ya barabara zinazohusuiana na Kamati yetu, lakini unapokwenda kukagua mradi wa barabara, hiyo ilishajengwa miaka mitatu iliyopita, leo ndiyo tumepata uwezo wa kwenda kukagua, utaikuta barabara hiyo. Kwa hiyo, kama walikula fedha, walikuwa huko, lakini vitabu vinaonyesha kabisa walijenga barabara. Lakini Mkurugenzi anakwambia mvua ilinyesha. Kwa hiyo, huwezi ukaona hii barabara kwa mwaka huu kwa sababu ilikuwa ya miaka mitatu, utashindwa kumchukulia hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna haja sisi Kamati yetu iende na wakati, tunavyokagua katika vitabu na tukague katika miradi ya maendeleo ili tulete majibu sahihi katika hili Bunge. Nilichojifunza ndani ya mwaka mmoja, ni kweli kabisa Watendaji wanaweza wakaiangusha Serikali. Nilichojifunza Watanzania wajue kwamba Katiba Mpya ndiyo kinyang'anyiro chetu. Katiba Mpya ndiyo jibu kwa kuondoa Mawaziri ambao ni Wabunge kuja ndani ya Bunge kutujibu maswali. Wanatakiwa watokee hapa Watendaji wa Serikali, sio Wabunge ambao wao ni marafiki zetu, tunakaa nao pamoja, tunakunywa nao chai. Unajua ukitaka kumpiga nyani, usimwangalie usoni. Sasa Waziri umetoka hapa, unamwambia nini? Leo unakuja unamwuliza maswali hapa ya ajabu! Lakini anakwambia bwana, watendaji kule! Kwa hiyo, ni Katiba Mpya iwe jibu. Watendaji watokee ndani ya Bunge, watujibu maswali kwa bajeti

tulizopitisha, sio hawa Wabunge ambao ni Mawaziri. Kwa hiyo, kama tutaitengeneza hivyo na Watanzania wajue Katiba Mpya ndiyo jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali inatisha katika Serikali za Mitaa, wala sitaki kuzungumzia sana kwa sababu wengi wamezungumza na mambo yanajulikana. Nadhani hata kwenye Jimbo lako una kero nyingi kuhusu Watendaji. Kama wewe huko huku, bajeti kule inapitishwa, wewe unajua wamepitisha nini na wewe ndiyo Mwenyekiti wa ile Kamati ya Halmashauri pamoja na wewe Mjumbe wa Kamati ya Fedha. Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa. Ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri zetu na wenyewe ni tatizo. Dhana ya Serikali kufika mwaka 2025 Halmashauri zijitegemee, ni ndoto. Leo kuna Halmashauri zinakusanya mpaka kwa asilimia moja. Kweli leo mwaka 2012 unakusanya asilimia moja kiwango cha kujitegemea mwaka 2025, haya malengo yatafikia? Sasa uvujaji huu wa mapato katika Halmashauri unahamia mpaka kwenye Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini kwamba nchi hii tuwe na utegemezi asilimia 45! Kumbukumbu sahihi, eti tutegemee kutoka nje wakati sisi tuna rasilimali chungu nzima hapa katika nchi yetu! Leo tunawaambia Halmashauri kule wajitegemee, sisi wenyewe tuanze basi tujitegemee tuonyeshe mfano katika Serikali Kuu. Sisi wenyewe tunategemea wafadhili wa nje, kule tunawaambia wajitegemee. Hapo tunakuwa kama tunafanya mchezo wa kuigiza ndani ya nchi yetu. Suala zima nadhani Waziri wa TAMISEMI anajua na tulimwambia kwamba tunahitaji mrejesho wa hoja tunazozipeleka kwake na utekelezaji wake. Lakini unakuta mwaka unapita hoja hazijajibwa. Tunakuja tena hapa tunawasilisha hoja nyingine, yaani zinalundikana. Kwa hiyo, zinalundikana kwenye Halmashauri, zinalundikana na kwenye Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utendaji wa ufanisi utapatikana wapi wakati Halmashauri na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa zinafanya kazi na wao wanaangalia juu? Je, wamejibu hoja? Aaaha, kumbe hawajajibu hoja na sisi si watakuja tu Kamati ya Serikali za Mitaa watatutoza asilimia 15, watatutoza kutupa maonyo basi, kesi zitakwenda kwa DPP. Hata kama ushahidi unajionyesha kwenye vitabu CAG anakamata wezi kwa vitabu vyake, fedha zimepotea. Lakini DPP anaatamia kesi hata miaka mitano. Kwa hiyo, kuna haja Serikali kuleta sheria hapa tubadilishe, DPP achunguze kesi, tumwekee muda maalum kwa ushahidi ulioko kwa CAG kama ilivyo kwenye Kesi za Uchaguzi, wanassema ziishe ndani ya miaka miwili na nusu na kesi hizo za ubadhirifu tuziwekee muda maalum ili tuokoe hili Taifa. Kwa hiyo, kuna kamchezo kanachezwa pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha bora kwa kila Mtanzania. Siwezi nikamaliza bila kutaja Maisha Bora kwa Kila Mtanzania, hususan Mkoa wa

Morogoro na ubinafsishaji wa viwanda. Kama kuna Mkao umepata matatizo, basi ni Mkao wa Morogoro. Waziri aje na majibu, Morogoro ilikuwa na viwanda vingapi kabla ya ubinafsishaji? Wamebinafsisha vingapi? Vinavyofanya kazi vingapi? Wananchi wamefaidika vipi? Leo kuna wananchi walikuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo cha Polytex Morogoro, wananchi wa takriban 1,200 tangu mwaka 1998 hawajalipwa fedha zao, mwaka jana eti wamewalipa wananchi 84 tu, wengine wote haijulikani hatima yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ije na majibu, hawa wananchi watalipwa lini? Maisha Bora kwa Kila Mtanzania hapa yako wapi? Ubinafsishaji una faida gani katika mwananchi wa kawaida? Labda kwa watu wachache walioingia mikataba ya kubinafsisha, wameongea ongea, wamepata vitu fulani, hao ndio wanasema kuna faida. Lakini mwananchi wa kawaida hana manufaa na huo ubinafsishaji. Hivyo viwanda vilivyobinafsisha kama tumbaku, watu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, hawana vitendea kazi pale, wanaathirika, wanakufa na hakuna mtu wa kuwasaidia. Mishahara ya ajabu ajabu, wanakuwa vibarua ndani ya nchi yao.

Kwa hiyo, naomba nipate majibu kama *General Tyre* inafufuliwa: Je, Kiwanda cha Mpira cha Mang'ula kinasemaje? Kwa sababu *General Tyre* bila Kiwanda cha Mpira pale Mang'ula na sisi tufaidike. Kiwanda cha Mazulia Kilosa, ukienda pale ni aibu. Tena kaka yangu Mkulo Waziri wa Fedha ndio mwenye lile Jimbo, yaani yamekuwa mahame, mabati yameng'olewa nyang'nyang'a! Hii nchi tunaipeleka wapi? Kiwanda kingine amekichukua ndugu yangu hapa Abood, hayupo hapa, yupo pale. Upande mmoja anafuga mbuzi, upande mmoja kilikuwa cha MOPROCO hakifanyi kazi ya aina yoyote, wananchi wamekosa ajira. Alizeti tunalima ndani ya nchi hii, kwa nini tusizalishe mafuta mazuri tukapata afya na kuondoa *cholesterol* ndani ya mwili wetu? Serikali inatupa majibu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Morogoro tumeathirika. Kiwanda cha Chuma pale Mang'ula kiko wapi? Chuma inagunduliwa, kiwanda kiko wapi? Hata hii *Kilombero Sugar* tunafaidika nini sisi? Leo sukari inazalishwa pale Kilombero kilo moja Sh. 2,500/=, Dar es Salaam kilo moja Sh. 2,200/= sisi tunafaidika nini kama wadau? Ubinafsishaji umefeli kwa Watanzania wa kawaida, lakini umefaidika kwa watu wachache ambao mnajua namna ya ubinafsishaji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana. Namwita Mheshimiwa Tundu Lissu, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Sillima.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia kwenye huu mjadala muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapoleta taarifa zake mbele ya Bunge lako Tukufu, huwa ni wakati mwingine tena wa kusoma *catalogue*, kama neno hili ni sawa sawa *catalogue* ya wizi wa fedha za umma. Huwa ni wakati mwingine wa kukumbushana jinsi ambavyo Serikali yetu na Watendaji wake, mfumo wetu mzima wa Kiserikali ulivyojaa wizi na ujisadi.

Kila mwaka Kamati za Bunge lako Tukufu zinazosimamia fedha za umma zinapoleta ripoti zake huwa ni fursa nyingine ya kukumbushwa jinsi tulivyooza kama Serikali na kama mfumo wa kiutawala na mwaka huu siyo tofauti. Ripoti ya mwaka huu haina tofauti sana na ya mwaka jana au ya mwaka wa juzi au ya miaka kumi iliyopita. Ni *catalogue* ya *theft, catalogue* ya *plundering of public resources* ya *pillage of state resources*. Nafikiri sitakuwa nakosea nikisema kwamba kwa muda wa miaka kumi au zaidi hatujaletewa taarifa ya Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali inayosema kwamba hali ya usimamizi wa mali ya umma, hali ya usimamizi wa fedha za umma imekuwa afadhali. *It is just a catalogue of abuses.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali kila mwaka anatuletea taarifa ya wizi hatujawahi kuona Serikali ikichukua hatua dhidi ya wale ambao taarifa hizi zimekuwa zimesema wamefanya huo wizi. Hatujawahi kuona Mtendaji yoyote akichukuliwa hatua kwa sababu ya kufanya haya mambo ya hovyo. Hatujaona Waziri akiwajibika kwa sababu ya wizi katika Wizara yake au kwa sababu ya kuhuishwa na huu uvundo wa wizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, mali za umma ambapo zamani mimi nikiwa mtoto ilikuwa tunaambiwa usiguse, hiyo ni mali ya Serikali. Leo Serikali imekuwa ni *site* ya *plunder*. Watu wanaingia Serikalini, watu wanataka wawe Wabunge, wawe Mawaziri, siyo wafanye kazi kama dhamana. Wanataka washike hizi nafasi *in order to plunder the state, in order to plunder the people*. Matatizo yetu ni matatizo ya mfumo ambao Waingereza wanaita **cleptocracy**, ni mfumo wa utawala wa udokozi, ni mfumo wa utawala wa wizi, ni mfumo ambao unalinda wezi, unaadhibu watu wa haki, unaadhibu wanaosema kweli. Leo mtu akisema fulani ameiba anaanza kushughulikiwa yeye. Leo ukitaka kuzungumza, mimi ni Mbunge, kwenye Halmashauri zetu, uliza au anza kufuatilia fedha za Halmashauri uone utakavyong'ang'aniwa. Utakavyotungiwa kesi za ajabu. *We have built a cleptocracy! We have built a system of organized*

*theft.* Dawa ya *cleptocracy* siku zote, zama zote huwa ni mabadiliko makubwa ya kimapinduzi ya mfumo wa utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge tangu jana wamelalamika, kila mmoja anayesimama hapa anasema Serikali *ime-fail*, Serikali hivi, Serikali hivi, sijasikia bado na naomba nisikie nani amesema kwamba kwa sababu ya huu mfumo wa udokozi *tu-move motion* ya kutokuwa na imani na Serikali na Waziri Mkuu. Nasema hili siyo kwa sababu nina hila yoyote na Mheshimiwa Mizengo Pinda, sina hila na Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini ni Serikali yake. *We should take him, he should account for this cleptocratic behaviour* ya Serikali anayoisimamia. Sijasikia Mbunge yejote akimshika huyu *bull by the horns*, *it is time we stopped whining, kwa sababu hii ni whining. It is time we move the motion of no confidence against this corrupt government. Vinginevyo we either put up or we shut up.* (Makofi)

*Haya maneno kwamba wizi, wizi, Serikali imefanya, take action! You have a mandate! You have the power under the constitution ya kusema hii Serikali haichukui hatua, Mheshimiwa Waziri Mkuu wajibika kwa madudu ya Serikali yako! We should stop whining, we should stop complaining, we have the power! Unless we dont take it too seriously.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitaomba Wenye viti wangu wa Kamati hizi zilizoleta hizi taarifa Bungeni, wanapofanya majumuisho *wa-move a motion* kama tuko *serious*, kama siyo kelele tu. *Wa-move a motion of no confidence against this government for this cleptocratic behaviour.* Kwa kujenga mfumo wa kislasa wa udokozi, *a cleptocracy*, tukifanya hivyo wananchi watatuamini. Hii *responsibility* ni kubwa kwa Chama kinachotawala, *the majority party in Parliament.* Ninyi ndio mnaosababisha yote haya. Mna nguvu ya kuyafuta, mna nguvu ya kuyazuia kama mtatumia *majority* yenu sawasawa. Sisi hatuna nguvu hiyo, tuko wachache. Lakini nyie wengi badala ya kupiga makofi ya ushabiki, *take action* ya kuzuia huu uozo! Mkifanya hivyo, mtaheshimika, msipofanya hivyo, mnaelekea kwenye *scrapheap* ya *history.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tundu Lissu. Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Silima, atafuatiwa na Mheshimiwa Chami.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mawazo yangu kwenye mjadala huu. Awali ya yote naomba niwapongeze Wenye viti wa

Kamati hizi tatu, si tu kwa kutuletea ripoti zenyenye nia ya kufanya marekebisho katika utaratibu wetu wa usimamizi wa fedha, lakini pia kutumia nafasi na fursa walizonazo katika kutushauri. Nawapongeza sana Wenyeviti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwenye baadhi ya maeneo ambayo yametokana na ripoti za Kamati hizi. Eneo la kwanza ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala la kuongezeka kwa deni la Taifa. Naomba nieleze kwamba lengo kubwa la kukopa ni kupanga ili tufungue mapato ya baadaye na fursa za baadaye na nchi zote duniani zinakopa na zinafanya hivyo kujaribu kufunga pengo ambalo linatokana na tofauti ya mapato wanayokusanya na haja ya matumizi ya maendeleo hata ya kawaida. Deni letu limeongezeka kwa sababu tumekopa kwa nia ya kutaka kufungua au *ku-unlock opportunities* ambazo zipo na hasa kwa ajili ya miradi ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za nyuma, tulikuwa hatukopesheki na tulikuwa hatuwezi tukakopa. Baada ya kutokea utaratibu wa *HIPIC* tukaonekana tunakopesheka na Serikali ikawa inahisi ni vyema tukope tujenge hasa miundombinu kuhakikisha kwamba unaongeza fursa ya uchumi kukua na kuweka matumaini ya baadaye. Kwa hiyo, kukopa kuna nia nzuri na tusiogope kukopa. Katika kukopa, jambo muhimu ni kutazama: Je, tuna uwezo wa kulipa na kuna kitu kinaitwa *debt sustainability analysis* ambacho kuna vitu vingi vinaingizwa kwake ili kutoa dira ya kuona kwamba sasa mimi niliyekopa ninakopesheka au nafikia kikomo ambacho naweza kufilisika? *Analysis* zilizofanywa kwa deni la Taifa la Tanzania bado linahimilika na kama tunakopa deni linahimilika na tunaweka miundombinu kwa ajili ya kukuza uchumi na kukaribisha usogezaji wa huduma kwa wananchi, hili nashauri tusiliogope.

Pamoja na yote, tunalohitaji kufanya ni kuhakikisha siku zote kwamba tuko karibu na hesabu zetu za deni. Tuangalie deni bado tunaweza kulilipa na kama ni hivyo nafikiri tunasikia wenzetu wanafanya hivyo kama njia moja ya kupata maendeleo. Sishangai, leo hapa karibu sote tunazunguka Majimboni au sehemu nyingine kwamba wananchi wajunge na *SACCOS* wakope, wajenge maendeleo yao ya baadaye. Serikali tuishauri hivyo hivyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nilitaka kuchangia ni kuhusu upungufu ambao umeripotiwa na Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (*PAC*) katika page ya 15. Katika taarifa hiyo, kuna maelezo kwamba kulikuwa na tatizo la kutotimiza masharti ya Sheria ya Manunuzi na kwa hiyo, kukawa na hisia kwamba pengine Shilingi bilioni 50.7 zimeibiwa.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, walilipokea hili kama wizi na nafikiri walitimiza haki yao kabisa. Lakini naomba nitoe taarifa kwamba ni kweli hili lilitokea kwa sababu kulikuwa na tofauti kati ya *Procurement plan* na ununuzi au bajeti ambayo ilitengwa. Kwa hiyo, kukawa na hiyo gap na hiyo *definitely* ilikuwa ni kinyume na kifungu cha 45 ya Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2004, na pia Kanuni ya Ununuzi Na. 25, na 46 (9).

Kwa hiyo, CAG akasema hapa kuna dalili ya kuwa tatizo na baada ya hapo kuna mambo ambayo yalifanyika katikati na mambo haya yalisawazishwa. Naomba nitoe taarifa kwenye Bunge lako kwamba baada ya maelezo na kupatikana na nyaraka na taratibu zilizofuata, hii hoja imefungwa rasmi na Mheshimiwa CAG. Kwa hiyo, haitaonekana au haikuonekana kwenye taarifa yake ya mwaka 2010/2011 na hata haipo kwenye hoja ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa haraka nizungumzie suala la mishahara hewa. Ni kweli kwamba tuna tatizo la mishahara hewa na ndani ya mishahara hewa pengine pana mbinu ya baadhi ya Watendaji wetu. Suala hili tunaendelea kulifanya kazi na hivi sasa tumeunda timu ambayo imeshakwenda kwenye Halmashauri zote kulifuatilia. Kuna Wabunge walitaka kujua ile siku tuliyosema tunaitenga kwa ajili ya kufanya hivyo, siku hiyo imeshatekelezwa, tumeshafanya kwenye *Local Governments* na Taasisi tofauti na sasa hivi tunaendelea kwenye Serikali Kuu. Taarifa za awali zinaonyesha kwamba ni kweli kuna matatizo, lakini baada ya kupata taarifa, ndiyo hatua zitafuata. Pamoja na hilo, uboreshaji unaendelea kufanya ili kuanzishwa mifumo ambayo *periphery* na *core* itakuwa inawasiliana na kujua kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kwa haraka suala la misamaha ya kodi. Nchi yetu ina utaratibu wa kutoa misamaha kwa baadhi ya maeneo na kwa baadhi ya Taasisi. Ni kweli kwamba tunaongoza kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa misamaha ya namna hii na ni budi tufanye jithada za kuhakikisha kwamba hili tunaliepuka. Kwanza ni kupoteza mapato ambayo yangetusaidia katika ukuaji wa uchumi au kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi tatu kwa taariza zao ambazo wameziwasilisha katika Bunge lako Tukufu. Jambo kubwa ambalo limesemwa kuhusu Wizara ya Viwanda na Biashara katika Bunge hili ni juu ya utendaji wa *TBS* na

zimejengeka hisia kwamba pengine labda Wizara inalinda Menejimenti au Mkurugenzi Mkuu wa *TBS* katika mambo ambayo anatuhumiwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa Watanzania ambao wanatuangalia na ambao watatusikiliza, ni vizuri tukasema ukweli na ukweli kama ulivyo. Taarifa iliyoko Serikalini hadi sasa hivi na ambayo Bunge hili lina taarifa ni taarifa ya Kamati Ndogo ambayo iliundwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe mwaka 2010 ya kwenda kukagua utendaji wa *TBS* katika suala zima la ukaguzi wa magari nje ya Tanzania. Kamati ile ndogo iliongozwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi aliyekuwa Mbunge wa Mbarali. Taarifa yake imesainiwa tarehe 10/4/2010 takribani miaka miwili mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa ile inaainisha changamoto nydingi ambazo *TBS* inakumbana nazo, inaainisha upungufu mwingi ambao umeonekana na ikatoa mapendeleko ya nini kifanyike ili ukaguzi wa magari uwe mzuri zaidi kwa faida ya Watanzania. Lakini anahitimisha Mheshimiwa Kilasi kwa kusema kwamba, pamoja na utendaji kazi wa *TBS* katika mazingira magumu, *TBS* inapongezwa pamoja Wizara lakini Wizara ikashauriwa kwamba itoe bajeti kubwa kwa *TBS* ili *TBS* ifanye mambo yafuatayo:-

La kwanza, iongeze ukaguzi wa magari, siyo tu katika zile nchi tatu ambazo ile Kamati ilitembelea isipokuwa kila mahali ambapo magari yanatoka kwa wingi, *TBS* ihakikishe kwamba kuna mtu anakagua magari ambayo yanakuja Tanzania. Lakini vilevile *TBS* ijengewe uwezo wa kukagua siyo tu magari, isipokuwa na bidhaa nyininge muhimu ambazo zinakuja katika nchi yetu. Hiyo ndiyo taarifa tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana mwezi wa Nane, Mheshimiwa Zitto tena akatuma Kamati yake kwenda kukagua maeneo mengine ya ukaguzi wa magari, katika nchi ya Singapore na Hong Kong. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba, Wizara haikuagwa kuambiwa kwamba tunakwenda kumkagua mtu wenu au tunakwenda kukagua Taasisi yenu ya *TBS*. Kamati ile imekwenda mwezi wa Nane.

Baada ya kwenda mwezi wa Nane, imekaa na taarifa ile mwezi wa Tisa, Kumi, Kumi na Moja, Kumi na Mbili, mwezi wa Kwanza tarehe 27 kila mtu aliyekuwa anaangalia luninga akashangaa kuona kwamba Wajumbe wa Kamati ile wakiwa wanamtuhumu Mkurugenzi Mkuu wa *TBS* kwamba ni mwongo, ameidanganya ile Kamati na kwamba ana kampuni hewa. Mara moja Wizara iliomba taarifa hiyo ya Kamati Ndogo ili tufanyie kazi mara moja. Lakini tukaambiwa kwamba Kamati ile

haijakamilisha taarifa yake. Tukaambiwa tutapewa baada ya siku tatu, lakini hatukupewa taarifa ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 10 mwezi wa Pili mwaka huu, Kamati tatu; Kamati ya POAC, Kamati ya PAC na Kamati ya Viwanda na Biashara zikakutana kujadili suala hili la magari *TBS*. Katika kikao kile Wizara yetu ikaagizwa ipeleke taarifa zote za Ukaguzi wa magari kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ili akazikague. Tarehe 18 mwezi wa Pili, Wizara ikapeleka taarifa zote kwa CAG kama tulivyoagizwa na Kamati.

Juzi Mheshimiwa Naibu Waziri akiwa anajibu swalii hapa Bungeni kuhusu swalii linalohusu masuala ya *TBS* akaona taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ikiwa kwenye mikono ya Mheshimiwa Mbunge mmoja na katika kujibu, Mheshimiwa Naibu Waziri akasema kwamba taarifa ile imetoka na tutaifanya kazi. Lakini kwa hakika kabisa, taarifa ile ilikuwa haijafika ofisini kwetu japokuwa Waheshimiwa Wabunge hapa walikuwanayo na taarifa kwamba kuna Waheshimiwa Wabunge walikuwa nayo wiki moja kabla ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana hiyo nimekwenda kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge kuomba taarifa hiyo. Katibu wa Bunge anasema hana hiyo taarifa. Nimepiga simu kwa Katibu Mkuu wangu akasema hana hiyo taarifa. Katibu Mkuu amepiga simu Ofisi ya CAG kuulizia hiyo taarifa CAG akaomba msamaha kwamba walitoa kwa Wabunge, lakini wakasahau kuipa Wizara. Nimejaribu kuomba taarifa hiyo kwa Wabunge hapa Bungeni sjafanikiwa kupata isipokuwa mpaka saa 9.00 jana Mheshimiwa Zitto Kabwe akaniazima nakala yake. Ndiyo mara ya kwanza nimeona taarifa ya CAG kuhusu *TBS* na tukiwa hapa Bungeni saa 12.40 ndipo mtumishi wa Bunge anaitwa Katherine akanilettea taarifa kutoka kwa CAG Kanda ya Dodoma. Ndiyo maana nimeipata jana 12.40. Mara baada ya kuipata, nimeagiza Bodi ya *TBS* kufanya kazi mara moja ili kuweza kuishauri Wizara na Serikali nini kifanyike kutokana na mambo haya ambayo yamesemwa na CAG. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme maneno machache pengine kwa uchungu kwa sababu inaonekana kwamba pengine sisi Wizara tunamlinda Mkurugenzi Mkuu wa *TBS*. Mimi naamini kabisa kwamba maneno hayo yanapelekea kuona kwamba kuna maslahi binafsi ya Watendaji wa Wizara labda Daktari Chami. Nimesema kabla na nasema leo, kama kuna mtu ye yeyote ambaye ana uthibitisho kwamba Daktari Chami au ndugu yake au rafiki yake ana kampuni hewa au ana maslahi kutokana na ukaguzi wa magari, atoe uthibitisho huo na mimi

nitaweka Uwaziri wangu rehani, nitajiuzuru Uwaziri kama mimi nina maslahi hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo basi, haina maana kwamba mimi nitaamua tu kumfukuza kazi mteule wa Rais bila kufuata taratibu, kwa sababu taratibu zote ambazo zimetakiwa na Kamati ya Bunge lako Tukufu nimezitekeleza. Nimekosea wapi mpaka natuhumiwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba labda mimi namlinda Mkurugenzi Mkuu wa *TBS*? Kile ambacho nimeambiwa nitekeleze nimeteketeleza. CAG jana ndiye amenipa taarifa, nimeanza kuifanyia kazi.

Nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, muelewe na muamini kabisa kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara hailindi uozo wa aina yoyote. Hakuna mtu ambaye atalindwa au atakingwa asichunguzwe na *oversight Committees* au na vyombo vya usalama ambavyo vinaangalia maslahi ya nchi yetu, na kwa hakika kabisa tukilazimisha kwamba tufanye maamuzi ya kumsimamisha mtu bila kufuata taratibu, tutakuwa tunakiuka haki ya msingi ya mtu ambayo tumekula kiapo cha kuitetea. Mimi nataka niseme waziwazi hapa kwamba taratibu zote zitafuatwa, na hata Bunge likipenda kuunda Kamati nyingine, tuko tayari kuipa ushirikiano wa kuchunguza jambo hilli mpaka lifikie mwisho wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niyaseme hayo kuweka jambo hilli sawa ili Watanzania wote watambue kabisa kwamba Wizara haifurahii. Kama kuna bidhaa ambayo inaingia Tanzania ambayo ni feki au bidhaa ambayo siyo nzuri na kama kuna mtu yeote ambaye anashiriki katika kuingiza bidhaa hiyo hapa Tanzania, Wizara itakuwa ya kwanza kabisa kuhakikisha kwamba mtu huyo anachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango kwa mawazo kufuatia Wenyeviti wetu watatu kutoa taarifa zao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu wa Nchi, Mheshimiwa Mkuchika, tumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya *Local Authorities Accounts Committee*. Tunamshukuru kwa sababu ameeleza mambo haya kiutu uzima. Napenda kumwambia kwamba hata leo asubuhi tumemsikia alipozungumza katika kipindi kile cha *TBS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi tumewasikia Wabunge walivyozungumza hapa toka jana mpaka leo. Mimi naamini kwamba atakuwa ni mtu tu haelewi nini kinachotokea katika nchi hii, atakayesimama hapa apinge kwamba wanachosema Wabunge siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nisimame hapa kwa niaba ya Serikali kusema kwamba, haya yanayozungumzwa, hasa hasa mimi nasemea kwa upande wa *Local Government*, ni kweli yako, yanafanyika, na tumekwenda katika Halmashauri. Tutakachofanya kama Wizara ni kuhakikisha kwamba tunaweka thamani katika mazungumzo yaliyozungumzwa hapa. kwa sababu *this is a serious business*, tunataka tuwaombe Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi tunakwenda, tumeingia, mahali popote ukisoma akina David Ricardo, ukisoma akina Adam Smith, wanakwambia mahali popote ambapo mambo hayaendi kama yanavyotakiwa, Serikali itaingilia kati. Ndicho ambacho kimekuwa underscored hapo. Kama kuna *market failure*, Serikali itaingilia kati, kama kuna mahali ambapo mambo hayaendi kama yanavyotakiwa, Serikali itaingilia kati. Nataka nithibitishe hapa kwamba kazi hiyo tumeifanya na kazi hiyo tutaendelea kuifanya. Chonde chonde, msitushike mkono mkatuambia kwamba inatosha sasa. Hatutapunguza *break* hapa, tutakwenda mpaka tutekeleze ambayo yamezungumzwa hapa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda Bagamoyo pale, aliwasimamisha watumishi wale wote pale *including* Mkurugenzi. Jioni, Waziri wangu atapata nafasi ya kuja na orodha hapa ya kusema hatua ambazo tumezichukua TAMISEMI. Jioni, mimi sitaki nim-pre-empty Waziri wa Nchi hapa. Atasema kuhusu wale ambao tumewasimamisha, wale ambao wamepelekwa Mahakamani na wale wote ambao tumewachukulia hatua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wenzetu, tunawaomba katika hili mtusaidie. Tusaidieni! Wabunge wa Kigoma tusaidieni, wa Lindi tusaidieni, Mtwara, nchi nzima Tanzania tusaidieni, msituache tu hivi hivi, msiombe suluhu! Tumezungumza habari hapa kwamba hakuna kumhamisha mtumishi ye yeyote ambaye ameonyesha ubadhirifu katika eneo lake. Asije akatoka tena mtu hapa akatuambia naomba huyu mtuondolee hapa mumpeleke pale. Hatumhamishi! Hatatoka pale! Hatutamhamisha mtumishi ye yeyote ambaye ametuhumiwa, atabaki hapo hapo. Hatumhamishi na tutamchukulia hatua hapo hapo! Hili tuelewane vizuri hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ni kweli kabisa ukiangalia utaratibu huu tunazungumza hapa, kwa Wizara, pale kwenye Halamashauri, mtumishi mmoja tu ambaye ndiye yuko kwenye ngazi ya Waziri wa Nchi na Ngazi ya Waziri Mkuu ni Mtendaji yule Mkuu kwa maana ya Mkurugenzi. Wale wengine wote waliozungumzwa, Wakuu wa Idara wote wako chini ya Halmashauri inayohusika pale pale kwenye Halmashauri. Kwenye hili mnalozungumza hapa sasa, maana yake nini? Maana yake tumefika mahali, ukisoma Ibara ya 145 na Ibara ya 146 ya Katiba, inaonyesha mamlaka kamili yaliyoko katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unipe nafasi kidogo nielezee. Baraza la Madiwani ndilo ambalo limepewa *mandate* na *power* ya kuamua mambo yake pale kwa niaba ya Halmashauri na *it's not questionable!* Hakuna mahali popote ambapo unaweza uka-question! Kwa maana ya *thrust* ya mazungumzo ambayo yamezungumzwa hapa leo, hata kama sisi hatuhusiki pale, kwa maana ya *intervention*, tutaingilia kati pale. Tukifika kwenye Halmashauri pale tutasimamisha watu. Hizo taratibu nyingine mnazorisema, zifuate basi!

*Please, tunawaombeni, tunawaombeni! Sisi haya mliyosema hapa, turuhusuni tukafanye. Ni Mkurugenzi Mtendaji tu, ni Municipal Director tu na City Director tu ambaye mamlaka yake yako kwa Rais ndio ambao sisi tunawachukulia hatua. Wale wengine wote, mamlaka iliyoko katika Halmashauri ina mandate na power ya kuchukua. Lakini kwa thrust ya mazungumzo yaliyofanywa hapa leo. Tuachieni, msitushike mkono. I shall deal with them perpendicularly; left, right and centre. Hiyo mtuachie kabis!* Hiyo mtuachie! Wala hatutaulizana hapa!

Unajua Utumishi, tutakuomba wewe Mheshimiwa Mama Hawa Ghasia, wewe kwanza tutaweka pemberi hiyo, tuta-organize an organized war and un-organised katika jambo hili. Tutaelewana vizuri ili tutatue tatizo la msingi linalojitokeza hapa. Sasa msichoke tena mkachomoka, mkaanza kutuambia, jamani chonde chonde, chonde chonde! Mimi hilo rungu nimeshapewa. Mwenzangu Mheshimiwa Majaliwa ameshapewa, Waziri wa Nchi ameshapewa hilo rungu, na Waziri Mkuu mwenywewe analo hilo rungu. Tunayo! Kwa hiyo, hatuna haja ya kuwaomba hapa mturuhusu. Sisi tuachieni. Tuachieni sisi, na Mheshimiwa Mrema nakuomba utuamini. Wewe tutakwambia hivi, kaa pemberi, tupishe sisi. Tukifika kwenye Halmashauri pale, mimi nakwenda na Agano Jipya na Biblia yangu naweka mfukoni, naingia mle ndani, vurugu tutakazosababisha pale kwa maana ya mazungumzo yaliyotokea hapa, asitoke mtu akakuomba suluhu. Viongozi wangu wanansikia hapa! Asituombe mtu suluhu baada ya mazungumzo yaliyozungumzwa hapa ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwako pale Kongwa, tukija Mpwapwa, msituombe suluhu, tuachenii hapa! Sisi TAMISEMI hapa tulizopokea ni trillioni tatu. Trillioni tatu kama ni noti kukuu ukizichenji utasikia harufu ya tumbaku. Na kama ni noti mpya utasikia harufu ya dawa. Unachukua hatua gani, kwamba unakwenda kwenye Halmshauri unaambiwa wamepata hati safi, *it's not enough!* Maana yake ni kwamba vitabu vime-balance tu. Sisi huwa hatuangalii hiyo. Tunamshukuru Controller and Auditor General, ametuletea. Tukienda kwenye Halmashauri, tunatafuta thamani halisi ya pesa iliyopelekwa katika Halmashauri. Hakuna Halmashauri hapa inapelekewa chini ya Shilingi bilioni 15 kwa mwaka mmoja. Unakwenda kule, halafu unaambiwa, unajua mzee, sasa wote ni watoto wa Mungu. Hakuna cha watoto wa Mungu, mtoto wa Mungu hawezi kuiba hela za Halmashauri. Hakuna, hatutawaachia! Sisi tunachukua maneno yenu, tunachukua maelekezo yenu, tutakwenda kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa *in addition to that*, tumeulizwa habari ya mafunzo. Hivi tunavyozungumza sasa hivi, Madiwani wote nchi nzima wako darasani. Mheshimiwa Mkuchika alikwenda Mtwara, mimi nitakwenda Korogwe kwa ajili ya kufunga mafunzo hayo. Tunataka waelewe hiki tunachozungumza hapa, wapate elimu ili wasije wakasema kwamba hawakujua. Madiwani ni chombo muhimu sana katika Halmashauri. Wakisimama, wakaweka thamani katika mazungumzo yaliyozungumzwa hapa, tutaondoka hapa tulipo. Tumekubaliana pia, vikao vyetu hivi vya Bunge vinapofanyika, kule kwenye Halmashauri wasifanye vikao vingine, *unless* kwa mambo ambayo ni *emergency*. Kwa mfano, mambo ya bajeti, ndipo hapo wanaweza wakakutana. Nalo hilo tumelichukua, nalo tutaliwekea utaratibu. Wala msiwe na wasiwasi, tutahakikisha kwamba na ninyi mnakuwa kule, kazi moja tu kutia kashi kashi ndani ya Halmashauri kushoto kulia na katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu mwengine anayenisikiliza hapa, unaweza kusema lugha hii mbona siyo ya Kiserikali. Lugha hii imetokana na mazungumzo hapa ndani! Lugha hii imetokana na mazungumzo hapa ndani! ndivyo ilivyokwenda. Kwa hiyo, sisi we are on top of business. Hili jambo tutasimamia, tunaomba mtuamini na tunaomba kwamba twende wote kwa pamoja, msiombe suluhu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia, mwisho, mwisho kabisa. Ziko hizi Halmashauri ambazo zimepewa hati chafu na zile nyingine ambazo zilikuwa zimepata hati chafu. Mnisikilize na Mheshimiwa Waziri atakuja kueleza hapa, tunawaandikia barua na tumeshamwagiza Katibu Mkuu, tutaeleza na hatua tulizochukua kwa wale wengine ambaa walihusika na

19 APRIL, 2012

jambo hili. And we shall never leave any stone unturned katika suala hili. Haiwezekani, mimi hapa ni Mkurugenzi Mtendaji, Shilingi bilioni 6 zimeondoka nisijibike!

Mheshimiwa Naibu Spika, you can leave this house hapa, mkijua kwamba tumepokea ushauri na maelekezo mliyotoa hapa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Nakushukuru.

**MHE. HASNAN M. MURJI:** Taarifa! Taarifa!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika! Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Tuanze na taarifa.

### **TAARIFA**

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Naibu Waziri kwa maelezo yake aliyoeleza hapa kwamba Wakuu wa Idara wote wako chini ya Halmashauri. Manispaa ya Mtwara – Mikindani, Baraza la Madiwani lillimsimamisha Mweka Hazina, lakini Mweka Hazina huyo bado yuko kazini na amekwenda kusoma kwa fedha za Serikali hii, pamoja na Baraza kumsimamisha. Nilikuwa naomba nimpe taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwamba ukichukua *Hansard* ya mwaka jana 2011 kwenye taarifa, ukasoma maelezo ya majibu ya hoja ambayo Mheshimiwa Mwanri aliyatoa kwa tarifa ya LAAC, hayana tofauti na haya anayotaka kutuaminisha leo kwamba ni tofauti. Nilikuwa naomba mwongozo wako, tupate *Hansard* ya mwaka jana ya maelezo ya Mheshimiwa Mwanri, tuyalinganishe hapa Bungeni na maelezo ya sasa ili Bunge liweze kumwazimia Mheshimiwa Mwanri kama aliyoyasema mwaka jana ameyatekeleza na kama aliyoyasema sasa atayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nitautoa baadaye.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zilizotolewa na Kamati zote tatu. Awali ya yote, naunga mkono hoja zote tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie na alipoishia Mheshimiwa Mwanri. Alipoishia Mheshimiwa Mwanri anasema kwamba Wilaya ya Bagamoyo wale watumishi tayari wamepelekwa Mahakamani baada ya Waziri Mkuu kwenda kule na kwenda kuzungumza na kuwasimamisha wale watumishi. Lakini jambo la ajabu, huu ni mwaka wa pili na nusu sasa, hakuna hata kesi moja iliyofunguliwa Mahakamani. Hii kesi haijamalizika, ni miaka miwili na nusu, watumishi hawa wanalipwa mishahara kama kawaida. Wamepelekwa watumishi wengine pale, kesi haijaanza kusikilizwa miaka miwili na nusu. Tunatarajia nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali hili nalo iliangalie. Wanapopeleka kesi Mahakamani, basi ianze kusikilizwa haraka kwa sababu ushahidi upo. Kitu gani kinachosababisha mpaka hii kesi ichelewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kuhusiana na wenzetu wa TBS. TBS imeonyesha wazi kwamba kuna fedha ambazo wanakusanya kutokana na tozo za magari kuyaingiza katika nchi yetu. Kuanzia mwaka 2002/2003 – 2009/2010, kwamba jumla ya *USD17Million* zilikusanya na wale mawakala. Baada ya kukusanya na mawakala, Dola millioni 14 za Marekani zililipwa kwa Mawakala na Serikali yetu ilipata Dola za Marekani milioni tatu tu. Serikali ina wachumi, waliobobea kabisa katika masuala haya ya namna gani ya kukuza mapato yetu kutokana na ushuru huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kukusanya mapato zaidi kuliko mawakala. Toka wakati huo wanaona kabisa kwamba fedha hizi za Serikali zinazokusanya ni chache mno ukilinganisha na zile za mawakala. Hivi Serikali hili hawalioni? Hivi chombo hiki pamoja na sheria zilizoundwa, zimeundwa kwa ajili ya kuwanufaisha mawakala? Chombo hiki kimeundwa kwa ajili ya kuinufaisha Serikali yetu tupate fedha nydingi. Lakini zaidi ya 75% zinakwenda kwa mawakala, sisi Serikali tunapata 25%. Tunafaidika na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaishauri nini Serikali sasa baada ya kuona hili limetokea kwamba hatufaidiki chochote na uwakala huu? Hili ni suala ambalo vile vile Serikali ijiulize, hao wachumi wake wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jana alizungumza Mheshimiwa Serukamba, leo amezungumza Mheshimiwa Tundu Lissu kuhusiana na uwajibikaji wa Serikali. Mheshimiwa Serukamba amesema kwamba, Chama cha Mapinduzi tuna uwezo wa kuiwajibisha Serikali. Mheshimiwa Tundu Lissu alirudia hilo, leo tena. Lakini mimi nasema sisi sote ni Wabunge, tuna uwezo wa kuikosoa, bila kujali chama chako wala nini, tuwe kama Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuanzia sasa tuwe na sheria kama wenzetu Wakenya walivyoweka. Siyo mbaya kuiga wenzako wamefanya nini. Kenya wameweka Kamati inayoitwa *Implementation Committee* kwa ajili ya Kauli za Mawaziri na Kauli za Serikali. Waziri anaposema jambo lolote lile Bungeni kwamba tutalitekeleza suala hili kwa muda fulani, Waziri yule anapewa miezi miwili. Akishapewa ile miezi miwili, lile jambo kama halijatekelezeka, Waziri anaulizwa kwa nini hili hukulitekeleza? Kama hakulitekeleza, maana yake hawajibiki huyu! Kama hawajibiki, weka nje! Wameshafukuzwa Mawaziri watatu. Hili na sisi tuanzie hapa, ni lazima tuazimie kwenye Bunge hili tuwe na *Implementation Committee* ambayo Waziri akizungumza lolote, basi ile Kamati iwepo ki-Kanuni kabisa ya Bunge letu ili ihakikishe kuwa wazo hilo la Waziri linatekelezeka, kama halikutekelezeka, Waziri hawajibiki na Serikali haiwajibiki, awekwe nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni jambo ambalo tunatakiwa na sisi tulifanye. Bila hivyo, tukisema leo tuitimue Serikali yote, hapana. Kuna Mawaziri wanafanya vizuri sana, lakini kuna Waziri hafanyi vizuri. Ni lazima tuwe na mahali pa kuanzia na ili tuanze, basi tuwe na Kanuni itakayouna hiyo Kamati itakayoongoza yale yote yanayozungumzwa na Waziri, basi yatakelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linanipa shida ni kwamba kuna Wilaya ambazo zimesimamisha watumishi wake kutokana na matumizi mabaya. Mojawapo ya Wilaya hizi ni Wilaya ya Kilosa. Sasa hivi inakaribia miaka mitatu, Serikali ipo, Mawaziri wapo, wale watumishi waliowekwa pale Kilosa wote wanakaimu kwa miaka mitatu. Hivi mtu anayekaimu, kweli anaweza akafanya kazi zake vizuri?

Mimi nashukuru kwa upande wa Serikali Kuu, wenzetu hawana taabu. Ameondolewa Bwana Jairo, amepelekwa Eliakim Maswi, amethibitishwa. Kuna ugonjwa gani kwenye Halmashauri zetu? Watu wanaokaimu wanakaa miaka mitatu hawajathibitishwa katika nafasi hizo ambazo wanakaimu na Serikali imetulia tu. Hivi huu ndiyo utawala bora?

19 APRIL, 2012

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo utawala bora? Mtu anakaimu miaka mitatu, na sheria inasema mtu yeote akiwa na sifa, akishakaimu baada ya miezi sita anatakiwa kuthibitishwa. Hawa wana kasoro gani, wanaendelea kukaimu? Hilo la tatu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni matumizi makubwa sana yanayofanywa na Serikali kwenye sherehe zetu. Nalo hili ni lazima tuliangalie. Wenzangu jana walizungumza vizuri tu kwamba Wizara moja ilikuwa ni Wizara ya Afya, kwenye sherehe za Nane Nane peke yake walitumia zaidi ya Shilingi bilioni 1.1. Hii ni Wizara moja. Lakini tuna Wizara karibu 28 kwenye nchi yetu hii.

Katika Maonyesho yale ya Nane Nane peke yake kila Wilaya inatakiwa iende pale kupeleka vitu vichache ambavyo wanavionyesha, na kila Wilaya inatoa magari, watumishi wanaokwenda pale wanalipwa, wakulima na wao wanalipwa. Kundi lile linakuwa kubwa mno!

Hivi, kama Wizara moja inachukua Shilingi bilioni moja, Wizara 28 ni kiasi gani cha fedha? Halmashauri zetu zote ni lazima zihudhurie. Hivi sasa Halmashauri ziko kwenye harakati ya kutengeneza mabanda na watu wanaandaliwa kwenda kwenye sherehe hizo. Wachumi wapo, hivi *impact* ya sherehe hizo ni nini? Toka Nane Nane ianze, kuna mabadiliko gani ya kilimo yaliyopatikana ndani ya nchi yetu? Kwa nini Sherehe hizo zisifanyike ndani ya Wilaya badala ya kuwachukua watu, kutumia fedha nydingi za Serikali ambazo hazipo kwenye bajeti na matokeo yake Serikali tunasema hatuna fedha wakati fedha tunazo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Serikali nayo ikae iangalie. Hivi toka tulivyoanza sherehe hizo, tuna manufaa gani? Siyo Nane Nane tu, ziko nydingi kweli! Tunanufaika na ninii? Hivi mabadiliko ya kilimo katika nchi yetu yamepatikana? Hivi nchi yetu hii mazao yameongezeka au ndiyo yanarudi chini? Ni lazima tujiulize! Siyo kwamba iwe kama vile ibada ya dini kwamba kila siku ya Ijumaa uende Msikitini kusali na siku ya Jumapili uende Kanisani, isiwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makof!*)

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo!

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, pale ambapo Waziri au Naibu Waziri anapolidanganya Bunge, ni hatua gani zichukuliwe dhidi yake?

Naibu Waziri/Waziri wa Viwanda na Biashara amesimama hapa bayana akasema yeye alitekeleza maagizo yote aliyopewa na Kamati ya PAC. Lakini, agizo la kwanza ambalo Kamati ya PAC ilitoa kwamba CAG anapokwenda kufanya uchunguzi, Mkurugenzi Mtendaji wa TBS asimame pbeni. Hilo ndilo lilikuwa agizo la kwanza na uchunguzi ufanyike. Lakini, kinyume chake uchunguzi umefanyika, agizo hilo halikutekelezwa, Waziri anasema alitekeleza maagizo yote, uchunguzi umefanywa Mkurugenzi wa TBS akiwa kazini.

Kwa hali hiyo, tunataka kujua Waziri anapolidanganya Bunge, anachukuliwa hatua gani? Kwa sababu tuna ushahidi wa kutosha kwamba watu wa kwanza wanaongoza kwa kutafuna nchi hii, siyo Watendaji wa Halmashauri. Watu wanaongoza kwa kiumiza nchi hii ni Mawaziri wenyewe, Mawaziri wetu ndio wezi namba moja, tutataja majina kwa majina na ushahidi tunao. (*Makofi*)

Sasa Waziri anapolidanganya Bunge tunamchukulia hatua gani? Waziri amelidanganya Bunge kwamba ametekeleza maagizo yote!

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

## **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Kuhusu utaratibu tu Naibu Spika. Ningeelewa kama Mheshimiwa Mbunge angejenga hoja yake kama anaona Mheshimiwa Chami amedanganya. Kwa sababu wao ndio walitoa maagizo kwa Waziri na Waziri amethibitisha ametekeleza. Wangeweza kuwa na nafasi ya kumwita kwenye Kamati akathibitishe. Lakini, wakitaka, anaweza akathibitisha hata hapa. Lakini hiyo conclusion aliyoitoa sasa hivi haikubaliki kwamba Mawaziri wote ni wezi. Haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa aliyoitoa hapa kwamba Mawaziri wote ni wezi, athibitishe basi, midhali mwenyewe amesema yuko tayari kuthibitisha, basi naomba akukabidhi uthibitisho kwa wizi uliofanywa na kila Waziri aliymo humu ndani. (*Makofi*)

19 APRIL, 2012

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Nimesema Mawaziri wengi ndiyo wanaongoza kwa wizi na ushahidi tunao humu ndani. Nitautoa ushahidi mkitaka nitoe. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia muda wetu ukutani hauturuhusu kuendelea, tutaendelea saa 11.00 jioni.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Nimekwishasimama, kwa hiyo, haiwezekani kuuchukua tena. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo.

(*Saa 7.02 mchana Bunge lilitfungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mara ya kwanza mkono wangu wa kulia wameingia Mtera eeh! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Ahsante sana, hoja za Kamati tunaendelea na majadiliano yetu kuhusiana na taarifa za Kamati za Fedha ambazo ni Kamati ya Fedha za Hesabu za Serikali Kuu, Kamati ya Fedha ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Fedha ya Hesabu ya Mashirika yetu ya Umma. Tunaendelea na uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na atakayefuata ni Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Zungu ajiandaye.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia kwa jioni ya leo, jioni ambayo tunachangia na Serikali inawakilishwa na watu wawili, Serikali inawakilishwa na Waziri mmoja na Mwanasheria Mkuu wake, lakini wengine wote wapo kwenye kikao cha kujifungia kujadili mustakabali wa Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maadamu tunawajibika kuendelea kuchangia bila kujali uwepo wa Serikali hiyo na pengine tukipendekeza zaidi kutokuwepo moja kwa moja kwa Serikali hiyo, naomba nielekee

kwanza kuwapongeza sana Wenyeviti wote wa Kamati zetu za Bunge za Fedha za Umma, wamefanya kazi nzuri na ninajua kwamba kazi yao itakwenda kuwa na manufaa kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ambalo ningependa Watanzania waelewe maadamu Serikali yenyewe haipo sasa ni lazima tuzungumze na Watanzania na kwamba Watanzania waelewe kwamba tunachokijadili ama ambacho taarifa zilizowasilishwa na Wenyeviti wetu wa Kamati hizi Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Daktari Augustino Mrema na Mheshimiwa Kabwe Zitto zinajadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha Juni 2009/2010. Kwa hiyo, Watanzania waelewe tu kwamba tunajadili mambo ya miaka miwili au mitatu iliyopita siyo ambayo ni *current*. Kwa hiyo, madudu mengi yanayozungumzwa kwenye taarifa hizi yametokea katika Bunge lililopita Bunge la Tisa wala siyo Bunge la Kumi. (*Makofii*)

Mheshimwia Naibu Spika, sasa bado tumepata vilevile taarifa ya CAG ya mwaka 2010/2011 ambayo hiyo itajadiliwa mwaka ujao kwa mujibu wa taratibu na utamaduni wetu wa Bunge na yale yote yanayotokea katika matumizi ya Serikali ya leo *current affairs* yatajadiliwa mwaka wa keshokutwa which means ni mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeweza kuona madudu, Wabunge wameweza kubaini madudu makubwa kama haya na hatua zilizochukuliwa ni hatua ambazo ni dhaifu mno ambazo haziwaridhishi Wabunge hadi kufikia hatua ya Wabunge kusema Serikali hii iwajibike na Mawaziri wawajibike, mimi nachelea kusema kwamba Serikali hii siyo Serikali sikivu, haisikii malalamiko ya Wabunge, haisikii malalamiko ya Vyama vya Upinzani, haisikii malalamiko ya Watanzania na haijali matatizo ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi yasiyo ya malengo na matumizi yasiyo na maana kamili ndiyo tatizo kubwa la Serikali yetu kuwa na matumizi makubwa kuliko mapato, lakini mbali ya kuwa na matumizi makubwa kuliko mapato, Serikali hii vilevile imeendelea kuwa na ubadhirifu wa kutisha na ugonjwa huu sasa unakuwa ni kansa kwa sababu matumizi ni makubwa mno na yale kidogo yanayokuwa ni halali basi yanatumika vibaya, sasa tunajiuliza kama Serikali inashindwa kusikia kilio cha Wabunge ambao wana wajibu wa Kikatiba wa kuihoji Serikali na kuisimamia Serikali watasikiliza kilio cha nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Serikali haielewi ugumu wa maisha ambao Watanzania wanayapata leo kutokana na uzembe na ubadhirifu unaofanywa ndani ya Serikali, sasa katika misingi kama hii kwa kweli

CHADEMA na vyama vingine vyatupu na Watanzania wote wanaoitakia mema nchi hii tutawaomba Watanzania wachukue hatua za ziada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu pengine inaelekea tiba hii inashindwa kupatikana kuitia Bunge, kwamba kuitia Bunge Serikali haijali, inaambiwa haijali, inaambiwa haichukui hatua, Serikali inaambiwa inalindana na kama ni utaratibu kulindana, basi labda tukubaliane kwamba Serikali hii imetuanguisha, inaweza ikawa na uhalali wa kisheria wa kuwepo madarakani lakini ikakosa uhalali kwa raia wa kuwepo madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa Watanzania wamesikia Wabunge hapa wanasema, Wabunge wengine wa Chama cha Mapinduzi wanasema tukaonane kwenye *caucus* ya chama chetu yaani kwenye vikao vyatupu chama, kwamba tunakwenda kuweka rehani maslahi na mustakabali wa Taifa hili kwenda kwenye kikao cha chama, na ndiyo sababu unaona Waziri Mkuu na Mawaziri wake wengi wametuletea Mawaziri wawili kutusikiliza kama vile ni utani, wao wapo kwenye kikao cha chama wakati wanastahili kufanyakazi ya wananchi hapa ndani ya Bunge. Tunasema hii ni dhara! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dhara kwa Watanzania na hili ni la Watanzania tuna kila sababu yak *u-ask for regime change* katika nchi hii, hii nchi sasa ni wakati wa kuibadilisha Serikali, hii Serikali haina dawa nydingine yoyote inayoweza kuisaidia kupona ama kuokoa kansa iliyokuwanayo zaidi ya kuibadilisha Serikali hii katika ujumla wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi tangu nchi hii imepata Uhuru na Bunge limeanza kuoneshwa kwenye televisheni sijawahi kuona siku moja Serikali yote na Wabunge wake wamekimbia Bungeni wamebaki watu sita wa kulinda viti na ile nafasi ya chama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika misingi hii, hii ni historia, lakini nasema *party caucus* ya chama kinachoongoza Bunge ni kitu cha hatari sana, kwa *party caucus* ya chama kinachoongoza Serikali kuflikia hatua ya kukimbia na kutuachia sisi Bunge ina maana hawa wapo tayari kutuachia ikulu na wapo tayari kutuachia ofisi tuweze kui-control. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Watanzania wenzetu huko kote ambako mpo mnatusikiliza muelewe huku tunapambana kwa sababu Serikali hii kwa kweli siyo sikivu, Serikali hii inachanganyikiwa katika mambo

tunayoyaona hapa ni mambo ambayo ni *unprecedented* ni mambo hayajawahi kutokea tena katika historia ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa, watu hapa wanakopa bila kujali analipa nani, na sasa tumekopa katika taasisi za fedha za Kimataifa, tumefikia *saturation point* tunaanza kukimbia haraka haraka kukopa kwenye mabenki ya biashara ambayo riba zake zipo juu sana na matokeo yake Deni la Taifa limeng'oka kutoka trillioni kumi kwenda trillioni 14 katika kipindi cha mwaka mmoja. Sasa tukiendelea na *trend* hii kwa miaka mingine mitatu tukaiacha Serikali hii madarakani kwa miaka mingine mitatu huenda deni hili likafika trillioni 20 ama 25 na watakaolipa ni watoto wetu, watoto wa watoto wetu na wajukuu wa watoto wetu. Ni kwamba watu wanakopa kwa sababu hawalipi na pengine hawana utamaduni wa kulipa. Inflation inapanda, mfumuko wa kodi, lakini bila kujali ushauri wa Wabunge na ushauri wa watalaaam mbalimbali wa mambo ya kiuchumi bado tunaendelea kutoa misamaha ya kodi kwa makampuni hayo hayo mengine ambayo yanatutapeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika hakuna *solution* ambayo ipo inaonekana katika siku za karibuni na kama wependwa Watanzania wenzetu wanategemea kwamba kuna mabadiliko yoyote, kuna unafuu wowote utakaotokana na maisha, kuna unafuu wowote wa gharama za maisha utakaotokana na Serikali hii iliyopo madarakani kuendelea kuwepo madarakani, hakika mwaka 2015 maisha ya Watanzania yatakuwa magumu mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha ziada ambacho ningependa kikitahadharisha katika Bunge hili, kwa utamaduni ambao nchi yetu inaongozwa sasa hivi, kwa utamaduni wa Serikali kutokusikiliza, kwa utamaduni wa Serikali kulindana, kwa utamaduni huu ambao unapelekea kuwafanya Watanzania maisha yao yazidi kuwa magumu zaidi, nina hakika mtawafanya Watanzania watarudi barabarani na mimi kama Mwenyekiti wa CHADEMA nawakumbusha kabisa Watanzania huku ndani ya Bunge hawatusikilizi na ninaomba Watanzania waelewe hatusikilizwi, lakini tukiandamana barabarani tunasikilizwa, kwa hiyo, sasa ni lazima tufanye *regime change* katika nchi hii, wananchi ni lazima wafanye *uprise*, waandamane, pengine Serikali itasikia na itaweza kuwachukuliwa hatua wale wote ambao imeshindwa kuwachukulia hatua kwa miaka mingi mfululizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ingekuwa Serikali inasikiliza vilio vya Wabunge hapa leo kutoka pande zote za Chama cha Mapinduzi, na Serikali yake na kutoka upande wa Upinzani kisingekuwa kilio ambacho kimefika kwa *level* ambayo imefika leo. Kwa hiyo,

tunawaomba Watanzania wenzetu kwamba wakati Wabunge wanaendelea kuweka pressure ndani ya Bunge nao waendelee kuweka pressure huko uraiani ili hatimaye kieleweke. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (Makofi)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili jioni hii niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hotuba za Kamati tatu zilizowasilishwa hapa Bungeni tangu jana. Naomba kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati hizo na Wenyeviti wao waliowasilisha vizuri ripoti za Kamati zao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kusema na kuijulisha Serikali kuwa kuzuia ni bora kuliko kuponya na woga wa mambo ya hasara ni namna nyingine ya ushujaa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa sana la kutowajibika katika ahadi za Serikali kwa wananchi, hali hii inapelekea wananchi wetu kupunguza imani kubwa na Serikali na hivyo kutuletea hata matatizo baadhi ya viongozi ambao hatuko juu tupo katika *level* ya kawaida kama Wabunge. Wabunge kwa namna moja ama nyingine wamekuwa wakiishauri Serikali na kuiomba Serikali itatue matatizo haraka yaliyo mengi lakini utekelezaji wake umekuwa mdogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano iko mingi, tumeona baadhi ya Mawaziri wetu wakitofautiana kwenye hoja, tumeona namna ambavyo wananchi wetu wanavyoshindwa kutuamini sana na hata kwa namna nyingine tumeona Serikalini wasipoaminika kwa mashirika yaliyo chini yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwamba tubadilike katika ngazi yote kwa nia nzuri ya kujenga nchi yetu, hata mambo yanayotokea kule Tandahimba, asubuhi mimi nimeongea hapa kwa Waziri Mkuu ni urasimu tu usio na msingi unawasababishia wananchi kuumia bila sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili Wabunge wa Mtwara tulianza nalo tangu mwezi Februari tukiwa hapa Bungeni tulipoona kuna kila dalili kwamba tatizo la wakulima kupata malipo yao ya korosho lingewaathiri sana. Lakini tangu Februari mpaka leo watoto wao wameumia kwa kutokwenda shule, huduma nyingine za kijamii zimeshindwa kapatikana kwa *long procedure* tu ya kutatua mambo ambayo haikuwa na ulazima wowote, naomba Serikali sasa waamke na kwa sababu Waziri Mkuu leo hapa ametoa kauli angalau inayotia matumaini ili mambo yale yamalizike. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tamko lile liwe sababu ya Watendaji wetu kuamka kwa sababu kwa namna moja ama nyingine mimi Mawaziri siwalaumu sana lakini watendaji ni tatizo hata Mawaziri wanapowaagiza hawafanyi inavyotakiwa, nami natoa rai hapa kwamba tubadilishe utaratibu, hawa Makatibu Wakuu na watendaji kwenye Idara zetu au Mashirika yetu sasa wasiteuliwe na Rais, Mawaziri tu ndiyo wateuliwe na Rais, wao kuwe na utaratibu wa kuwateua ili pale wasipowajibika Mawaziri waweze kuwajibisha ipasavyo na siyo hali iliyopo sasa ambayo inasumbua ya kutoleta tija kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo *MSD*, wakati *MSD* ndiyo tunawategemea itusaidie kupata huduma za dawa na vifaa vya tiba kule kwenye vituo vyetu vya afya na vijiji, lakini Serikali inadaiwa na *MSD* jumla ya shilingi bilioni 43; hivi tutegemee nini? Tutegemee utendaji mzuri wa *MSD*, tutegemee Watanzania kuboreka kwenye afya zao huku dawa zikiwa ni za shida kwenye *level* ya vijiji ambako Watanzania ni wengi, tuna haja ya Serikali ya kujiangalia mara mbili mbili kwenye eneo hili ili *MSD* ifanye kazi yake inayostahili na hivyo kuboresha maisha na afya za Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la manunuzi, kwanza niseme asilimia 70 ya bajeti ya Serikali huwa inaenda kwenye manunuzi ya vifaa na huduma, lakini maeneo haya ndipo sehemu kubwa ambayo imekuwa ikitumika sana na watendaji wetu au kuwaibia Watanzania. Mifano ni mingi, kwa mfano kwenye ripoti ya Mwenyekiti wa Hesabu ya Mashirika ya Umma utaona *TANESCO* imefanya manunuzi yasiyofuata taratibu na Sheria ya Manunuzi yanayofikia bilioni 258 katika mwaka wa fedha 2009/2010, hili ni jambo gani? Hizi ni nyingi sana lakini ujanja ujanja tu, lakini hata kule *TBS* (Shirika la Viwango), kumekuwa na matatizo makubwa, utaratibu wa kupata wakala wa kukagua magari nje na kwa wale wenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ukisoma ukurasa wa 14 mpaka ukurasa wa 15 yapo mambo mengi pale yanatajwa, hii ni dalili ya kutosha kwamba maeneo haya ndiyo yanayotumika kubamiza, kuleta ubadhirifu, watu kufaidi kivyao vyao huku Watanzania wengi wakiendelea kuumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaje kwa haraka haraka tu, kwenye ripoti inasema Ofisi ya CAG iligundua kuwa baada ya *TBS* kutoa tangazo la kwanza kuhusu ukaguzi wa magari iliweza kuchagua kampuni moja inayoitwa Jay kuanza kukagua magari kuanzia mwaka 2002, hakukuwa na tangazo lingine lilitolewa kati ya mwaka 2002/2005 lakini cha kushangaza ni kwamba mwaka 2003/2004 wakala mwingine anayeitwa *Total Automotive* ya Dubai ilianza kukagua magari. Utaratibu uliotumika

kuchagua *Total Automotive* ulishindwa kutolewa ufanuzi wa kina na Mkurugenzi wa Ubora wa *TBS* kwa kushindwa kutoa maelezo kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine tunaambiwa kwamba *Quality Motors* ya *Hong Kong* haikuwa na vifaa vinavyostahili lakini alipewa leseni ya kukagua magari. *Quality Motors* hiyo hiyo ya *Hong Kong* hawakuwa wakiwasilisha tozo kwa *TBS* kama ilivyooneshwa kwenye tangazo lakini kila mwaka wamekuwa wakiendelea kupewa leseni mpya, kwa nini iwe hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sehemu hii ya manunuzi imekuwa tatizo na chanzo cha kutuletea kutoaminika kwa Watanzania wenzetu waliotupa nafasi ya kuwatumikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningetoa rai kwa Serikali tubadilike sana, mambo mengine ya maandamano, ghasia, uvunjifu wa amani unatokana na Serikali kutofanya kwa wakati na kutozurekebisha matatizo kwa wakati na kutochukua hatua kwa wakati, maana kwa mfano yale niliyoyasema Tandahimba hivi kama wananchi wangalipwa korosho zao kwa wakati mtu angeandamana? Yule mwanasiasa mwingine aliyeenda kupiga maneno kule angeandamana? Hakuna! Maana asingekuwa na base ya kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Mungu akubariki. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru sana Mheshimiwa Juma Njwayo, najaribu kuangalia kama upo katika orodha yangu ni vizuri ukakaa mahala pako, nisipokuona mahala pako basi inabidi nikuruke. Mheshimiwa Thuwayba Muhamed atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani zangu kwa kunipa nafasi hii na mimi walau nichagie machache katika ripoti hizi za Kamati tatu zilizoletwa mbele hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru hawa Wenyeviti wetu wa Kamati hizi tatu ambao wameweza kutoa ripoti zao nzuri zenye kueleweka na kuchambulika kwa vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia kwanza kuhusu bajeti. Bajeti nzuri ni ile yenye matumizi mazuri, bajeti mbaya ni ile

ambayo matumizi yake huwa si mazuri au mabaya. Bajeti yetu ina changamoto nyingi na halafu ni tegemezi, kwa nini nikasema hivyo kwa sababu tukiangalia bajeti yetu asilimia 40 zipatikane kutoka kwa wahisani na asilimia 60 ni Serikalini. Sasa hizi asilimia 40 zilizotoka kwa wahisani ni fedha ambazo Serikali imeweka kuwa zitusaidie katika miradi mbalimbali. Fedha hizi huwa haziji kwa wakati kwa hiyo, miradi yote ya Serikali inaweza ikaharibika kwa kutopata fedha hizi au zikija huwa zinakuja nusu nusu. Tukitazama Serikali yenyewe asilimia 60 inayotoa Serikali pia inasuasua kwa sababu utaona Wizara nyingi hazipati fedha ambazo walizokuwa wanazihitaji. Hii inatokana na kutokuwa na fedha hizi za asilimia 60 kwa hiyo, hapa inakuwa ni matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kujua tu mie Wizara ya Fedha au Waziri huyu wa Wizara ya Fedha ambaye anawagawia mafungu mbalimbali Mawaziri wenzie kwa kuendesha shughuli zao huwa kweli anawapa kiasi kama kile anachokichukua yeye? Hapa ninasema kwa sababu inaweza kuwa yeye anachukua fedha zilizokuwa nzuri ambazo zitaweza kumfanyia shughuli zake zote bila matatizo na kuacha wenzie wako katika hali mbaya ambaa fedha hazipatikani. Halafu sisi tunalaumu Wizara haifanyi hivi, Wizara haifanyi hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa la kufanya ningeomba mimi tuwe tuna mfumo mwingine ambaa mfumo huu unaweza ukatusaidia katika kutekeleza bajeti zetu. Mfumo huu ni ule ambaa CAG na Kamati ya PAC imeweza kuzungumza kwanza tuweze kuzishughulikia hizi Wizara katika mafungu yao mbalimbali tukishapata, nini wanataka kiasi gani wanahitaji halafu ndio tuje tuiangalle Bajeti ya Serikali Kuu inataka nini. Hivi itakuwa ni vizuri zaidi kwa sababu yale mapungufu yote ambayo yamejionyesha katika mafungu mbalimbali ya Wizara mbalimbali yameweza kurekebishwa na kupitishwa na Bunge hili na baadaye kinakuja kitu kikubwa ambacho ni kizuri wandakichukua Wizara ya Fedha na wao wanaweza kuleta bajeti iliyokuwa nzuri, bajeti ambayo itaweza kuwasaidia kila mmoja katika shughuli zake atakazoweza kuzifanya. Hilo ninaliomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuja sehemu ya pili, kuna fedha hizi ambazo tumesema matumizi mabaya ya fedha. Nataka kuzungumzia kidogo kuhusu matumizi mabaya ya fedha, matumizi mabaya ya fedha yamejionyesha wakati tulipokuwa tukiangalia Fungu la Wizara ya Afya. Kuna fedha bilioni 1.101; fedha hii zimetumika katika sherehe au nizungumze hivi kwamba shughuli hizi za sherehe za kila siku zinazofanywa tuzipunguze. Kwa sababu fedha nyingi zinapotea katika sherehe. Ukiangalia utaona kwamba tuna sherehe ya Sabasaba, tuna

sherehe ya Nanenane, tuna Sherehe ya Muungano, hivi karibuni tumefanya sherehe ya Uhuru, zote hizi zinahitaji fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sherehe ya Nanenane, Wizara moja tu ya Afya imetumia bilioni 1.101, tuangalie tuna Wizara ngapi, tuna Wizara 30, Wizara 30 hizi zinakwenda kwenye bilioni 33.03 zilizotumika tutakuwa kiasi gani kila siku tunatumia fedha hiki, tuna mambo mengi ambayo tunataka kufanya. Tukija katika sherehe ya Uhuru iliyofanywa shilingi bilioni 56 zimetumika kwenye Sherehe ya Uhuru mpaka ya hayo tuangalie keshokutwa tukijaaliwa tarehe 26 Aprili, tutakuwa na Sherehe ya Muungano sijui tutatumia kiasi gani. Sasa fedha hizi zote tunazozifanya hivi ni fedha za walalahoi, wao hatuwashughulikii, wao hatuwahangaikii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa hiyo haitoshi kuna nyumba ya Waziri iliyokarabatiwa kwa shilingi milioni 480 hiyo ni nyumba ya Waziri imekarabatiwa. Mimi najiuliza nyumba hii ya ghorofa, kama ya ghorofa ina ghorofa ngapi? Nyumba hii ya chini kama ya chini ina vyumba vingapi na ilivyokarabatiwa maana kila nikikaa siwezi kufahamu milioni 480 nyumba moja ya Waziri. (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Waziri nani huyo?

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni nyumba ya Waziri wa Afya. Je, Mawaziri hawa wote tuliokuwa kama tukisema tukarabati nyumba zao itakuwa ni kiasi gani? Jamani fedha tunazozitumia zitakuja kutupa matatizo kwa sababu hapa Bara tunasema shule hazina madawati, shule hizo hizo hazina vitabu, shule hizo hizo hazina *laboratories*. Tukija katika hospitali, hospitalini hakuna dawa, hakuna vifaa. Jana nilikuwa nasikiliza taarifa ya habari kuna hospitali moja ya Tumbi haina X-ray. Je, jamani fedha hizi zote kwa nini tunaziharibu? Hatuzitumii kwa mambo haya? Nafikiri ni vizuri tukaweza kutumia fedha kwa uangalifu. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kwa kunipa fursa ili kusudi niweze kuchangia taarifa za Kamati tatu ambazo zimewasilishwa hapo jana. (Makofi)

Kwanza kabisa naomba nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati tatu ambao waliwasilisha taarifa zao jana kwa sababu zimesheheni mambo ambayo kimsingi kama tunaweza tukafuata ushauri wake tunaweza pengine kuokoa mamilioni/mabilioni ya shilingi ambayo yamekuwa yakipotea mikononi mwa watu wachache. Naomba pongezi

za pekee ziweze kuwaenda Wenyeiti hawa pamoja na Wajumbe wote wa Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumukuu mtu mmoja ambaye alipata kusema; “unaweza ukawadanganya watu fulani kwa wakati wote na wakati wote,” unaweza ukawadanganya watu fulani, lakini huwezi ukawadanganya watu wote kwa wakati wote.

Naomba Serikali mjaribu kusoma upepo na alama za nyakati. Zama hizi siyo zama za kuja kumwambia mtu kwamba hii rangi ni nyekundu wakati ni nyeusi au hii ni nyeusi na wakati rangi ni nyekundu na wakati watu wote tuna akili timamu. Mwenyezi Mungu ametujalia milango mitano ya fahamu ili kusudi tuweze kutambua mambo mbalimbali, tuna macho na tuna masikio. Tunaweza tukasikia na vilevile tunaweza tukaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wanaposimama katika nyakati tofauti tunapokuwa ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge wanalamika fedha za miradi ya maendeleo hazifiki katika Halmashauri zao, lakini hata zile kidogo ambazo zimekwenda katika Halmashauri bado zinachakachuliwa kwa kiasi kikubwa. Wanapajaribu kutoa *feedback* kwenye Wizara kwa maana ya Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi mbalimbali wa Wizara zetu bado *feedback* inakuwa ni hali ambayo ni ya kusikitisha. Imefika mahali Waheshimiwa Wabunge, wengi wamelalamika tangu jana na hata leo na wananchi wameanza kuona Bunge linafanyakazi kweli kweli. (*Makofii*)

Naomba nisome ujumbe mmoja wa mtu mmoja alinitumia anasema; “Kaka naona mko kazini kweli leo, washikeni sawa sawa hawa Mawaziri hawajui kuwajibika na wanawaona Wabunge wengine kama mazuzu.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni *message* ya mtu kwamba imefikia mahali Waheshimiwa Wabunge, tunatafsiriwa kama ni mazuzu pale ambapo tumekuwa tunapitisha Bajeti za Serikali halafu utekelezaji wake unakuwa ni wa kusuasua, matatizo chungu nzima huko tunakotoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi sipendi na sioni furaha kwa kweli kuendelea kuitwa mazuzu au kuna Mbunge anapenda kuitwa hivyo? Sijui Wabunge wenzangu wa kutoka Chama cha Mapinduzi, wa kutoka CHADEMA, NCCR, CUF, TLP na UDP kuna Mbunge hata mmoja ambaye anapenda kuitwa zuzu? Sidhani kama yupo, kama yupo ana matatizo yake binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo taarifa za Wenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Daktari Augustino Mrema, Mheshimiwa Kabwe Zitto pamoja na Mheshimiwa John Cheyo wameeleza tatizo la mishahara hewa ambayo imekuwa inalipwa katika Halmashauri zetu na hata katika maeneo mengine takribani shilingi bilioni moja na kidogo zimekuwa zinapotea kwenda kwenye mishahara ambayo ni hewa. Natoa mfano mdogo tu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, ukisoma taarifa ya Hesabu za Serikali za Mitaa takribani shilingi milioni 63 imekuwa ni mishahara hewa. Hii siyo kosa la bahati mbaya ni kosa la makusudi kwa sababu hawa watu wana taarifa. (*Makofi*)

Sasa leo tunapokuja kujadiliana hapa Wabunge wamelalamika fedha kidogo ambazo zimekuwa zinakwenda huko kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni kidogo, hata fedha ambazo tayari bajeti inajulikana kwamba ni kwa ajili ya mishahara wafanyakazi wengine wamekufa, wengine wametoka tu wamekwenda kwenye shughuli zao mbalimbali, hawapo kazini kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi, lakini bado zile fedha zinachakachuliwa. Mawaziri wanatupiga danadana wanatuambia watachukua hatua, moja ya Mawaziri ambao nawaheshimu ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri lakini kauli yake ya leo ya kusema kwamba watachukua hatua tuwalinde, hizi kauli zimekuwa zinajirudiarudia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaweza tukaendelea kulalamika na kupiga kelele kila siku mahali hapa lakini tusifikie suluhisho la kudumu. Tutaendelea kulalamika lakini hatutafikia suluhisho la kudumu kama hatuwezi wenyewe tukaamua kuweza kurudi kwenye sheria, kanuni na taratibu ambazo zinatuongoza kwenye kuchukua hatua dhidi ya Mawaziri ambao wamekuwa hawawajibiki kikamilifu ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge vilevile. (*Makofi*)

Kauli hizi/hotuba ambazo zimekuwa zinajirudiarudia zimekuwa ni za mara kwa mara. Ifike mahali ndugu zangu tufanye maamuzi magumu kama walivyofanya Taifa la Ujerumanî miaka 1870. Tumekuwa tunazungumza hapa wakati Chancellor Bismark alipozungumza Taifa la Ujerumanî lilikuwa linakabiliwa na matatizo makubwa ya kiuchumi akaona na baada ya kukaa na washauri wake aliquja na kauli moja akasema *the great question of the day shall not be solved by speeches and resolutions but only by iron and blood.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanatoa maeleo yale yale, suluhisho ni lile lile la aina moja sasa akaona kwamba tunafanyaje, tumvamie Mfaransa twende kuchukua yale majimbo ambayo yalikuwa ni muhimu sana katika masuala ya madini.

Sasa leo hii tunaposimama hapa na kuzungumza wale wote ambao wamekuwa wanaharibu Serikalini wakamatwe ikiwezekana utaratibu wa kisheria ufuatwe na hata wanyongwe hadharani ili kusudi iweze kuwa fundisho kwa watu wengine. Watu wanasema vijana wamechanganyikiwa, hatujachanganyikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza kabisa tukiwa tunatambua kitu gani ambacho tunakisema. Tunasimamia na kumaanisha hiki ambacho tunakizungumza, haiwezekani ATCL ni matatizo, TRA ni matatizo hata leo jambo la kusikitisha Mawaziri wengine wanachakachua kauli za Wabunge hapa hapa Bungeni tumekaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano Waziri wa Nchi, amechakachukua kauli ya Mheshimiwa Deo Filikunjombé alipozungumza kwamba Mawaziri wengi ndio ambao wanatafuna nchi yetu, yeye akasema kwamba amesema Mawaziri wote, siyo kweli. Mheshimiwa Waziri wa Nchi itakuwa ni vizuri iwapo kwa kweli utaliomba Bunge na Watanzania radhi tumefuatilia mpaka kwenye *Hansard* tunayo ulichokifanya ilikuwa ni kumchonganisha Mheshimiwa Deo Filikunjombé pamoja na Mawaziri wenzako kitu ambacho hujalitendea haki Bunge hili. Sasa kama mnachakachua kauli ambazo zipo wazi na tuna macho na masikio tunasikia kwenye haya mengine ambayo hatuyaoni huko kwenye makaratasi mmeatamia, mnatuchakachua na kudanganya kwa kiasi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena unaweza ukawadanganya watu wote kwa wakati fulani na wakati fulani unaweza ukawadanganya watu wote lakini siyo kila wakati utawadanganya watu wote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hivi nikiwaomba Mawaziri wajiu zuru hasa wale ambao tukifanya uchunguzi na wote wale watakaoonekana wana matatizo wawajibike mtaunga mkono hoja?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi naomba tushikamane, tutapiga kelele na kulala mahali hapa lakini matatizo kwenye majimbo yetu yataendelea na Miswada mbalimbali ambayo haitupi meno Waheshimiwa Wabunge, itaendelea kuja ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani za dhati kabisa kutoka kwangu na wananchi wa Kilwa kwa Kamati ya Nishati na Madini, inayoongozwa na Mheshimiwa Januari Makamba. Lakini vilevile naomba nitoe shukrani kwa Kamati Ndogo ya Nishati na Madini iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Selemani Zedi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru sana wajumbe wenzangu wa Kamati ya POAC tukiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Kabwe Zitto.

Leo hii nazungumza katika Bunge hili tangu dunia ilipoanza kwa mara ya kwanza wananchi wa Kilwa wamepata gawio la fedha za gesi. Nawashukuru sana Wabunge wote waliokubali kuunga hoja mkono na sisi tunaweza kupata japo kidogo kile ambacho tulikuwa tunakistahili. Namshukuru Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake lakini na Katibu Mkuu Bwana Maswi ambaye alisimama kidete kabisa kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kusema kwamba Bunge hili liliundwa kwa kuzingatia masharti ya Kikatiba. Lakini pia Bunge limetunga Kanuni ambazo zinatumika katika kuendesha shughuli zake. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuzisome kanuni na tuzielewe. Nasema hivi kwa maana kwamba sisi Wabunge ambao tupo kwenye Kamati za *oversight* mara zote tumekuwa tunashutumiwa kwamba tunaingilia mamlaka ya Kamati nyingine, tunavuka mipaka na hii yote inatokana na kuwa tunakuwa *influenced* kwa kupewa fedha, na kuna Mbunge aliwahi kutamka ndani ya Bunge hili kwamba Kamati yetu tumepewa fedha lakini Mungu hamfichi muongo, leo imedhihirika nani ambaye anachukua fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika ripoti za CAG, ripoti zinatokana na mapungufu ambayo yanakuwa yamebainiwa na hizi Kamati ndipo ambapo CAG anafanya kazi. Hakuna kitu ambacho kimekuja tu duniani bila kuwa na chanzo.

Kwa hiyo, tunafanya kazi kwa kuzingatia misingi na hatumlaumu kumshutumu wala kumhukumu mtu yeyote na wale ambao wanapenda kukimbilia katika vyombo vyaa habari kukashifu Kamati na kukashifu Wabunge mjue kwamba sisi ambao tunawawakilisha kule tunadhalilika wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Ukiangalia ripoti hii maeneo mengi, pamoja na ripoti ya hesabu za Serikali Kuu kuna uchelewashaji mkubwa sana ambao umejitokeza kupeleka Mafungu na Kasma za Bajeti katika maeneo husika na hili ndilo ambalo linapelekea mianya ya wizi na inapelekea mianya mikubwa sana ya uvujaji wa pesa. Ukiangalia taarifa hii mpaka leo kuna Halmashauri kadhaa hazijapata gawio la Mfuko wa Maendeleo ambayo ukiangalia kwenye ripoti hiyo ya PAC inaonyesha kwamba kutokupelekwa kwa pesa mara zote kumekuwa kunachangia kwa miradi mingi kukwama na inapokwama hii miradi inatoa mianya ya watu ambao si waadilifu kutumia vibaya hizi pesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye taarifa hiyo, kuna maeneo mengi ambayo yanaonekana kabisa kwa namna za makusudi watendaji wamefanya *duplication* ya miradi, lakini mimi nasema pamoja na mambo mengine yote tuangalie pia mfumo wa kibajeti. Mfumo wa bajeti zetu tunaangalia uwiano na tunapeleka pesa nyingi sana katika maeneo ya mijini tunapopeleka pesa, hata kama hawana mahitaji nazo watatengeneza tu kitu chochote ambacho hakipo matokeo yake sasa pesa zile zinaingia katika mfumo wa kutafunwa. Huu ndiyo ukweli uliokuwepo, hakuna haja ya kuficha na ni jambo ambalo limedhihiiri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye ripoti ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, lipo jambo ambalo mimi linanikera sana. Ripoti ya CAG ukienda kwenye ukurasa wa 40, 4.16 inasema hivi; "*Communication inefficiencies between Institutions, Ministries, Ministry of Finance, PMOs Offices.*" Taasisi ambazo zimetamkwa humu na CAG, kwenye Kamati yangu mimi nataka nitoe mfano mmoja tu, Mwenyekiti wa Chuo cha Tiba Muhimbili ni Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Zarina Madabida alikuja kwenye Kamati akiwa analalamika kwa kipindi cha zaidi ya miaka tisa Serikali imeshindwa kujibu maombi ya Chuo ili zitolewe pesa bilioni 1.6 kianzishwe Chuo cha Uugazi pale Mloganzila. Tulikuwa tunaelekeea kupoteza mradi wa zaidi ya shilingi bilioni 134 ambazo tumezipata kutoka kwa Wakorea. Barua inaandikwa leo, halijibwi mpaka miaka mitatu inayokuja, hivi tunataka Serikali hii iende wapi? Yule mama alivyokuja kwenye Kamati na si jambo zuri kusema lakini machozi yalimtoka. Hii tuone ni jinsi gani ambavyo Serikali inasita kuchukua maamuzi katika mambo muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ambao tumeupata hapa ni mchache, lakini niseme tu pamoja na mambo mengine yote kwa kuonyesha ni jinsi gani Kamati inafanya kazi, tunashukuru Serikali imekubali kupokea mapendelekezo yote ambayo tumeyatoa kuhusiana na General

Tyre. General Tyre imerudi na sasa tunaangalia utekelezaji kwa vitendo na si kwa maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo ambalo nimelizungumza awali kuhusu utendaji mpaka hii leo, tumezungumza jana hapa Mwenyekiti wakati anawasilisha ripoti yake. Kwa kipindi cha miaka kumi, Serikali imeshindwa kuunda Bodi ya Wakurugenzi kwa Shirika la Masoko la Kariakoo. Hivi ni kweli kwamba haifahamiki kwamba Bodi ile haipo active? Nani ambaye anaipa mamlaka *management* kutengeneza bajeti? Nani ambaye amempa mamlaka leo *management* kwa ajili ya kuingia ubia kwa kuendeleza eneo la soko lile? Bado tumekaa hapa, majibu hayaji. Tunategemea kitokee nini ili muweze kuchukua hatua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ambalo nilitaka kusema; Mheshimiwa Mbunge wa Rufiji hapa alizungumza yapo mapungufu ambayo tunayaona katika utendaji na utekelezaji wa shughuli zetu za kila siku. Tunaweza tukasema kwamba tukae mwaka mzima hapa, lakini isije ikawa ni sawasawa na tunakamua chui maziwa, tutafanya kazi kubwa, lakini kitakachotokea hakitakuwa kile ambacho tunakitarajia.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia katika mada hizi tatu za Kamati zinazosimamia Serikali. (*Makofi*)

Kwanza naunga mkono hoja zote zilizotolewa na Kamati hizi tatu kwa kuzingatia kwamba ndizo zinazosimamia masuala ya fedha katika Serikali yetu. Nianze kwanza kutoa pongezi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya hasa hasa ukizingatia kwamba anafanya kazi kubwa sana katika Serikali kwa kukagua Serikali Kuu, Halmashauri, Mashirika ya Umma, Mikoa na kadhalika. Kwa kweli kazi wanayoifanya ni kubwa sana na inabidi wapongezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hizi tatu hazina meno, tunaongea hapa wee, tunabwabwaja hapa wee, lakini mwisho wa siku hakuna chochote kinachofanyika, hatuna meno. Lakini wenzetu kwa mfano Uganda, Kamati ya Hesabu za Serikali inapokwenda kwenye kikao chake kukagua hizi hesabu, wanakuwepo na polisi. Kwa hiyo, Afisa Masuuli au Mtendaji ye yeyote akionekana kwamba amefuja fedha pale pale askari anaambiwa mchukue huyu nenda nae. Lakini sisi hatuna meno, tupo tu hapa tutaongea, tutaongea mpaka mwisho hakuna kitakachofanyika. Tulipitisha Azimio hapa Bungeni ya kusema magari haya yasikagulie nje ya nchi, yakaguliwe hapa hapa nchini, hakuna chochote kilichofanyika, huo ni mfano mmojawapo. Kwa hiyo, mimi nasisitiza kwamba Kamati hizi

tatu ziwe na meno ambayo kwao yanaweza kufanya maamuzi ya papo kwa hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali yetu inashindwa kufahamu mali zake. Ni sawa sawa unajenga nyumba hujui ina vyumba vingapi. Nyumba ya kwako mwenyewe, lakini hujui ina vyumba vingapi, ni kitu cha ajabu sana. Serikali yetu ina mali nyingi lakini katika mahesabu yake ya mwisho hakuna chochote kinachosemwa kuhusiana na thamani ya mali Serikali ilizonazo. Kuna majumba, kuna viwanja, kuna wanyama porini, kuna barabara hizi tunazojenga kwa lami yote haya ni mali ya Serikali, lakini mwisho wa siku Mhasibu Mkuu haonyeshi mali tulizonazo katika Serikali yetu hii ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya barabara. Kamati yetu ya PAC ilitembelea mradi wa barabara ya Ndunu – Somanga. Barabara hii wakati mimi nasoma enzi hiyo bado ilikuwa ina matatizo na mpaka leo hii ina matatizo. Kamati hii ya PAC, Wajumbe wake wamesota kweli barabarani kipande cha kilometra 60 tu. Sasa sielewi tatizo liko wapi? Usimamizi mbovu, kuna Maafisa kule wa TANROADS wa Mikoa hiyo miwili ya Pwani na Lindi, hivi wanafanya nini kuhakikisha kwamba barabara hii inakwisha? Magari yanakwama njiani, mvua ikinyesha kidogo tu, barabara haiishi kila siku tunaambiwa baada ya miezi sita itakwisha, baada ya miezi sita itakwisha, lakini hakuna chochote kinachofanyika. Jamani tuwajibike. Naomba tuwajibike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imeonyesha kwamba MSD imeharibu au mwisho wa mwaka ilikuwa na vifaa ambavyo vilikuwa ni vibovu, vimepita muda wake na vingine vipo chini ya kiwango, vikatupwa vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.7, madawa yameharibika, vifaa vingine vipo chini ya kiwango, sasa hapa kwetu tunafanya dampo la kuleta hivyo vitu. Jamani mtatuwa na dawa zenu zilizokwisha muda, mtatuwa.

Sasa mimi ninachoomba ni kwamba kwa mfano hizi bilioni 4.7, ndugu zangu wa Nanyumbu wanadai pesa ya korosho tena nawashukuru sana, nawapongeza sana kwa uvumilivu wanaouonesha wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Poleni sana lakini Serikali imetamka kwamba baada ya siku mbili, tatu, mtapata pesa zenu. Lakini hizi bilioni 4.7 zingeweza kulipa hizi korosho, kwangu hakuna madawati kwenye shule za msingi, kwangu dawa ni matatizo, Wilaya ya Nanyumbu tuna hospitali pale haina vifaa, zahanati hazina dawa, vituo vya afya havina dawa. (*Makofii*)

Hizi dawa za bilioni nne zilizotupwa, zilizokwisha muda wake zingeweza kwenda kufidia pengo hili ambalo liko pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA*. *TRA* imepewa dhamana ya kukusanya kodi, lakini katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inasema Serikali imepata hasara ya bilioni 15.4 na *US Dollars* millioni 2.6 na eti *TRA* hiyo hiyo imetaka kuleta hasara hii hapa Bungeni sisi tufute. Mtaletewa, sasa hatukupata mchanganuo wake kwa nini *TRA* hasara hii imetokea lakini nawatahadharisha Waheshimiwa Wabunge kwamba kitu hiki kitakuja hapa naomba tukiangalie kwa macho mawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa. Limezungumzwa sana hapa ndani kuhusu Deni la Taifa, lilikuwa trillioni 10 sasa hivi ni trillioni 14. Lakini tunapata habari hapa kwamba baadhi ya Wizara zinatumia fedha nydingi kwa ajili ya maonyesho, kwa ajili ya anasa tu ambazo si za muhimu sana. (*Makofi*)

Sasa mimi ninachoomba, yasije yakatokea yale yaliyotokea Ugiriki. Ugiriki wananchi wanaandamana kwa sababu ya maisha magumu, kwa sababu ya deni kubwa la Taifa, naomba sana Mungu apishilie mbali kwamba jambo hili lisitokee hapa kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni, Serikali inadaiwa sana na mashirika haya ya kwa mfano NSSF, LAPF, PPF tumejenga majengo pale *UDOM*, Serikali bado haijalipa. Tafadhali sana naomba hizi fedha sio fedha za Serikali ni fedha za wanachama, kama tulikopa kujengea *UDOM* basi tuhakikishe kwamba madeni haya Serikali inalipa haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu uchache wa wataalamu katika Ofisi ya CAG. Mimi naomba sana tena sana Serikali iwape uhuru, waipe uhuru ofisi ya CAG iweze kuajiri watu wake wenyewe, ipange maslahi yake yenyele ili kazi hizi waweze kuzifanya kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sana Serikali isiingilie mamlaka ya CAG kwa sababu tulitunga hapa sheria kuipa kila uhuru na hivyo naomba wapewe kila uhuru unaowezekana waweze kuajiri watumishi wao wenyewe ili wafanye kazi kwa ufanisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu, lakini pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuchangia kidogo katika mada zilizopo mbele yetu. (*Makofi*)

Ningependa kuwshukuru pia Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote tatu hizi walioolutea ripoti ambayo tumejadili tokea jana, lakini pia shukrani zangu ziende kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutuletea mchanganuo au mambo ambayo ameyaona katika mahesabu ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika toka jana wenzangu wamejaribu kueleza hisia zao, mapendekozo yao kwa hali tofauti, kuna waliosema kwa ukali, kwa uchungu, lakini lengo kubwa kabisa ni kutengeneza au kutafuta mustakabali wa nchi yetu, ni jambo zuri. Lakini pia ningemshukuru sana, ningempongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kufanya mabadiliko ya sheria hii mwaka 2007 na kumpa mamlaka CAG kuchambua Serikali, Mashirika na Serikali za Mitaa kila kinachoendelea na baadaye kiweke hadharani jambo ambalo huko nyuma ilikuwa hakipo wazi kama hivi. Hii ni kuonyesha kabisa jinsi Mheshimiwa Rais alivyokuwa na imani kabisa na nchi na wananchi wake na kujua kuna nini kinachotendeka huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo Bunge hili tumekaa tunayazungumza mambo ambayo kwa wale waliokuwa hawana habari haya mambo siyo ya jana wala ya juzi, ni mambo ambayo yametokea miaka mingi, lakini sasa hivi kwa imani tu ya Mheshimiwa Rais akampa mamlaka CAG na ikawa ofisi yake ina mamlaka ya kuyafanya yote haya na bila kuingiliwa na kuweza kuyaleta hadharani hapa tukachumbua, tukaona kunatendeka nini, huo ni uadilifu na imani kubwa sana kwa wananchi wa Tanzania, namshukuru sana hilo. (*Makofi*)

Ndugu zangu Watanzania wote, tujue kwamba Mheshimiwa Rais na Serikali ina imani kubwa na wananchi, kuna matatizo kwangu mimi ninayoyaona ni watendaji na wenzetu wanaopewa dhamana ya utekelezaji wa mambo haya yanayozungumzwa hapa, wengi wanalamika mambo yanayotendekea kwenye Halmashauri na kule ndiyo kwenye madudu yote yanayotokea hapa. Mawaziri wamekuwa kama ni mbuzi wa kafara tu, lakini kuna Maafisa Masuuli ambao wao ndiyo wenyе mamlaka yote wanayofanya huko, wengine hata hawapiti, baadhi tunakumbuka hapa yaliyotendeka katika Wizara ya Nishati na Madini, Mawaziri walikuwa hawana habari yoyote, Katibu Mkuu akajiamulia tu yanayotendeka, tulijadiliana hapa hapa Bungeni. Sisemi

kama Mawaziri hawakosei, wanakosea kwa sababu wao ndiyo wadhamini na waswahili wana sema mkamatwa na ngozi ndiyo mwizi wa nyama. Sasa ninyi ndiyo tumewakamata na ngozi hii, kwa sababu nyie ndiyo tumewapa mifugo kulinda mifugo yetu. Tuna wajibu wa kuwasema na pale ambapo mlikuwa mnaona hakuna mtu anakusikiliza basi achia sema mimi bwana hawa watu wamenishinda na kwa mpango huu mimi siwezi kwenda, acha tumtafute mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutawaambia na mtusikilize kwa madhumuni ya kuweza kuijenga nchi yetu pamoja. Kuna kitu kimoja mimi kuna kitu kimoja kinanichukiza sana, hii mipango ya matumizi ambayo yanatumika na mashirika pamoja pia na Serikali Kuu haya mambo ambayo wanayazungumza wenzangu sana ya maonyesho, maonyesho, tunakionyesha nini? Hebu tuambieni ni kitu gani mllichokifanya kizuri cha kukionyesha. Watanzania hawataki kuonyeshwa, wana macho yao wataona wenyewe na tufanyeni tu wataona wenyewe hawataki kuonyeshwa, mtaonyeshana nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ukifanya kitu kizuri kila mtu akikiona atasema eeh, mmeonyesha kitu gani. Mimi nisingependa haya mambo ya maonyesho maonyesho kila siku, fedha zitatumika, ma-*t-shirt*, umekuwa mtindo sasa hivi watu wakikaa barazani wakizungumza tutengeneze vi-*t-shirt*. Ni mpango mbaya tu wa kuweza kutumia matumizi ambayo hayana umuhimu wowote. Tunatumia fedha bila kutegemea, bila kuangalia nini hasa madhumuni hasa yanakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kingine sitaki kukizungumzia ni suala la ATCL. Shirika la Ndege, Shirika la Ndege ni shirika la umma ambalo hujuma zimeanza muda mrefu sasa na ilikuwa lina jinamizi ambalo la huku na huku, kwa sababu Shirika la Ndege zamani liliikuwa lina shirika moja ambalo liliikuwa linaitwa DAHACO ambalo sasa hivi linaitwa Swissport, Shirika la Ndege liliikuwa lina share pale, nafikiri sina uhakika kama percent 49 na asilimia 51 mwenye Shirika Swissport na zile asilimia 49 ndiyo zenyewe zimetoka kwenye stock exchange lakini ile asilimia 51 ambayo ya Swissport haikupelekwa pale kwa madhumuni tu ya kulinda maslahi ya mtu fulani. Na mambo haya yametendeka, ni makusudi ya kuweza kuliwa Shirika la Ndege lisiwe na mtaji upande mwingine na upande mwingine watu wanajinufaisha wenyewe bila kutegemea kwamba hiki ni chombo cha muhimu sana katika nchi hii. Lakini watu wanakula fedha as if shirika halina mwenyewe.

Mimi nafikiri tubadilishe sheria, yale mashirika ambayo Serikali hata kama hisa hazikufika asilimia 50 CAG awe na mamlaka ya kwenda kuchunguza kwa sababu kwa sheria ya sasa hivi hana mamlaka ya

kwenda kuchunguza mashirika yale. Serikali ina *investments* kule lakini hatuna fursa hata ile Kamati ya Mashirika haiwezi kwenda kuchunguza kwa sababu Sheria hairuhusu. (*Makofi*)

Mimi nafikiri kuna haja ya kuweza kupitia sheria zetu na mashirika yale pia tuweze kuyachunguza kwa sababu na huko nako kuna fedha chungu mzima za Serikali zinazotumika bila ya sababu yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi tena kwenye watendaji. Watendaji wetu ndiyo hasa wanaotumaliza katika nchi hii. Kwa sababu wao ndiyo wanaoamua mambo, ndiyo wanaopanga mambo na ndiyo wanaotekeleza mambo. Fedha zinakwenda na baadaye zinaishia katika mikono yao, wawe na makampuni yao binafsi. Wawe na mipango yao binafsi kwa maslahi yao. Suala hili ni jambo ambalo mimi nafikiri huu muundo kwamba Wakurugenzi hawawezi kuwajibishwa na Mawaziri, tungekuwa na utaratibu mzuri tukabadiishi taratibu za sheria kama sheria hii inawazuia Mawaziri wasiwajibishe, basi Mawaziri wawe na fursa ya kuweza kuwawajibisha kwa maslahi ya kuweza kulinda Wizara ambazo walikuwa wanazongoza ili kusudi tuone ufanisi unatendeka na yale makusudio ambayo ni ya maendeleo ya nchi yetu yapatikane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi mchango wangu ulikuwa ni huo. Ahsante. (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mkapa.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia, nilisema kwamba Serikali imepata hasara kutokana na udanganyifu na ukwepajji kulipa kodi kwa takribani shilingi trillioni 15, taarifa ni kwamba ni bilioni 15; samahani. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba mliweke sawa *Hansard*. Nashukuru sana. Mheshimiwa Vincent Nyerere atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Filikunjombe. (*Makofi*)

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika.

Kwanza nipende kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa kunipa ujasiri wa kufuutilia yale ambayo wenzetu kwenye Kamati walikuwa wakifuutilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nichangie sehemu nyingine lakini nimeona nijikite kwenye *TBS*. Nimeshangaa sana majibu niliyoyapata jana kwenye swalii nillouliza namba 62, Wizara ikanipa majibu ya uongo na niliyakataa hapa na nikamwuliza Naibu Waziri kama tutaleta ushahidi kwamba baadhi ya watumishi wa Wizara yako wanahuksika na hizi kampuni hewa upo tayari kujiuzulu? Hakunijibu. Na nilikuwa naomba niweke wazi, tarehe 25 mwezi wa tisa mwaka 2007 MovenPick walikaa kikundi cha watoto wa mjini wakatengeneza kampuni hiyo wakagawana deal. Wakatengeneza makampuni ya ukaguzi wa magari wakisema kwamba ni makampuni ya nje, siyo ya nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *WTN* ya *UK* ya mtani wangu mmoja anaitwa Wilson Mutabazi. Kuna kampuni Dubai inaitwa JK (Jabal Kilimanjaro), mwenyewe ni Rashidi Kimanga, *Quality Garage* ya Hong Kong, mwenyewe ni Abdul Tash na Mbunge wake yuko hapa wa Mafia. *EAA* ya Japan - Prosper Nguku, Mbunge wake yule pale Filikunjombe, Jaffer Mohamed Al-Geregi, Said Aboud, Zanzibar na *Planet Automotive Shamir Thuweyn* wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nasema namaanisha ni uongo. Kwanza hakuna magari yanayokaguliwa na watu hawa. Kwenye jibu la Waziri sehemu ya jibu anasema magari mengine yanaweza kuwa na mionzi yenye athari kwa binadamu. Hakuna hata mtu mmoja anakagua mionzi kwenye gereji, zote hizi zimeshafika zingine hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003 wakati wanaanza kukagua *Total Automotive* ya Dubai ambayo inafanya kazi ya *local* kukagua magari, ilikuwa inafanya kazi vizuri sana, waliwanyima kazi hiyo kwa sababu hawakuwa tayari kutoa kitu kidogo ndiyo kampuni zingine hizi zikatengenezwa.

Kulikuwa kuna kampuni Hong Kong inaitwa *Seme Darby*, ilikuwa inafanya kazi vizuri ya Kiserikali. Kwa sababu ilikuwa inafanya kazi vizuri ya Kiserikali kwa sababu ilikuwa hawawezi kutoa kitu kidogo wakaiacha. Akapewa Bwana mmoja Kigamboni anaitwa Cassian Mbagate afanye kazi hiyo, hakuleta fedha akanyimwa kazi hiyo wakampa huyu kijana wa *Quality Garage*, hana garage hana na nashangaa tarehe 10 mwezi wa pili wakati *TBS* wanaleta ripoti hapa wakaleta picha za uongo ambazo wanatuonyesha kwamba kuna garage pale na kuna wakaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya mimi ni mwenyeji sana hapa duniani japokuwa sikuzaliwa zamani, nikawaambia watu hawa hii ni *garage* ya MM Auto part, mkiendelea kudanganya hivi tutawaumbua na CAG tarehe 15 mwezi wa pili wakapeleka ripoti nyingine. Bahati ile ripoti ya zamani ninayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hoja ilikuwa ni kwamba haya magari hayakaguliwi. Nina ushahidi kwa *chassis number* yapo magari ambayo tumeyaingiza hayakukaguliwa kwa sababu kampuni hazipo. Lakini yalitumiwa *certificate*. Bahati nzuri wakati Mheshimiwa Kabwe Zitto anawatuma Wabunge waende wakakague kama kampuni ipo waliuziwa *certificate* hata gari hawana. Hii habari ya kusema kwamba fedha nyingi za ukaguzi wa magari inazuia fedha zisiende nje ni uongo. Fedha zinaenda nje zinarudi hapa hapa watu wanagawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, inawezekana hujui. Mimi nilikuwa nadhani ungetuita wakati jana naongea na *Chief Whip* ukaniuliza nikusaidie nini cha kufanya na *the way forward*. Wewe ukang'ang'a kubisha, aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni nyingine ambayo haifanyi ukaguzi ni hii ya JAAI. Niliwahi kununua gari GX 100 ambayo ilipata usajili wa namba T410AUA, ikapewa *certificate* ya kukaguliwa na nilinunua *online*. Ikaja hapa ina matairi ya snow, nikabadilisha. Tanzania hakuna snow kama walikagua gari ile isingeingia hapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunavyosema magari hayakaguliwi tunamaanisha hayakaguliwi na kampuni hizi siyo za nje ni za watu wa hapa hapa, tunawajua mpaka wanapoishi. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kusema ni vizuri watu hawa tungewashauri wayafungue makampuni hayo hapa, wakagulie hapa ili watu wetu wapate ajira kuliko kudanganya na kupoteza fedha nyingi sana za kigeni kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia fedha ambazo makampuni haya yamekusanya tangu wameanza kukagua magari ni dola milioni 18, lakini sisi tumepata dola milioni 2.2 peke yake nyingine zote wamegawana watu wengine, halafu tumekaa tuna matatizo, shule hazina madawati. Watu wanakula hela, halafu watu wapo hapa wanacheza sarakasi na tauko, watabaki uchi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakushukuru. Naomba muda wangu nimwachie Mheshimiwa Deo Filikunjombe kwa sababu yeye alikwenda kule na Kamati, mimi nimekuwepo kule tangu miaka ya 1990 najua kila kitu na namjua kila mtu. Waziri akitaka *the way forward* nipo

tayari kumsaidia kwa sababu niliapa kusaidia Taifa hili. Nashukuru sana na naunga mkono hoja za Kamati. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vincent Nyerere. Nashukuru kwa mchango wako Mheshimiwa Deo Filikunjombe atafuatiwa Waziri Mheshimiwa Jumanne Maghembe. (*Makofii*)

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kusema kwamba hizi ripoti za Kamati hizi tatu nimezipitia na zote kwa ujumla ndani yake zinaonyesha kuna ubadhirifu mkubwa sana kwenye Serikali za Mitaa, kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma kwenye mashirika yetu ya umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza nashangaa kwa maneno yanayosemwa kutoka jana na leo mpaka sasa hakuna Waziri hata mmoja aliyejiuzuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unafika mahala unashangaa kwa sababu tunasema hii ni Serikali sikuvi, Watanzania wanaona, mambo yenye ndiyo haya, kila kitu ushahidi upo. Lakini na huu ndio ushahidi kwamba tunasema hapa kila siku wanaona mambo yale yale. Mambo hayaendi kama kawaida yao kwa Mawaziri wetu na kwa hawa watendaji wetu haya tunayoyasema ni kelele za chura ambazo hazimnyimi tembo kunywa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza nashangaa sana, nilisema leo asubuhi nchi yetu inatafutwa, nchi yetu inaangamia, sote tunaona, Watanzania wanashuhudia. Nimesema asubuhi wanaofanya nchi yetu iangamie, wanaofanya Taifa letu liangamie; wanaofanya ubadhirifu huu mkubwa utokee ni Mawaziri wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuliopewa dhamana baadhi yetu siyo waaminifu, hatuwatendei haki Watanzania waliotutuma. Baadhi ya Mawaziri mnafanya maamuzi kwa maslahi yenu binafsi na siyo maamuzi ya kuwatumikia Watanzania waliotupatia dhamana ya kutuongoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahala tuisubiri upinzani waseme. Nchi yetu hii ni ya kwetu sote sisi. Nchi hii siyo mali ya CCM, Tanzania ni mali ya Watanzania wote. Tunapoona mambo hayaendi sawasawa ni lazima tuseme, tunajua mnalindana, hiyo tunajua na huo ulinzi tunajua siyo bure. Ingekuwa ni bure msingetoa nguvu za namna hii. Nitamtaja Waziri mmoja. (*Makofii*)

### **MBUNGE FULANI: Mtaje!**

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ambaye anaongoza kwenye kutafuna mali za Watanzania. Waziri wetu wa Fedha si mwaminifu, Waziri Mkulo si mwaminifu na aliyesema Waziri Mkulo siyo mwaminifu ni CAG na ametajwa humu ndani na kila Mbunge ana ripoti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Mbunge asome vizuri ataona madudu ambayo Waziri anafanya. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge tulifika hapa ndani, miezi kadhaa tumejibishana sana kuhusu ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, Waziri analeta Muswada hapa wa kutaka Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma (CHC) liuawe, Wabunge ambao tumetumwa na wananchi tulilipigania, tulitetea. Waziri alisema liuawe kumbe ilikuwa ni maslahi yake binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha alitaka liuawe kwa sababu anataka yeye achukue zile mali pamoja na Mawaziri wenzake na mifano tunayo, kwa sababu kabla ya hapo ameanza kuuza viwanja kadhaa vya Serikali bila kuishirikisha CHC na alipoona Mkurugenzi wa CHC anaulizia na kufuatilia, alimsimamisha kazi, akavunja Bodi ili yeye aendelee kufanya mambo yake vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana, tuna Bodi kadhaa zinaonesha kabisa na kwa ushahidi hapa kuna shida hawavunji. Tumekwishesema hapa mara kadhaa msifanye maamuzi kwa maslahi yenu binafsi. Tumekuja mara kadhaa hapa na kusema Bodi ya Pamba ni *one of the worst Boards we have ever mate*, vunjeni, haivunjwi. Vunjeni Bodi hii undeni nyingine, hamvunji. Tunajua kabisa ulinzi huu mnaowapa siyo bure. Lakini penye maslahi yenu binafsi mnaingia na mnnavunja na mnawenza hata kuthubutu mkalidanganya Bunge kwamba Wabunge siyo wakweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, msema kweli ni mpenzi wa Mungu, CAG ametuonyesha leo hapa walikuwa wanadanganya, siyo Mheshimiwa Kabwe Zitto. Waliokuwa wanadanganya hapa ni Waziri wa Fedha analidanganya Bunge, Waziri wa Fedha alikuwa ni mwongo na bahati mbaya sana Tume hii aliunda yeye mwenyewe, ni yeye mwenyewe alimwangiza CAG akachunguze akidhani CAG angempendelea. Napenda sana kumpongeza CAG kwa kuwa muwazi na mkweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Watanzania zinapotea, mali za Watanzania zinapotea, nchi inakufa, nyie mnalindana. Mawaziri wetu bahati mbaya sana maana yake tunasingizia sana Watendaji wa

Halmashauri, Mawaziri wetu wamegeuka kuwa mchwa. Baadhi ya Mawaziri wetu wanaitafuna nchi yetu mchana kweupe na sisi hatukuwatuma kufanya haya. Nazungumza kwa kirefu sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu hatuna imani na baadhi ya Mawaziri wako. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tunayoyasema siyo ya kwetu tumetumwa na Watanzania tuyaseme. Tumesahau tupate dhamana, tumefika mahala kuna makosa tunafanya, tumepitia hesabu za Mashirika ya Umma, Serikali yetu inafanya makosa ya wazi mchana mno na ni bahati mbaya sana haki haitendeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmoja mdogo tu ambao sehemu nyiningine fedha za umma zinatafunwa, ni fedha za wanafunzi toka Bodi ya Mikopo. Watoto wa maskini hawasomi, watoto wa Ludewa hawasomi, lakini fedha zinapelekwa vyuoni, baadhi ya vyuo vinatafunya. Wakuu wa Vyuo, Mkuu wa Chuo cha Mkwawa ameshiriki kwenye ufujaji wa fedha, Mawaziri wahusika wapo. Mambo haya yanafanyika mchana kweupe halafu wanafunzi wanyonge, wanafunzi maskini wanapoandamana kudai haki yao tunawapiga mabomu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopaswa kupigwa mabomu wamekaa, wametulia ofisini, aliyetafuna fedha ndiye alipaswa kupigwa mabomu. Yule Mkuu wa Chuo ilibidi tukampige mabomu na tumuulize kwa nini umekula fedha za wananchi. Badala yake tunawapiga wananchi hawa wanyonge, wananchi na watoto wa maskini, tumewasahau waliotupatia dhamana, Serikali ni ya kwetu, ni lazima tuseme kwa uchungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, CHADEMA hii siyo Serikali yenu, hii ni Serikali yetu ni lazima tuiseme sisi wenyewe. Mmefika mahali mnajisahau mno Waheshimiwa Mawaziri amkeni sasa. (Makofi)

Kuhusu Shirika la Viwango (*TBS*) ambalo halina viwango napenda kumthibitishia Mheshimiwa Waziri hatukwenda kule kutafuta ni nani anahuksika, hapana. Hatukwenda kutafuta Kampuni ni za nani sisi kwenye hadidu rejea, hapana. Napenda kusema bayana mbele ya Bunge hili, Waziri Chami hatukuona anahuksika kwenye Makampuni yale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichokiona sisi ni vitu viwili, kwanza, ukaguzi haufanyiki na pili fedha zile haziji Tanzania kutoka Hongkong na Singapore, hili napenda kulithibitisha. Sasa tunajua Waziri mhusika, Waziri Chami pamoja na Katibu wake Mkuu, wanailinda Taasisi hii kwa nguvu zao zote. Lindeni, hata jana Mbunge Mpya amefika Mheshimiwa Nassari,

ana ripoti zote ziko wazi, lakini Waziri unasema, mimi ripoti sina. Hebu tuwajibike jamani, tutumie akili zetu zote, tuwe wazalendo, kama kuwajibika inashindikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania leo hii wanakula vyakula vyenye sumu. Kuna *Blue Band* zenyе sumu, mafuta ya ndege mabovu, sabuni zenyе sumu, matairi mabovu, ajali zimekuwa nyingi na hata ndege ya *ATC* imedondoka huenda ikawa ni mafuta mabovu; maana mafuta mengine ya ndege yameingia ni mafuta *fake*, sisi bado tu tumemkumbatia mtu huyu mmoja. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua huu ulinzi mnaotoa sio bure. Kama kuna kosa kubwa tunafanya Serikali ya CCM ni kudhani nchi ya Tanzania ni mali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Filikunjombe. Kama nilivyosema, sasa nina orodha ya Waheshimiwa Mawaziri, najaribu kumange muda ili Wenye viti wetu wa Kamati wapate dakika 15 kila mmoja ya ku-wind up. Napata tabu kidogo, lakini nitajitahidi kwa sababu ya orodha ya Waheshimiwa Mawaziri, nataka kujaribu kuichukua ikiwezekana yote niliyonayo hapa ili tuweze kuchangia kwa pamoja.

Mheshimiwa Waziri Jumanne Maghembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Mponda. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kutoa maelezo kwenye maeneo machache ambayo yamelalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge. Napenda niwashukuru wote ambao wametoa michango yao katika maeneo na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ambalo nataka niliseme kidogo ni juu ya ununuzi wa korosho. Katika msimu huu Bodi ya Korosho ilitoa leseni 56 za wanunuzi wa korosho. Kati ya hao, wanunuzi 19 peke yao ndio walijitokeza kununua korosho na wengi walikuwa ni wale ambao wanabangua korosho humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wengine wote wallobaki hawakuja kununua kwa visingizio mbalimbali, lakini tulichoona kikubwa ni kwamba, walikuwa wanataka kuvunja utaratibu wa kununua korosho kuititia

Stakabadhi Ghalani. Kwa sababu hiyo, tuliunda Kamati Ndogo ya Watalaam itueleze ukubwa wa tatizo na kuleta mapendekezo ni kitu gani tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 Februari, 2012 Kamati ile ikaleta mapendekezo yake. Moja ya mapendekezo, pamoja na mapendekezo mengine, ikashauri kwamba Serikali itafute dhamana kwenye Mabenki, ili wakulima ambao mwanzoni walilipwa 70% ya thamani ya korosho zao, walipwe 30% iliyobaki na wakulima wachache ambao walikuwa hawajalipwa kabisa waweze kulipwa korosho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 Februari, 2012 tukapokea taarifa hiyo na kuifikisha kunakostahili na tukapata *assurance* kwamba, *guarantee* itapatikana. Kwa hivi tukawa tunafuatilia kila siku, lakini kwa kweli utaratibu wa fedha za Kibenki ni mrefu sana na ndio uliotufikisha hapa. Hali ambayo imefikia sasa ni ile ambayo alieleza Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa asubuhi kwamba, hivi sasa Benki ya *NMB* *ime-disburse* fedha kupeleka kwenye Matawi yake kule Wilayani na wakati wowote Vyama vyta Ushirika ambavyo vimenunua korosho kwa wakulima, vitaanza kupokea fedha hizo ili kuwalipa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa nilitolee maelezo kidogo, linahusu wizi ambao uligunduliwa na Kamati ya Mashirika ya Umma katika Bodi ya Pamba. Kwanza, napenda niwapongeze Kamati ya Mashirika ya Umma na Mwenyekiti wake, kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Taarifa ile kutufikia, tulichukua hatua mbili; hatua ya kwanza ni kuomba Mamlaka ya Uteuzi iteu Mwenyekiti mwingine wa Bodi ya Pamba na wakati mwingine utaratibu unachukua muda kwa sababu, wale watu ni lazima wafanyiwe upekuzi. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, tunaendelea kufuatilia na Mheshimiwa Waziri Mkuu amesikia na kwamba, nina uhakika muda usio mrefu tutapata Mwenyekiti wa Bodi ile. Kwa hiyo, si kweli kwamba, hatujachukua hatua kuhusu Bodi ile. Jambo la pili ambalo tumefanya, tumemuomba CAG akague mahesabu yote ya Bodi ya Pamba pamoja na fedha zilizotolewa kwa ajili ya kuwakwamua wale ambao waliumia wakati uchumi ulipoporomoka katika nchi za Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa sana athari ambazo Makampuni mengine yamepata na kwamba, mengine yanaweza kutoka kabisa katika biashara kama hawakuweza kupata msaada wa Serikali. Kwa hiyo, jambo hili tutaendelea kulifuatilia ili kujua ni nani hasa amehusika katika kutafuna fedha hizi za wananchi, fedha hizi zilitolewa

mwaka 2008. Wote ambao wamehusika na jambo hili, watachukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka niliseme na nategemea kwamba, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji itakapowasilisha nitaweza kutoa maelezo mengine ya ziada. Lakini lingine ambalo ningependa niliseme hapa ni suala la mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuchapisha vocha kwa ajili ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha umewekwa kwamba, baada ya bajeti ya Wizara kupita, basi tenda kwa ajili ya uchapishaji wa vocha hizi ndio inaitwa. Kwa kawaida bajeti kama mwaka jana ilipita karibu mwezi Agosti na mchakato ule ulifanya vocha zichelewe. Kwa hivi, hatua ambayo Kamati ya Vocha ya Taifa ilichukua ni kutengeneza utaratibu mbadala ambao utawahisha pembejeo kwa wakulima, halafu vocha zikija ndio sasa wakulima waweze kupewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu pia ulikuwa na faida kwamba, Mawakala wanapeleka pembejeo kwanza, kabla ya kukimbiza vocha. Tuliamini kabisa kwamba, utaratibu huu utapunguza wizi na ubadhirifu katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya katika Wilaya nyingine, Mawakala kwa kuona kwamba hakuna urahisi wa kuchukua zile fedha kwa kutumia fomu ambazo tulipeleka kama utaratibu wa awali wa kupeleka pembejeo kwa wakulima, waligoma kutumia utaratibu huo. Moja ya Wilaya hizo ni pamoja na Wilaya ya Mbozi...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Maghembe.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo kutokea wapi tena? Aah, Mheshimiwa Murji eeh, kwa kifupi sana tafadhalli, maana muda wangu mdogo kweli.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba Mwongozo wako kwa Kauli aliyotoa Mheshimiwa Waziri

kwamba, fedha za kuwalipa wakulima wa korosho, mchakato wake ni mrefu kwa sababu fedha hizi zinatoka Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye tarehe 27 au 28, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yake, alikwenda kwenye *Television* na kwenye *Vyombo* vya Habari vyote na kuwatangazia wakulima kwamba, hela zao ziko tayari na waende wakafuate hela wawalipe wakulima. Sasa ni nani mkweli, ni yeye au Naibu wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unapolinganisha neno la Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo hiyo na Waziri wake au Naibu Katibu Mkuu yeoyote yule na Mheshimiwa Waziri, tena akiongea Bungeni; halafu ukauliza na mwingine aliyeongea nje ya chumba hiki. Kwa kweli, jibu liko wazi kabisa kwamba, sisi tunashika neno la Mheshimiwa Waziri na hasa alilolizungumza hapa ambalo tunaliweka katika *Hansard*. Ahsante.

Tunaendelea na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa Daktari Mponda, dakika kumi.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii angalau nichangie kwa kutoa ufanuzi na kutoa hali halisi, ambapo mengine yaliyozungumzwa yanaweza yakaeleweka vinginevyo kabisa mionganini mwa Watanzania. Nitaomba nzungumzie mambo matatu; nitazungumzia suala la hasara za billioni 4.7 zilizosababishwa na kuharibiwa kwa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi dawa zimeharibiwa ni utaratibu wa kawaida, dawa zinapopita wakati wake. Jinsi ilivyotolewa ripoti, hizi dawa ni mkusanyiko kwa miaka 5. Na thamani ya hizi dawa zilizoharibiwa na thamani ya dawa ambazo ziliagizwa au kutumika, kiuwiano kuna *standard* ambazo zimewekwa na Mashirika ya Kimataifa mojawapo likiwa ni WHO kwamba, dawa hizi zisizidi thamani ya 5%. Kwa sababu, kwa vyovypote vile wakati unapoagiza dawa, aidha dawa hizi zinaweza zikapitwa na wakati kwa ajili ya matumizi au inawezekana umeagiza ukitarajia zitatibu magonjwa haya, lakini hayakupatikana. Sasa Tanzania kwa kipindi hicho ambacho kinahusika, zile dawa zilizoharibiwa ni chini ya ile *standard*, tuko 2%. Kwa hiyo, hii nataka niwape tu Watanzania, sio suala la watu mpaka wakafikia kwamba, basi tumepoteza dawa nyingi sana, lakini ziko ndani ya *standard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, imechukua muda mrefu kutoa hizi dawa kuziharibu ndani ya miaka hiyo mitano kwa sababu ya utaratibu; maana

*stock verifier* anaye-approve hiyo yuko mmoja Makao Makuu, Hazina. Sasa kwa utaratibu huo, mpaka tumefikia hiyo miaka mitano tumeziharibu hizi dawa. Naomba niseme tena ni utaratibu wa kawaida na tuko ndani ya *Standards*. Lakini lingine, hizi dawa zimeharibika pengine ni matatizo ya utendaji na hili tumeliona na tumeshaanza kulifanyia kazi kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tulikuwa tunatumia mfumo wa kuhifadhi au ku-stock hizo dawa, mfumo kwa njia ya kumbukumbu; tulikuwa tunatumia mfumo wa kuweka hizi kumbukumbu wa *Orion*. Huu nao ulikuwa una changamoto nyingi, wakati mwingine hautoi taarifa sahihi. Hilo tumeliona, kuanzia Julai mwaka huu tunaanza na mfumo mpya ambao unatumia *EPICOR*. Huu ni wa kisasa zaidi, wale ambao wamesoma mambo ya *Stores*, unatumia ule mtindo wa *FIFO* kwamba, zile dawa zilizokuja mwisho, ndio zinaanza kutolewa. Kwa hiyo, itatuhakikishia zaidi kwamba na yenyewe ina *indicators*, inamwamsha yule mweka dawa kwamba, sasa umefikia wakati utuangalie na sisi, karibu tunazeeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la deni la *MSD*, Waheshimiwa Wabunge, wamechangia sana. Naomba nifafanue zaidi kwamba, deni la *MSD* hili linatokana na dawa ambazo zinapitia ile miradi mikubwa, miradi misonge, ambayo tunapata kwa njia ya misaada. Hizi ni dawa za *ARV*, za malaria, *TB* na nyinginezo. Sasa katika kipindi hiki tulikuwa na dawa za thamani ya bilioni 200. Sasa hatukubajeti dawa hizi kwa sababu, zinakuja kwa misaada. Kwa hiyo, hatukubajeti kwamba, tuweke, maana kuna għarama nyingine pamoja na kwamba, tumeletewa kwa misaada, bado kuna għarama za kugomboa bandarini, bado kuna għarama za kuzihfadhi na għarama za kusambaza. Kwa hiyo, għarama hizi zote ukiangalia zinifikia 18%, sasa ndio maana tumefikia hiyo bilioni 37, lakini hii ni *cumulative*, ni deni la muda mrefu ambalo *MSD* wanaidai Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza kulipunguza hilo deni, mwaka huu tumelipa bilioni 3.4, lakini kadiri tutakavyopata hali nzuri tutazidi kulipunguza ili tuwape nafasi zaidi ya uwezo wa kifedha hawa *MSD* wawzeze kutoa huduma, tusije tukakwamisha mtaji wao. Lakini naomba tu nitoe taarifa kwamba, *MSD* suala la *cash flow* sio tatizo kubwa sana, bado wana mzunguko mzuri tu wa kifedha kwamba hili deni halivezi likaathiri usambazaji au upatikanaji wa dawa kwenye vituo vyetu vya tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee lile jambo la tatu kwamba, tumefanya sherehe za bilioni 1.1 kipindi cha Nane Nane; naomba nirekebishe kidogo kwamba, hela tulizotumia kipindi kile cha Sherehe cha Nane Nane tulitumia milioni 700,029,000.

**WABUNGE FULANI:** Mmmh!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio kama ni ndogo au ni kubwa, lakini tumezitumia hizo, lakini lengo letu kubwa pale sio kufanya sherehe; tumekwenda kama Wizara, kwamba, tunafahamu tuna changamoto kubwa bado wananchi wetu wengi uelewa dhidi ya kujikinga na maradhi bado ni mdogo. Kwa hiyo, tumetumia nafasi hiyo kuongeza elimu, kuwaelimisha, tumetumia nafasi hiyo tena kubadili tabia na mwenendo wa Watanzania. Hatuna tabia za kupima afya zetu mara kwa mara, kwa hiyo, ilikuwa ni nafasi nzuri basi, tumefanya hiyo kazi. Tumewapima, tumewahudumia watu kipindi chote cha siku nane watu 30,000 na wengine waligundulika mpaka unashangaa huyu mtu amefikaje hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii huwezi kuthamini fedha na uhai wa binadamu na afya yake wakati mwengine. Lakini kilichotokea hapa, Watendaji wangu kwamba, wakati wanafunga hesabu za mwaka walichukua bilioni 1.9 kwa sababu, waliona kwamba, hizi hela zisipotumika wakati tayari miradi ipo pale; walizihamishia wakazipeleka Taasisi ya NIMR, ambako Taasisi ya NIMR wao wana Mfuko mwengine wa kifedha wa Kiserikali. Lakini hizi hela baadaye tulizitumia na maelezo yake kwa sababu ya muda, tulizitumia kama ifuatavyo:-

Maonyesho ni zile milioni 700, kumalizia Kiwanda cha Kusindika Dawa za Asili Mabibo milioni 400, Mafunzo kwa Watafiti wa NIMR tulitumia milioni 170 na milioni 600 kumalizia kibanda cha Nane Nane. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Mmmh!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine liliojitokeza hapa kwamba, zimetumika milioni 400 kukarabati nyumba ya Waziri Dodoma. Waziri mpaka sasa hivi, hana nyumba Dodoma iliyokwisha; utakarabati vipi nyumba haijkwisha? Kwa hiyo, zile hela zimetumika kuendeleza ujenzi ambao unaoendelea sasa hivi wa nyumba ya Waziri hapa Dodoma. Katika ripoti yao Kamati, wamesema wakipata nafasi watakwenda kuangalia na hiyo wakipata kuangalia jengo, itadhihirisha kwamba, sio ukarabati bali ni kujenga nyumba mpya ya Waziri wa Afya hapa Dodoma. Ndio tunajitayarisha kuhamia Makao Makuu ya Dodoma.

(*Hapa Wabunge walizomea*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema nitachangia matatu tu, haya nakushukuru.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cheyo kwa heshima yako.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana, mimi naona hakuna haja ya kubishana na Waziri juu ya pesa kwa sababu Afisa Masuuli amekuja kwenye Kamati yetu ametuletea *figure* zote na zimehakikiwa na CAG, sasa kuanza kutamka takwimu tu hapa haitasaidia Mheshimiwa Waziri. *May be* kinachofaa nenda kwa Afisa Mhasibu wako angalia ni kitu gani kilisemwa kwenye PAC, halafu chukua hatua zinazostahili ili mambo haya yasijirudie. (*Makofi*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nilikuwa na taarifa kwanza kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, lakini pia nataka kupata ufanuzi wa Kiti. Wakati Mheshimiwa Maghembe anajibu hakugusia kabisa suala la mbolea. Tumekuwa tukipigiwa simu sana huko mikoani kwa wakulima kutaka majibu sahihi ya suala hili. Sasa je, kutakuwa na kauli nyingine ya Serikali kuhusiana na suala hilo au laah! Lakini pia nimesikitishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, anaposema tatizo la bajeti kwa *MSD* siyo tatizo, kwa hiyo, hata hilo deni likilipwa kidogo kidogo ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli *MSD* wanapokuja kwenye Kamati yetu kila siku wanalamika ucheleweshwaji wa fedha za kununua dawa za Watanzania unaofanywa na Wizara ya Afya, halafu leo Waziri anakuja kutuambia maneno kama haya wakati *MSD* wanababisha fedha zao za miradi washindwe kuendelea na matokeo yake fedha ambazo wanapaswa kufanya miradi ndiyo waagize hela za Watanzania. (*Makofi*)

Leo hii Mheshimiwa Waziri anatuambia maneno gani haya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nawaomba Waheshimiwa wote wenye taarifa na kadhalika tuvumiliane ili ratiba yangu iweze kwenda vinginevyo itakuwa vigumu sana kumaliza kikao hiki, natambua kabisa mambo muhimu mliyonayo. Naomba nimwite Mheshimiwa Ole-Medeye na atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuchika.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza niwashukuru Wenyeleviti wa Kamati walioandaa na kuwasilisha taarifa hizi na pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ya kuchangia katika taarifa hizi niliomba tu nitoe ufanuzi katika taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma ambayo ndani ya taarifa hii ukurasa wa tatu, iko orodha ya Mashirika ya Umma ambayo hayajawasilisha taarifa ya hesabu zilizokaguliwa. Moja ya mashirika yaliyoainishwa pale ni chuo cha Ardhi Morogoro. Ningependa nijulische Bunge lako Tukufu kwamba Chuo cha Ardhi Morogoro siyo shirika la umma na wala siyo taasisi inayojitegemea, ni kitengo kilicho chini ya Idara ya Utawala katika Wizara ya Ardhi.

**WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kuipongeza Kamati ya LAAC kwa taarifa ambayo imeletwa hapa Bungeni. Sisi kwa upande wa TAMISEMI tunafanya kazi kwa ukaribu sana na Kamati hii na tumeitwa mara kadhaa kwenye Kamati hii. Nataka pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii Dr. Augustino Mrema ambaye hata inapokuwa kwamba Kamati haipo kwenye *session*, akisikia jambo muda wowote ananyanya simu na kupiga kutaka ufanuzi na wakati mwingine kutaka kuonana na Waziri wa TAMISEMI na tumekuwa tukionana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, lazima muwe wakali kama mlivyokuwa kwa sababu katika nchi 14 zilizopo katika honi ya Afrika kuanzia Afrika Kusini mpaka Djibout, Serikali ya Tanzania inaongoza kwa kupeleka percent kubwa ya fedha zake katika mamlaka za Serikali za Mitaa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Afrika unataka Serikali za Mitaa zipelekewe angalau robo ya bajeti ya nchi, sisi Tanzania tumevuka kwa sababu katika trilioni 13 za bajeti ya mwaka huu tayari trilioni tatu zinapita mikononi mwa Serikali za Mitaa. Sasa ninachotaka kusema hapa ni kwamba, Serikali yetu kwa dhamira nzuri ya kusukuma maendeleo inapeleka fedha nyingi katika mamlaka ya Serikali za Mitaa. Tatizo tulilonalo sasa ni ufuatiliaji wake kuhakikisha kwamba fedha zinafanya kazi iliyokusudiwa. Kwa hiyo, ndiyo maana na mimi nasema *spirit* ya Wabunge kutusaidia au kusaidiana maana ni nchi yetu sote, ili mambo yaende vizuri ni jambo la kupon gezwa na ni jambo ambalo halina haja ya kufanyiwa ubishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mfupi, ningependa nizungumze jukumu la Baraza la Madiwani. Baraza la Madiwani ndiyo Serikali ya Wilaya, Baraza la Madiwani ndilo linalohusika kupokea taarifa ya fedha kutoka Serikali Kuu, fedha zilizokusanywa *own sources* na ndiyo maana Kamati ya Fedha inatakiwa ikutane kila mwezi, kazi yake ni *ku-monitor*,

kuona kama fedha zile zinafanya kazi iliyokusudiwa. Kwa hiyo, mlinzi namba moja wa mali ya umma katika Halmashauri ni Waheshimiwa Madiwani na hao Waheshimiwa Madiwani tukiwemo na sisi Waheshimiwa Wabunge, naomba sana tuendelee kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sisi Wabunge wengi ni Madiwani. Imetolewa rai hapa kwamba tutoe mafunzo kwa Madiwani na leo asubuhi palikuwa na swali hapa Naibu Waziri ameeleza kwamba tumefungua mafunzo tarehe 2 Aprili, 2012 kwa Madiwani nchi nzima kwa siku tatu tatu kila Halmashauri. Hatujawakusanya kuwaweka pamoja, tunakwenda kila Halmashauri Wilayani kwao kwa sababu matatizo ya Halmashauri moja hayafanani na Halmashauri nyingine. Tarehe 15 Mei, mafunzo hayo yatamalizika kwa kumalizia pale Korogwe ambako Naibu Waziri TAMISEMI atakwenda kuyafunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, sisi TAMISEMI tunaheshimu maamuzi ya Baraza la Madiwani. Katika taratibu zetu za utendaji kazi katika Sheria za Serikali za Mitaa, mtendaji wa Halmashauri ambaye mamlaka yake ya nidhamu ni Waziri mwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa ni Mkurugenzi peke yake. Wengine wote mamlaka yao kuhusu masuala ya nidhamu ni Baraza la Madiwani. Kwa hiyo, nataka niseme Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi waliomba *special audit*. Taarifa zilipotoka walipitisha maazimio pale ya kuwakataa Wakuu wa Idara 11, wametuletea TAMISEMI tume-comply, tumetekeleza maamuzi ya Baraza la Madiwani, Serikali ya Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeandaa utaratibu japo tumechelewa kidogo, lakini kwa sababu waliondoka wamelaumiwa laumiwa tumetaka tupate watu wazuri, tumepeleka watu Kilindi ili waende wakazibe mapengo ya wale ambaa wameondoka pale. Sasa tangu asubuhi hapa na jana pia imekuwa inatolewa hoja hapa kwamba, pengine TAMISEMI hatuwachukulii hatua za kinidhamu watendaji wetu. Hapa nina orodha ya Wakurugenzi 35 waliochukuliwa hatua na TAMISEMI, wengine wamefungwa, wengine kesi ziko Mahakamani, wengine kesi ziko TAKUKURU, wengine kesi ziko mikononi mwa Polisi, muda ungetosha ningesoma jina kwa jina na Halmashauri inayohusika. (*Makofii*)

**WABUNGE FULANI:** Somaa!

**WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie dakika kumi zangu zile nikisoma hapa, kwa sababu nina majina aina mbili, hizi nitawagawia Waheshimiwa Madiwani, 35 wakurugenzi watendaji waliochukuliwa hatua na hapa kuna watendaji

197 kutoka Halmashauri mbalimbali waliochukuliwa hatua na Baraza la Madiwani na TAMISEMI tukaridhia. Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ile hoja ya kwamba hatuchukui hatua tunajitahidi kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini moja nataka niliseme ni kwamba, hawa watumishi ni binadamu, hawa watumishi tumewaa jiri, ziko kanuni za utumishi ndani ya Serikali, si kwamba tukiona tu basi wewe unatuhumiwa hivi ondoka, acha kazi, hapana. Tumekuta ziko taratibu zimepitishwa na Bunge za namna ya kuwashughulikia watumishi wanaokwenda kinyume na maadili ya utendaji kazi ndani ya Serikali. Kwa hiyo, mnapoona pale kwamba tumechelewa chelewa ni kwa sababu ya kufuatilia kuhakikisha kwamba tunafuata sheria. Kwa sababu huko nyuma imewahi kutokea, yakafanya maamuzi, watu wakaenda Mahakamani, wakashinda na baadaye wamelipwa pesa nyingi sana. Looh! Muda umepotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi majukumu mengine itabidi niyaruke kwa sababu ya muda. Suala la posho ya Madiwani na maslahi ya Madiwani nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu amelieleza asubuhi hapa na sisi ametuagiza hapa tuliweke katika bajeti. Sisi wote hapa ni Wabunge, tunafanya kazi katika Mabaraza ya Madiwani, Madiwani tunaofanya nao kazi wako katika mazingira magumu, kwa hiyo, hakuna Waziri ye yeyote au Mbunge ye yeyote anaweza kupinga hoja ya kuwaongezea posho Madiwani. Waziri Mkuu ametuagiza tunaweka katika bajeti inayokuja tunaomba tu kwenye Kamati mtukubalie na tunaomba kwa dalili nilizoziona hapa nina uhakika tutakapokuja hapa kuomba tutaungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema hilo, lingine nalotaka kusema hilo ni majukumu ya ofisi za Wakuu wa Mikoa na majukumu ya Sekretarieti za Mikoa kusimamia mamlaka ya Serikali za Mitaa. Sheria ya *Regional Administration Act*, ya mwaka 1997 inasema ni jukumu la Mkuu wa Mkoa, jukumu la Sekretarieti ya Mkoa kusimamia na kuziwezesha mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopo katika maeneo yao kuhakikisha kwamba zinafanya kazi. Inawezekana huko nyuma tulikuwa hatufanyi vizuri, lakini tumekutanisha sasa ma-RAS, tumekutanisha Wakurugenzi wote hapa Dodoma, tumekutana nao pamoja kuwasisitizia kwamba masuala ya Halmashauri haya, kabla hajaulizwa Waziri TAMISEMI, kabla hajaulizwa Naibu Waziri, kabla hayajakwenda kwa Waziri Mkuu watu wa mwanzo wanaotakiwa kufahamu na kuzilea Halmashauri hizo na kuziwezesha Halmashauri kufanya kazi ni Sekretarieti za Mikoa wakiongozwa na Wakuu wa Mikoa. Nataka nikuhidi kwamba sisi katika TAMISEMI tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kutekeleza yale yanayoamriwa hapa ndani, yale yanayolimwa na wakati tunesikia, tumelewa tutaendelea kukaza uzi. Nashukuru.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Miongozo yote nitachukua mwisho sasa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda niwashukuru Wenyeviti wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika hoja mbalimbali napenda tu niwaombe radhi yanayonihusu huenda nisiyamalize yote kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala kubwa ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la Watumishi hewa, tumeombwa tueleze kama Serikali tumechukua hatua gani kuhakikisha kwamba tatizo hili tunaliondoa. Kwanza, tatizo hili lilikuwa linasababishwa na masuala ya kimfumo na pili udhaifu wa usimamizi wa rasilimali watu katika mamlaka zetu mbalimbali za ajira.

Sasa kuhusu suala la mfumo, mfumo ambao tulikuwa tunatumia kwa malipo ya mishahara ulikuwa ni ule wa *Lawson, Toleo la Saba* ambao kwa kweli ulikuwa umepitwa na wakati. Sasa Serikali tumechukua hatua ya kubadilisha kuweka mfumo mpya wa *Lawson, Toleo la Tisa*. Pia kwa kutambua usumbufu au mianya ambayo ilikuwa inatokana na toleo namba saba ambalo lilikuwa ni vigumu kumkamata hasa mhusika wa watumishi hewa. Kwanza kabla ya kuingia katika toleo la tisa tulisafisha takwimu zote za watumishi kwa kujiridhisha kwamba watumishi ambao tutawaingiza katika toleo la tisa ni wale ambao kweli wapo wanafanya kazi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo tumetoa mafunzo kwa maafisa watumishi wawili wawili kwa kila Halmashauri, kila Wizara na taasisi zote za Serikali pamoja na vyuo vikuu. Baada ya hapo tumewafungia mfumo huu ambao ni wa *Lawson, Toleo la Tisa* na tumewaondoa wahasibu kwa sababu huko nyuma ambao walikuwa wanaingiza takwimu za watumishi katika mfumo huu malipo ya mishahara walikuwa ni wahasibu na wataalam wa *IT* au *computer*. Sasa hivi jukumu hilo tumelirejesha kwa maafisa utumishi. Sasa hivi badala ya kazi hii kufanywa na Utumishi, Hazina na Waajiri, tumeondoa kutoka Hazina sasa hivi tunashughulika utumishi na waajiri peke yake. Kazi ya Hazina sasa hivi ni *ku-process pay roll* peke yake lakini hawana uwezo wa kuingia katika mtandao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mtumishi akiajiriwa, akifariki, akibadilishiwa mshahara au akiacha kazi, mwajiri ikiwa kama Halmashauri

au cheo pale pale anamwingiza kwenye *payroll*. Tunachofanya Utumishi ni kuhakiki ili tuweze kuidhinisha au kutoidhinisha. Iwapo itajitokeza kwamba mtumishi ameingizwa kwa makosa au labda ni mtumishi hewa, sasa hivi tuna uwezo wa kujua ni nani aliyemwingiza, wakati gani, wapi na ametumia mashine gani. Kwa hiyo, tuna uwezo sasa hivi wa kuweza kumkamata na kumwajibisha moja kwa moja mtumishi ambaye atahusika na watumishi hewa na hakutakuwa na kisingizio kwamba utumishi hawakumtoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda niihakikishie Bunge lako kwamba, kwa upande wa kuzuia tumejitalidi kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na Vyuo Vikuu vyote, Halmashauri tumezifungia, Idara za Serikali zote tumezifungia mtandao na kuanzia mwezi Januari, 2012 mpaka mwezi Juni, 2006 mwaka huu tunaendelea na zoezi la kuwalipa watumishi dirishani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua tutumie mbinu zote hizo ili kujihakikishia kwamba tunapoingia hii *Lawson, Toleo la Tisa* kwa kweli tunaingia tukiwa na takwimu za watumishi zolizo sahihi. Tayari tumeshalipa dirishani watumishi katika mamlaka za Serikali za Mitaa na zoezi hilo limekamilika. Awamu ya pili sasa hivi tunaendelea na zoezi hilo katika Taasisi za Serikali pamoja na Vyuo Vikuu, zoezi hilo linaendelea na mwezi Mei tutakuwa tunamalizia katika Wizara na Idara zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumefanya kikao kwanza na Maafisa Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Rasilimali Watu na Wakuu wa Rasilimali Watu wa Wizara na Idara Zinazojitegemea na Maafisa Utumishi wote ambao tumewapa mafunzo katika Halmashauri zote ili kujifunza kutoka kwao kama kuna changamoto zozote wanazozipata kwa sababu huu mfumo ni mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nichukue nafasi hii kuelezea kwa kirefu hatua ambazo tunazichukua katika kuhakikisha tatizo la watumishi hewa tunalimaliza na tuna uhakika kabisa kwamba kwa mfumo huu kama siyo kuondoa kabisa, basi kwa zaidi ya asilimia tisini au 99 tatizo hili tutakuwa tumeliondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumechukua hatua gani kwa wale ambao wamehusika na katika kusababisha watumishi hewa. Katika maeneo ambayo tumehakiki na kuona watumishi hewa kwanza tumewapelekea wenzetu wa TAKUKURU ili wawashughulikie wale ambao wako nje ya utumishi wa umma, kwa sababu wengine wamestaifu na wengine wamehama wako katika *private sector*, wafanye uchunguzi

pamoja na waliopo katika Utumishi wa Umma na walioshirikiana nao kuchukua pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wapo katika hatua za mwisho ili kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Pia kwa wale ambao wako katika utumishi wa umma pamoja na mambo mengine tumewataka wazirejeshe pesa hizo. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza tayari zaidi ya milioni 800 zimesharejeshwa na zipo katika akaunti iya Benki Kuu kwa hiyo, bado tunaendelea kuzipokea. Kwa wale watumishi ambao walistaafu wakati wanasubiri *pension* zao wakawa wanaendelea kuchukua mishahara ya Serikali baadhi yao walikatwa mishahara hiyo kutoka kwenye *pension* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelezea tu kwa kifupi, lakini suala lingine ambalo nataka nilizungumzie ingawa Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI* amelielezea, ni suala la kukaimu na suala la watumishi kuwa na kesi nyingi Mahakamani. Ni kweli tatizo hilo tumeliona kwamba kuna watumishi wengi wana kesi Mahakamani na zinachukua muda mrefu na hivyo inazorotesha utendaji wa kazi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewaandikia Halmashauri zote na Wizara zote tujue idadi kamili ya watumishi ambao kesi zao zipo Mahakamani ili tuweze kuona kama ziendelee kukaa Mahakamani au tuziondoe ili tuwachukulie hatua nyingine za kinidhamu. Kwa zile ambazo tunaweza kuzichukulia hatua za kinidhamu ili tumalizane nao ili tuweke watumishi wengine katika nafasi zao. Kwa sababu kama mtumishi ametuhumiwa, yuko Mahakamani, ukimweka mtu mwingine kukaimu huwezi kumthibitisha kwa sababu nafasi hiyo nafasi haipo wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa muda uliopo nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii na kutoa ufanuzi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na nakushukuru sana, sasa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda niwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati hizi tatu zilizotoa hizi taarifa kwa uchambuzi mzuri sana ambao umetusaidia sisi wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuchangia hivyo tulivyochangia.

Nasimama hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ameniagiza nitoe baadhi ya maelekezo kulingana na uzito wa taarifa hizi.

Lakini kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge kwamba hizi taarifa ni za muda mrefu yaani mwaka 2009/2010. Kwa hiyo, kwanza lipo tatizo la utaratibu hasa mawasiliano kwa sababu taarifa hizi zikitolewa mwaka 2009/2010 zinaishia katika uhai wa Kamati za Wabunge katika mafungu matatu kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, kila fungu wanajua wao, Kamati moja moja zinajua kwa mwaka mmoja. Baadhi ya Wabunge tulio wengi tunajua vile vitabu yaani tunasoma, lakini uchambuzi wa Kamati moja moja tunaupata baada ya mwaka mmoja. Bahati mbaya hata sisi Serikalini wanaohudhuria katika hizo Kamati ni watendaji wetu, hata sisi Mawaziri hatujui maelekezo gani na kazi gani imefanywa na Kamati kwa mwaka mzima, mara nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, zipo hitilafu fulani za mawasiliano kati ya Kamati na Wabunge tulio wengi na kati ya umma vilevile maana yake taarifa hizi zikishatolewa zinakuwa *public* yaani zinakuwa kwenye mtandao. Wanausoma udhaifu ule kwa mwaka mzima kana kwamba Serikali haifanyi kitu kwa mwaka mzima. Lakini ndani ya Serikali tunatekeleza hayo ila hakuna fursa yoyote ya wazi ya kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Bunge hili kila mara tunapewa taarifa zenye udhaifu za CAG yaani udhaifu dhidi ya Serikali lakini zikija taarifa za Kamati vile vile bado zinaigonga Serikali na udhaifu wake. Lakini Serikali imefanya kazi hivyo hivyo kuzipitia hizo taarifa kwa mwaka mzima, hakuna nafasi kwa Serikali kutoa taarifa hapa Bungeni. Huwa tunakuja tu kuparamia zikitolewa taarifa za Kamati na sisi tunajibu kwa muda mfupi kama hivi au baadaye tunaleta taarifa za maandishi. Kwa hiyo, hata uwiano wa taarifa kunakuwa na upungufu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi ndani ya Serikali tumeuona huo upungufu kwamba lazima na sisi Serikali tutengeneze utaratibu ambao utatuonesha jinsi tulivyotekeleza maelekezo na maagizo ya CAG na maagizo ya Kamati na yatangazwe na Waheshimiwa Wabunge wote wayapate, wayasome kwa ujumla na kwa uzito unaostahili kama wanavyopata taarifa za Kamati na za CAG, kwa sababu mmesikia hapa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kuna hatua zilizochukuliwa lakini mwaka mzima inawezekana walio wengi ndiyo tunasikia leo lakini kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na hitilafu hiyo ya mawasiliano, ili wananchi na ninyi Waheshimiwa Wabunge mpate kwa uhakika namna gani imeshughulikia taarifa hizi, hizi za kwenu lakini pia taarifa za CAG. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameamua kutoa maelekezo kama ifuatavyo:-

Kwanza, mwaka huu tumejaribu taarifa hii ya CAG ya mwaka 2009/2010, Serikali tumejaribu kwa kuanzia na taarifa hii. Tumefuatilia kila jambo lilitoripotiwa na udhaifu wote ulitoripotiwa kwenye taarifa ya CAG ya Hesabu za Serikali na ilipofika mwezi Machi tumetengeneza, tunayo *matrix* inayoonesha kila hoja ilivyojibiwa. Hata pikipiki zilizohojiwa Singida zimepatikana kwenye taarifa hii.

Sasa bahati mbaya tu ni kwamba, tulimpelekea CAG mwezi Machi ili asome je, majibu haya ya Serikali za Mitaa yalivyotekelawa yanafanana? Maana yake ndiyo tunaanza na sisi kutoa vitabu vyetu, lakini je, yanafanana na vile anavyojua yeye? Bahati mbaya hajaturudishia. Tulitaka wakati Kamati leo inawasilisha taarifa na Serikali tuwe na majibu yetu ili Wabunge waweze kuona Serikali imetekeliza vipi na Kamati inaona kitu gani, lakini bahati mbaya hatujaona, lakini taarifa hii inaonesha majibu yote pamoja na haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasema.

Kwa hiyo, kuanzia sasa baada ya kupata uzoefu huu, Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema kwamba, kwa taarifa ya *Local Government* kwa kuwa inatolewa mwezi wa tatu, basi hii kama tulivyofanya tutazirudisha hizi taarifa na kuwaelekeza watu wa Serikali za Mitaa, Mikoa kati ya mwezi Mei na Julai Halmashauri lazima ziwe zimeshajibu hoja zote. Siyo kujibu tu kwa kujifurahisha lakini na hatua ziwe zimechukuliwa. Baada ya hapo tunataka tuwashikishe tena Waheshimiwa Wabunge kabla hamjaja kwenye vikao vya RCC, tunataka hizi taarifa za majibu na hoja zote zilizotolewa kwa mwaka huu na CAG zijadiliwe na vikao vya RCC.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakishajibu Halmashauri zote Sekretarieti itaunganisha na itakuwa moja ya *agenda* ya RCC na baada ya hapo bila shaka RCC itatoa maelekezo, zitarudishwa kwenye Halmashauri kama hazikujibiwa vizuri. Kama kuna mtu hakutakiwa kufukuzwa amefukuzwa au hakuchukuliwa hatua watazirekebisha. Kwa hiyo, tungependa kusema kwamba kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye *agenda* zote za vikao vya RCC *agenda* za taarifa za CAG lazima ziwepo ili Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wengine wapate taarifa ya uhakika kutoka huko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, baada ya hapo taarifa zote za uhakika lazima zije kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili mwezi wa tatu tuweze kuchapisha kitabu chenye majibu ya uhakika juu ya utekelezaji wa hoja zote zilizojitokeza za CAG, kwa uhakika. Haja aliyoyasema Mheshimiwa Mkuchika ya majina, nani kafukuzwa na nani yuko jela lazima ionekane kwenye hiyo taarifa na taarifa hizi zitakabidhiwa kwa Mwenyekiti wa LAAC, zitapitiwa na Kamati na taarifa hizi zitakabidhiwa kwa Wabunge

wote ili Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati anapoleta taarifa hii, Wabunge wawe na taarifa ya Sekretarieti ya utekelezaji na kuwe na ulinganishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, safari hii pamoja na utekelezaji tulikuwa tunaufanya ambao kwa ujumla ulikuwa hauna taarifa kwa umma na Waheshimiwa Wabunge walikuwa hawajui kwa mwaka mzima. Safari hii na sisi tutachapisha kama Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema ni lazima kitabu kichapishwe, Wabunge wapate, lakini taarifa hizi ziwe zimeshirishirkisha wadau wote katika Mkoa ili wajue fedha za wananchi zinatumikaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa za PAC na POAC yaani mashirika ya umma, mara nyingi hata sisi baadhi ya Mawaziri tunaozisimamia taarifa hizi wakati mwingine hatuwezi kujua mambo mengi sana ambayo ninyi mnayaelekeza kwenye Kamati. Kwa hiyo, na zenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza kwamba mashirika yote yaliyotajwa kwenye taarifa hizi tulizopokea za mwaka 2010/2011, lazima wahakikishe kwamba ifikapo mwezi wa Tisa taarifa hizi zote ziwe zimejibwa kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuzuii kazi za Kamati kwa hiyo Kamati zitaendelea na kazi zake lakini sisi upande wa Serikali Mashirika yote na taasisi ziwe zimepitisha taarifa hizo na ziwe zimepitia kwenye utaratibu wote wa Bodi na kila kitu. Hizo nazo zitakuja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Novemba kama zile za Mikoani ili na sisi tupate nafasi ya kuzipitia, kuzihakiki na kuchapisha kitabu kwa taarifa hizi za Mashirika ya Umma. Lakini Mawaziri na wenyewe watajihuisha kwa sababu taarifa hizi zitakuja na mwamvuli wa Mawaziri ili mwezi wa Tatu tulete taarifa zenyе majibu sahihi na hatua tulizochukua kutokana na taarifa zote tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa muda ulionipa, lakini nataka nikuhakikishie mwakani kutakuwa na mapinduzi juu ya utoaji wa taarifa za Serikali kuhusiana na taarifa za CAG.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa taarifa hiyo ya matumaini.

Sasa kabla sijaanza kuwaita Wenyevitii kwa upenyo huu Mheshimiwa Kigola ultaka Mwongozo?

19 APRIL, 2012

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mimi ni Lugola na mwenzangu ni Kigola wa Mufindi Kusini.

**NAIBU SPIKA:** Samahani narekebisha Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) naomba Mwongozo wako.

Wakati Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI* anachangia amesema kwamba Madiwani ni wasimamizi wazuri wa Halmashauri zetu na kawaida kwamba ndiyo Serikali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kinachoendelea kwenye Halmashauri zetu ni kwamba ni Kamati moja tu ya Fedha na Uchumi ndiyo inayoruhusiwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo ilihali Kamati nyingine kwa maana ya Madiwani wote ambao wako kwenye Kamati nyingine hawaruhusiwi kutembelea wala kukagua miradi ya maendeleo.

Pia Mheshimiwa Waziri amekuwa akitoa Mwongozo wa mara kwa mara kuwakumbusha Wakurugenzi ni Madiwani gani na Kamati gani ambazo zinaruhusiwa kukagua miradi.

Sasa naomba Mwongozo wako sambamba na anavyoliambia Bunge kwamba Mkuu wa Mkoa anasimamia Halmashauri ilihali RC ni Serikali Kuu na Halmashauri ni Serikali za Mitaa. Sasa naomba Mwongozo wako Madiwani ambao wamesikia kauli hii waichukulle kwamba sasa kweli wanaruhusiwa kutembelea na kukagua miradi kama Serikali ya Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Sasa naomba niwaite Wenyeviti, tukianza na Mwenyekiti...

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifungu hicho chicho cha 68(7) kwa maelezo ambayo yametolewa hapa na Waziri wa *TAMISEMI* kwamba Waheshimiwa Madiwani wana jukumu la kuchukua hatua kwa watendaji ambao wako chini yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nikuhakikishie na Bunge lako kuwa, matatizo mengi ya fedha ya watumishi waliopo chini ya Halmashauri yanamuunganisha Mkurugenzi ambaye Mkurugenzi huyo mamlaka yake iko kwa Waziri. Sasa lolote lile unalotaka kulichunguza kuhusu fedha kwa sababu katika Halmashauri hakuna fedha yoyote ambayo inaweza kutoka bila idhini ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Lakini pia na tatizo kubwa la TAMISEMI kumekuwa na waraka nydingi sana ambazo zimekuwa zikiwazuia Waheshimiwa Madiwani kuchukua hatua pale Mtendaji anapokuwa amekiuka misingi ya fedha na hata anapopatikana na tatizo la fedha. Kinachofanyika wanaagiza uchunguzi ufanyike, uchunguzi ufanyike lakini inapita miaka mingi uchunguzi haufanyiki na Mtendaji yule anabaki akiendelea kula fedha za umma.

Pia bado katika maelezo afadhali labda Mnadhimu Mkuu wa Serikali alivyozungumza hapa, lakini hatua ambazo anazizungumza Mheshimiwa Waziri na Mnadhimu alivyozungumza kwamba Wizara zinatuma watendaji wake tu kwenda kusikiliza taarifa kwenye Kamati. Lakini je, *flow of information* ikoje kutoka kwa aliyetumwa, kwa Katibu Mkuu na kwa Waziri? Kwa hiyo, siyo sahihi pia Bunge hili kuamini leo kwamba, watendaji wanaotumwa kwenye Kamati hawapeleki taarifa mahali walipotumwa. Kwa hiyo, siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kwamba turidhike na Serikali ikubali kwamba ufuatiliaji makini kama Mkaguzi mwenyewe alivyokiri kwenye taarifa zake zote, ukisoma taarifa ya Mkaguzi ya kuanzia mwaka 2007/2008 na mwaka 2008/2009 na mwaka 2009/2010 amelalamika kila mwaka kutokutekelezwa kwa maagizo anayoyaagiza Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako sasa kwamba kwa kuwa TAMISEMI imekuwa ndiyo kigezo cha kukumbatia hawa walaji wa fedha za umma na wafujaji wa fedha za umma, Waziri wa TAMISEMI atasema nini sasa kwa sababu hata akiletewa taarifa za ubadirifu wa fedha za umma hachukui hatua. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wawili na niwajibu tu kwa pamoja Mwongozo wangu kama ifuatavyo:-

Kwamba, kwa kiwango kikubwa mllichokitoa ni ushauri, jambo ambalo ni wajibu wetu kama Waheshimiwa Wabunge kwa Serikali na Serikali imesikia ushauri wetu. Nina hakika itafanya kazi na kwa wakati muafaka huko mbele tunaweza tukapata namna ya kuenenda

kuhusiana na jambo hili linalohusu Kamati za Madiwani na wataalam wetu. Nimekaa hapa siku mbili nawasikiliza na mimi pia ni Diwani na kwa hiyo niiambie TAMISEMI kwamba pamoja na malalamiko yote makubwa haya ambayo yanatoka, tatizo mojawapo kubwa sana ni namna gani watu wanaoitwa Wakuu wa Idara wanavyopatikana nchi nzima, hawa Wakuu wa Idara wanapatikanaje? Lipo tatizo!

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wao hawafai kabisa lakini kwa kuwa tunaletewa kutoka Dodoma au tunaletewa kwenye Wilaya kutoka tunakoletewa sasa sisi tufanyaje? Mnapiiga kelele, mnaondoa hawa, mnaletewa seti nyingine ya wabovu. Sasa ipo haja ya kuwa na *performance indicator* za hawa hasa Wakuu wa Idara mbalimbali ili asiyefaa *system im-check out* vinginevyo mtalalamikiwa leo, mtalalamikiwa kesho na kadhalika. Unaletewa Afisa Elimu ambaye kwa kweli yaani hafai, yaani sijui amepatikanaje. Unaletewa Bwana Kilimo sijui amepatikana vipi, yaani Yarabi toba! Sijui wamemtoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili ndiyo tatizo la msingi nani anawapa vyeo hawa? Hii ndiyo kelele yote tunayoiona hapa ya Halmashauri. Tuweke uwazi ili watu waombe, pawe na uchujaji ili watu wapate hizi nafasi kwa uwazi, asiyefaa achukuliwe hatua na kadhalika, mtaona kelele zote hizi zitapungua. Kwa kweli hadi sasa namna wanavyopatikana hawa watu na hamishwa hamishwa zao tunahamisha tu, wanaolalamika na tunaonyamaza lakini shida ipo hapo. (*Makof*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napongeza taarifa zilizotolewa pamoja na mapendelekezo na maoni yaliyomo kwenye taarfia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kutelekezwa viwanda. Serikali yetu ina viwanda vingi sana lakini vingi havifanyi kazi au vibovu. Nani anaafuatilia ubovu wa viwanda hivi, hayupo! Kama yupo hafanyi maamuzi yaliyo sahihi. Kwa mfano viwanda vilivyoko Mwanza, Kiwanda cha Nguo na Ngozi vilivyoko Wilayani llemela vemetekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni *TBS* na bidhaa feki. Katika kitengo hiki, Serikali haiko makini kabisa. Wanaofanya biashara hizi za bidhaa bandia/feki ni aidha kwa:-

- (i) kuuza bidhaa zilzoishia muda;

(ii) kubandua lebo ya muda wa matumizi ya bidhaa hiyo na kuweka lebo ya bandia; na

(iii) kuchanganya bidhaa feki na zisizo feki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuwa na ukaguzi wa mara kwa mara katika maduka au maeneo mbalimbali kunakouzwa bidhaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuhamasisha watumishi wabadirif. Serikali hufanya makosa makubwa sana pindi anapopatikana mtumishi mbadhirifu badala ya kufukuzwa kazi hupewa uhamisho tu toka mahali alipokuwa na kupelekwa pengine. Hiyo si sahihi mtumishi huyu hapaswa kufukuzwa kazi mara moja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kukopa pesa katika Mifuko ya Jamii na kushindwa kulipa kwa wakati pesa hizo kunafanya mashirika hayo ambayo yanatokana na michango ya wanachama kuwa na hali mbaya sana kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la utunzaji risiti katika manunuhi hayaifi sheria na taratibu na hii inatoa mwanya wa kutafuta risiti za kughushi na kusababishia Serikali kupata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utaratibu wa ununuhi wa magari ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Serikali inanunua magari kwa bei kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi inayokwenda vijijini haina viwango kulingana na pesa. Watumishi wa Halmashauri mfano ya Nkasi wameigeuza kama kichwa cha mwendawazimu, kila mfanyakazi anafanya kazi atakayo. Utashangaa baada ya kuanza kazi tu baada ya mwaka anajenga nyumba wakati hana mkopo wowote, mwaka wa pili ana gari, ukiangalia mshahara wake na mali aliyonayo utashangaa kabisa. Cha ajabu hao wazuia rushwa wana ofisi hapohapo mbele ya uso wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ifanye utaratibu wa kuchunguza sana kuhusu rushwa, mishahara hewa pia utumiaji wa magari haswa wakati wa kununua vipuri na mafuta hapo ndio wizi mkubwa sana unafanyika pia sherehe za ajabuajabu hazina umuhimu kwa wananchi na wakati wananchi hawana huduma muhimu sana kama maji, dawa, barabara na pia karibu shule nyingi hazina madawati hata Walimu hawatoshi kabisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema lingine kuhusu baadhi ya Mahakama zetu kshirikiana na baadhi ya watumishi wezi, kesi zao zikifika huko, wezi wanapewa haki na kuiingizia Serikali hasara kubwa sana, Mahakama nazo zichunguzwe.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2009/2010 imedhihirisha kuwa matumizi mabaya ya rasilimali za umma ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Hata hivyo, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Hesabu za Serikali na ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009 hayajatekelezwa kwa ukamilifu. Hivyo mkazo wa maoni na mapendekezo ya Kamati kwenye sehemu ya tano, kifungu cha 5.0 ulipaswa kuanzia kwa pendekteko la Kamati juu ya hatua ambazo Bunge linapaswa kuchukua kutokana na Serikali kutoteketeza mapendekezo ya Kamati kutokana na taarifa iliyopita. Hivyo wakati wa kuhitimisha hoja, naomba Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali atoe pendekteko ili Bunge lipitishe Azimio Maalum kuhusu maoni na mapendekezo ambayo hayajashughulikiwa na hivyo upungufu husika kujirudia katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2009/2010, katika sehemu ya pili, ya tatu na ya nne, taarifa ya Kamati ya Fedha za Serikali, imechambua vizuri ukiukwaji wa sheria, kanuni za fedha na tuhuma za ubadhirifu zilizoibuliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha husika. Hata hivyo, katika sehemu ya tano ya taarifa ya Kamati hakuna maoni na mapendekezo yaliyotolewa kwa ajili ya hatua kuchukuliwa dhidi ya waliohusika na kusababisha hali hiyo. Hivyo napendekeza kuongezewe katika sehemu ya tano, kipengele cha (x) kuhusu maoni na mapendekezo kuhusu kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha Na.6 ya mwaka 2001 na upungufu ulioelezwa na CAG na Kamati unaohitaji hatua za kinidhamu na kisheria kuchukuliwa, kiwe kifungu cha 5.16 chenye maoni na mapendekezo ya kuwezesha hatua kuchukuliwa na Serikali kutoa taarifa kwa Bunge. Kama siyo kuongeza katika taarifa ya Kamati, napendekeza Bunge lipitishe Azimio la kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Maafisa Masuuli wa Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ambao wamethibitika kukiuka sheria au kusababisha matumizi yasiyostahili ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye sehemu ya tano, kipengele cha (iv) na kifungu cha 5.8 katika utekelezaji wake, Serikali ichukue hatua za dharura kwenye Mkutano wa Nane wa Bunge la Bajeti kuleta Muswada wa Sheria ya Kodi ili kudhibiti mianya ya misamaha ya kodi ikiwemo kuweka ukomo

wa kisheria kuwa misamaha ya kodi isizidi asilimia 5% ya kiwango cha ujumla cha mapato ya kodi. Tatizo kubwa la nchi yetu na uchumi wetu kwa sasa ni kuwa na matumizi makubwa kinyume cha makusanyo na kuwa na matumizi yasiyo ya lazima na mengine yakiwa na mianya ya ufisadi. Hali hiyo ipo mpaka mwaka wa fedha 2011/2012 ambapo kwa mfano tarehe 20/3/2012, makusanyo ya Serikali yalikuwa takribani shilingi bilioni saba (7), wakati malipo shilingi bilioni 18 huku tarehe 21/03/2012 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 58 wakati malipo ni shilingi bilioni 142 hali ambayo inakwamisha miradi ya maendeleo na inaongeza deni la taifa. Matumizi hayo yasiyo ya lazima ni pamoja na ya safari na malazi mfano katika Benki Kuu pekee Ofisi ya Gavana (A/C no. 9949610801 na 9949613701) zaidi ya shilingi milioni 500 zimetumika mpaka mwezi Machi 2012. Hivyo, Kamati pamoja na kupendekeza kupunguzwa matumizi ya maonyesho kama ilivyotoa maoni kwenye 5.5, iisimamie Serikali kudhibiti matumizi ya safari na kumshauri CAG kufanya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha za sherehe za miaka 50 ya uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taarifa ya Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, mashirika ya umma ni vyombo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi kwa kuongeza ajira na kuchangia katika kutoa huduma kwa wananchi. Hata hivyo, mchango wa mashirika ya umma na ya binafsi ambayo Serikali ina hisa zenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni kumi, ni mdogo ukilinganisha na fursa zilizopo. Hali hii inatokana na kasoro zilizopo kwenye hesabu za sehemu kubwa ya mashirika husika, ufanisi mdogo wa mashirika na upungufu uliojitekeza katika utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30, 2010, nimesoma mjadala wa maudhui na uchambuzi wa taarifa husika, nina mchango ufuatao kwa Kamati husika na Serikali kutokana na maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, utekelezaji wa mapendekezo ya kifungu cha 7.2.5 kuhusu STAMICO 7.2.6 na 7.2.12 kuhusu TPDC na 7.2.13 kuhusu TANESCO uzingatie pia maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu masuala tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naunga mkono pendekezo la ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendesha Uchunguzi Maalum (*inquiry on privatization policy and process*). Hata hivyo, wakati uchunguzi huo mpana ukiendelea, Serikali iwasilishe Bungeni taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ya mashirika 69 yaliyobinafsishwa uliofanywa mwaka 2011 ambapo inaonyesha kwamba mashirika yanayofanya kazi vizuri na

kuzalisha faida ni chini ya 10%. Aidha, Serikali iwasilishe Bungeni taarifa za tathmini ya ubinafsishaji iliyofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2009 na mwaka 2010. Kati ya viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo naomba Kamati ivishughulikie ni vya eneo la viwanda la Ubungo (Urafiki, Ubungo Garments, Ubongo Farming Implements, Ubungo Maziwa, Ubungo Polysacks n.k.) kwa kuzingatia mapendekezo na mchango wangu wa mwaka 2011 kwa Serikali na Kamati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, katika kuhitimisha hoja, naomba Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma aongeze pendelekezo la 7.2.15 kuhusu mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30, 2009 kama lilivyowasilishwa Bungeni tarehe 6 Aprili, 2011 na mapendekezo ya CAG ya mwaka 2007/2008 ambayo mpaka sasa Serikali haijayatekeleza. Pendelekezo hilo itawezesha Bunge kupitisha Azimio la kuweka muda maalum kwa Serikali kutekeleza mapendekezo husika ili hatua za ziada zichukuliwe iwapo mapendekezo husika hayatakelezwa. Hii itawezesha hatua za haraka kuchukuliwa kuhusu mashirika ya umma mbalimbali ikiwemo kuharakishwa kuundwa kwa Bodi ya Shirika la Masoko Kariakoo ambapo Jiji la Dar es Salaam limewasiliana na ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI bila majibu yoyote; kushughulikia mashirika 34 ambayo mpaka sasa yapo specified huku mali zake zikiendelea kuteketea; kushughulikia kasoro zilizo jitokeza katika ubinafsishaji wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam ambapo Waziri Mkuu alielekeza CAG kufanya ukaguzi maalum kwa mwezi mmoja toka Agosti, 2011 lakini mpaka sasa taarifa ya uchunguzi husika haijawasilishwa Bungeni na kuongeza uwekezaji kwenye DAWASA na DAWASCO kama ilivyopendekezwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono uchambuzi wa Kamati kwenye kipengele 3.6 kuhusu Ruvu Chini, hatua za haraka zaidi zinahitajika ikiwemo Rais kufanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri, Bunge lipitishe Azimio la kutokuwa na imani na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kuhusu hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010. Hata hivyo nitaelekeza mchango wangu katika sehemu ya tatu ya mapendekezo na changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Hoja/Pendekezo 3.1.2 la kuongeza mapato na makusanyo ya fedha katika Halmashauri, ikiwemo kuitaka Serikali, kuwasilisha taarifa ya tathmini ya ufanisi wa Sheria na mfumo wa kuitumia Mamlaka ya Mapato (TRA) kukusanya kodi ya

majengo katika Halmashauri za Manispaa, ikiwemo ya Kinodnoni. Katika kutoa taarifa hiyo, Serikali itoe maelezo kuhusu tathmini ya majengo (*Property Valuation*) ambayo Serikali ilitoa kandarasi kwa makampuni mbalimbali kufanya kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, lakini matokeo ya kazi hayalingani na kiwango cha fedha kilichotumika mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 3.1.6, pamoja na Serikali kutoa taarifa kuhusu mikataba na matumizi ya fedha ya mradi uliokufa wa machinjio na kiwanda cha nyama katika Jiji la Dar-es-Salaam, Serikali ichukue hatua juu ya wote waliohusika na ubadhirifu wa zaidi ya billioni mbili. Aidha, Kamati ipanue wigo wa hatua hii ya usimamizi wa vyanzo vya mapato na vitega uchumi vya Jiji la Dar-es-Salaam, kwa kushirikiana na CAG kufanya ukaguzi wa kiufanisi (*Performance Audit*) kwa vitega uchumi vya Jiji vya Shirika la Maendeleo Dar-es-Salaam (*DDC*), *Machinga Complex*, Shirika la Masoko Kariakoo, kama ambavyo pia niliomba hatua hizo kuchukuliwa na Kamati, pamoja na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Kamati iitake Serikali, hususan Ofisi ya Waziri Mkuu, ieleze ni lini mapendekozo ya CAG kwa jiji la Dar-es-Salaam, kuhusu Ukaguzi Maalum (*Special Audit*) ya mapato na mikataba katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo (*UBT*). Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, ieleze ni lini Ukaguzi Maalum kuhusu Shirika la Usafiri Dar-es-Salaam (*UDA*) ambalo Waziri Mkuu aliahidi Bungeni mwezi Agosti, 2011 kuwa, ukaguzi ungefanyika katika kipindi cha mwezi mmoja, lakini mpaka sasa miezi zaidi ya saba imepita bila ripoti husika kuwasilishwa wala wahusika kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kifungu cha 3.1.10; uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba, upo ulegevu katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri. Naomba katika kutekeleza maoni na mapendekozo hayo, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na CAG, kufanya ukaguzi wa thamani (*Value for Money Audit*) katika miradi ya maji kwenye Manispaa ya Kinondoni kwa mwaka 2010/2011. Aidha, kuhusu 3.1.10 (b), kuwa elimisha Madiwani kuhusu mipaka yao; wakati wa kuhitimisha hoja Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, aishauri Serikali kutoa nakala kwa Wabunge na Madiwani, Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2011 na Kanuni zilizotungwa kufuatia Sheria hiyo mpya. Hii ni kwa kuzingatia kuwa Sheria hii mpya imeongeza Mamlaka ya Madiwani na nafasi yao katika mchakato wa zabuni na usimamizi wa mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, badala ya suala la Serikali kutokujibu hoja za miaka iliyopita, ikiwemo za 30 Juni, 2009 kuwekwa

kwenye changamoto, ni muhimu likawa sehemu ya maoni na mapendekezo ya Kamati kwenye 3.1 badala ya 3.2. Hivyo, Bunge lipitishe Azimio Maalum kutaka Serikali itoe maelekezo kwa kushindwa kushughulikia hoja zilizopita, ikiwemo agizo la LAAC kuhusu fidia ya wananchi wa nyumba tisa *River Side* na ujenzi wa barabara ya Makoka, Kata ya Makuburi.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi leo kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi taarifa za Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kupongeza kazi kubwa iliyofanywa na Wenyeviti wa Kamati na Wanakamati wote wa Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utaanzia kwenye ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwenye maeneo sugu juu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Ukurasa wa 12 wa Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, umeainisha mipango ya kibabe ya Serikali Kuu katika vyanzo vya mapato vilivyopo kwenye Halmashauri. Katika hoja hii ya Kamati, Napenda kujikita juu ya tabia ya Serikali Kuu ya ama kuchelewa au kutopeleka kabisa malipo ya *export levy* ya korosho zinazouzwa nje kwenye Halmashauri inayoongoza katika kilimo cha korosho katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma. Kamati hii imekuwa ikitoa mapendekezo ya Halmashauri zote kulipwa *export levy* tangu mwaka 2008/2009 lakini Serikali haijawahi kulifanyia kazi pendekezo hili mpaka sasa. Mpaka sasa makato ya asilimia 65 ya *export levy* ambayo mkutano wa wadau uliofanyika mwezi August, 2011 hapa Dodoma uliamua pesa hizo zipelekwe kwenye Halmashauri husika lakini mpaka leo hii Serikali haijawasilisha marekebisho ya sheria hiyo juu ya *export levy*. Naiomba Serikali itueleze ni kigugumizi gani kimeipata mpaka sasa imeshindwa kuwasilisha katika Bunge hili marekebisho hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka 2010/2011, Serikali iliamua kurudisha chanzo cha leseni katika Manispaa, Majiji na Halmashauri mbalimbali nchini. Serikali ilitoa ahadi ya kwamba mpaka Januari 2012 *regulations* zitakuwa zimekamilika na mapato ya leseni yataanza kukusanywa. Hata hivyo mpaka sasa hakuna *regulations* zozote zilizoletwa, mapato ya leseni hayajaanza kukusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo zito kuliko yote ni Serikali kuamua kusitisha kupeleka ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato ilivyofuta wakati ikijua wazi haijakamilisha utaratibu wa kuziwezesha Halmashauri

mbalimbali kuanza kukusanya mapato hayo ya leseni. Hatua hii ya Serikali kusitisha kupeleka fidia bila ya kulishirikisha Bunge lako Tukufu imeletwa athari kubwa katika Halmashauri zote nchini na kuzipunguzia uwezo Halmashauri hizo katika kutekeleza mipango mbalimbali iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Halmashauri hizo zimeshindwa hata kufanya vikao vyake vya kikanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuhusu mishahara hewa inayolipwa kwa wafanyakazi ambao pengine wamekufa, wameachishwa kazi au kustaaifu. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya mishahara hewa ya shilingi 583,221,297 zililipwa. Tatizo hili ni sugu na limeendelea kujitokeza katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Inasikitisha kuona kwamba tatizo linaendelea. Mfano mwaka huu ripoti ya CAG ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ukurasa wa 81, jumla ya shilingi 961,394,959 zililipwa. Ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 378,128,662. Naiomba Serikali itoe tamko ni lini tatizo hili litakomeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Fedha za Umma (*Public Audit Act*) ya mwaka 2008, imempa mamlaka CAG kuwasilisha ripoti kwa vyombo vya TAKUKURU DCI, DPP ili ripoti hizo zifanyiwe kazi. Lakini ufanisi wa kifungu hiki bado haujaonekana, ripoti za CAG zinazoashiria ubadhirifu katika baadhi ya maeneo pamoja na kupelekwa kwa DCI, DPP na TAKUKURU hakuna ripoti yoyote/au hatua zozote zilizochukuliwa na taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ukaguzi Maalum wa Halmashauri ya Kishapu zaidi ya shilingi bilioni tano zimegunduliwa kutumika vibaya. Pamoja na taasisi hizo kuanza kuzifanyia kazi, tuhuma za ubadhirifu kwa muda wa mwaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na mamlaka hizo na hakuna mtu yejote aliyefikishwa Mahakamani kwa kuhusika na ubadhirifu huo. Mimi mawazo yangu ni kwamba pengine taasisi hizo zinashindwa kutimiza wajibu huu kwa mujibu wa kifungu cha 27 kwa kukosa weledi katika uchunguzi huo. Haiwezekani uchunguzi huo uchukue muda mrefu zaidi ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kushauri kuwa licha ya kifungu 27, sheria zingine za uchunguzi zifanyiwe marekebisho ili kuzipa mamlaka DCI, DPP, TAKUKURU katika suala zima la uchunguzi wa tuhuma za matumizi mabaya ya pesa. Mamlaka hizi zikipewa muda maalum wa kufanya uchunguzi ili hatua za kisheria zichukuliwe mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono mapendekezo yote yaliyowasilishwa na Kamati zote za Fedha.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia katika taarifa hizi tatu zilizowasilishwa na Kamati pia na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Wenyeviti wa Kamati hii kwa maagizo waliyoyatoa kwa Serikali. Pia kwa namna ya pekee, nimpongeze CAG kwa taarifa zake na maagizo aliyoyatoa kwa Serikali kuhusu utendaji na ubadhirifu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka huu, Serikali iliangularie kwa kina suala la kuiongezea bajeti ya kutosha Ofisa ya CAG na kurekebisha sheria itakayoruhusu kumpa uhuru wa kuajiri watumishi wanaofaa ili wamsaidie katika kazi zake. Pia ni ili aweze kufanya kazi kwa upana zaidi ikiwemo kufanya kaguzi maalum angalau tano (5) akishirikiana na watendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi iliyokaguliwa, ufinyu wa bajeti umekuwa ukichangia kwa kiasi kikubwa miradi iliyotekelawa kutomaliza ukaguzi. Ipo baadhi ya miradi ya mwaka 2008/2009 ambayo haikufikiwa na Kamati, pia ipo baadhi ya miradi ya 2009/2010 pia nayo haikuweza kufikiwa na Kamati kwa ukaguzi. Kwa miradi iliyopangia fedha ni vyema kuiona kuliko kuipitia katika vitabu na mara nydingi katika kaguzi tunazofanya tumekuwa tukigundua miradi iliyotekelawa haifanani na fedha iliyotumika na hata mikataba nayo haifanani na fedha iliyotumika. Hivyo basi, naiomba Serikali katika bajeti ijayo iangalie namna ya kuiongezea bajeti Fungu Na. 42 ili kuwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Pia fedha za miradi ya maendeleo ziongezwe angalau zifanane na miradi iliyopo ili kuweza kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa kujitegemea, bado Halmashauri hadi sasa hazijaweza kujijengea uwezo wa kujitegemea. Udhifu huu umesababishwa na kutokuwa na utalaam wa kujipangia makusanyo zaidi kutokana na vyanzo vya mapato walivyonavyo. Tulijaribu kama Kamati kwa baadhi ya Halmashauri kwa mfano Halmashauri ya Hanang kuwapangia makusanyo kwa maana ya kujenga uwezo wa kujitegemea wakavuka lengo tulilowawekea. Hivyo basi ni vyema Serikali ikawa karibu na Halmashauri kwa kuwapatia ushauri mbalimbali ili kuondoa utegemezi nchini. Pia kuendelea kupeleka asilimia 20 za vijiji kwani bado idadi kubwa ya Halmashauri wanaendelea kujilimbikizia madeni ya vijiji siku hadi siku. Nashauri wapeleke fedha hizo vijijini ili navyo viweze kutekeleza miradi waliyojipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la taifa hadi sasa linaendelea kukua kutoka asilimia 10.5 trillioni hadi 14.4 trillioni mwaka jana ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 38. Hapa ni vyema kujuliza maswali ya msingi yafuatayo ili kuweza kutoa majibu ya ongezeko la deni hili. Ni kweli kwamba deni la taifa halikwepeki lakini, je, baada ya kukopa deni hili linaendelea kuongezeka zaidi sababu ni nini? Je, Serikali kutoa fedha nydingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa wananchi? Au ni kutohana na jitihada za kuwapatia mikopo wananchi wa Tanzania ili kujiongezea kipato? Au ni kutohana na ubadhirifu wa fedha za umma unaoendelea kufanyika? Au ni kutohana na fedha za watumishi hewa zilizofikia shilingi 1.18 bilioni? Au ni kutohana na misamaha ya kodi zinazoendelea hadi kufikia 1.02 trillioni?

Baada ya majibu ya maswali haya ya msingi sasa Serikali iangalie namna ya kuchukua hatua zinazofaa kuepuka au kulipunguza kwa kiasi kikubwa deni hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Watumishi hewa. Ni muda mrefu sasa katika ripoti ya CAG na hata zile taarifa za Kamati zimekuwa zikieleza kuhusu suala hilo ambalo limekuwa likiathiri sana juhudhi za Serikali. Lakini bado leo hii Serikal hajajaleta jibu lolote linalohusiana na hatua zilizochukuliwa. Leo Serikali imetupa majibu kwamba imeunda Tume ya kushughulikia watumishi hewa. Je, taarifa za CAG haziaminiki? Je, Kamati za Bunge nazo haziaminiki?

Ni nani aliyeunda Tume hiyo ambayo imeongeza tena matumizi ya fedha za umma kwa kuwalipa Tume posho za kujikimu na *sitting allowances*. Hii ndiyo taratibu kwa mujibu wa Katiba pamoja na kwamba CAG anafanya kazi kwa mujibu wa Katiba.

Hivi Serikali baada ya kusema pamoja na kwamba hatujachukua hatua kwa waliohusika, lakini tumelazimika kutoa taarifa ya kurudishwa fedha hiyo Hazina mpaka hapo baadaye. Naomba Serikali itupatia majibu yenye kuridhisha kuhusiana na fedha hizi kwani fedha zinaendelea kuathiri maendeleo na kukosesha miradi mingine kupata fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muda mrefu wa kukaimu kwa Watendaji ndani ya Halmashauri pamoja na ubadilishaji wa vituo vya kazi baada ya kugundulika na ubadhirifu. Kutohana na muda mrefu kwa watumishi kuendelea kukaimu. Naomba Bunge likubali kuleta sheria hapa Bungeni kufanya marekebisho, badala ya miaka saba na badala yake

angalau iwe miaka mitano au minne. Muda mrefu kukaimu kunachangia kwa kiwango kikubwa kutokufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kubadilishwa vituo vya kazi watumishi waliogundulika na ubadhirifu wa fedha. Naomba Serikali kuwachukulia hatua zinazofaa watumishi hao kama maagizo ya Kamati yaliyowasilishwa. Kuendelea kubaki vituo vingine ni kueneza sumu za matumizi mabaya ya fedha za umma.

Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Singida. Naomba niwapongeze Halmashauri ya Mkoa wa Singida kwa kuanzisha na kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Naiomba Serikali kuendelea kuwatengea fedha za kutosha ili kumaliza maeneo yaliyobaki. Kufanikiwa kwa hospitali hiyo ni manufaa kwa Singida na mikoa jirani. Kwa sasa imeshatumia jumla ya shilingi 50 bilioni. Hospitali ya kisasa na ina viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja za Kamati.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongozi kwa taarifa na ripoti ya mwaka na hoja za Kamati kuhusu hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu siyo sikivu na Mawaziri wetu hawajali wala kuwaonea huruma Watanzania wake wao wanajali nafasi zao na kutaka sifa tu.

(1) Taarifa ya CAG inayotolewa kila mwaka hakuna hatua zilizochukuliwa kwa watuhumiwa. Pia wale ambao wamefanya ubadhirifu wowote wa fedha za umma hutetewa na Mawaziri hao na kuwakumbatia.

(2) Taarifa ya ukaguzi na Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Wilaya kwa mwaka 2009/2010 na mwaka 2010/2011, imeonyesha ubadhirifu, sababu ya ubadhirifu, vipindi vya ubadhirifu, athari za ubadhirifu na wahusika wa ubadhirifu huo, lakini hawakuchukuliwa hatua matokeo yake hukumbatiwa na kulindwa mfano Kishapu, Hanang, Singida, Babati, Kiteto na Wilaya zingine. Nashauri kwamba wote wanaohusika wafikishwe Mahakamani, waachishwe kazi na kuflisiwa mali zao walizopata bila uhalali au kwa kuiba fedha za wananchi kwa ajili ya miradi yao.

Katika Halmashauri kuna utaratibu mbovu wa:-

(i) Kufungua Akaunti hewa na kudai zinapelekwa hela vijijini. Akaunti za Kata hakuna fedha zilizoenda kijijini. Fedha na vyanzo vya mapato ya vyanzo vilivyofutwa na mapato ya ndani.

(ii) Fedha za miradi kutopelekwa vijijini mfano:-

(a) Fedha za *Road Toll* za Wilaya kuonyesha miradi hewa kwenye karatasi, barabara hazikutengenezwa.

(b) Fedha za MAMM

(c) Fedha MESS

(d) Fedha MEM

(e) Fedha ya maji

(f) Fedha za Kilimo *DADs*

(g) Fedha za *CDG*

(h) Mapato ya ndani.

(3) Ripoti ya CAG 2010/2011, amesema NSSF iko hatarini kafilisika kwa kutokurejeshewa fedha zilizokopwa na Serikali. Kwa kuwa Serikali ilidhamini miradi hiyo mbalimbali irejeshe hiyo fedha haraka sana kwa kuwa hayo mashirika yana wanachama wao. Hata hivyo, wanachama wanaokatwa hizo fedha hawajaombwa. Mashirika hayo NSSF -i 234.1 bilioni, PSPF – 105.9 bilioni, PPF – 39.99 bilioni, LAPF 22.00 bilioni, NHIF – 13.4 bilioni.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya ubinafsiahaji kupitiwa upya, nashauri iongezewe uzito kwa mikataba yote kuwekwa wazi. Hapa tunaweza kujifunza uzoefu wa nchi ya Ghana ambapo mikataba sio siri baada ya kusainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Kamati iongeze uzito kufuatilia kinachoendelea Mgodi wa Chumvi Uvinza kwani mpaka sasa *CHC* imekamilisha taarifa ya uchunguzi ambayo imepelekwa kwa Waziri lakini hatua hazijachukuliwa. Mwekezaji ameuza mitambo na nyumba za mgodi kinyume cha mkataba. Hapa hoja ni mkataba uvunjwe. Uvunjwe kwa sababu mwekezaji amekiuka na kwa maelezo niliyopewa na Kaimu Mkurugenzi wa *CHC* ni kwamba mwekezaji amekiri kukiuka baadhi ya maeneo ya mkataba.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina haya ya kuchangia:-

- (1) Wakuu wengi wa Idara kukaimu, hili mpaka lini?
- (2) Kucheleweshwa kwa fedha za maendeleo kupelekwa katika Halmashauri za Tanzania. Ucheleweshaji wa fedha kunadumaza maendeleo ya nchi.
- (3) Viwanda vyta korosho vilivyobinafsishwa kutoendelezwa tena ni kwa nini? Mikoa ya Lindi na Mtwara yenye viwanda hivyo haiendelei kwani viwanda hivyo hadi sasa havifanyi kazi na vilevile korosho hazinunuliwi.
- (4) Mpaka sasa wakulima wa korosho hawajapata pesa mara ya pili.
- (5) Madiwani hadi sasa hawajongezewa pesa za posho au mishahara. Ninaomba ufanuzi.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nizipongeze Kamati zote tatu kwa taarifa zao nzuri zinazolenga kuonyesha matatizo halisi yanayostahili marekebisho ya haraka kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali za Mitaa ndio utekelezaji wa miradi ya maendeleo na maisha bora kwa kila Mtanzania. Niiombe Serikali ihakikishe kuwa inapeleka ruzuku ili Serikali za Mitaa kuitia Halmashauri zao ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, watendaji wa Halmashauri katika Halmashauri zilizo nyingi ni aidha hawana taaluma ya kutosha au ni ufisadi kwa maana hawatoi mikataba na wala kufanya/kutekeleza miradi ya maendeleo kuitia wakarandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Madiwani hawana nafasi ya kushiriki katika maamuzi muhimu ya matumizi ya fedha hizi kwa sababu hawashirikishwi katika mchakato wote wa kutoa zabuni. Niiombe Serikali iangalie upya usimamizi wa Halmashauri zetu hizi kwa kuhakikisha kila mtumishi anawajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Mashirika ya Umma yamezidi kudorora kwa sababu Serikali imezidi kuingilia utendaji wa kila siku wa mashirika haya. Muda umefika uongozi wa mashirika haya wapewe uhuru

Iakini malengo na Serikali yabakie kupima malengo kwa maana ya utendaji wake na hapohapo Serikali ichukue hatua kwa utendaji usiofikia malengo. Serikali itoe mitaji ya kutosha na isimamie vyema fedha hizi za Serikali? Mbona nchi nyingine za Afrika Mashariki, mashirika yake yanafanya vizuri mfano mashirika ya ndege, utangazaji, bandari, simu, reli kwani kuna mdudu gani Tanzania? Nashauri sasa Serikali iamke na ifanye kazi kwa malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Serikali sasa itoke mahali ipange bajeti halisi (*realistic*) ili iweze kupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa utekelezaji. Serikali ichukue hatua ya kuziba mianya ya wizi, mikataba mibovu, rushwa na kudhibiti watendaji wake ili kurudisha heshima ya Serikali na adabu ya matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika Kamati hii ya Mashirika ya Umma kama ifuatavyo:-

Kwanza, manunuzi mabaya katika Mashirika ya Umma au kwa maneno mengine ni kutozingatiwa Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake. Ukiukwaji huu umekuwa ukiisababishia Serikali hasara kubwa na kutotumia hela au kufanya matumizi mabovu ambayo mengi yanafanyika tu pale mtu/watu wanapoona wana maslahi katika utekelezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama manunuzi haya hayatakiukwa yataokoa ufujaji wa fedha za umma, yatasaidia wananchi kupata huduma za lazima kwani hela zitaenda katika miradi ya maendeleo mfano kutengeneza barabara, hospitali, elimu n.k.

Mfano mzuri hapa ni Shirika la Umeme TANESCO ambalo kwa mwaka wa fedha 2009/2010 lilitumia kiasi cha shilingi bilioni 258. Fedha hizo ni nyingi sana, hivyo ni bora taasisi hizi zifuate na kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda pia kuchangia kuhusu upungufu katika ukodishaji wa ndege uliofanywa na Shirika la Ndege Tanzania - ATCL. Serikali ilitoa dhamana kwa Shirika hili mwaka 2007 ili liweze kukodisha ndege aina ya Air-bus 420-214 kutoka nchini Lebanon kwa muda wa miaka sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza iligundulika kuwa mkataba ulitiwa saini kinyume cha Sheria /ushauri wa wataalamu ambao katika

taarifa walisema sio sahihi kukodi ndege ambayo baada ya miezi sita italazimika kupelekwa katika matengenezo ya lazima. Vilevile ndege hiyo ilikuwa inakodiwa kwa kiasi kikubwa sana cha pesa shilingi bilioni 108 na pia ndege hiyo ilipokodiwa iliendelea kubaki mikononi mwa mkodishaji kwa muda mrefu toka mkataba usainiwe mwezi Oktoba, 2007 hadi Mei, 2008 kutokana na kuchelewa kwa dhamana ya Serikali. Hata hivyo, ndege ilipowasili nchini mwezi Mei, 2008 ilifanya kazi kwa miezi sita tu na kupelekwa nchini Ufaransa kwa matengenezo makubwa kama ilivyokuwa katika mkataba huo. Huu ni utumiaji mbaya sana wa fedha za umma na kutokujali nini makubaliano katika mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndio mchango wangu katika Kamati hii.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mawazo yafuatayo kuhusiana na Hesabu za Serikali za Mitaa. Tumesikia ubadhirifu mwangi katika Halmashauri zetu za Wilaya wa mabilioni ya pesa na tumeona wafanyakazi wa Halmashauri hizo wakihamishwa kutoka Halmashauri moja hadi nyingine bila kuchukuliwa hatua. Hali hii inasababisha watumishi hawa hata kule wanakokwenda kuendelea kufanya ubadhirifu wakijua kwamba baadaye watahamishwa na kupelekwa katika Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine nililoliona ni kutowashirikisha Madiwani wakati wa utaratibu mzima wa michakato ya zabuni mbalimbali zinazotolewa katika Halmashauri na hivyo kuwapa mwanya watumishi hawa wa Halmashauri kuiba fedha nyingi. Ninafikiri Madiwani waruhusiwe kuingia ndani ya vikao vyta tenda wakati wa kuchagua wazabuni husika. Hii itapunguza ubadhirifu huu mkubwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miradi mbalimbali kama vile shule kwa maana ya madarasa, zahanati na miradi mingine kujengwa kwa kiwango cha chini, ni kwa nini inatoka hivyo wakati ujenzi wa miradi hii tayari ilishapangiwa bajeti ya kutosheleza ujenzi huo, ni kwa nini sasa ujenzi huo uwe chini ya kiwango? Kwa maana hiyo, hayo yanafanywa kwa makusudi kabisa kwa nia ya kufanya wizi na ni nani sasa anapokea mradi huo ambao umejengwa chini ya viwango? Inapotokea ubadhirifu ndani ya Halmashauri zetu, ni vema wafanyakazi hawa wafukuzwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kushukuru kwa taarifa ya Kamati zote za Mahesabu kwa kutoa taarifa zenye ushauri wa kutukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kama ifuatavyo:-

(1) Kutekeleza maoni ya CAG kuhusu ubadhirifu wa mali ya umma. Hatua zinazochukuliwa zifahamike kwa wananchi.

(2) Waziri Mkuu awe mkali sana kwa Baraza la Mawaziri ili wawajibike kwa wananchi na kusimamia miradi mbalimbali na ahadi zao kwa wananchi.

(3) Taarifa ya CAG ipate majibu ya Serikali na Wabunge wasome majibu hayo ili ufahamu uwe mkubwa zaidi na kuondoa mkanganyiko unaojitokeza katika jamii.

(4) Mawaziri wawe na mahusiano mazuri na Kamati za Bunge, kwani inaonekana kuna udhaifu mkubwa.

(5) Vikao vya Madiwani vifanyike wakati Wabunge hawana vikao.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lisiloingia akilini na inafanya mtu uwe na akili kama ya mwendawazimu kuyaelewa. Ni jambo linalotia hasira wananchi kwani kila mwaka fedha zimekuwa zinapotea na Serikali Kuu haikuchukui hatua. Ripoti ya CAG kila mwaka imekuwa ikitoa maoni yake bila Serikali kuchukua hatua kwa wahusika. Jambo hili limekuwa likiwakatisha tamaa sana wananchi, inasikitisha kuona hata katika Halmashauri zetu fedha za miradi ya maendeleo zimekuwa zikitafunwa na wafanyakazi wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taarifa zote tatu za Kamati za Usimamizi wa Fedha za wananchi wetu zinaonesha dhahiri upotevu mkubwa wa fedha na wananchi wanazidi kuwa maskini, basi ni vyema Bunge liazimie kutumia Kanuni zake ili wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa taarifa ya Hesabu za Serikali. Serikali inatumia pesa nydingi sana katika matumizi ambayo siyo ya lazima. Mfano ziara za Rais nje ya nchi, idadi ya wasafiri ipungue ili kupunguza matumizi. Pia viongozi wa Serikali kuruhusiwa kukaa hotelini kwa muda mrefu ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye kazi na donors kwa umakini zaidi. Mfano kukatisha Ubalozi wa Uholanzi ambao ni washiriki wetu wa muda mrefu. Kwa muda wa miaka 20 Ubalozi haujarudishwa. Matokeo yake kero zinatolewa na Balozi kuhusu kutoa au kutokutoa misaada, Serikali (Hazina) hajibju barua, wala kwenda kwenye mazungumzo. Mfano Euro milioni 80 ziliikuwa zilipwe na Serikali ya Uholanzi lakini Serikali kwa kutokujibu kero wanazozidai kuhusu mwekezaji kutoka Uholanzi kufutiwa mkataba, inawezekana kabisa mwekezaji huyu ndiye mwenye makosa, tatizo ni Serikali kutokujibu barua/kutokuhudhuria vikao husika mara wanapotakiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EDF* // inategemewa imalizikie mwaka 2014 mpaka sasa Serikali hajajipanga ni namna gani huo mfuko utaendelea. Wakati huohuo *EU* wanashinikiza kuiwekea kikomo katika *Revolution 1528* ili nchi za dunia ya tatu (Tanzania ikiwepo) ziji tegemee hata katika kuza mazao yao, yaliyokuwa yanauzwa kwa *Quotas (Commodity protocols etc)* *Revolution 1528* ikifutwa itakuwa tatizo kwa Tanzania. Serikali inatakiwa i-negotiate ili hizo *commodity protocols* zisifutwe na hata zikifutwa basi kuwepo na mpango mwingine wa kuiwezesha Tanzania kuza mazao yake bila kodi ili fedha itakayopatikana ya ziada ifufue viwanda nchi ipate ajira kwa watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *PEFA reports* inayotoka kwa wahisani ipewe Wabunge mapema ili waweze kuisimamia Serikali kwa upungufu ambao utakuwa umeainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itengeneze idara ya *Consultant/Property Management* ambayo itashughulikia majengo ya Serikali yaliyoko nje ya nchi. Yapo majengo Washington, USA na New York/London ambayo yanaweza kutengenezwa yakaleta fedha nyingi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweza kupata mapato ya kutosha kwa ku-*identify* walipa kodi wote. Serikali ituambie *TRA* ina mpango gani wa ku-*identify* walipa kodi walioko vijijini. Mfano Ukanda wa Ziwa, mfugaji ana ng'ombe zaidi ya 10,000, *TRA* inamfikia vipi? Inakadiriwa walipa kodi ni milioni 1.6 ingawa idadi ya Watanzania ni milioni 40. Watanzania zaidi ya 80% hawalipi kodi, Serikali itueleze mkakati wa kuwapatia walipa kodi hao. Serikali itapataje kodi from the informal sector?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani wa kumpa Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG mamlaka zaidi ili aweze

kupeleka Mahakamani wale wafanyakazi wote anaogundua wamefanya ubadhirifu wa fedha ya Serikali? Mamlaka aliyonayo sasa hivi wanagubikwa na urasimu wa kupeleka kesi kwa *DPP* na mwisho wa siku wabadirifu wengi hawajibishwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa nyngi zingepatikana kutoka kwenye mazao ya misitu. Serikali inakosa pesa hizi na badala yake watu wabaya wanaiba na kuvuna misitu bia kibali. Je, ni lini hii Serikali itashirikisha wananchi wanaozunguka misitu/hifadhi na kuwalipa asilimia ya staili yao ili wailinde na kuihifadhi misiti hiyo? (*Performance Forest Management*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke umuhimu katika mavuno ya gesi inayotarajiwa kuvunwa. Mikataba ya gesi hii iwe na uwazi na usambazaji wake uwe wa msaada kwa Watanzania. Wananchi wakipata gesi wataacha kukata miti na hivyo misitu itaboreka na tutapata mvua nyngi hatimaye kuondokana na tatizo la njaa. Serikali itueleze Bunge hili limejiandaa vipi kwa hili zao la gesi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata ufanuzi, ndiyo nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nashukuru kwa Taarifa ya Hesabu za Mashirika ya Umma yenye umakini. Serikali, ifungue viwanda vilivyofungwa, ili kuleta pato zaidi na ajira. Inawezekana vikafunguliwa kupitia *Public Private Partnership*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yapunguze ghamra za matumizi, kwa mfano, tiketi za daraja la kwanza za ndege kwa Wakurugenzi Wakuu na Wasaidizi, watumie daraja la pili (*Business Class*). Mashirika yaliyo chini ya *CHC* yauzwe kwa wawekezaji wenyе uwezo, ili waanzishe viwanda kuleta pato la Taifa na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni za kigeni zinazopata punguzo la kodi (*Tax Holiday*), ziangaliwe vizuri zinapouziana hisa. Gawio la *Capital Gains Tax*, litozwe pale inapofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika, wachukuliwe Watanzania wenyе uwezo wa kuongoza (*Management Skills*). Wapatikane kwa njia ya ushindani, ili wapatikane wanaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tanzania Investment Centre*, isaidie Serikali kupata *Land Bank*. Mikataba na wawekezaji hawa, iwe ya uwazi na kamilifu, isifungwe na rushwa. Mikataba hii, iwe ya manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Umeme lina mzigo mkubwa, sababu mojawapo ni kutokuwa na mpango mkakati wa kudumu. Muda wote Serikali imekuwa na mpango wa dharura. Mara nyingi mikataba imekuwa ikigubikwa na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilieleze Bunge, kuna mkakati gani wa kudumu wa kuhakikisha Watanzania wanapata umeme wa kudumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maji la Dar-es-Salaam (DAWASCO) nao wana *Private Sector*. Waweke bomba vizuri, maji yasipotee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Shirika la Nyumba (*NHC*). Waendelee kujenga nyumba na pale inapowezekana wauze kwa wananchi. Bei pia, ziangaliwe zisiwe za juu mno, ili Mtanzania wa kawaida asishindwe kulipa kodi ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufanuzi kuhusu suala la TANESCO.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya zikusanye mapato zaidi kutoka vyanzo vyake, yapo maeneo mengi kama Serikali itawaachia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi zinatafunwa sana na Halmashauri ya Wilaya. Mfano, fedha za UKIMWI. Semina zinafanyika ambazo wadau sio walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Idara husika (mfano, Ujenzi) wana *team up* na wakandarasi na mara nyingi wanatoa siri za tenda (bei).

Mheshimiwa Naibu Spika, tenda nyingi zinazofanyika ni za Madiwani ambao wanajificha nyuma ya vivuli vya watu binafsi. Tenda ikishapatikana, utekelezaji haufanyiki ipasavyo kwa vile wadau au watendaji wanajenga hofu kwa Diwani na wanaogopa kumuuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zenyet hati, zenyet mashaka na chafu, Wakurugenzi wawajibishwe, wasipewe muda kwenda kurekebisha. Kama walikosea tangu mwanzo, marekebisho wanapata wapi? Mfano, kama Halmashauri ya Wilaya haikuweza kuonesha vitabu vya mapato 30 wakati wa ukaguzi, akipewa nafasi atakwenda kuvipata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya zenyе ripoti ambazo ni chafu zifikiriwe pia kufutwa angalau kwa muda ili wajifunze.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU au Usalama wa Taifa, wachunguze utekelezaji wa Halmashauri ya Wilaya, watoe taarifa Serikalini mapema, wasingoje mpaka pesa ziibwe ziishe. Rushwa inatembea kwa wakaguzi wa nje pia wanapokwenda kukagua vitabu katika Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya zitunze vyanzo vyake vya maji na kutunza misitu au hifadhi za misitu walizonazo. Utunzaji utachochaea mvua zaidi na hatimaye chakula zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zilizoko katika maeneo ya ufugaji, wahamasishe wafugaji kufanya biashara na mifugo yao, wafuge ng'ombe bora, wachache wenyе tija na wafanye pia biashara nyingine (*diversification*). Hili litamfanya mwananchi wa kawaida kupata kipato zaidi na pato la Halmashauri ya Wilaya na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zenyе mazao yanayoweza kusindikwa wanaasiwa au Halmashauri za Wilaya wasaidiane waanzishe viwanda vidogo vidogo kusindika mazao. Mfano, Ukanda wa Kaskazini Mashariki (Tanga) wasindike matunda, ukanda wa Ziwa wasindike nyama, samaki, ngozi, maziwa, jibini. Ukanda wa Kusini wasindike viazi na mbogamboga. Ukanda wa Kaskazini tangawizi na mbogamboga; wote wakisaidiwa na wafanyabiashara au Serikali au Mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufanuzi nitaunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali ndugu Ludovick Utoah pamoja na watalaam wote kwa kazi nzuri wanayofanya katika kudhibiti na kukagua mahesabu ya Mashirika ya Umma (POAC) kwa umakini na ufanisi wa juu. Kazi hii nzuri imesaidia sana Kamati ya Bunge ya POAC kufanya kazi yake vizuri kwa kukemea na kusaidia Serikali kujua dosari zinaonekana kwenye mahesabu ya mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, CAG na timu yake wanafanya kazi kubwa sana ya kugundua ubadhirifu wa matumizi ya fedha za Serikali kwa kutekeleza Miradi chini ya kiwango, kubadili matumizi ya fedha bila idhini ya Serikali ama kufuja fedha. Ninaiomba

Serikali iendelee kuwaongezea vitendea kazi ili wazidi kufanya kazi zao kwa ufanisi na wakati unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo na kutokuwatendea haki Ofisi ya CAG kama sitawapongeza kwa kusajiliwa kwa kuwa Wakaguzi wa Kimataifa, jambo ambalo limeiongezea sifa nchi yetu na kuongeza fedha za kigeni nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu pamoja na Kamati yake yote kwa kazi nzuri wanayofanya kuainisha upungufu wote wa taarifa za mahesabu ya Mashirika ya Umma (*POAC*) na kutoa taarifa na ushauri kwa Serikali. Kazi nzuri inayofanya na Kamati hii ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma kupewa Udhamini na Hazina katika kupewa tenda na taasisi za Serikali mfano tenda ya *UDOM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kwa wakati huu tayari Shirika la NSSF limekwishapewa udhamini na Hazina ya tenda yake ya kujenga majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), ingawa ukweli upo palepale kuwa udhamini huu ulichukua muda mrefu kitendo ambacho kiliifanya NSSF kufanya kazi hiyo kwa hofu kubwa kwa kuogopa kupoteza fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishauri Serikali kuwa Mashirika ya Pensheni yaani *PSPF*, *NSSF*, *PPF*, *LAPF* na *TPA* yanaweza kusaidia sana kutekeleza miradi mingi ya Serikali yakipewa tenda na kudhaminiwa na Hazina kwa wakati muafaka ili utekelezaji huo uanze mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma kusaidia miradi ya maendeleo. Napenda kutumia nafasi hii kuyapongeza mashirika yote ya Serikali ambayo yamekuwa yakisaidia miradi ya kijamii mfano ujenzi wa shule za sekondari, madawati na kadhalika. Ninaiomba Serikali kutoa hamasa na mashirika mengine kuiga mfano huo na yale yanayofanya hivyo yapongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono ushauri wa Kamati ya *POAC* hivyo namwomba Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma kuendelea kuhimiza Serikali na kuibana ili kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumaliza kwa kuunga mkono taarifa hizi mia kwa mia, Serikali iliongezee Bunge bajeti ili

waongeze muda wa Kamati kwa lengo la kunusuru fedha na umma na kubaini maeneo yanayotumia fedha hizo vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza CAG kwa kugundua watumishi hewa ambao wanasababisha kupotea kwa mamilioni ya fedha. Ushauri wa Kamati ufuatwe ili kubaini zaidi watumishi hewa na na kuwachukulia hatua za kisheria wanaohusika na uharibifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Kamati ya Bunge ya Mahesabu ya Serikali kwa ushauri wao wa matumizi mabaya ya magari, kwa kununua magari mengi zaidi ya matumizi, kununua magari ya kifahari, ambayo hata hayaendani na barabara za vijijini na safari nyingi ambazo siyo za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iangalie upya mipango mizuri ya kutumia magari ikiwa ni pamoja na kununua magari yanayoendana na barabara zetu, kupunguza idadi ya magari na kuepuka safari ambazo siyo za lazima au kupunguza misafara ya magari ya Serikali, yaani watendaji kutumia gari moja au mawili endapo safari ni moja. Hii itapunguza uharibifu wa fedha za mafuta au magari kuchakaa bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana, Serikali mara nyingi imekuwa ikipeleka fedha Wilayani na Mikoani chini ya kiwango kilichoombwa na kusababisha utendaji kukwama. Hivyo, ni vyema Serikali ikatekeleza viwango vinavyohitajika ili kuepuka madeni. Vile vile itaongeza ubora wa utendaji kwenye Ofisi zetu za Wilaya na Mikoa, Taasisi za Serikali na Wizara za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Kamati ya Mahesabu ya Serikali kuwa kuna tatizo la kutenga fedha kidogo za kutekeleza Miradi ya Serikali, jambo ambalo hufanya Miradi mingi huchukua muda mrefu kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema utekelezaji uwe wa Miradi michache kuliko kuwa na Miradi mingi kwa wakati mmoja, jambo ambalo linafanya Miradi mingi kuchukua muda mrefu kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la watendaji wabadhirifu kwenye Taasisi za Serikali kutokuchukuliwa hatua za kisheria, jambo ambalo linapoteza fedha nyingi na kusababisha utekelezaji wa Miradi kuwa chini ya kiwango au kusababisha watendaji waadilifu kukata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka pale CAG anapotoa taarifa ya ubadhirifu wa fedha ili kukomesha tabia hizi mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kushauri Serikali kukataza utaratibu wa Serikali kununua samani za ofisi na za nyumba za Serikali nchi za nje ambazo wala siyo imara; ni vyema litolewe tamko kuwa samani za ofisi zinunuliwe nchini kwani tuna miti imara ya mbao mfano mininga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii nikitegemea Serikali itapokea ushauri wangu na wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa kujadili kwa umakini mkubwa hesabu hizi kisha kutoa mapendekezo Serikalini pamoja na kushauri na hata kukemea kwa makosa yaliyo wazi. Naiomba Serikali ipokee ushauri wa Kamati na kuufanya kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi kuna tatizo kubwa sana la kutoa tenda kwenye miradi mbalimbali kwani Kamati ya Tenda ni wataalam watupu na inasemekana makampuni mengi humilikiwa na wataalam hao hao. Hivyo, kuna haja ya kuangalia upya Bodi ya Zabuni kuwa na Wajumbe mchanganyiko, yaani wataalam na Madiwani. Hii itasaidia kuwapata Wakandarasi wenyе kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna tatizo la baadhi ya Mikoa kukosa Wakandarasi wazuri wenyе miundombinu ya kutosha na imara, hivyo kusababisha Halmashauri zetu kutoa tenda kwa Wakandarasi ambaо hawana uwezo au vifaa vya kutosha. Napenda kushauri kila Mkoa kuwezeshwa kununua miundombinu ya ujenzi ili kuachana na makandarasi wasio na vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa masikitiko yangu kwa Watendaji wa Halmashauri kuendelea kutoa mishahara hewa kwa watumishi ambaо walishafariki siku nyingi, walishafukuzwa kazi ama kustaafu, kitendo ambacho kinapoteza fedha za Serikali ambazo zingeweza kunufaisha Watanzania maskini wakiwemo watoto yatima, wajane, au kununulia vifaa shulenii na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema uhakiki wa watumishi ufanyike upya ili kubaini watumishi hewa kisha kuwachukulia hatua kali Watendaji wanaohusika na uzembe huu wa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo la mgawo wa fedha za miradi ya maendeleo. Kumekuwa na tatizo la Halmashauri kutopewa mgao wa fedha za miradi ya maendeleo pale inapofanya vizuri kwa wananchi kushiriki ama Halmashauri kutafuta wahisani kwa juhudi zake. Ukweli, utaratibu huu ni mbaya, kwani unawanyima haki yao na pia unawavunja moyo. Ni vyema na wao waendelee kupewa mgao wa fedha ili kuwatia moyo kuliko kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo la Waheshimiwa Madiwani kuwa na uelewa mdogo wa kukagua hesabu za Halmashauri zetu. Hivyo, kuna kila sababu ya Serikali yetu kutenga fedha za kutosha za kutoa mafunzo kwa Madiwani ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kudhibiti fedha za Halmashauri zetu. Hii inatokana na Madiwani kuwa na uelewa wa fani tofauti na fani ya Uhasibu. Hii itawasadia sana Madiwani kuwa na upeo mkubwa wa uelewa wa kusimamia hesabu za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna kila sababu ya kuondoa kigezo cha kupata hati ya mashaka kuwa sababu ya Halmashauri kunyimwa fedha za maendeleo wakati uzembe huo hautokani na wananchi wa Halmashauri hiyo. Kosa la Watendaji wa Serikali ama Serikali yenye kuhusika, mfano, Halmashauri kuwa na Kaimu Wakuu wa Idara, nani aulizwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile lipo tatizo la Watendaji kumheshimu Mwajiri, lakini Madiwani hawaheshimiwi, ni jambo ambalo linawapa kiburi Watendaji wa Serikali na kusababisha wafanye maamuzi ambayo hudhalilisha Serikali. Kwa mfano, kuanza kutoza kodi kwa wananchi ambazo hazikupitishwa na Halmashauri hasa kipindi Madiwani wakijiu zulu kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu. Utaratibu huu huwafanya wananchi kuichukia Serikali yao kwa kosa la Watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu watumishi wa Serikali kuboreshewa mishahara na marupurupu yao. Nimekuwa nikitafakari muda mrefu ni kwanini wizi ndani ya Halmashauri zetu na Taasisi za Serikali hauishi? Nimegundua kwamba ni ukata mkubwa tu walionao ambao unasababisha kushindwa kumudu hali yao ya maisha ya kila siku pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuendelea kuboresha mishahara na marupurupu mengine ya watumishi ili kuwaondolea tamaa wafanyakazi ya kuendelea kuiibbia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuitaka Serikali kuzitolea maelezo hoja zangu zote. Ninatamka rasmi kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ambavyo ameweza kusimamia utendaji wa Kamati zote za Kudumu za Bunge. Pili, niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zilizotoa taarifa zao katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za CAG na za Kamati za *PAC*, *POAC* na *LAAC* zimeshabihiana kwa maana kwamba pamekuwepo na matumizi mabaya ya fedha za umma. Serikali haioni kwamba ni vyema ikazifanya kazi taarifa hizi muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu? Ni kweli pia kwamba taarifa hizi zimepatikana baada ya fedha nydingi za walipa kodi kutumika. Serikali haioni kwamba huu ni wakati muafaka kuwawajibisha watendaji wasio waaminifu kwa kuwafukuza na kuwapeleka Mahakamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji walio wengi katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini wamekuwa wafujaji wa fedha za umma kwa kutekeleza miradi ambayo miradi hiyo hailingani na thamani ya fedha iliyotumika (*value for money*). Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba watendaji wazingatie matumizi bora ya fedha za umma ili kupata tija na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *PAC* kama inavyooneshwa ukurasa wa 25 kwamba Serikali kwa makusudi haishirikishi Bunge kuhusu taarifa za *PEFA* na kwamba hali hii imelifanya Bunge lishindwe kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha za umma na kupelekea bajeti inayopitishwa na Bunge lako Tukufu ishindwe kufikia malengo. Hali hii ni hatari kwa mustakabali wa Taifa. Naomba Waziri wa Fedha na Uchumi aliambie Bunge sababu za msingi za kuficha taarifa ya *PEFA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la CAG kutokuwa huru katika masuala yahusuyo ajira ya watumishi. Hii pia ni hatari ndio maana Taifa zima linalalamika kuhusu wafanyakazi hewa. Nashauri kipengele kinachomzuia CAG kukagua masuala yahusuyo ajira ya watumishi kifutwe. Watumishi hewa wamelisababishia hasara ya mamillioni ya fedha Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine baya ni kuwepo kwa bajeti isiyokuwa na uhalisi. Naiomba Serikali ipange bajeti halisia yenye kuzingatia uwezo wa Serikali kukusanya mapato ili kutekeleza kazi za

mpango kwa ufanisi. Vilevile naiomba Serikali, Wizara ya Fedha ambayo ndio msimamizi wa masuala ya Serikali iache tabia ya kuchelewesha kutoa fedha kwenda kwenye taasisi zake ili zitekeleze mipango na kazi zake mbalimbali kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma vilevile inatisha hasa pale tunapoona Mashirika ya Umma baadhi yake yanaendeshwa kwa hasara. Mashirika ya Umma kama TANESCO linaendeshwa kwa hasara huku tukishuhudia Tanzania ikiwa sehemu kubwa haina huduma ya umeme, ni 16% tu ndio wanapata huduma ya umeme ambao pia ni wa mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naishauri Serikali yangu isikie kilio cha Waheshimiwa Wabunge, Mashirika na Wizara zake. Mwenye macho haambiwi tazama na mwenye masikio asikie.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwanza kuipongeza Kamati hii kwa namna ambayo inafanya kazi kwa dhamira kubwa ya uzalendo wa hali ya juu. Kipekee kabisa nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Augustino L. Mrema, kwa jinsi anavyosimamia Kamati hiyo, kwa kweli ni muwazi na nampongeza sana na kumwomba aendelee na moyo huohuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa ruzuku ya maendeleo katika Halmashauri zetu. Imekuwa ni utaratibu uliozoeleka Serikali Kuu kuchelewa kupeleka ruzuku za maendeleo katika Halmashauri zetu jambo ambalo linaleta hasira kubwa kwa Halmashauri zetu kama ifuatavyo:-

- Kutokana na ucheleweshaji huo, miradi iliyokusudiwa kutekelezwa kutotekelvezwa;
- Serikali kuonekana inapanga mambo yasiyotekelvezeka;
- Kupunguza imani ya Serikali kwa wananchi;
- Pindi fedha zinapokuja, miradi hutekelezwa harakaharaka kwa kiwango cha chini kisichokidhi vigezo vyta kitaalam;
- Kupewa wakandarasi wasiokuwa na sifa;
- Miradi kutokamilika kwa wakati;
- Fedha kuletwa nusunusu;

- Halmashauri zetu kuonekana dhaifu; na
- Ongezeko la bei ya bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, natoa ushauri ufuatao:-

(1) Muda wa kupanga bajeti ya Serikali ubadilishwe tofauti na ilivyo sasa ili kuwahisha fedha za maendeleo, ufuate misimu na vipindi vya mapato.

(2) Halmashauri zirejeshewe vyanzo vingi vya mapato ili malengo ya mapato na matumizi yafuate mipango yao kama walivyojipangia.

(3) Serikali ipeleke waandisi wenyewe uwezo katika Halmashauri zetu ikiwa ni pamoja na Maafisa Mipango wenyewe uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa nidhamu na matumizi yasiyo ya kuridhisha. Tatizo hili linasababishwa sana na mambo yafuatayo:-

- Kuwa na watumishi wasio na sifa na wasio waaminifu;
- Kutochukua hatua kwa watumishi wanaobainika kuwa na tabia ya wizi na wasiokuwa waaminifu;
- Hatua ya kuhamisha mtumishi anayeonekana siyo mwaminifu na kumpeleka Halmashauri nyingine; na
- Kulindana kwa watumishi na viongozi toka ngazi ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la watumishi hewa ni tatizo sugu hata Serikali inalijua na ndio maana kila mara hufanyika sensa ya watumishi katika Halmashauri zetu. Cha kushangaza matokeo ya sensa hiyo huwa ni siri, wanaohusika na Halmashauri huwa hawapewi taarifa ya matokeo hayo ili waweze kuchukua hatua husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri baada ya sensa ya watumishi kufanyika, taarifa itolewe kwa Halmashauri husika kupitia Mabaraza ya Madiwani ili wachukuliwe hatua. Vilevile Halmashauri inayobainika na tatizo hili, Mkurugenzi afukuzwe kazi pamoja na watumishi wote waliohusika na tatizo hilo akiwemo Afisa Utumishi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, manunuzi yasiyozingatia taratibu, nashauri:-

- Kitengo cha Manunuzi cha Halmashauri husika kichukuliwe hatua;
- Madiwani wahuishwe kikamilifu katika suala la manunuzi;
- Bei za vifaa au bidhaa iwe ya wazi na iwepo katika mbao za matangazo kila inapobidi ili kila mmoja aitambue; na
- Elimu itolewe vya kutosha kwa Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Idara nyingi za Halmashauri kuwa na Makaimu kwa muda mrefu. Tatizo hili ni kubwa sana na matokeo yake linasababisha utendaji dhaifu katika Halmashauri zetu. Nashauri walio na sifa wathibitishwe na kama wanaokaimu hawana sifa basi waajiri watu wengine. Kwa tatizo hili, ofisi ya Utumishi Kitaifa inapaswa kuwajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu katika ukusanyaji wa mapato unasababishwa na:-

- Baadhi ya Halmashauri kuwa ni vyanzo hafifu vya mapato;
- Uaminifu mdogo, fojari ya vitabu vya mapato;
- Ukosefu wa nyenzo za ufuatiliaji; na
- Ukosefu wa Wakaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kitendo cha Serikali kuweza kuruhusu matumizi ya fedha zaidi ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Huu ni utaratibu unaofanana na ufisadi. Hivyo Serikali iwachukulie hatua wote waliohusika na kuitisha matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni na mikopo. Hivi kweli kitendo cha Serikali kufikiri deni la shilingi 14 triliuni, hii Serikali ina mwenyewe au haina mwenyewe kwa kweli hii Serikali kwa hali hiyo tuseme ilishaflisika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali itoe ufanuzi ufuatao:-

Nani aliruhusu mikopo iliyopitia hadi zaidi ya bajeti yote ya mwaka mzima wa Serikali. Mikopo hiyo imeleta manufaa gani kwa Taifa letu? Ni miradi gani imetekeliezwa kwa mikopo hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni, kumekuwa na madeni makubwa ambayo Serikali inawadai watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituletee orodha ya majina ya watu wanaodaiwa na Serikali kwa mchanganuo ufuatao:-

- kusudio la mkopo na manufaa yake;
- Kiasi alichokopa;
- Muda unactakiwa kulipa, je, amefuata?
- Mkataba wa Mkopo huo;
- Anao uwezo wa kulipa deni hilo; na
- Dhamana aliyoiweka inakidhi mkopo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wote ambao wamekiuka mkataba na mwelekeo wa kulipa deni hilo hauonekani, nashauri ichukue hatua za kafilisi mali yote aliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali iliyopo sasa ofisi au Wizara ya Fedha imeshindwa kumudu udhibiti wa fedha au kama ni muungwana ni bora kujiuzulu kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei. Hivi huu mfumuko wa bei unazidi kuongezeka siku hadi siku, hivi nchi yetu haina wasomi wa uchumi? Kama ndivyo ilivyo hatunao nchini, basi tuombe msaada katika nchi nyingine zilizomudu jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe ufanuzi juu ya mambo yote niliyoandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipata hasara ya kulipa mishahara watumishi katika Makampuni mbalimbali wakati Makampuni hayo hayana faida yoyote, yalishasimama kufanya kazi mfano, watumishi wa Shirika la Ndege (ATCL) na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kuwalipa watumishi hao mapato yao na kuachana nao kuliko Serikali kuendelea kubeba mzigo ambao ni hasara kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kufanya ukarabati wa kukarabati ndege badala kununua ndege mpya, ni kuweka rehani maisha ya Watanzania. Hivyo, ni vema Serikali ikafanya utaratibu wa kununua ndege mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo maoni yangu, nampongeza CAG na nazipongeza Kamati na naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja ya taarifa tatu zilizowasilishwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi kwa ujumla wake ni muhimu sana na mimi naomba nitoe mawazo yangu hasa katika maeneo yafuatayo:-

1. Ucheleweshaji wa fedha kufika katika Halmashauri nane ni tatizo kubwa kiasi kwamba hata zikifika zinarudishwa tena kwa sababu muda wa kuzipeleka katika maendeleo unakuwa karibu unakwisha. Je, kuna vikwazo gani vinavyosababisha fedha hizo zisitolewe mapema hasa fedha za maendeleo?

2. Je, katika Halmashauri zetu, kuna watalaam wa kutosha kusimamia fedha ambazo Serikali inazipitia Halmashauri? Asilimia kubwa ya fedha ya Serikali hupelekwa huko.

3. Mara kadhaa katika Bunge niliwahi kuuliza swali kwa nini bei ya cement ya kiwanda cha Songwe Mbeya inauzwa kwa bei kubwa kuliko bei inavyouzwa Dodoma, Dar es Salaam na kadhalika?

4. Mbeya vijijini imebahatika kuwa na misimu miwili ya kulima, kilimo cha kiangazi na kilimo cha masika. Nimejaribu mara nyingi kuomba pembejeo kufika mapema hasa mwezi wa sita na mwezi wa kumi lakini bado imekuwa ni tatizo kubwa kuzipata pembejeo hizo. Je, ni kwa nini Serikali haiwezi kutathmini hali ya mahitaji ya pembejeo kwa kila eneo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja zilizotolewa na Kamati zote tatu.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninafuraha kukuletea mchango wangu kwa njia hii ya maandishi. Fedha za Serikali nyingi zinapotea kwa njia za wizi. Serikali haichukuwi hatua kwa watendaji. Lipo tatizo la maagizo ya Wakaguzi wa Hesabu za Serikali kwa

Makampuni Idara, Wakala kutotekelawa ili kuweza kumsaidia Rais na Chama chake kutawala na kuwaletaa Watanzania maisha bora. Zipo taarifa zinaonyesha kuwa mfumo mzima wa Serikali upo katika mashaka kuanzia ngazi ya Halmashauri, Mikoa na kufika ngazi ya Wizara yaani kitaifa. Hakuna maamuzi yanayotolewa kwa wabadhirifu, hatua inayochukuliwa ni uhamisho wa wezi kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya hata maamuzi ya Baraza la Mawaziri nayo yanapindishwa. Kwa mfano, maamuzi ya NSSF kukabidhiwa Mgodi wa Kiwira ili izalishe umeme. Kwa sasa zipo taarifa kuwa mmoja wa Mawaziri amepindisha maamuzi haya na uwezekano wa NSSF kupewa mradi ule haupo. Je, kwa nini Waziri wa Serikali wa aina hii anakuwa na nguvu za jinsi hii? Yupo na anaonekana kuwa na nguvu kuliko Rais inakuwaje? Napendekeza NSSF wapewe mgodi haraka ili kuepuka uwezekano wa Serikali kupelekwa Mahakamani na wadai wa mgodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maoni ya CAG ufuatwe. Vinginevyo CAG pamoja na watendaji wake watakata tamaa na mwisho wa siku kila kitu kitakuwa hohehahe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo Serikali ikikopa ikumbuke kurudisha pesa. Vinginevyo tutaua mashirika na makampuni mengine.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtindo huu wa bajeti zetu, ni vigumu sana kwa nchi kuondoka katika umaskini uliokithiri. Ni vyema Serikali ikaangalia zaidi uwiano wa ruzuku inayopelekwa katika Halmashauri zetu. Taarifa inaonesha sehemu kubwa ya bajeti inatumika kwa matumizi ya kawaida na sehemu ndogo sana kutengwa kwa ajili ya maendeleo na hata pengine fedha hizo kutopelekwa kabisa. Tukitaka kuondoka katika umaskini, Serikali iongeze ruzuku kwa shughuli za maendeleo na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla taarifa nzima imejaa ubadhirifu mkubwa wa fedha na hilo ni tatizo sugu kwa nchi yetu. Wabunge wamelipigia kelele siku nyingi bila mafanikio kwa mfano malipo hewa, manunuzi yasiyofuata utaratibu, udhaifu wa usimamizi wa miradi na kadhalika. Hii ni sawa na kupigia mbuzi gitaa iliacheze na Wabunge tumebaki kulalamika tu, sasa tuchukue hatua zaidi badala ya kulalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, kuna udhaifu mkubwa sana katika uongozi wa viongozi kutowajibika. Hakuna wa kumwajibisha mwingine maana yake viongozi wengi si sehemyu ya matatizo/ubadhirifu

wa fedha za umma. Bunge kama chombo cha kuisimamia Serikali liache kulalamika badala yake litumie haki yake ya kikatiba kuisimamia Serikali. Bunge ni kama linatwanga pilipili kwenye kinu na kulia lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi CAG amekuwa akitoa taarifa na *indicators* kwa matumizi mabaya ya fedha za umma na Serikali imekuwa kimya, kiziki sasa nafikiri kuwa ni muda muafaka kuondoa ofisi hiyo ya CAG maana inaonekana kama vile inaikoseshaa Serikali usingizi kwa kuweka maovu, uozo wa Serikali wazi au Serikali iwjajibike ipasavyo. Kwa kuwa Serikali imekuwa kiziki isiyosikia – ukiangalia taarifa zote za Kamati za POAC, PAC na LAAC, ubadhirifu ni wa kutisha na hakuna hatua inayochukuliwa, napendekeza Bunge kutumia Kanuni na haki yake ya kikatiba na kutoa Azimio la kutokuwa na imani na Serikali isiyojali Bunge na wananchi wake. Nafikiri Wabunge watoke na kuicha Serikali kama ishara ya kutokubaliana nayo. Bunge limekuwa likitoa Maazimio na Serikali haitekelezi au kutekeleza kwa sehemu ndogo sana bila hata *feedback* kwa Bunge hili, hiyo ni dharau kwa mhimili huu wa Bunge. *Strongly, I propose to have vote of no confidence* kwa Serikali. Angalia Mashirika ya Umma, Serikali inajifanyia inavyotaka kutumia fedha za umma bila Bunge kutoa kibali, mikataba mibovu isiyojali maslahi ya nchi, Serikali imekosa uzalendo kwa nchi, Bunge litumie meno yake ipasavyo.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji hapa nchi limekuwa sugu. Wananchi na hasa akina mama na wasichana, ndio wanaoteseka na kuhangaika wakitafuta maji kwa ajili ya familia. Inafahamika kwamba kuna vikwazo vingi katika ufanisi wa mamlaka ya maji hapa nchini. Jambo ambalo linapelekea maeneo mengi kutokuwa na maji. Uchovu wa miundombinu na pia ukusanyaji hafifu wa maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sana imefahamika kwamba mradi wa upanuzi na uzalishaji wa maji DAWASCO kwenye eneo la Ruvu chini ungeweza kuzalisha mita za ujazo 270,000/- tatizo kubwa ni miundombinu mibovu ya kusafirisha maji kutokuwa na uwezo wa kuleta maji Dar es Salaam. Ni kwa nini fedha isitengwe ya kutosha ili kuondoa tatizo hili sugu? Aidha, maji yanayofika Dar es Salaam ni machache kutokana na kupotea njiani na pia wizi wa kutoboa bomba la maji kwa ajili ya utengenezaji wa matofali. Tatizo hili linafahamika na naomba Wizara husika ifuatilie na kuwapa adhabu za kisheria wale wote wanaobainika kutoboa bomba hovyo kwa ajili ya utengenezaji wa matofali kwani wengi wanaosaidia wananchi kutoboa mabomba ni vishoka wa DAWASCO. Maji ni uhai na bila maji safi na salama magonjwa ya mlipuko hayatakoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yamekuwa ni tatizo lisilokomeshwa na wenyewe mamlaka kwa muda mrefu sasa. Uendeshwaji wa Serikali za Mitaa haufanywi kisayansi. Hakuna ufuatilijji mzuri wa miradi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini miaka 50 baada ya uhuru mwanamke wa Arumeru Mashariki bado anashirikiana na punda kunywa maji? Kwanza punda anywe ndipo na mama ayachote kupeleka nyumbani. Mishahara hewa inayolipwa, ingeweza kabisa kuchimba visima vya maji katika maeneo ya nchi yetu yasiyo na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachukuliwe hatua za kisheria wale wote wanaobainika kuendelea kujilli pa mishahara hewa na kufanya manunuzi yasiyozingatia taratibu. Ni vema Serikali ikawa makini kuzuia fedha nyingi zinazopotea katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu, ahsante.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naml napenda kuchangia katika hoja zilizopo mbele yetu. Kwanza, naomba kuzipongeza Kamati hizo kwa kuwasilisha Bungeni shughuli zao za kazi na kwa uwazi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba pesa za Serikali zinaliwa bila huruma wala watendaji kuona haya. Katika Halmashauri zetu, hali ni tete, pesa zinaliwa bila haya, tazama Halmashauri ya Rombo, Kibaha, Kishapu na nyinginezo nyingi kama sio zote. Miradi haiendi na kama ikienda inasuasua tu lakini pesa zipo huko na zinapelekwa kila kukicha lakini hakuna kinachofanyika ukitazama wao hujenga manyumba makubwa tofauti na mishahara yao, kununua magari ya kifahari kwa mashindano. Huu ni wizi ambao hautavumilika. Sasa basi ni vema watu hawa wakafuatiliwa na kufikishwa katika vyombo vya Sheria na wafilisiwe mali ambazo wamezipata kinyume na haki yao, hiyo yaweza kuwa fundisho. Ni vizuri kwanza kuwashughulikia hasa Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo fedha zimetafunwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Halmashauri zetu watendaji wanawaona Madiwani kama kikwazo kwao, hasa pale ambapo wanaona Madiwani hawana mshahara, wana posho tu ya kuganga njaa na wao wana mishahara. Ni vizuri sasa Madiwani wakapewa mishahara na sio posho tena nao waweze kusimamia kazi bila kuhangaika kwa maisha magumu. Pia napenda ni vyema sasa Wenyeviti wa Mitaa nao wakafikiriwa, kwani wanafanya kazi ngumu. Hawana saa

kamili ya kufanya kazi. Hufanya kazi toka saa moja asubuhi hadi saa moja asubuhi kesho yake lakini Serikali imewasahau hasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuihimiza Serikali tunapopitisha bajeti, ni vyema fedha hizo zikafika kwa wakati na kwa utimilifu na sio kupeleka pesa kidogo kidogo. Ninaomba Serikali kuwa makini na haya. Watanzania ni watu maskini hivyo kutumia pesa vibaya ni kuzidi kuwatia umaskini Watanzania. Hivyo ni bora kuwa na watumishi wachache ambaao ni safi na wawe mfano kwa watumishi wengine. Lazima sasa tuamue kuwashughulikia watendaji wabovu na ambaao hawana uzalendo.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo. Ripoti ya CAG ya mwaka 2010/2011, inasema kwamba Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) uko hatarini kufilisika na kupoteza fedha za michango ya wanachama wake kutohana na Serikali kushindwa kurejesha mabilioni ya shilingi iliyokopa katika mfuko huu au kudhaminiwa miradi mbalimbali. NSSF pekee imeikopesha Serikali shilingi bilioni 234.1 wakati mkataba uliosainiwa ni wa shilingi bilioni 35.2 tu kwa ajili ya ujezi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Vilevile mifuko mingine nayo iko hatarini kufilisika mfano PSPF iliikopesha Serikali shilingi bilioni 105.9 PPF, shilingi bilioni 33.99, LAPF shilingi bilioni 22 na NHIF bilioni 13.4 fedha zote hizo pamoja na riba yake hazijarejeshwa mpaka sasa ambazo zilitolewa pia katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya POAC kwamba Serikali itie saini haraka makubaliano ya mkopo baina yake na mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji wa viwanda vya korosho. Naunga mkono mapendekezo ya Kamati kwamba viwanda vyote vya korosho vilivyobinafsishwa virejeshwe Serikalini kwa kuwa wawekezaji ambaao ni wazawa wameshindwa kuviendaoleza na wamevunja mkataba kwa kubadili matumizi ya viwanda hivyo ya kubangua korosho na kuvifanya maghala ya kuhifadhia korosho. Hii imelifanya Taifa liendelee kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi kitu ambacho ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi viliuzwa kwa bei ya kutupwa mfano Kiwanda cha Newala I, kiliuzwa kwa shilingi milioni 75, tena kikiwa kipyaa na wanunuzi wake ni watu ambaao walikuwa viongozi wakubwa Serikalini. Watu hawa hawakuona uchungu wa kuchezea mali ya umma badala yake waliitumia kwa maslahi yako binafsi. Ushauri wangu ni kwamba, ili kuinua soko la korosho badala Wabunge kuwa wanapewa pipi hapa Bungeni, napendekeza wawe wanapewa korosho ili kutangaza vema soko lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu wa fedha za umma katika Halmashauri zetu. Kamati ya LAAC pamoja na ripoti ya CAG ya 2010/2011, imeonyesha ubadhirifu mkubwa katika matumizi ya fedha kwenye Halmashauri zetu. Mfano mahsus ni Halmashauri ya Wilaya Singida haijaweza kupeleka asilimia 20 ya vyanzo vya mapato ya ndani na fidia ya vyanzo vya mapato vilivyo futwa vijiji kwa miaka mitatu mfululizo tangu mwaka 2008 mpaka 2010. Baada ya kelele nyingi za Wabunge ilionekana kwamba fedha hizo zilitumika kwa matumizi mengi yasiyo na maelezo bila kufuata utaratibu. Haikuishia hapo mwaka jana Mkurugenzi wa Halmashauri akishirikiana na watendaji wengine aliandaa akaunti hewa kwa kila kijiji na kuonesha kwamba imelipa fedha hizo. Kamati ya LAAC iliagiza ufanyike ukaguzi mahsus tangu mwaka jana lakini haujafanyika kwa madai kwamba *audit fee* bado haijalipwa, hivi nani anatakiwa kulipa hiyo *audit fee* na hizo pesa zimekwenda wapi? Naomba maelezo na naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaandika kwa masikitiko makubwa kutoptana na taarifa zilizowasilishwa hapa. Inasikitisha kuwa, Taarifa hizi za Kamati ni matokeo ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkazi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2011, lakini uchafu umeendelea kutokea katika Ofisi za Serikali, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni nani anawalinda hawa wezi? Nani amewatuma kwenda kuiba fedha ya Umma bila huruma kiasi hiki? Sasa hivi limekuwa jambo la sifa kwa Mtumishi wa Umma kupata utajiri wa kupindukia kwa kipindi kifupi tu. Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Wahasibu wao wamekuwa matajiri wa kutisha. Kila Wilaya wanapopelekwa wanajenga majumba na magari lukuki huku Miradi ya Vijiji imedorora, shule hazina madarasa, hakuna madawati, hakuna zahanati na madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nani amewatuma kuiba hivyo na anawalinda? Wanalindwa kwa kuhamishwa vituo tu, imetokea kishapu, Lindi, Mtwara na kwingineko. Hata Mawaziri wanaotoa kauli kali hapa Bungeni lakini kwa ukweli ni kama maigizo au kiini macho kwani ukweli unajulikana kuwa kuna mtandao wa ulaji kuanzia chini hadi Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha zaidi, ulaji huu hususan unaofanyika kwenye Bodi za Mazao kama vile Pamba na Korosho, unawaongezea umaskini wananchi wa kawaida. Maudhi zaidi kwa Wakulima hawa ni uamuzi wa kuacha kulima zao hilo na badala yake kulima mazao mengine tu. Fikiria hasara ya fedha ya kigeni itakayopotea

kwa nchi yetu. Kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kurekebisha hali hii, basi lazima iwe na meno. Vinginevyo, hasira za wananchi zitaiangukia Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja za Kamati zote.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha siku ya leo kuamka salama na nikiwa na afya njema. Vile vile namshukuru Muumba huyo huyo, kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa sijawatendea haki iwapo sitowapongeza Wenyeviti wote waliota hoja za Kamati zao kwa jinsi walivyoziwasilisha na kuzifafanua vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia juu ya mishahara hewa. Hii inatia aibu kwanza kwa nchi na hata kwa Mawaziri husika. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa Serikali hii inayojiita sikivu. Kwa imani yangu, suala hili la mishahara hewa ni jambo ambalo halizezekani ila tuambiwe ni mpango maalum wa watu na Mawaziri kujipatia maslahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie upotevu wa fedha kwenye Halmashauri. Hata hili itakuwa ni aibu kubwa sana kwa Serikali hii ikiwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale anapotoa taarifa kwa Serikali hii kuhusu upotevu wa fedha kwenye Halmashauri hizo na wahusika wakuu wanajulikana na hakuna hatua yoyote ambayo watachukuliwa isipokuwa hatua ambayo wamekuwa wakichukuliwa ni kuhamishwa Halmashauri moja na kupelekwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni aibu au ni mipango maalum. Nchi ambazo tumepekana nazo za East Africa au nchi nyingi zinifuatilia sana Bunge lako hili na wanalipenda sana, lakini mambo ambayo yanajitokeza kwenye Bunge letu ni aibu kwa nchi yetu na kwa Serikali hii inayojiita sikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikwenda Kenya nilipofika nikaulizwa na kuambiwa na rafiki yangu mmoja ya kwamba, Bunge lenu la Tanzania tumekuwa tukilifuatilia sana na tunalipenda sana, lakini jambo ambazo tumekuwa tukilionia kuna kashfa nyingi ambazo zimekuwa zikiibuliwa na Wabunge juu ya Wizara au Waziri lakini hatuoni au hatujasikia *action* yoyote ambayo imekuwa ikichukuliwa na Serikali yenu. Mwisho, akaniambia ni tofauti na Bunge letu la Kenya, kashfa inapoibuliwa na Wabunge wetu basi itafuatiliwa na ikithibitika kila aliyehusika anawajibishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu juu ya Serikali yetu na juu ya kuliondoshea aibu kwa wale wanaoliangalia Bunge letu, wale ambao wako nje ya nchi yetu, basi endapo mtu yeyote atabainika na kashfa ya ufujaji wa fedha za Umma au rasilimali za nchi hii, awajibishwe na hatua kali zichukuliwe dhidi yake ili isionekane kuna kulindana katika Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niseme Serikali lege lege inazaa Viongozi lege lege.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kusema kwamba, kadiri siku zinavyosogea, ndivyo maisha ya Mtanzania yanavyokuwa magumu. Nasema hivyo kwa sababu uchumi wa nchi hii pamoja na kusema unakua, lakini siyo kweli kwani kipato cha Mtanzania hakiongezeki kwa uhalisia wake, hivyo hawamiliki hata mlo wa siku moja na hili linachangiwa na Viongozi wetu ama Watendaji wetu kutokujibika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo ambayo tuliweka kaulimbiu ya "KILIMO KWANZA" tumeshindwa kufikia lengo kwani Wakulima wetu hatuwawezeshi ipasavyo. Pembejeo hakuna, mbolea hakuna, mbegu hakuna na bado Kilimo chetu siyo cha kisayansi; hivyo, Pato la Taifa halikui na kwa sababu ya utendaji mbovu na tunaona aibu kuwajibisha, Watanzania wanaendelea kuumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, TBS huko nje haifanyi jambo lolote zaidi ya rushwa kwani wafanyabiashara wanalipa tu kiasi cha fedha ili mizigo yao iweze kusafiri, hakuna ukaguzi unaofanywa, zaidi ni kuikoseshaa mapato Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inazalisha matunda mengi sana ambayo wakati wa msimu mengine yanaoza. Je, kwa nini Serikali isiongeze viwanda vya usindikaji ili kuokoa mazao haya na hatimaye kuongeza Pato la Taifa? Tunangoja nini jamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa mwisho, Serikali iwasaidie sana kwa kuwapunguzia riba hawa ambao wanaanzisha hizi SACCOS na VICOBA ili waondokane na tatizo la kushindwa kurejesha mikopo na hatimaye kafilisiwa mali zao.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ihakikishe manunuzi yote yanafanyika kwa kufuata taratibu za manunuzi katika maeneo yote, yaani Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha manunuzi kufanyika bila mikataba halali ni kosa kubwa. Ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba, manunuzi yote yanaendana na mikataba halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri manunuzi yafanywe kulingana na bajeti iliyopitishwa na Bunge, kitendo cha kutumia pesa iliyoidhinishwa ni kosa kubwa lisilopaswa kurudiwa na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuhamishwa Watendaji wa Serikali walioharibu eneo moja kupelekwa eneo lingine ni kitendo kisichovumilika. Nashauri Serikali iwachukulie hatua kali Watendaji walioharibu kwa kuwafukuza kazi badala ya kuwahamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwachukulie hatua watu wote waliohusika katika Mkataba ulioingiwa kati ya ATCL na Kampuni ya Lebanon.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa, fedha jumla ya Sh. 1,587,780,350 ambazo zilitakiwa zitolewe kwa ajili ya mikopo ya wanawake na watoto katika Halmashauri zetu na baadhi ya Manispaa, zipo au zimebaki *Bank* bila ya kupewa wahusika amba ni Akina Mama wa Tanzania, wanaoishi vijijiini, amba wanahitaji kujikwamua kiuchumi katika wimbi kubwa la umaskini walilozama na vijana amba wangejikwamua kiuchumi. Je, kweli Serikali ina dhamira ya dhati ya kuwakomboa Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya CAG inaonesha fedha zipatazo Sh. 44,086,650 za Mfuko wa *CHF* ambazo zimechangwa na Watanzania wanyonge, wanaokosa dawa na matibabu sahihi katika Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati, zinatumika tofauti na makusudio katika Manispaa ya Dodoma, Songea na baadhi ya Halmashauri za Ulanga na Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inawaeleza nini Watanzania wanaoendelea kuchangia fedha katika Mfuko huu? Ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote zilizowasilisha Ripoti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Wajumbe wa Kamati ya Serikali za Mitaa, kuhusiana na kupunguza kwa idadi ya Maafisa

wanaohudhuria vikao vya uwasilishaji wa taarifa zao kwenye Kamati. Ni kweli kabisa Halmashauri zetu zinatumia kiwango kikubwa cha fedha kwa ajili ya posho na masurufu bila sababu pamoja na mlolongo wote wa Maafisa wanaotoa ripoti ni Mkurugenzi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mingi ya Halmashauri inaonesha haina viwango, haya yote yanatokana na Miradi hiyo kutokaguliwa na kuziachia Halmashauri kufanya inavyotaka na kusababisha kodi za Wananchi kuliwa bure, ubadhirifu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mwanri, Naibu Waziri wa TAMISEMI, alipofanya ziara yake katika Mkoa wetu wa Iringa, aliweza kujionea mwenyewe jinsi Miradi mingi ya Halmashauri ilivyokuwa haina kiwango. Halmashauri zina Wataalam lakini wanashindwa kusimamia Miradi hiyo na kusababisha Miradi mingi kujengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukomesha jambo hilo, ningeomba sasa hatua na adhabu kali sana zitolewe dhidi ya hawa Watendaji wabovu na siyo kuwahamisha, kwa sababu unapohamisha Mtaalam mbovu kutoka sehemu moja na kumpeleka sehemu nyingine ni kuhamisha tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sasa Serikali yetu isiwafumbie macho, ituletee mwafaka na suluhisho la uozo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia kuhusu udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri. Halmashauri nyingi zimeathirika sana kuhusu uondoaji wa baadhi ya vyanzo vya mapato vya Halmashauri. Kwa nini Serikali Kuu inachukua vyanzo hivyo si Halmashauri zote zinaweza kuijendesha na bado utaona pesa za maendeleo hazipelekwi katika Halmashauri kwa wakati? Serikali ilikuwa ina nia nzuri sana ya kuhamisha hizi Serikali za Mitaa ili kusogeza huduma jirani na wananchi. Ninaomba hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Halmashauri nyingi sana zimekuwa na mikataba mibovu sana na kusababisha wajanja wachache kushirikiana na baadhi ya mawakala na kutafuna pesa za Halmashauri. Ninaomba hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wetu ni Viongozi wanaokuwa karibu na wananchi lakini posho wanazopatiwa hazikidhi mahitaji na kazi zao. Sielewi mfumo huu tuliiiga wapi? Ninaomba Madiwani sasa

wapatiwe mishahara na siyo posho kama ilivyo sasa, kwa sababu wao ndiyo Wasimamizi Wakuu wa pesa zetu za Halmahauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Taarifa ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, kwa mujibu wa Taaria ya Msajili wa Hazina, ilibainika kuwa jumla ya Mashirika ya Umma 11 hayakuwasilisha Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa Msajili wa Hazina. Kwa mwendo huo kweli tutafika? Baada ya kupokea Taarifa hizo ni vyema Serikali ingekuwa inaweka utaratibu wa kutoa taarifa kwa Bunge na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mshangao wangu kuhusiana na Shirika la Ndege (ATCL) kuendeshwa kwa zaidi ya miaka miwili bila Bodi; kweli tutafika? Ningombaa wakati wa majumuisho ya Taarifa hizi tupatiwe maelezo ni kwa nini Shirika halina Bodi; tatizo ni nini na kwa nini haikuteuliwa kwa wakati na ndiyo maana Shirika halijiendeshi linavyotakiwa? Matatizo yote haya yanayolikabili Shirika ninaamini kuwa pengine Bodi ingeundwa kwa wakati ingeweza kulishauri Shirika likaweza kuijendesha kwa maslahi ya wananchi.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujikita katika hoja ya Kamati ya Hesabu ya Serikali za Mitaa, ambayo inagusa moja kwa moja jamii inayotuzunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona ni jinsi gani Halmashauri zetu zinavyotumia pesa ya Watanzania kinyume cha utaratibu na kuwaachia watusika wakiendelea na kazi, aidha, kwa kuhamishwa kituo cha kazi au kubakia pale pale. Halmashauri zetu zimekuwa kitovu cha Viongozi wasio waadilifu kujipatia fedha bila jasho.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hoja za Kamati hii ni ucheleweshaji wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Kamati imelizungumzia kwa kina na kwa mapana kabisa. Tatizo hili lipo karibu Halmashauri zote nchini zimekuwa zikicheleweshwa sana. Madhara ya kucheleweshwa kwa ruzuku hii yanababisha Miradi mingi ya Maendeleo katika Halmashauri kukwama na kushindwa kumalizika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 ilipokea robo ya kwanza mwezi wa Desemba 2011. Tokea bajeti imepitishwa mwezi wa saba hela inapelekwa mwezi wa Desemba; hii maana yake nini? Moja kwa moja Miradi ya Maendeleo itasimama na iliyokwishaanzishwa itashindwa kumalizika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia inafanya Madiwani ambao wanatumia pesa nyingi katika Vikao vya Baraza ambavyo ndiyo vinavyoidhinisha Miradi ya Maendeleo kutokuwa na kazi ya kufanya hasa usimamizi wa Miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ni bora yazingatiwe kwa umakini mkubwa kwani chimbuko la maendeleo katika maeneo yetu ni Halmashauri, kama ruzuku zinachelewa ni dhahiri kabisa hakutakuwa na maendeleo katika Halmashauri husika, kwa kuchelewa kutekeleza Miradi iliyoidhinishwa na hivyo kuchelewesha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine ya Kamati hii ni pamoja na Wakuu wengi wa Idara Kukaimu. Madhara ya Kukaimu nafasi na hasa kwenye Halmashauri zetu, kunarudisha nyuma maendeleo ya wananchi. Mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kuna Wakuu wa Idara kama *Municipal Treasurer (MT)*, *Municipal Agriculture and Livestock Development Officer (MALDO)* na Mganga Mkuu wapo kwenye *vetting* wanasubiri kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inachukua muda gani Mtumishi anakuwa kwenye *vetting*? Hii inapunguza morali ya Mtumishi kufanya kazi kwani anakuwa hana uhuru na kazi anayoifanya. Ni vyema Wizara isichukue muda mrefu kupandisha vyeo Wakuu wa Idara kwani kunapunguza kasi ya maendeleo katika Halmashauri na pengine kuwafanya wasifanye kazi kwa umakini kwani ni wafanyakazi ambao wanakaimu tu nafasi hizo na muda wowote chochote kinaweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine ambayo imejitokeza kwenye Taarifa hii ni udhahifu wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri. Kamati imelieleza hili kwa mapana sana na kutoa mapendekezo. Imeonekana katika Halmashauri 36 vitabu vya kukusanya mapato vimepotea; hii maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri hizi zimekusanya mapato na kupoteza vitabu kwa makusudi kabisa ili kupoteza ushahidi. Mamillioni ya pesa yanakusanya lakini hayaonekani, matokeo yake hakuna maendeleo yoyote; shule zinakosa madawati, zahanati hazina dawa na pengine hata madarasa yanakuwa hayatoshi. Je, Serikali inaona na inajua Halmashauri zinazohusika na ubadhirifu huu; ni lini sasa suala hili la ukusanyaji wa mapato linafanyika na kuishia mikononi mwa watu wachache?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Halmashauri ambazo zimejiwekea mpango wa kujikusanya mapato ili ziweze kujiendesha bila matatizo kwa kutotegemea ruzuku kutoka Serikalini kwa asilimia kadhaa. Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imeweka utaratibu wa kukusanya mapato kutoka kwa wafanyabiashara. Imekuwa ikikusanya Sh. 50,000 kwa ajili ya leseni ya duka la rejareja, Sh. 200,000 vifaa vyta ujenzi na Sh. 500,000 biashara kubwa kwa miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji huu wa mapato haukuzingatia vipato vyta wenye maduka na mitaji waliyo nayo, matokeo yake umeleta manung'uniko mionganoni mwa wafanyabiashara hao kuwa ni uonevu. Mwananchi wa kawaida yawezekana ameweka kiduka nje ya nyumba yake kina viberiti, sabuni mafuta, vitunguu, nyanya na kadhalika, mtaji wake hauzidi Sh. 50,000. Kwa akili ya kawaida hiyo ni kumrudisha nyuma na kibaya zaidi ada hii ya leseni inalipwa kila baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kupitia Wizara husika, waangalie viwango hivyo kama vinaendana na mitaji waliyonayo wafanyabiashara hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya mwisho ambayo imenigusa ni kuhusiana na Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Wilaya Kishapu. Kamati imetoa Ripoti na kutaja majina maafisa ambao wamehusika na ubadhirifu huu, lakini mpaka sasa hakuna kitu kilichofanyika, watuhumiwa wapo na zaidi wamehamishwa kupelekwa Halmashauri zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi hii Serikali yetu ipo makini kweli? Inataka ushahidi gani zaidi ili watuhumiwa waweze kufunguliwa mashtaka? Kamati imetaja pia kuhusika kwa Wafanyakazi wa NMB, Tawi la MANONGA, lakini haikutaja majina yao; je ni hatua gani ambazo zimechukuliwa kwa Wafanyakazi hawa na kuyaweka wazi majina yao kama ilivyofanya kwa Maafisa wa Halmashauri ya Kishapu?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopotea ni nyingi mno na matokeo yake Wilaya ya Kishapu imekuwa nyuma kimaenedeleo kwa sababu ya Viongozi wasio waadilifu. Ninamalizia kwa kuiuliza Serikali ni lini watu hawa wote waliohusika watafikishwa Mahakamani na adhabu yao iwe kali ili liwe fundisho kwa Maafisa wengine? Mchezo huu nina imani haupo Kishapu tu ni Halmashauri nyingi zinafanya hivyo. Naomba sana Serikali ichukue hatua kali ili irudishe imani kwa watu wake ambao sasa hawana imani nayo tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na kupendekeza Serikali iamue kufanya kazi sasa.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na uzembe mkubwa sana wa kukusanya kodi na sababu kubwa ni ukusanyaji mdogo na upotezaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nydingi imeonekana kuwepo wizi mkubwa na rushwa ya hali ya juu ya Wafanyakazi wa *TRA*. Kumekuwepo na ugumu mkubwa wa kuondoa tatizo la rushwa *TRA* na hii yote ni kwa sababu ya usimamizi mbovu na hii inafanyika kwa sababu ya utaratibu mbovu wa ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu kufuatwa na mkusanyaji wa kodi wakapanga ngapi atoe na ngapi asitoe na shilingi ngapi atoe kwa *TRA*, hali hii inasababisha kukusanya kidogo na kingi kuangukia kwa wakusanyaji wa kodi, yaani Wafanyakazi wa *TRA*. Matokeo yake wafanyakazi wa *TRA* wanaishi maisha ya hali ya juu huku wananchi wakiteseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mianya mingi ya ukwepajji kodi. Hii imesababisha hasara kubwa ya Sh. 15,431,444,821.13, ambazo ni fedha nydingi zingeliweza kutusaidia katika kuleta maendeleo ya nchi na hakuna adhabu wala maelezo ya kutosha kuhusu udanganyifu huo. Kwa jambo hili, lazima mtu kuwajibika na hasara hii haitafutwa bila kupewa maelezo ya kina na ya kuridhisha. Hoja hii nitaipinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha manunuzi kufanyika bila kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, hii yote ni kuidhoofisha Serikali na lazima kuwepo adhabu kali kwa ye yote atakayekiuka ikibidi afukuzwe kazi kabisa na hii itakuwa mfano kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa vifaa kwa bei ya uongo; vifaa vingi bei siyo zinazopatikana madukani. Uchunguzi uwe una fanyika ili kujua bei kama ndizo zilizo sokoni. Pia kuza mali za Serikali kwa bei ndogo za kutupa na kuuziana wenyewe kwa wenyewe, hii ikigundulika wahusika washughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fedha kucheleva kutolewa limekuwa tatizo sana na kusababisha hali mbaya katika Halmashauri zote nchini. Suala hili linasababisha kuzorotesha maendeleo ya Taifa letu na hii inasababishwa na uzembe mkubwa wa Watendaji na pia bajeti inayotolewa hailetwi kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itueleze tatizo ni nini; Bajeti inapitishwa lakini fedha hazipelekwi kwenye Halmashauri na wala Serikali haisemi tatizo ni nini? Naiomba Serikali itueleze Bajeti ya Mwaka 2011/2012 tatizo ni nini mpaka sasa?

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja na kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri sana waliyoiwasilisha mbele yetu. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato ya Serikali; lazima Serikali iongeze wigo wake wa mapato. *TRA* iongeze wigo wa kodi ikiwezekana kutumia sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima *TRA* iweke malengo yenyе uhalisia. Kwa sasa *TRA* inaonesha kama malengo yao ni madogo kuliko uhalisia na hivyo makusanyo yao ni madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, yapo mambo ya msingi yaliyobainishwa na Kamati; naishauri Serikali kuwa endapo hatua hazichukuliwi kwa maeneo yenyе udhaifu huko ni kuidhoofisha Serikali ya Chama cha Mapinduzi kilichounda Serikali. Hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, atathmini utendaji wa Serikali yetu ambapo mimi ni Mheshimiwa Mbunge wa CCM kwamba, mchelea mwana kulia hulia yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima hatua kali na madhubuti zichukuliwe kwa Watendaji wanaoiaibisha Serikali yetu Tukufu.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, muda wa kujadili Ripoti za PAC, LAAC na POAC ni mdogo sana. Kanuni za Bunge haziliweki wazi hili. Muda umefika sasa wa kuliweka hili kwenye Kanuni za Bunge. Pia muda uwe wa kutosha.

Pili, mapendekezo ya CAG, PAC, LAAC na POAC lazima yafanyiwe kazi na Serikali na Bunge lazima lifuatilie haya.

Tatu muda umefika sasa wa kuanza mchakato wa kuanzisha *Budget Office* hapa Bungeni. Hii *Office* ndiyo itashirikiana na *PAC*, *LAAC* na *POAC* kufuatilia matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Mkaguzi Mkuu (*CAG*) anapokagua Hesabu za Mashirika ya Umma, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na kukuta baadhi ya Mashirika kuwa na Hati Chafu, yaani isiyoridhisha, huwarudisha watusika wakarekebishe na walete upya hesabu zao.

Je, hii inamaanisha nini? Maana yake ni kwamba, Ofisi na Mashirika husika huenda na kukaa upya kutengeneza hesabu zao kwa maana kwamba ziwe safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dalili ya rushwa na wizi wa pesa za Serikali ambazo zinapaswa kutumika katika shughuli za maendeleo. Je, kwa mtindo na *style* hiyo ya utendaji tutafikia Malengo ya *Millennium* ambayo yanalenga kumwondolea mwananchi umaskini ambao unazidi kukithiri siku hadi siku.

Je ni kwa namna ipi au gani mwananchi maskini ataokoka na umaskini huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kushauri, pindi Halmashauri au Mashirika yanakuwa na Hati Chafu, wanaohusika wachukuliwe hatua kali za kinidhamu na kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusu adhabu ambazo zimekuwa zikipewa Halmashauri ambazo hazifanyi vizuri, yaani kupewa pesa kidogo kutohana na bajeti iliyoombwa. Kitendo hicho cha Serikali kuweka adhabu kama hizo siyo kuiadhibu Halmashauri bali ni kuwaumiza wananchi haki zao za msingi kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu inaongozwa na sheria, basi pindi inapobainika wapo watusika waliosababisha hasara hizo, wachukuliwe hatua za kinidhamu ikiwemo kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taarifa ya Kamati za Kudumu za Hesabu (*POAC*), napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubinafsishaji wa mashamba yaliyokuwa ya mkonge hususan Tanga. Mashamba mengi yameachwa kuwa mapori na hayaendelezwi wala hayazalishi kwa namna inavyotakiwa. Kwa mfano, shamba kama la Ubena Zomozi, mwekezaji pale anachokifanya ni kulima eneo dogo, eneo lingine ametenga kwa kilimo cha miembe na eneo lingine amefanya kwa ajili ya kuhifadhi wanyamapori kama swala na wengineo. Kwa maana hiyo mashamba hayo yamebadili matumizi ya awali ya mashamba hayo na hivyo kuyafanya mashamba hayo kutozalisha kwa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hati za mashamba. Wamiliki wengi wamekuwa wakikamata mashamba hayo kwa lengo la kuchukulia mikopo au fedha kutoka benki ili waweze kujipatia mabilioni ya mapesa na hivyo baadaye pesa hizo hutumiwa kwa matumizi au biashara mbadala na hivyo kuyafanya mashamba hayo kufa.

Korona ya mashine za ku-process singa au nyuzi za mkonge. Katika mashamba mengi hayana korona za kisasa na hivyo kuwafanya wakulima wadogo wadogo kukata tamaa ya kuendelea kulima zao hilo. Nashauri Serikali iangalie namna ya kuwawezesha wananchi kupata korona mpya na za kisasa ili waweze kuendeleza zao la mkonge na hivyo kujipunguzia au kuondokana kabisa na umaskini na hivyo kuongeza pato la Taifa na familia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri zao la mkonge lipewe kipaumbele kwani ni zao ambalo lina faida nyingi kama kuzalisha umeme, mbolea na ni zao vumilivu kwa ukame, hivyo ni vema suala hili litazamwe kwa mtazamo chanya kwa maendeleo.

**MHE. PHILIP A. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ifike mahali tukubaliane kwamba, wale tuliuwakabidhi madaraka kwa ajili ya kumsaidia Rais katika Wizara mbalimbali hususan Wizarani ya Fedha, wameshindwa kazi. Pia pesa katika Halmashauri zetu zinaliwa na wajanja wachache huku wananchi wakiteseka katika nchi yao kwa kukosa huduma muhimu. Napendekeza Waziri wa Fedha na Katibu wake, wawajibishwe kwa manufaa ya Taifa na Umma wa Watanzania. Naomba kuwasilisha.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maslahi ya Madiwani. Imechukua muda mrefu sana jambo hili kupewa umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na matumizi ya ovyo na ubadhirifu mkubwa wa matumizi ya fedha za umma. Aidha,

kumekuwepo na uhamishaji holela wa fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu; hivyo basi ni wajibu wa Serikali sasa kuamua kupitia CAG kufanya *Special Audit* kwa Halmashauri zote nchini badala ya utaratibu wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mingi ya Halmashauri zetu nchini inajengwa chini ya kiwango. Aidha, kumekuwepo kuchelewa sana kwa Miradi kukamilika kwa ukosefu wa fedha. Utaratibu huu ni lazima uangaliwe upya wa kuhakikisha fedha za Miradi zinapatikana kwa wakati hususan Miradi ya Wananchi kupata maji na umwagiliaji, afya na barabara kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa inaonesha jinsi Wizara zinavyoingilia utendaji wa kazi za Mashirika ya Umma; ni vyema Wizara sasa zisiingilia kazi za Mashirika haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ukusanyaji wa kodi na Sheria ya Kodi inapaswa kupitiwa upya ili kuongeza wigo wa mapato na kuondoa mianya ya ukwepajji wa kodi; ni vyema tujipange vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utegemezi wa Bajeti za Maendeleo; tunafahamu karibia ulimwenguni kote hali ya uchumi siyo nzuri hivyo nchi wahisani nao pia wana matatizo na inabidi kuwasaidia nchi za huko Ulaya kama Greece na Spain; hivyo inapelekea wakati mwingine kuleta fedha pungufu kuliko ahadi au kutotoa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ni kwamba, inabidi Serikali kutafuta vyanzo vingine vya mapato; kwa mfano, katika Nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania pekee ndiyo yenyewe kiwango cha juu cha misamaha ya kodi. Kutokana na Ripoti ya CAG, kuna misamaha ya kodi isiyopungua triliioni moja. Huu ni msamaha mkubwa sana unaolipotezea Taifa mapato na misamaha mingi inatokana na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni matumizi mabaya ya fedha za umma na manunuzi yasiyofuata Sheria za Manunuzi. Kiasi cha shilingi 50,685,371,565.58 zilitumika kupitia Wizara tofauti bila kufuata Sheria za Manunuzi. Baadhi ya Wizara wanatumia fedha nyingi kupongeza Viongozi kupitia Vyombo vya Habari kwa Matukio ya Kitaifa; mfano,

Pongezi kwa Sherehe za Muungano, Uhuru Saba Saba, Nane Nane na kadhalika.

Je, ni kiasi gani Serikali inakusanya kupitia madini yetu, mashirika ya simu na kadhalika? Huu ni wakati Wizara sasa waanze kumiliki ofisi zao badala ya kukodi na waanze kujenga hapa Dodoma. Mfano, Wizara ya Afya inakodi pango kwa mwezi shilingi 38,000,000 na kwa mwaka shilingi 456,000,000 na Wizara ya Ujenzi kwa mwezi shilingi 40,000,000 kwa mwaka shilingi 480,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinatosha kabisa kujenga jengo lao hapa Dodoma wakitumia kodi ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi imetokea mtindo pale inapokosekana pesa ya kujenga mfano Chuo cha Dodoma, Daraja la Kigamboni na kadhalika, Serikali inakwenda kukopa kwenye Mifuko ya Kijamii kama NSSF, PPF na kadhalika. Hizi ni fedha za wanachama, siyo vibaya kukopa lakini walipe; mpaka leo ni kiasi gani imeshawenza kuwalipa NSSF kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma? Hii ni hatari kwa Mifuko hii na siyo hilo tu, bado Deni la Taifa linazidi kukua, mpaka Juni 2010 liliifikia trilioni 14 na zaidi na mpaka sasa hivi deni hili halijalipwa hata kidogo; je, kwa mwendo huu tutafika?

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Kamati kwa kutimiza majukumu yake ya Kikanuni. Kamati wamefanya kazi kwa umakini mkubwa sana na kutoa mapendekezo. Kwa kuwa ubadhirifu huu ni wa muda mrefu, kila bajeti wizi unatokea ni afadhalii sasa Bunge lichukue hatua ya kutoa maamuzi magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo hewa ya mishahara yanayofanywa kila Wizara, wale wote wanaolipa na wanaolipwa washtakiwe na kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu manunuzi hewa, kuna ushirikiano mkubwa wa timu ya wataalam kwenye wizi huu. Mkurugenzi au Mkaguzi wa Ndani nao hawawajibiki mpaka ukaguzi toka Ofisi ya CAG au Kamati ya Mahesabu ya Fedha za Serikali kuja kugundua. Lazima Wakurugenzi wabanwe kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya magari; Mkuu wa Idara anapeleka gari kwenye matengenezo na kuleta bili kubwa mno na hakuna ukaguzi wa kuhakikisha kwamba malipo hayo ni halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba mibovu inaendelea kuwa kikwazo kwenye Mashirika ya Umma hata kwenye Halmashauri zote hapa kuna wizi mkubwa. Ninapendekeza kuwe na Tume itakayochaguliwa kupidia Mikataba ya Mashirika ya Umma na Halmashauri na kutoa usiri mkubwa wa Mikataba kwani inachukua muda mrefu kutokugundulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwamba, asilimia kubwa ya mashirika yaliyobinafsishwa hayajafanikiwa kutohana na mikataba mibovu. Pili, mengine yamegeuzwa matumizi tofauti na matumizi ya awali. Tatu, mashirika mengine kuacha viwanda bila kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ya mashamba ambayo yamebinafsishwa kuachwa bila kutumika na kuleta mgogoro na wananchi, kwani sasa wananchi wamevamia hapa. Wananchi waliovamia maeneo ambayo hayatumiki waachwe watumie kwani yameleta migogoro mikubwa. Mashamba yatumike kwa huduma za kijamii kuliko kukaa bila matumizi, kila Halmashauri wamepitisha bajeti zao kwenye ngazi zote na kupidishwa, bado asilimia 30 tu ndiyo inapelekwa tena kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na asilimia ndogo, bado wizi, manunuzi mabovu, huku unakuta fedha zimeingia kwenye Miradi lakini inatekelezwa kwa kiwango cha chini. Serikali ipeleke fedha za Halmashauri kwa wakati na ukaguzi ufanyike kwa Miradi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye mabadiliko makubwa kujisafisha ili wale wote ambao hawawezi kufanya kazi za wananchi kwa kila Idara au Wizara, hata Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa nafasi mbalimbali, waondolewe ili kuangalia kama ufanisi wa shughuli za Serikali zitafanyika kwa uwazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wenyeviti wote na Wajumbe wote kwa taarifa nzuri. Hongera Mwenyekiti, kazi nzuri huzaa mafanikio. Ahsante sana.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kuwashukuru sana na kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati, kwa jinsi walivyowasilisha Taarifa za Kamati zao na nawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niende moja kwa moja kwenye Halmashauri; kwa kweli wanatuangusha sana na sijui ni kwa nini wanafanya hivyo maana haiingii akilini kabisa Mkurugenzi na watendaji wengine, kuzifanya Halmashauri zetu kama shamba la bibi na kuwaacha

wananchi ambao ndiyo walengwa hawapati kitu kabisa wala huduma yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye huduma zote kama vile elimu, maji, afya, mafungu yote ya fedha yanapokuja wao wanagawana tu kana kwamba hazina pa kwenda, wanajinufaisha wao wenyewe tu na watu wetu yaani wananchi wanabaki kuilalamikia Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda vijijiini utashangaa sana vituo vyote nya afya hawana dawa kabisa na siyo kwamba mafungu hayapo, yapo ila ni uzembe tu wa watendaji wetu. Pia shule hazina madawati, madaftari na mabweni, watoto wanalazimika kupanga kwenye nyumba za watu binafsi ma wanakaa bila usimamizi wa mtu yeyote, matokeo yake watoto hawa wamekuwa wakipata mimba ovyo na kibaya zaidi wanaambukizwa magonjwa ya zinaa ukiwemo UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sheria ichukue mkondo wake, watendaji hawa wawajibishwe wasilindwe wanatupeleka pabaya. Naomba kumalizia kwa kuiomba sana Serikali isikie kilio hiki cha Wabunge, haiwezekani kabisa watu wajikuchukulie tu fedha za Serikali kama zao binafsi. Ahsante.

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kutokuwa na Kamati imara za ununuzi katika Mashirika ya Umma, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa Kamati za Manunuzi zinaundwa na kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutofanyika kwa tathmini ya utendaji wa wafanyakazi *performance audit* kunazorotesha sana utendaji wa wafanyakazi. Kitendo cha Wakurugenzi wa Halmashauri kushirikiana na Watendaji wa Benki ya NMB katika kufuja fedha za Serikali, ni tatizo linalohitaji kufanyiwa ukaguzi maalum kwa Halmashauri zote, kwani kuna habari za uhakika kwamba *Bank Statements* zinatengenezwa kwa kuchapwa na *computer* na sio zile *original* zinazokua *printed* kutoka kwenye *system*.

**MHE. KHERI ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubinafsishaji wa viwanda nya korosho maamuzi haya yamesababisha Taifa letu kupata hasara katika maeneo kadhaa yakiwemo:-

- Kukosekana kwa bidhaa zinazotokana na ubanguaji *by-products* ambazo zinasababisha nchi yetu kupata bidhaa kwa ajili ya viwanda vingine;

- Kuwakosesha mapato stahiki wakulima wa korosho kwa kuwanyima uwezo wa kubangua korosho zao;
- Kuikosesha Serikali mapato ambayo ingalistahili kuyapata kwa njia ya kodi inayotokana na bidhaa za viwandani; na
- Kuitangaza Tanzania kuwa ni nchi inayozalisha korosho bora duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ubinafsishaji wa viwanda hivi unaitia hasara Serikali kwa kuviuza viwanda hivyo kwa bei ya kutupa ambayo hailingani na gharama halisi za ujenzi wa viwanda hivyo au hata bei ya soko (*market price*). Hali hii imetokana na tathmini ya viwanda hivyo kwa sababu zisizoeleweka ama hazikufanywa kabisa au hazikufanywa kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hizo, naunga mkono pendeleko la Kamati la kuvirejesha viwanda hivyo vilivyobinafsishwa ili wapewe wawekezaji mahiri na makini wenye huruma na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mashirika ambayo kulingana na shughuli yanazofanya, yanayo nafasi nzuri ya kuendeshwa kwa faida endapo yatapata fedha za kuendeshea kazi (*working capital*). Aidha, yapo mashirika ambayo yameanzishwa, lakini Serikali imeshindwa kuyapatia mtaji wa kutosha. Kutokana na hali hiyo, nakubaliana na maoni ya Kamati ya kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya kuyapatia mashirika hayo mtaji wa kutosha wa kujilendesha. Mfuko huo utaweza siyo tu kuyasaidia mashirika hayo, lakini pia unaweza kusababisha kupata nafasi ya kuyasimamia mashirika hayo kwa karibu zaidi na hivyo kuongeza ufanisi na gawio kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo baadhi ya mashirika yamekaa kwa muda mrefu bila ya kuwa na Bodi za Wakurugenzi. Mamlaka husika inapochelewa kuteua Bodi za Wakurugenzi inasababisha kukosekana kwa watu wa kuwajibisha wakati Menejementi za mashirika hayo zinapofanya vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mambo mengi yanayohusu sera na mipango ya muda mfupi na ile ya muda mrefu ya shirika, yanakosa chombo cha kuyapitia na kuyaiddhinisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika ambayo hayana Bodi yanakuwa yanaendeshwa kama Idara ndani ya Wizara na kupokea maelezo kutoka Wizarani. Hali hii siyo tu inayaondolea uhuru *autonomy*

mashirika hayo, lakini pia inadumaza maendeleo ya mashirika kwa kuwa mara kwa mara hulazimika kwenda Wizarani kwa ushauri na maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoptera na hali hii, nashauri kwamba mamlaka husika ijiwekee utaratibu wa kufuatilia mashirika yao na kuteua Bodi mara tu Bodi zilizopo zinapomaliza muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kuwapongeza Wenyevitii wa Kamati zote kwa uwasilishaji wa Taarifa za Kamati ambazo ni nzuri na zimebeba mapendekezo mazuri yanayoitakia mema Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo manne katika Taarifa ya POAC.

Kwanza ni uanzishwaji wa Mfuko Maalum wa Uwekezaji wa Umma (*PIF*). Pendekoz hili leo ni mara ya tatu au nne linaletwa tena hapa Bungeni. Pendekoz hili liliashaletwa tarehe 21/4/ 2010. Kama ambavyo ilikuwa imependekewa hapo awali na Mdhhibitii na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mwaka jana, Kamati ililetii tena mapendekezo haya haya na kuweka msisitizo mkubwa, lakini bado Serikali imelala. Mwaka huu, yaani leo Kamati imependekesa, tena tunaiomba Serikali hii iwe mara ya mwisho kuleta pendekoz hili.

Serikali ikiamua, hili linawezekana, kwani tuna Mashirika ya Umma yanayozalisha ziada (*surplus*) kama Mifuko ya Hifadhi za Jamii, *EWURA*, Mamlaka ya Bandari, *TCRA*, *SUMATRA*, *TANAPA* na mengineyo. Hizo *surpluses* ziwekwe kwenye Mfuko huo kwa madhumuni ya uwekezaji na upatikanaji wa mitaji. Mfuko huu utawekeza kwenye mashirika yenye kuhitaji mitaji kama *STAMICO*, *NDC*, *TTCL*, *NIP* ambayo ni *strategic parastatal*, na hivyo kuipunguzia mzigo mkubwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna Bodi mbovu katika Bodi tulizokutana nazo, ni Bodi ya Pamba. Mimi napendekeza na naunga mkono asilimia mia kwa mia Bodi hiyo iundwe tena, na iliyopo isimamishwe, ichunguzwe na wahusika wakikutwa na hatia washtakiwe na wafilisiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini upungufu mkubwa na ambao unaendelea kuitia Serikali hasara kubwa ambao ni ukodishwaji wa ndege aina ya *Airbus 420*. Mheshimiwa Mwenyekiti ameelezea vizuri kabisa katika eneo hili, na mimi naomba kuweka msisitizo katika eneo hili.

Kosa la kwanza kabisa walilolifanya Menejementi ya ATCL ni kusaini mkataba wa kukodi ndege hiyo kabla ya kutolewa dhamana ya Serikali ambapo ni kinyume kabisa na sheria inayosimamia utoaji wa dhamana za mikopo Serikalini.

Pili, mkataba ulitiwa saini kinyume na ushauri wa wataalamu ambao katika taarifa yao walielekeza waziwazi kuwa siyo sahihi kukodi ndege ambayo baada ya miezi sita itatakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa *12 years check*. Menejementi ya ATCL ilidharau ushauri ule na kuingia mkataba na *Walls Trading* kukodisha ndege hiyo ya *Airbus 420* kwa muda wa miaka sita. Ndege hiyo ilipokuja nchini mwezi Mei, 2008 iliruka kwa miezi sita tu na kutakiwa kipelekwa Ufaransa, wakati huo mkataba unasema kuwa *lease rate* ni US\$ 370,000 iwe imeruka au iko katika matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla deni tunalodaiwa mpaka tarehe 30 Januari, 2010 ni Shilingi bilioni 320 ambayo ni sawa na US\$ 200 milioni ambayo ni sawa na kununua ndege mpya mbili. Kutokana na Menejementi kuingia mikataba mibovu, nami naomba hatua za kisheria zichukuliwe kwa wote waliohusika na uingiaji huo wa mkataba. Pia kulifufua Shirika hilo la ATCL siyo *economical*, tunaomba Serikali iunde upya Shirika la Ndege la Tanzania.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Aidha, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonyesha kwamba fedha nyingi za Taifa hili zimekuwa zikipotea kwa kupitia Halmashauri zetu za Serikali za Mitaa. Kama ambavyo ripoti ya Kamati imeeleza, *value for money* imekuwa haipatikani katika kandarasi nyingi na hili limekuwa likifanyika kwa makusudi kwa kushirikiana baina ya Wakandarasi na Watendaji wasio waaminifu kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshindwa kuelewa inatokea vipi au mzabuni anawezaje kulipwa fedha kabla ya kutoa huduma? Hili limetokea katika fedha za mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ujasiri wa kiasi hiki unaweza kuonyeshwa kwangu, mimi Mbunge tafsiri yake ni kwamba mambo kama haya yamezoeleka na yanafanyika kila siku na ndiyo mwanzo wa manunuzi hewa. Inanishangaza kwamba katika utaratibu wa malipo, iliwezekanaje *documents* zikakamilika ikiwa ni pamoja na *delivery note*?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri zetu, Maafisa Mipango wanaonekana kuwa na nguvu kubwa na inategemea na *influence* yao katika upatikanaji wa fedha za miradi. Mara nyingi nimikuwa nikisikia kwenye vikao vya Halmashauri zetu kwamba Afisa Mipango aangalie namna ya kuangalia vifungu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri nyingi hatuna *transparency* katika utoaji wa taarifa ya fedha zinazopatikana kutoka Serikali Kuu.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora katika Mashirika ya Umma ni pamoja na kutekeleza majukumu yao kama yalivyoainishwa katika *mission* na *vision* zao, kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, kufanya kazi kwa uhuru bila kuingiliwa, Shirika kuwa na kiwango cha juu cha tija na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Menejimenti za Mashirika mengi ya Umma zinaingiliwa na Bodi za Mashirika yao na wakati mwagine na Wizara na wanasiasa. Hali hii ni hatari kwa uendeshaji wenye ufanisi wa mashirika hayo. Wenyeviti kadhaa wa Bodi wamejitwalia madaraka ya Wenyeviti Watendaji, wakati ni kinyume cha sheria iliyoanzisha mashirika hayo. CAG alitolea mfano Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kuhusiana na Wakurugenzi wake wa Bodi kwenda kwenye maonyesho ya kimataifa ya Utalii katika kipindi cha kati ya Julai, 2010 na Juni, 2011. Hii ni kinyume cha utawala bora na Waraka wa Ikulu No. HSC/B.40/6/21 wa tarehe 28/3/1994. Bodi inapofanya kazi za Menejimenti kwa sababu ya maslahi ya kifedha, haitakuwa na nguvu ya kuhoji juu ya kushindwa kufikiwa kwa malengo na kubariki kufanya maamuzi yanayolinda maslahi yao katika Bodi.

Naunga mkono pendekezo la Kamati la uanzishwaji wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma (*Public Investment Fund*) ili kusaidia baadhi ya Mashirika ya Umma yenye umuhimu mkubwa kwa uchumi wa Taifa hili. Lengo ni kuyapa mtaji mashirika hayo ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu kama ilivyo dhamira ya kuanzishwa kwa Mashirika hayo ya Umma.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kuhusu taarifa ya Kamati ya Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

Serikali, inatoa pesa nyingi katika Halmashauri nchini na pesa hizo ni kama 70%, lakini katika Halmashauri nyingi, pesa hizo hazitumiki ipasavyo. Pesa zinaliwa na watu wenye tamaa na kujinufaisha wao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, mtindo wa kukagua hesabu za miaka miwili nyuma, haufai. Pili, tunaomba watu wote wanaohusika na ubadhirifu wa fedha za umma wanaotambuliwa na CAG wachukuliwe hatua kali na ikibainika kama kweli wamefanya kosa basi tupitishe Sheria kuwa, adhabu yake iwe kama ifuatavyo:-

Adhabu iwe miaka mitano na mali yote ikithibitishwa kuwa, mali ile aliiapata kwa pesa aliyoiba afilisiwe. Kwa kweli, pesa za Serikali za Mitaa zinaibowiwa sana na kama tungepata watu waaminifu, nchi yetu ingekuwa na sura mpya.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo sugu la kutopeleka gawio litokanalo na zao la korosho, hivyo kuzua migogoro kwa wananchi isiyo na lazima. Pendekezo, Serikali isikilize malalamiko ya Vyama vya Msingi na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali itambue kuwa, *General Purpose Grand imefutwa*, hivyo Halmashauri inategemea sana rasilimali za maeneo yote. Lakini ni lazima minara ya simu, uchimbaji wa kokoto na madini, wawekezaji walipe *service levy* kwa kuwa, Halmashauri inatoa huduma mbalimbali ikiwemo barabara, maji na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ili iweze kufanya kazi yake vizuri na kutimiza ahadi zake kwa wananchi, ni lazima ihakikishe inasimamia kikamilifu makusanyo ya kodi kutoka katika sekta mbalimbali za biashara na katika viwanda vyote vya uzalishaji mali, pia, katika makampuni yote ambayo yapo na yanafanya kazi. Ikiwa, kila mfanyakia biashara, makampuni na wafanyakazi wanawajibika katika utoaji kodi, basi nchi yetu itaendelea bila kutegemea misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ya Tanzania, inakuwa na bajeti ya mwaka trilioni 11, ikiwa kama kadirio la bajeti ya mwaka 2011/2012. Hii bajeti, inategemea makusanyo ya kodi ambayo yanatoka kwa wananchi wa Tanzania, lakini ukiangalia utajiri ambao tunao, hii bajeti ni ndogo; ndio maana kuna miradi mingi sana haiishi kwa muda uliopangwa na tunashindwa kuwalipa Wakandarasi wetu kwa muda tuliokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi inapangwa kwa kutegemea fedha za wafadhili, ambao mara nyingine hawaleti fedha zote au hawaleti kabisa. Kwa mfano, mradi wa maji wa *World Bank*, mpaka leo bado mradi huu unasuasua. Napenda kutoa ushauri kwa Serikali kuwa,

tusimamie kikamilifu kwa uaminifu katika makusanyo ya kodi, kama makampuni ya madini, maliasili na utalii, viwanda vikubwa, makampuni ya simu, wawekezaji katika sekta mbalimbali na kodi ikakusanywa kwa uhakika, hatuwezi kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi. Ukiwa umefanya makusanyo au mapato tunategemea ufanye matumizi sahihi kwa manufaa ya Taifa. Tunapofanya bajeti, lazima kuwa na maeneo mawili tu, hayo ni mapato na matumizi, maana yake, fanya makusanyo halafu fanya matumizi sahihi kwa kufuata bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ambayo tunayaona, mengine siyo sahihi. Kwa mfano, kutumia bila kufuata bajeti, ndiyo maana nchi yetu inaingia katika madeni, ili kufanikisha mipango iliyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nazipongeza Kamati zote zilizowasilisha Taarifa zao hapa Bungeni. Naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara kwa watumishi hewa. Tatizo hili limeendelea kuisumbua Serikali, kwa kupoteza fedha nyingi za umma kwa ujanja wa watu wachache. Nashauri Serikali, itupe mkakati wa kudumu wa tatizo hili. Udhifu katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, tatizo kubwa ni kucheleweshwa kwa ruzuku ya fedha za maendeleo na nyingine kupelekwa muda mfupi kabla ya kwisha kwa mwaka wa fedha. Hivyo, kusababisha miradi hiyo kutokamilika kwa wakati. Hii ni pamoja na ucheleweshaji au kupeleka au kutopeleka kabisa fedha za matumizi mengineyo (*Other Charges – OC*). Ucheleweshaji wa OC unainyima nafasi Halmashauri yoyote kusimamia miradi yote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kukaimu Idara au Ukurugenzi wa Halmashauri, mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, imekalmiwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili bila ya sababu ya msingi. Naiomba na kuisihi Serikali kwa mara nyingine, iipatie Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, Mkurugenzi Mtendaji au imthibitishé yule anayekaimu nafasi hiyo kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Medical Stores Department (MSD)* imeshindwa kutekeleza majukumu yake kwa kutopeleka dawa zinazotakiwa kwa wakati au kutopeleka kabisa dawa wakati fedha za

wananchi zinaendelea kukaa kwenye akaunti ya MSD, badala ya kuzipatia Halmashauri fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa Kamati ya LAAC kuzikagua Halmashauri, Manispaa na Majiji ni mfinyu, uongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Ukweli ni kwamba taarifa zote za Kamati tatu zinasikitisha sana, naiomba Serikali ichukuwe hatua za haraka kuwachukulia hatua za kinidhamu wote wale waliofanya ubadhirifu wa pesa za walipa kodi na kufilisiwa mali zao na kufungwa, sio kuwahamisha watuhumiwa ili kuijengea Serikali heshima kwa wananchi wake. Ukweli hali inatisha sana, wizi ni mkubwa sana.

**MHE. LOLESTIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kushukuru kwa taarifa za Hesabu za Serikali. Ni kweli kwamba taarifa hizi zinagusa hali halisi ya utendaji kazi katika nchi yetu. Katika taarifa ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika ukurasa wa 12 kipengele (c) kinazungumzia kuhusu mipango ya ubabe ya Serikali Kuu katika vyanzo vya mapato vilivyoko kwenye Halmashauri. Hii ni dhahiri kabisa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita yapo makampuni mengi sana yanayofanya kazi katika mgodi wa Geita (GGM) lakini makampuni hayo yanalipa kodi kwenye Ofisi za Makao Makuu ya kampuni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasababisha Halmashauri yetu kukosa mapato pamoja na kwamba shughuli za uchimbaji zinafanyika ndani ya Wilaya yetu. Suala hili tumelifuatilia sana bila mafanikio. Mapato ambayo tungepata kutoka kwa makampuni haya yangetumika kuongeza mapato ya Halmashauri yetu lakini kwa sasa mapato tunayopata ni kidogo sana. Hivyo, naomba Serikali iangalie upya namna ya ukusanyaji wa mapato. Endapo kampuni inafanya kazi Geita basi mapato yakusanywe katika Halmashauri husika. Hii itasaidia kuboresha hali na kuchochea maendeleo ya mahali hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ni changamoto kubwa kwa Halmashauri zetu ni namna ambavyo ruzuku ya miradi ya maendeleo kutopelekwa kwa wakati. Hili ni tatizo kubwa sana na linasababisha miradi hii kutekelezwa chini ya kiwango. Hivyo basi Serikali iangalie namna na njia nzuri ya kufanya ili kurekebisha tatizo hili la sivyo shughuli za maendeleo katika Vijiji, Kata na Wilaya zetu hazitafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watumishi wabadirifu, ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuchukua hatua kwa wale watumishi

wabahirifu, kwa sababu wanagharimu Taifa na wananyonya mapato ya wananchi msipochukua hatua, hali hii itaendelea kwa watumishi walio wengi. Hivyo watumishi wabahirifu wachukuliwe hatua kali za kinidhamu ili iwe fundisho kwa watumishi wengine. Dhana ya kuwahamisha wabahirifu toka sehemu moja kwenda kwingine ni dhana ambayo haikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mapendekezo ya Kamati.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Hata hivyo nina hoja zangu kama ifuatavyo:-

Muda wa kujadili Kamati za fedha zote hautoshi kwani ni sekta muhimu zaidi zinazosukuma uchumi wa nchi na mustakabali wake wa Taifa. Mashirika ya Umma yamekuwa ni tatizo. Taifa linapata hasara sana, pato la Taifa ni dogo sana, nchi inaendelea kuwa maskini kisa mapato hafifu, ufanisi na uadilifu hakuna tatizo ni nini?

Mashirika haya kuingia mikataba mibovu, pato la Taifa kupotea kama vile *TBC verse Star Media* na kadhalika, *negotiation skills* za *win win* ina maana haipo? Nchi yetu ni tajiri sana kwa rasilimali, lakini ajabu ni mojawapo ya nchi maskini sana duniani, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, manunuzi ya umma kwenye mashirika ni mabovu, pesa nydingi zinaliwa kijanjanja. Hatua hazichukuliwi kwa nini? Ubinafishaji wa Mashirika ya Umma hauoneshi mafanikio, pesa yanayouzwa ni ya kutupwa, viwanda vyenyewe pia vinakufa, wananchi wanapata tabu, mifano mizuri ni mgodi wa Kiwira Coal Mine, Uvinza, ATC na kadhalika ni dana dana tu zinapigwa. Je, hatma yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wengi wanasuasua sana katika utekelezaji wa kazi, kwa nini na inatibiwaje kansa hii? Maofisa wengi wanakaimu kwa muda mrefu sana hivyo morali na ufanisi wa kazi unakuwa hafifu, ni kwa nini? Wakurugenzi wa Halmashauri wafanyiwe usaili kwa uadilifu na ufanisi. Mambo yanayosikitisha ni mengi, hayo ni machache tu, je hatma yake ni nini?

Kitendo cha Wabunge kuteuliwa kwenye Bodi mbalimbali kinasababisha ufanisi wa kazi usiwepo, maingiliano ya kazi, *conflict of interest* na mengineyo. Wasipokuwepo kwenye Bodi hizo kwani haiwezekani? Faida zake ni zipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kuchangia kwa maandishi katika hoja hii iliyio mbele yetu. Kwanza kabisa naunga mkono maamuzi ya Kamati zote tatu zilizowasilisha maoni yao, naomba nijielekeze katika hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu zinayumba kwa kiasi kikubwa kwa kuwa baadhi ya Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wanatumia ovyo fedha za Serikali. Miradi mingi ya Halmashauri inatekelezwa chini ya kiwango na hivyo thamani ya fedha kutokuwepo katika miradi mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule utaratibu wa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara kupatikana na tuhuma za ufujaji wa mali au fedha za Halmashauri kuhamishiwa maeneo mengine, usifanyike bali wafukuzwe kazi na warejeshe kile walichochukua kwa mujibu wa Sheria. Kwa sababu suala la kuwahamisha unakuwa unatoa tatizo sehemu moja na kupeleka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana mamlaka ya Madiwani yapewe nafasi kwani ile hoja ya kusema Madiwani siyo wataalam hivyo hawawezi kukataa kitu chochote ambacho mtaalam amekipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nielekee *TBS*. Inasikitisha sana kuona nchi hii imekuwa na vitu vingi vinavyoingizwa nchini visivyokuwa na kiwango mpaka mbolea sasa inaletwa feki, iliyio chini ya kiwango, hivi tunakwenda wapi? Maana yake sasa tunaleta mchezo kwenye ajira iliyio na watu wengi hapa nchini ambao ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kariakoo simu ambazo hazifai zimejaa madukani, kwa nini tunaruhusu vitu hivi nchini kwetu? Kuna maduka ukienda wanakuuliza unataka *original* au feki? Hivi ni wapi tunapeleka nchi hii *TBS* wanafanya kazi gani, hata hayo hawayaponi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja. Mawazo yote yalitolewa na Wenyeviti wa Kamati zote tatu ukizingatia hata huo ubinafsishaji hauna manufaa yoyote katika nchi hii, viwanda vingi vimekufa, havifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja maoni yote yaliyotolewa na Kamati. Nakushukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote tatu kwa maandalizi mazuri ya taarifa zao. Nitazungumzia na kujielekeza kwenye taarifa ya Serikali za Mitaa. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi mingi inayotekelizwa na makandarasi mara nyingi haifuatiliwi kikamilifu. Si mara zorte ambazo miradi haitekelizwi kwa wakati kutokana na kucheleweshwa fedha kutoka Serikalini bali ni udhaifu wa ufuatiaji. Ufuatiliaji ambao ama unafanyika na Mkandarasi Mshauri au na Watendaji ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu watendaji wa aina hiyo wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kuchelewesha utekelezaji. Kuna tatizo pia la Serikali kutowajulisha wananchi wanaozunguka maeneo ya miradi ili wahusike kusimamia usalama wa miradi inayohusika. Serikali nayo iwe makini na kuhakikisha fedha za miradi zinapelekwa katika miradi husika kwa wakati ili kusiwepo na visingizio vya kucheleweshwa kwa kukamilika kwa miradi. Hata hivyo, zipo Halmashauri za Wilaya ambazo fedha za miradi inayotumwa na Serikali hufanyiwa matumizi yasiyoidhinishwa na matumizi ya ubadhirifu mkubwa. Serikali inaombwa kuchukua hatua za haraka dhidi ya wabadhirifu hao, mara Mabaraza ya Madiwani wanapoleta taarifa za ubadhirifu unaofanywa na watendaji wabovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri. Tatizo hili ni kubwa kwani ni dhahiri kwamba watumishi na watendaji wengi katika Halmashauri si waaminifu wakati wa ukusanyaji wa ushuru katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri. Ushahidi wa wazi ni pale ambapo watendaji wa chini hujitokeza kujenga majumba makubwa ya kifahari au kujilimbikizia mali nyingi. Hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na taasisi zinazohusika kuwafuatilia watendaji wa aina hiyo waoneshe ni kwa namna gani wamejipatia mali hizo. Hali hii inaleta manung'uniko makubwa kwa wananchi kwani Halmashauri hazifikii malengo yanayopangwa. Nashauri, Serikali ihakikishe kuwa watendaji wa aina hiyo wanafuatiliwa na kuwafikisha katika vyombo vinavyohusika kujieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali pia kwamba kutokana na watumishi wengi katika Halmashauri za Wilaya kukaa vituoni kwa muda mrefu sana na kufanya kazi kwa mazoea, hatua za kuwahamisha ni vizuri ili kurekebisha kasoro zinazojitokeza mara kwa mara.

Kuhusu upatikanaji wa hati chafu. Hati chafu katika Halmashauri ni aibu kubwa kwa watendaji na Madiwani pia. Halmashauri zinazopata

hati chafu, Wakurugenzi Watendaji wanaotoka katika Halmashauri hizo wanatakiwa kuwajibishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja hiyo.

**MHE. MOSHI SULEIMANI KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati kwa kuwasilisha hoja za Kamati zote kwa uwazi na kwa takwimu zenyé uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia matatizo makubwa yaliyo kwenye Halmashsuri ya Wilaya. Eneo hili lina matatizo makubwa sana, kuna wizi unaofanywa na watendaji wa Serikali hasa wizi wa fedha unaotumika juu ya watumishi hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapoteza fedha nyngi kwa kulipa watumishi waliokufa na kuendelea kupewa malipo ya mishahara kama wapo hai. Tunaiomba Serikali iwachukulie hatua kali wote waliohusika na mchezo mchafu wa kuiibia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la *TBS*. Shirika hili halifai hasa watumishi wake kushindwa kuwajibika ipasavyo kwa maslahi ya nchi na badala yake kutumika kwa maslahi binafsi. Serikali ichukue hatua kazi dhidi ya Mkurugenzi Mkuu wa *TBS* na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda wawajibishwe na hatua kazi za kisheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika hili limesababisha hasara kubwa kwa wakulima wa nchi hii kwa kuingiza mbolea ambazo hazina ubora wa kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Shirika la Ndege lazima ufanyike uchunguzi wa kina na viongozi wote waliohusika wachukuliwe hatua.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kuwasilisha maoni yangu na mashaka yangu juu ya mwenendo mzima wa usimamiji na utendaji wa Serikali kwani umekuwa chini kabisa ya viwango. Imethibitika waziwazi kuwa kumekuwepo na wizi mkubwa wa fedha za umma zinazochotwa na bila wezi wa makusudi kuchukuliwa hatua zozote. Hili jambo limekuwa sugu katika Kamati zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu ni kwamba, nakubaliana na Wabunge wote wanaoona kuwa watendaji wakuu wa Serikali ndiyo vinara wa mchezo mchafu unaoangusha nchi hii. Hivyo hatujachelewa sana kuchukua hatua muafaka kutibu donda ndugu hili.

Moja, wale wote walioibia mashirika kwa njia ya mikataba mibovu waorodheshwe vizuri halafu wafanyiwe uchunguzi wa mali kwa kila hali. Tunapounda Tume za kuwachunguza isiwe moja tu bali zaidi ya mbili na nyingine zisifahamike ili tuje tufananishe matokeo. Watakaothibitika bila kuchelewa wafilisiwe ili wasiendelee kutamba na kukwamisha maendeleo.

Pili, mtindo wa kutegemea *TAKUKURU* kuwa ndiyo chombo cha kutukamatia watoa rushwa; umeshindikana kabisa kwani kwa hivyo ilivyo hawa ndiyo wanaowasaidia njia za kuiba na kupokea rushwa. Hivyo, *TAKUKURU* haifai kabisa bora ifutwe kabisa ili tujue hamna msaada, tufunge milango yetu badala ya kuacha wazi. *TAKUKURU* ifutwe yote tuanze upya.

Tatu, suala lingine ni la kuona tabaka fulani la Watanzania ndiyo wanaongoza kwa kuhodhi viwanda, ardhi ya Watanzania na kadhalika. Mfano, *Chavda, Mohamed Enterprise* na jamaa zao utaona kuwa ndiyo wadhaniwa wakuu wa fedha ya Serikali. Je, wakuu wa fedha ya Serikali isiwa-organise vijana wake wanaomaliza vyuo vikuu mara wamalizapo vyuo kupatiwa dhamana ya namna hii ili waweze kufanya miradi mbalimbali mfano, wahitimu wa kilimo, mazingira na kadhalika. Kwa nini Serikali haziwezi kufikiria mambo muhimu kama haya kwa faida ya vijana wetu.

Pendekezo ni kuona kuwa Watanzania asilia siyo wageni ndiyo wanaopata fursa za kudhaminiwa kwanza na kujengewa mazingira ya kuwaendeleza. Kutokana na hili tungependa Serikali ifufue mtindo wa ku-truck (ufuatiliaji) wa utambulisho wa watumishi na wafanyabiashara. Ni wakati muafaka wa kupata orodha ya matajiri angalau kumi ambaa ni matajiri kupindukia kuanzia yule wa juu kabisa hadi wa mwisho. Iwe wazi kwa Wabunge na watu wote kwani uwazi ni mojawapo ya misingi ya Demokrasia.

Mwisho, ni mmonyonyoko wa maadili ya viongozi ya kutukuza wezi wa mali ya umma na kuwafukuza. Tunahitaji sana kufuta tabia hii kwa kuchukua hatua za kutoa adhabu kwa wahusika wote hadharani ili watoto wetu watambue kuwa tabia za wizi ni mbaya sana, hivi hata tukifundisha madarasani watatuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahusika wakuu wa wizi wote wachukuliwe hatua za haraka hata ikifaa kutoingia katika kipindi cha bajeti yetu kabla hatuja-recover fedha hizi toka kwa mafisadi na vizalia vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kusisitiza kwamba Chama Tawala (CCM) kimeshindwa kazi kabisa.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Watanzania wana imani na Serikali yao, lakini kitu ambacho kinasikitisha mno ni kuona watendaji wakiharibu hawafikishwi Mahakamani na hata wakifikishwa hujui wamechukuliwa hatua gani zaidi ya kuhamishiwa eneo lingine. Mfano, katika Wilaya ya Kondoa, Rombo na kadhalika. Suala hili liliwahi kutokea na Mkurugenzi huyo alihamishwa, utaona muda mfupi mtendaji analetwa ana magari ya kifahari, nyumba mbili au tatu za maana, je, wana mishahara gani ya kununua na kujenga nyumba zaidi ya mbili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ni chombo cha utetezi wa wananchi, utakuta ubinafsishaji unafanyika bila tafiti za kina na kuangalia madhara yake nini na bila kuangalia wananchi wananaufaikaje. Imekuwa ni migogoro takriban sasa nchi nzima inakuwa na kelele kwa kuisaidia Serikali iwe na uchunguzi wa kina na kuwaelimisha wakazi wa eneo husika, itapunguza migogoro.

Mfano kuna kiwanda cha Seera Babati kinavuna miti aina ya Misandale katika maeneo ya Monduli na Kondoa, je, Serikali haioni wananchi hawanufaiki na mali walizonazo, bado ni kero?

Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa wamekaa kama wapiga debe tu wakati wanafanya kazi usiku na mchana bila hata faida ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu kama Madiwani ndiyo waajiri katika Halmashauri lakini wanaonekana hawana kauli wala mishahara, badala yake wanaambulia posho. Naomba sasa Serikali iwaangalie nao wapate mishahara kuliko pesa nyngi zinaishia hewani i na kwa watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ina dhamana, hivyo iangalie kupata faida za ubinafsishaji bila wananchi wao kupata ahueni ya maisha (Mfano, uuzaaji wa kampuni ya maji ya (*Ivory Coast*). Jamii ilindwe, nchi ilindwe, tusibinafsische kila kitu tutajajikuta tupo matatani na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike wakati sasa wa kupitia kila mkataba, kila shirika liliopo nchini lina wafanyakazi wangapi na Watanzania au si Watanzania tuangalie Watanzania wapo hapa hapa hawana ajira na hata tukiajiri hawapati haki zao zinazostahiki. Mfano, *Jambo Plastic* Watanzania wenzetu wamefanya kazi pale miaka kumi na

wamefukuzwa bila kupata mafao yao na muhimu kuajiri wengine je, lini Mtanzania atajikomboa kupata haki yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la wakulima halina kipaumbele dhidi ya maneno tu, hawanufaiki na kilimo chao hebu Serikali iwasaidie hasa kuhusu vocha ya pembejeo, mbolea, ushauri wa msisitizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata suala la madini haliwapatii faida wananchi hasa ukizingatia nchi ina fadhili mali nyingi Serikali ipitie hayo yote na kuyaweka wazi na wananchi kufaidika. Ahsante.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati kwa kazi nzuri sana ambayo imewasilishwa mbele ya Bunge Tukufu. Dhana ya kuanzishwa Serikali za Mitaa ni nzuri lakini utekelezaji wa majukumu unavyofanywa na Serikali Kuu na kwa watendaji wa Halmashsauri unakwenda kinyume kabisa na malengo ya kuanzishwa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za wananchi zinaliwa hovyo. Suala la manunuzi yasiyofuata utaratibu au utaratibu unaotoa mianya kwa watendaji kula fedha. Watendaji wamekuwa wakichelewesha kazi hadi kampuni ambazo wameweke miyadi (*conspiracy*) wapatikane ndiyo wapewe kazi na kazi zinazofanywa na kampuni hizo ziko chini ya kiwango na hawahoji kabisa.

Makusanyo kwenye Halmashauri. Vyanzo vya mapato kwenye Halmashauri zetu nchini havisimamiwi vizuri na kuna mianya mingi inayotorosha mapato ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa vitabu feki vya kukusanya, kuwepo kwa tabia ya kutokurudisha vitabu vya kukusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuwa na mawakala ambao watendaji wa Halmashauri wanaohusika na fedha wanawaweke na kwa viwango vya chini, ili makusanyo mengi yabaki kwao, aibu kabisa.

Mishahara hewa pamoja na ufuutilaji na kubaini chanzo cha tatizo hakuna aliyewajibishwa huu ni uongozi mbovu kabisa.

Posho za Madiwani na Wenyeviti wa vijiji na vitongoji. Nasisitiza nakushauri kuwa viongozi hawa wanafanya kazi kubwa, walipwe mishahara kama siyo posho kwa viwango vifuatavyo:-

Madiwani 300,000 kwa mwezi; Wenyeviti wa Vijiji 100,000 kwa mwezi na 50,000 Wenyeviti wa Vitongoji kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri lazima ziangalie gharama za uendeshaji ambazo zinapanda sana. Jambo hilli lisipoangaliwa linadhoofisha mamlaka na Serikali za Mitaa, Serikali Kuu lazima iangalie na kufuata taratibu za utoaji ruzuku kwa Serikali za Mitaa.

Ucheleweshaji wa ruzuku kwa Halmashauri hauleti maana nzuri kwani kuna wakati Halmashauri inakaa bila kazi zinazoendelea katika miradi mbalimbali, hii ni hatari kwa maendeleo ya Taifa.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu ulionekana kwenye utendaji wa Serikali, kushindwa kusimamia mapato ya Taifa na hivyo kufanya hali ya uchumi wa nchi kuwa mbaya hivyo huduma muhimu za jamii kutokamilika ni usaliti kwa wananchi walioichagua Serikali. Kutokana na hali hiyo ili kulinusuru Taifa, kukinusuru Chama cha Mapinduzi wote waliohusika na ubadhirifu kufuatia taarifa ya CAG wawajibishwe bila huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Halmashauri fedha nyingi zimeliwa na Watendaji wa Halmashauri, lakini hakuna hatua kali zilizochukuliwa. Matokeo ya kupeleka watuhumiwa Mahakamani haisaidii, kwani wabadhirifu hawa kutumia fedha hizo kuharibu kesi na hivyo kesi kuchukua muda mrefu japo ushahidi wa wazi upo ambao umetokana na ukaguzi wa Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutochukua hatua kwa wabadhirifu wa mali ya umma, hutudhoofisha hata sisi Wabunge na hivyo kushindwa kukemea maovu mengi yanayofanyika kwenye Halmashauri; kwa sababu Watendaji Wakuu wa Halmashauri wana jeuri ya fedha. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, ukaguzi umebaini ubadhirifu wa fedha za wananchi zaidi ya milioni mia mbili sabini (Tsh. 270,000,000), lakini hakuna hatua iliyochukuliwa kwa wahusika hadi sasa. Katika hali hii Mbunge ukionekana unafuatilia unafanyiwa mizengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali isifumbe macho, iwachukulie hatua mara moja wote waliohusika, kuanzia Halmashauri hadi Serikali Kuu. Hatua za kuwachukulia kwanza ni kuwawajibisha na kutaifisha mali zao kuwa mali ya Serikali. Tofauti na hivyo tunaua Chama chetu cha CCM sisi wenyewe kwa mikono yetu, vinginevyo tutapishana na wananchi. Ahsante.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nashauri maeneo ambayo yana ubadhirifu wa fedha Mahakama ichukue nafasi yake. Ikiwa ni pamoja na maeneo ya pembejeo yaani vocha na kadhalika.

Kuhusu hesabu za Serikali za Mitaa. Naomba ushuru uliofutwa kwa Serikali ambao walihidiwa watapewa ruzuku, uangaliwe vema kwani Halmashauri zimechoka zinahitaji kuwezeshwa. Hadi vikao vya Madiwani vimeanza kuathirika.

Aidha, Sera ya *Public Private Partnership* pia itumike katika Halmashauri zetu.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie yafuatayo:-

- Madiwani wapewe mishahara katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013 ili waweze kupata uwezo wa kuadhibiti watendaji wezi wa Halmashauri za Miji kwani kipato chao ni kidogo kiasi wanakuwa na tamaa ya kupokea rushwa kuficha na kuwalinda wabadhirifu wa mali ya umma.

- Mheshimiwa Naibu Spika, pia Shirika la *MSD* lisambaratishwe, uongozi mpya uchaguliwe. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, inaonesha hawa viongozi na staff nzima imeshindwa kufanya kazi. Deni la *MSD* limefika bilioni 46, bado dawa zilizopitwa na wakati ya zaidi ya bilioni nane zimejazana stoo, vifaa tiba wameshindwa kugawa kwa wakati. Deni hili likalipwe haraka sana katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini wazi kuwa gawio toka kwenye Mashirika ya Umma kwenda Serikalini katika kipindi cha 2009/2010 kwenda 2010/2011, lilipungua toka 40.6 bilioni hadi shilingi 28.7 bilioni sawa na pungufu ya shilingi 11.8 bilioni.

Pungufu hili la gawio ni kubwa mno na kwa misingi hii inaonesha jinsi Mashirika ya Umma badala ya kuongeza ufanisi katika shughuli zake za usimamizi na uzalishaji yanarudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso langu ni kwamba, hatua kali zaidi zinapaswa kuchukuliwa kwa haraka kwa Watendaji na Viongozi wote waliopewa dhamana ya kusimamia Mashirika haya ili yalete tija na faida kwa Taifa letu.

Uingiaji na usimamizi usiofaa wa mikataba. Mkataba ulioingiwa baina ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Kampuni ya *Star Times International*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Hatua za kinidhamu hazina budi kuchukuliwa na Serikali kwa waliohusika kuingia mkataba huu ili kutoa fundisho kwa viongozi na watendaji wasiopenda kutanguliza maslahi ya Taifa ama kwa uzembe au sababu nyine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji usiokuwa na tija unaofanywa na baadhi ya Mashirika ya Umma. Nashauri Mashirika haya kabla ya kuingia katika mikataba ya uwekezaji ni vema Bunge lako Tukufu lipitie na kuona namna gani nchi inafaidika na uwekezaji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika wakati Serikali iangalie upya Sera ya Uwekezaji kwa kuwa kwa kiasi kikubwa hainufaishi nchi matokeo yake ni hasara kwa Serikali na kudumaza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujadili au kutoa maoni juu ya taarifa za Kamati za Fedha zilizotajwa hapo juu.

Nianze kwa kusema kuwa ukosefu wa uadilifu katika utumishi wa umma, ubinafsi na ukosefu wa uzalendo katika nchi yetu umemomonyoa nchi.

Nchi inapashwa kuandaa mkakati maalum wa kurudisha uzalendo ili kuwafanya Watanzania kujitambua na kutambua wajibu wao katika kuleta maendeleo ya nchi na watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi inayumba kimaadili, kwa ujumla wake, viongozi, Watendaji, Watawala, Majeshi na raia wote. Nchi itafute mbinu haraka kwa kuwajibishana, kutoa elimu kwa wananchi ili kurudisha imani. Nchi hii Viongozi wamepata upofu, hawasikii hawaambili matokeo ya haya ni mifarakanano na kutopendana, hivyo jamii yetu haitakuwa na mshikamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya katika Serikali, rushwa, ujisadi, mikataba isiyofaa, ubinafishaji usio makini kwa pamoja vimeliingiza Taifa hili katika umaskini.

Mamlaka zijitazame upya katika usimamizi wa kukusanya mapato na matumizi. Miradi ya Maendeleo isimamiwe kwa uadilifu katika viwango vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwawajibisha wale wote wanaohujumu nchi urudishwe na usimamiwe. Bila kuwa na dhamira na utashi katika kujenga nchi yetu tutabaki kusema na hatimaye kuingiza nchi hii katika machafuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni ya kurudisha uzalendo ianzie shule za awali, msingi, sekondari na kadhalika ili kizazi kinachokuja kitende yaliyo mema kwa nchi yao.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukubaliana nao kuhusu kuwepo matatizo makubwa kuhusu ukodishwaji wa ndege aina ya *Airbus* 320. Bali sikubaliani na kuamua kulipa deni hilo hasa kwa njia ya *arbitration*. Kama ni kwenda Mahakamani tufanye hivyo, hatuwezi kuogopa Mahakama kila siku. Wanasheria watushauri kwa makini sasa kuhusu hili.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mwenyekiti na Kamati yake ya LAAC kwa kazi nzuri na ngumu katika Taifa letu kwa maendeleo ya nchi yetu (ambayo ni watu na rasilimali zao).

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipanga kuchangia kwa mdomo, kwa bahati mbaya sijaweza kupata nafasi. Hata hivyo, vipengele viwili muhimu ni:-

Watendaji wa Halmashauri wanapokuwa hawana sifa za taaluma, wanapokuwa si waadilifu husababisha Halmashauri kupata hati chafu. Hapa wananchi hawana makosa, ila cha kushangaza ni kwamba Halmashauri inapopata hati chafu, *Council* inakatwa fedha za miradi na nyinginezo. Sielewi kwa nini *opinion* iunganishwe na *finance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndani ya Bunge lako Tukufu tuliomba endapo patatokeza hati chafu, basi waadhibiwe wahusika bila kuwaathiri wananchi. Naomba maelezo ya Serikali kuhusu ushauri huu

ambao ulikubalika ndani ya Bunge hili umefikia wapi na lini wataanza utekelezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la watumishi wenye sifa na uwepo wa Wakuu wa Idara. Naomba mamlaka husika ifanye tathmini ya watumishi walipo na sifa walizonazo kulingana na kazi afanyazo ili sasa fedha za Serikali ambazo kimsingi ni za walipa kodi ziwe zinatumika kwa mwongozo wa watumishi wenye sifa na uwezo. Naomba utusaidie hasa sisi *Council* ya Kilindi, watumishi hakuna si tu wenye sifa, ila hata hao ambao sifa zao za mashaka. Ahsante.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali, naunga mkono taarifa zote tatu. Nawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wenyeviti na Wabunge waliochangia kuhusu suala la bajeti isiyo halisia. Naishauri Serikali iwe inatengeneza bajeti halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya ya Serikali, Ukaguzi wa hesabu utiliwe mkazo na wahalifu wachukuliwe hatua katika muda muafaka (mfupi).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni makubwa ya Serikali, nashauri Serikali ilipe madeni inayodaiwa hasa madeni ya ndani. Kwa kutokulipa madeni hayo mapema inazidisha deni linaloumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi nje ya bajeti, nashauri Serikali ikomeshe jambo hili kwani ni kinyume cha Sheria ya Fedha na Katiba ya nchi. Nashauri Serikali isimamie kikamilifu utunzaji wa nyaraka za fedha (*manual and in software*) ikiwa ni pamoja na *asset register* ya mali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali za Mitaa, naungana na Waheshimiwa Wabunge kwamba miradi chini ya viwango ikomeshwe kwa kusimamia miradi hiyo kwa karibu kuanzia *foundation* mpaka *finishing stage*. Wahandisi wa Halmashauri na Madiwani wawe makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Halmashauri kuwa na watalaam na kuzuia ubadhirifu wa fedha za wananchi na watumishi wa Halmashauri za Wilaya hasa Watendaji wa Kata na Vijiji (WEOs & VEOs).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mashirika ya Umma, naunga mkono maoni ya Kamati kuhusu kuingiliwa utendaji wa watendaji na

wanasiasa, hii ikome. Ama watendaji wa mashirika na wao wachungwe kuhusu ubadhirifu kwa mfano; ATC, TANAPA na NCA.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napendekeza uanzishwaji wa *Budget Office* kwa ajili ya kufuatilia Bajeti ya Serikali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuendelea kuchangia kwa maandishi baada ya jana kuchangia kwa kuongea, lakini muda haukutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ukiukaji mkubwa katika uingiaji wa mikataba kwenye mashirika ya umma, na hii imekuwa inaliingiza Taifa kwenye upotevu mkubwa sana wa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana niliongea sana kuhusu ATCL. Katika hili bado napenda kujua ni lini sasa ile ndege itarudi kutoka Ufaransa ili iweze kufanya biashara kama ilivyokusudiwa kwa sababu Serikali kuacha kulipa gharama za matengenezo ambazo ni *USD 3,000,000* na kuacha kuendelea kubaki huko ni kuipatia hasara nchi hii. Nashauri ndege irudi mara moja na kuanza kazi kwani ATCL imeendelea kudaiwa gharama za kukodisha ndege wakati ndege haifanyi kazi. Hii ni fedheha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nasisitiza kuundwa kwa Kamati Teule ili tujue kwa nini ililazimishwa kukodi ndege wakati walishauriwa wasifanye hivyo. Hapa wachunguzwe, *Management*, Waziri wa Fedha na Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uingiaji mikataba, pia napenda kuchangia kuhusu Shirika la Utangazaji la Umma (*TBC*). *TBC* na *Star Media* waliingia ubia na kuunda kampuni tanzu inayoithwa *Star Media* ambayo wote tunaijua. Moja ya makubaliano ni kuwa *TBC* watasimamia miundombinu na kupewa hisa za 35% na *Star Media* watawajibika na teknolojia na kupata hisa 65%.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, baadhi ya ya teknolojia ya *TBC* vimekuwa vinatumika kama vile *satellite link up(495ml)* bila malipo yoyote yale na wala bila kurejea mkataba ili kuweza kuongeza hisa! Maana hii ni *common sense* tu, yaani uelewa wa kawaida tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kusikitisha ni kuona kwamba licha ya *TBC* kuingia ubia lakini hadi leo shirika hili halijui thamani halisi ya uwekezaji kwenye kampuni hii tanzu. Cha kuijuliza hapa ni je, kama hawajui thamani ya uwekezaji, wanawezaje kujua gawio (*dividend*)? Au ndiyo ule msemo wa kuangalia maslahi binafsi,

akishaweka chake mfukoni, basi hajali maslahi ya Taifa. Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo mana nikasema hivi, hawa watendaji wana ukweli wa kutosha au hawana kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu ubadhirifu wa fedha zilizotolewa kama ruzuku kwa wakulima wa pamba baada ya anguko la uchumi duniani ambalo ilisababisha bei za bidhaa nyingi duniani kushuka, ambapo pamba ilishuka toka 460/= hadi 360/= kwa kilo. Zilitolewa shilingi bilioni 18, lakini kati ya hizo shilingi bilioni 2.5 zilitumika na hazina maelezo yoyote wala stakabadhi. Tunaomba hili nalo lichunguzwe ili ijulikane zimekwenda wapi. Kama zilitumika visivyo, wachukuliwe hatua. Naomba kuwasilisha.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono ushauri wa Kamati zote zilizowasilisha taarifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni katika maeneo yafuatayo:- Matumizi ya fedha kwenye Halmashauri za Wilaya:- Usimamizi wa fedha zinazopelekwa Wilayani kwenye Halmashauri hauna budi usimamiwe vizuri na wahusika wachukuliwe hatua kali wizi unapogundulika mara moja. Pia uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmashauri na *RAS* na *DAS* waajiriwe kwa mikataba na waondolewe mara moja wanaposhindwa kutekeleza wajibu wao. Aidha, ukaguzi wa miradi ya Halmashauri ufanyike kabla ya miradi kukabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya fedha za Serikali Kuu. Tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Serikali lichukuliwe kwa kuwajibisha wanaosimamia na kuamua matumizi mabaya, wafikishwe Mahakamani bila kuomba kibali cha mamlaka yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa miundombinu, reli na barabara. Reli ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yoyote ile duniani. Nchi yetu tumezembea katika kutambua hilo na kuliwekea mikakati. Nashauri kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha mfuko wa ujenzi wa reli kama tulivoanzisha *Road Fund*. Pia Serikali itafute fedha hata za mkopo kwa muda mfupi ujao ili kurekebisha reli ya Kati na pia zitafutwe fedha za kujenga *standard gauge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara. Mgao wa fedha za barabara kwenda kwenye Halmashauri uimarishwe kwa kutoa taarifa kwa Wabunge za fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kupeleka madaraka Mikoani (TAMISEMI) ambapo fedha nyngi za umma zinapelekwa kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania, inasikitisha kuona kuwa ni katika Halmashauri karibu zote nchini fedha hizi zinafujwa, haziwafikii wananchi na hali hii inajirudia kila mwaka bila Serikali kuchukua hatua yoyote pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuainisha udhaifu huo katika ripoti zake za kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa Serikali ya enzi hizi za sayansi na teknolojia kuzungumzia suala la mishahara na watumishi hewa. Kutokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2010, katika Serikali za Mitaa kiasi cha shilingi milioni 583.2 zilitumika kuwalipa watumishi hewa. Hivi ni kweli Serikali pamoja na kuwa na kompyuta katika ofisi zake zote za Halmashauri, hawajui idadi ya watumishi wake! Ikiwa ndivyo, fedha hizo zinapolipwa zinapokelewa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la urasimu na utaratibu mbovu wa utendaji katika Halmashauri zetu hususan katika sekta au idara ya ardhi. Inachukua hata mwaka mzima au zaidi kwa mtu kubadilisha umiliki wa kiwanja alichonunua hata kama hakuna mgogoro wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Kinondoni ni moja kati ya Halmashauri ambazo zinashughulikia maombi na matatizo ya ardhi mengi ukilinganisha na Halmashauri zingine. Cha kushangaza ni kwamba, utaratibu uliopo ni kuwa Kamati za Madiwani hukaa mara nne tu kwa mwaka. Utaratibu huu ambao unafanana katika Halmashauri zote bila kujali idadi ya wateja wanaohudumiwa na Halmashauri hizo unasababisha Manispaa kama Kinondoni kushindwa kushughulikia maombi kwa wakati (rejea utaratibu wa maombi ya kubadili matumizi ya kiwanja) na hivyo kuchelewesha shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza zaidi ni kuwa Halmashauri zina utaratibu wa kuwataka wateja wake wanaohitaji kuhudumiwa haraka waghamarie vikao vya dharura vya Madiwani ili maombi yao yajadiliwe. Haingii akilini kumtaka mwananchi kugharamia huduma anayohitaji katika idara ya ardhi ilihali Halmashauri zinaendeshwa kwa kodi za wananchi. Katika hali kama hii mwananchi asiye na kipato atawezaje kupatiwa huduma kwa wakati stahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge ni Madiwani katika Halmashauri zao, cha kushangaza ni kuwa Halmashauri nyingi huendesha vikao vyao hasa vya bajeti wakati ambapo Bunge linaketi na hivyo kuwanyima fursa Wabunge kushiriki vikao muhimu vya Halmashauri. Nashauri utaratibu huo mbovu ubadilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa nafasi hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kuchangia hoja hii kwanza kwa kuipongeza sana Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, yaani CAG kwa kazi nzuri aliyofanya ya Ukaguzi na kutuwezesha kupata taarifa ambayo Kamati yangu ya POAC pamoja na Kamati zingine za Fedha tumeweza kuzifanya kazi. Ni dhahiri kwamba kama Mashirika ya Umma yangeliwa yanafanya kazi kwa umahiri mkubwa, mfano wa CAG, nchi yetu ingepiga hatua kubwa sana ya Watanzania kupatiwa huduma bora na za uhakika na huduma zilizo nzuri ikiwemo huduma ya usafiri wa anga kwa ndege zetu wenyewe, huduma za hifadhi za jamii, kilimo cha kisasa. Lakini pia tatizo kubwa la ajira lingeweza kupungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya POAC alipotoa taarifa ya Kamati alitoa rai kwamba Mifuko ya hifadhi ya jamii itashindwa kulipa mafao yake kutokana na Serikali kuchelewa kulipa madeni ambayo imekopa, hususan deni la Ujenzi wa Chuo Kikuu cha UDOM iliyofadhiliwa kwa kiwango kikubwa na Mifuko ya PSPF, NSSF na LAPF.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kulipa mafao ya aina mbalimbali kwa wanachama wake. Sifa kubwa ya wanachama kulipwa mafao hayo ni kuchangia asilimia tano hadi kumi ya mishahara ya wanachama. Hivyo ni dhahiri kabisa kwamba fedha zinazokopwa na Serikali ni mali ya wanachama, ni mali ya Watanzania. Lakini vile vile uimara wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unatokana na rasimali fedha, kama hakuna fedha basi Watanzania hawatopata stahiki zao na hivyo tatizo la kupunguza umasikini na uboreshaji wa maisha ya Mtanzania litazorota.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kwamba kuna kasumba iliojengeka na Wizara husika ya kuamini kwamba Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zinatoa fursa ya kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali yaani *Consolidated Fund* na hivyo Mifuko hii haiwezi kufa. Kwa hili nasema ni muda muafaka sasa fedha hizo za *Consolidated Fund* zilipe

madeni ambayo mifuko hii inadai Serikali ili kuinusuru katika kulipa mafao ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitishwa sana na mwenendo mzima wa uendeshaji wa Mashirika ya Umma. Mengi yao yamekuwa na Kaimu Wakurugenzi. Huu nasema umekuwa ugonjwa unaoitwa "Kaimu"! Kaimu Mkurugenzi Mkuu! Kaimu Mkurugenzi wa Fedha na Utawala! Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ndani!.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni nafasi nyeti za kiutawala siyo busara sana zikiwa na Makaimu na tena kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kukaimu kunaathiri utendaji kazi hasa katika upande wa maamuzi, lakini pia kukaimu kunaathiri "*professionalism*". Pia kukaimu kunaathri hata *management* ya matumizi ya fedha. Naiomba Serikali yangu ya CCM ichukue hatua madhubuti ili kuondokana na nafasi nyeti ambazo zinakaimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa na ufanisi wa kazi ni lazima tuwe na utamaduni wa kuheshimu rasilimali watu kama *Professional* muhimu sana inayozingatia *skills* za watendaji. Lakini pia tujenge utamaduni wa kuwa na *skills* endelevu kwa njia ya *succession planning*. Ninalitaja wazi Shirika la TPDC kwani imenishangaza kuona kwamba Shirika hili lina wazee wengi waliopo kwenye *Managerial positions* ambao sina shaka watastaifu ndani ya miaka isiyozidi mitano. Naisihi Serikali izingatie sana taaluma ya rasilimali watu hasa ukizingatia ukweli kwamba vijana wengi sana hawana ajira kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kusema, ili Mashirika ya Umma yaweze kujimudu ni lazima yawe na rasilimali fedha za kutosha, yawe na watu wenyewe taaluma na uwezo mzuri wa kazi. Hivyo Serikali ilipe madeni yake ili Mashirika haya hasa niliyoyaeleza yawe imara.

**NAIBU SPIKA:** Sasa tuwape nafasi Wenyeviti wetu na naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kama majina ambayo nitayasoma pia yatahesabiwa katika dakika 15.

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo ni dakika 15 kila kitu.

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Pamoja na kusoma majina?

**NAIBU SPIKA:** Unaweza ukayaingiza kwenye *Hansard* moja kwa moja lakini jaribu kuzitumia dakika 15 kwa kadri utakavyoweza.

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Itabidi niachane na majina, nitayapeleka *Hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, waliochangia kwa kuzungumza ni 38 na waliochangia kwa maandishi ni 21. Jumla Waheshimiwa karibu 60 wamechangia kwa kuzungumza na maandishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuzungumza Bungeni ni Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Esther Bulaya, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Ali Keissy Mohamed, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Stephen Julius Maselle.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mheshimiwa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa George Mkuchika, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa William Lukuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuandika ni Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Daktari Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Maria Hewa,

Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Modestus Kilufi na Mheshimiwa Moza Abedi Saidy.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nimekuwa katika Bunge hili na Mwenyekiti wa PAC, sijaona hatu siku moja watu wengi kiasi hicho wamechangamkia taarifa zetu kwa kiasi cha juu kama ambavyo imebainika katika Bunge hili. Kwa hiyo, nataka kuwashukuru sana Wabunge kwa sababu wengi wetu tulikuwa tunajuliza, kwa nini tunatumia muda na fedha kama Bunge halichangamkii taarifa hizi? Leo mmenitoa hiyo hofu na kweli naamini fedha ya Serikali haina Chama. Waliokuwa wakali zaidi mmeona ni kambi ambayo ndiyo inatawala katika Taifa hili na sisi Kambi ya Upinzani tumeongeza chumvi kwenye kidonda ambacho kilikuwa kinawaka. Kwa hiyo, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuendelee na mtindo huo, fedha ya Serikali haina chama, ni yetu wote na ni lazima tuchangamkie matatizo ambayo yanaletwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia mambo mengi, lakini labda tu niende kwenye mambo ya jumla. Jambo la kwanza ambalo limesemwa na watu wengi ni kuhusu muda kwamba ni mdogo sana na leo kwa taarifa hizi tumejitahidi. Tunapozungumzia bajeti ya Serikali tunachukua karibu miezi miwili na ushehe na Serikali yetu iko hapa lakini tunapozungumzia kuwajibika kwa fedha tullyotoa, Mawaziri tu ndiyo wako hapa, wale wanaosaini zile *cheques* siyo Mawaziri. Wanaosaini zile *cheques* ni Maafisa Wahasibu, wako wapi? Siku ya leo Maafisa Wahasibu wangkuwa wamejaa hapa wakiwasikiliza hawa Waheshimiwa Wabunge jinsi wanavyofanya madudu mbalimbali katika votes zao ambazo sisi tunaidhinisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, la kwanza ni hilo. Tunaomba tutakapowasilisha taarifa zetu mwaka unaokuja wawepo hapa ili watoe majibu yaliyo sahihi. Wanapozungumza na wale Wahisani kwenye PEFA ripoti, Wizara zote zinakusanyika pale kwenye Hoteli ile ya Manzese na wote wanazungumza kizungu. Siyo hivyo tu, wakimaliza wanapewa masharti haya; mtafanya hiki, mtafanya hiki na Bunge hili halijui. Ndiyo nikasema karatasi hii ije hapa ili na sisi tujue hao Maafisa Wahasibu wanakubaliana vitu gani kule na hawa Wazungu, ambavyo vingine vinalazimisha Bunge hili kutunga sheria ili fedha ije kutoka kwa wahisani? *This is not correct!* Watawala wa nchi hii ni Bunge hili, ni wananchi wa Tanzania wanaowakilishwa na Bunge hili. Kama wana mambo mazuri watuletee sisi katika Kamati mbalimbali na sisi kama Katiba inavyosema

tuikamate Serikali yetu kama tulivyofanya kwa siku mbili, kwa sababu ndiyo kazi yetu ya Kikatiba na yenyewe iwe hapa. Nimeona niseme hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, mawasiliano ya kibajeti. Inaonekana tukimaliza bajeti, tunaikabidhi Serikali, tunaiingoja tena hiyo bajeti ije karibu miezi 12 baadaye. Serikali inafanya mambo yake inavyotaka na ndiyo hayo mengine ambayo mmeyaona, maonesho shilingi bilioni moja kwa Wizara moja, *is too much money. Whether* watu walikuwa wanachomwa sindano au wanafanya nini, shilingi bilioni moja kwa maonesho ni *too much money*, Serikali haina fedha hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *I think* ni vizuri Serikali ikatengeneza utaratibu wa kufanya *budget review* na kuleta habari hizo kwenye Bunge hili. Kama mpaka Februari tumetoa shilingi bilioni 384 kwa Ujenzi na tulisema tutatoa shilingi trilioni moja na ushehe, kwa nini Waziri wa Fedha asije kwenye Bunge hili akalieleza kwamba mwenendo wa bajeti mpaka hivi sasa utakuwa A,B,C,D, tumekosa hapa, tutapata hivi, tutafanya hivi, Bunge hili lijue? Ndiyo maana nakubaliana na wote waliosema labda Bunge lako litengeneze sasa *Budget Committee* ambayo itafuatilia bajeti yetu mwezi hadi mwezi ili kuona yale ambayo tulikubaliana kweli yanatekelezwa kama vile Bunge liliwyofanya? La sivyo Bunge hili litakuwa ni *rubber stamp*, tunapiga stempu watu wanaenda kufanya madudu yao, baada ya miezi 12 CAG anakagua anatuletea madudu yale yale. Kwa hiyo, tufanye *budget review*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mawasiliano pia, mimi naishangaa Serikali, kila mahali duniani kote kuna *supplementary budget*. Mkishindwa mahali mnarudi kwenye Bunge. Hata mkipata fedha zaidi mnakuja kwenye Bunge. Sasa tumeputa fedha ya chenchi ya rada, Serikali haijaja kwenye Bunge hili na kutueleza shilingi bilioni 79 zitatumika namna gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakianza kuzitumia tutafanyaje? *Where is the appropriation* ambayo imepitishwa na Bunge hili? Kwa hiyo, mawasiliano haya ndiyo Wabunge wanasema mbona Serikali haiji kwenye Bunge lao na kulieleza? *What's happening?* Mimi natumaini karibuni, sijui ni lini, lakini leteni *supplementary budget* kwa ajili ya hii fedha ya chenchi na Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi tumeihangaikia sana hiyo fedha, tunataka kuona imefanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ni kuwajibika, *political responsibility*. Watu wakifanya madudu kwenye Wizara yako wewe kama

Waziri lazima uchukue *political responsibility*. Ndiyo! Duniani kote ndivyo wanavyofanya, wala siyo hapa tu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa rafiki yangu wa *TBS*, ndugu yangu kila ukimuuliza anasema sina taarifa. Tumeanza kulizungumza jambo hili tangu mwaka 2009. Wewe ulikuwa unaangalia wapi? Anasema sina taarifa, sina taarifa, kila wakati huna taarifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu tunamwambia *listen*, twambie ukaguzi haupo lakini umetengeneza utaratibu wa *ku-externalize finance* yetu ya *foreign exchange* shilingi billioni 30 kwa ukaguzi usiokuwepo. Tumekaa vikao na vikao, kikao cha Kamati tatu, Naibu Waziri alikuwa pale tukasema ili uchunguzi ufanyike kamwondoe huyu bwana akae pembeni. Leo tunaambiwa sina taarifa, sina habari, mtamuondoaje mtu? Hii ni kulinda watu, kulinda ubovu na nchi tukiendelea hivyo mnajua matatizo yatakayotupata kisiasa na wote hapa ni wanasiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Pamba. Mheshimiwa Waziri tumemwambia mambo mengi mwaka huu *including* yule Meneja anatuchafulia msimu na sisi tunahitaji msimu ili tujikwamue kutoka kwenye njaa. Waziri anatueleza hiki, hatamki, tumemwambia muondoe huyo. Aah, mpaka leo! Huyu anaambiwa kwamba kuna fedha imepotea shilingi billioni mbili. Aah, namwondoa yule Mwenyekiti. Mwenyekiti hasaini *cheque*, anayesaini *cheque* ni yule Mtendaji. Yule ndiye unamweka pembeni kwanza, halafu uchunguzi ufanyike. Hii ndiyo kawaida. Tunakwambia usimfukuze akae pembeni umchunguze kuna kosa gani? Kulinda watu huku ndiyo kutatufikisha pabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara tumeweka hapa mapendekezo yetu, lakini ukweli ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tukizungumza hapa na tukiazimia kitu hilo limekuwa Azimio la Bunge. Wewe ukitaka kuligeuza njoo Bungeni utupe taarifa A,B,C,D, naomba tuendelee nalo. Kama inakubalika, tunakubariki, lakini sheria yenyewe kwanza imeletwa mwaka 2009 haikuwemo. Wamefanya madudu yao tangu 2002 mpaka 2009, walipoona mambo yako hovyo hovyo ndiyo wanatuletea sheria *amendment* ndogo. Naomba jamani tulinusuru Taifa hili. Hakuna ulazima hata kidogo wa kukagua haya magari nje na hakuna ulazima wa kupeleka fedha shilingi billioni 30 nje wakati hapa tuna gereji lukuki ambazo zinaweza kufanya kazi hiyo. Watu wasitwambie kwamba utachelewesha au nini, toa gari. Unapotaka kusajili gari lako nioneshe *certificate* ya *worthiness*. *It is normal all over the World.* Uingereza you get MOT kabla hujaendelea na insurance.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya mambo Waheshimiwa Wabunge mimi nashukuru kwamba mljadili vizuri. Area ya matumizi sitaki kuirudia imejonesha wazi. Tunataka bajeti tukisema matumizi ni haya basi tuone matumizi hayo yanaenda sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba CAG office muiangalie. Tumepata sifa sasa CAG wetu anaweza kwenda UN lakini bado ana kipengele hiki. Kwenye *grading* ya INTOSAI anakuwa undergraded kwa sababu hana uhuru wa kuajiri. Unashikilia ya nini hiyo Mheshimiwa wa Ajira? Muachie! Yeye ndiye anahitaji kuwa na watu madhubuti. Sisi tuna bajeti ya shilingi trillioni 13, kwa nini asiwe na nguvu hata ya kuajiri watu na kuwapangia mishahara yao ili afanye kazi vizuri? Umeshikilia, leo 100, leo 50 kesho 25, why? Tumeamua kumpa uhuru, tumpe uhuru ndivyo dunia nzima inavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa sababu dakika hazitoshi, Waheshimiwa Wabunge sisi tutayapeleka haya yote ambayo mmetuandikia Serikalini, *Hansard* ipo, naiomba Serikali isome hiyo *Hansard* na itumie Ibara ya 40 ya Sheria ya Ukaguzi ambapo kisheria *PayMasterGeneral* lazima ajibu na alete majibu hayo hapa Bungeni. Sheria tumetunga sisi wenyewe, kwa miaka miwili hatujaiona taarifa hiyo hapa. Mkifanya hivyo, tutaendesha utaratibu wa kuangalia fedha ya Serikali katika misingi na sheria ambazo tumetunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya ku-*windup* hoja hii. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

Waheshimiwa Wabunge mkiangalia muda wetu umekwisha kabisa, naomba kutumia Kanuni ya 28(5) inayonipa mamlaka inapokuwa bado dakika chache kama hizi niongeze muda wa majadiliano yetu kwa muda usiozidi nusu saa ili tuweze kukamilisha kazi za Wenyeviti wetu.

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyininge nakushukuru sana kwa kunipa heshima hii ya kuzungumza mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza watu waliochangia kwenye hoja yangu kwa maandishi wako 26 na mmoja amenipa sasa hivi nadhani wako 27. Waliochangia hoja yangu kwa kuzungumza hapa Bungeni ni 14, jumla ni watu 41. Hapa ilipaswa niwataje kwa majina yao waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na waliochangia kwa maandishi, lakini kama alivyofanya Mheshimiwa John Cheyo, muda niliopewa ni mdogo, hautatosheleza kuwataja wote kwa majina yao. Nitaomba majina haya niyaandike na niyapeleke kwenye *Hansard*, kama kumbukumbu rasmi ya watu waliochangia Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kusoma michango ya waliochangia kwa maaandishi na pia nimejaribu kuwasikiliza kwa makini Wabunge wote waliozungumzia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Naomba Serikali mtuelewe kilio chetu sisi Wabunge. Kilio chetu sisi tuliosema hapa ndani, tumesema kwa uchungu mkubwa sana. Kama mnavyofahamu asilimia karibu 70 ya fedha za Serikali zinapelekwa kwenye Serikali za Mitaa ili kuleta maendeleo Vijijini, kutengeneza barabara, kuimarisha kilimo, maji, shule za msingi na sekondari na kadhalika. Fedha zinapelekwa kuondoa ufukara na umaskini uliokithiri huko vijijini. Kama eneo hili halitadhibitiwa, halitasimamiwa, tusahau kuondoa ufukara na umaskini katika vijiji vyetu. Kama fedha hizi tutakuwa tunazidhinisha ziangukie kwenye mikono ya watu wachache wajanja, kweli nchi hii hatutafika mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuona Waheshimiwa Wabunge hawa kilio chao ni kuhusu wizi mkubwa unaofanyika kwenye ngazi ya Serikali za Mitaa, Majiji na Manispaa. Wizi wa kutisha na hilo Serikali naomba mlione, ndiyo kilio cha Wabunge hapa. Tumefanya Ukaguzi Maalum uliofanywa na CAG kwenye Halmashauri ya Kishapu na Manispaa nyininge tano ili muweze kupata picha ya hasira na kilio chetu, kitu ambacho hatuwezi kukifumbia macho. Pale kwenye Halmashauri ya Kishapu, karibu shilingi bilioni 6.2 ni matumizi mabaya ya fedha za wananchi, ni wizi mtupu, ni ubadhirifu mtupu na hujuma. Hatuwezi kunyaamaza na kama Mawaziri mlivyo sema hapa kama mngekuwa na ushirikiano na sisi tukajua mnachokifanya pengine mambo mengi yasingekuja hapa na wala tusingeyaleta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka CAG alikuja kwenye Kamati yangu wiki moja kabla sijaja hapa. Aliita Halmashauri ya Kishapu tukakutana Dar es Salaam na Mawaziri wote wawili wa TAMISEMI. Nimesema vizuri sana, mna ripoti, mna makaratasi yenu mmeshikilia upande, hatujui mlichoandika, ndio sababu hata hapa wakasema someni. Hatuamini kama majibu ya matatizo tunayoyaona kwenye Serikali za Mitaa, mnayo hapa, tungejua wala tusingelalamika sisi sio

wendawazimu. Sisi wachokozi, sisi hatuko hapa dhidi ya Serikali. Serikali hii tumeichagua wenyewe, tumewaweka madaraka wenyewe hatuwezi kuipiga ngwala kwa ujanjaujanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokutana pale Dar es Salaam na watu wa TAMISEMI, ninao watu waliokuwa wanahudhuria vikao vya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kutoka TAMISEMI, mbona hayo majibu ndiyo unatembea nayo kama mchawi, mbona hukutuletea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, CAG alikuwa pale kutusomesha ile taarifa yake, Halmashauri ya Kishapu ilikuwa pale na nikuambie haya mnayosema sio ambayo yaliyojiri pale kwenye kile kikao. Wajumbe wote wanalia wanasema Mrema tusaidie nchi inafilisika, nchi inakufa, nchi inasambaratika ndicho walichosema pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ninaloliona, huu wizi sijui Waziri utafanyaje, kwa sababu tunachokiona hapa kama ni mtandao wa wizi nchi nzima. Ni tatizo kubwa kuliko tunavyofikiri. Mnaweza mkatunyooshea kidole kwamba tunataka *publicity*, tunataka ujiko, tunataka kujijenga, hakuna mtu anayeweza kujijenga kutokana na matatizo ya wananchi. Kama ni umaarufu nimeshakuwa Naibu Waziri Mkuu katika nchi hii, mtu wa tatu kwa madaraka kutoka Rais, Mungu anipe nini? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchungu ni kwamba mtafanyaje? Twende Kishapu tu, nataka Waziri Mkuchika na mwenzako Mwanri na wengine, wale watumishi walioshiriki katika ubadhirifu huo wa shilingi bilioni sita (6), walituambia bado wako pale wanatembeatembea, tungeambiwa wameshachukuliwa hatua wala tusingekuja kulisema hapa. Halafu ujue huu mtandao ni mkubwa, wanashirikiana na Maafisa wa Benki ya NMB-Manonga pale Kishapu, mtafanyaje? Pia wanashirikiana na wafanyabiashara mashuhuri! Kwa hiyo, ndio nasema hii nchi inaliwa kushoto, kulia, centre yaani sijui! Bila kufanya operesheni maalum ya kupambana na hawa majambazi, nchi hii watatufikisha pabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo la kwanza ambalo tumeliona. Ni mtandao wa watumishi wa Halmashauri, wafanyabiashara mashuhuri na mabenki. Sasa Mheshimiwa Mkuchika utafanyaje ndugu yangu katika muda huu uliotuambia? Ungetusomea hizo taarifa ungekuja kutuambia wamekula, kwa hiyo? Wameiba, kwa hiyo? Hicho ndio kitu unachotakiwa kufanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo tumeliona ni kuchukua hatua. Juzi nimesema kuhusu DCI. Polisi hawakagui, nenda pale kwenye Halmashauri hiyo ya Kishapu, hakuna upelelezi ambao uko pale. Polisi wapo, DCI anajua lakini hakuna uchunguzi uliokamilika. Miaka mitatu mnachunguza nini? DPP akipelekewa mafaili harudishi mrejesho, ni vizuri akatuambia washtakiwe au hawashtakiwe ili kijulikane kimoja, lakini huwezi kukaa na faili miaka mitano jamani nchi hii tunaipeleka wapi? TAKUKURU na wenyewe ndio mgogoro mkubwa pale Kishapu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu na hayo matatizo unayoyaona, mimi nashangaa nchi hii inakoelekea. Nataka nitoe mfano tu Waheshimiwa Mawaziri mlioko kwenye Serikali hii muweze kuilinda Serikali hii, muweze kuisaidia Serikali hii. Kuna shilingi milioni 551 kwenye ile ripoti ya CAG. Vile vishina vya hundi viro, hundi zilizoandikwa kwenda benki zipo, walioandikiwa hundi hizo wapo, walioenda kuzichukua fedha hizo wapo, unahitaji upelelezi gani, si mnitume hata mimi Mrema kwani mimi nashindwa kuwakamata wale? Ni kazi ya wiki moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawashangaa yaani badala ya mtu kula hivi (akionyesha kupitia mdomoni), unakula kupitia huku (akionyesha kupitia nyuma). Hii nchi inatushinda kwa sababu sijui ya umakini wetu wa kutenda kazi hizi, kazi nyingine ni ndogo sana. Mkiwa *efficient*, mkiwa makini ku-react kwenye matatizo ya wananchi, wala hatutagombana hapa Bungeni. Tunagombana nini, ni kwa sababu gani? Mnasema Serikali sikuvi lakini mimi nimekaa na Waziri Mkuchika. Waziri Mkuchika haya mambo ungekuwa unanifundisha, unanionyesha na mimi ni mwenzako, mimi nina uzoefu, nina ujuzi mkubwa, nitumie sasa tusaidiane, sasa kama hufanyi nikija kuyasema hapa itaonekana kama nakuvizia, mimi sikuvizii. Itaonekana nakupiga ngwala, mimi sina sababu ya kukupiga ngwala. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema, mfano hizo hundi na matatizo mengi katika Halmashauri zetu, mengi ni mambo madogo ambayo upelelezi wake uko wazi lakini upelelezi haufanyiki, hauishi, haukamiliki, wezi wako pale hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme mfano mmoja mdogo. Ripoti ya CAG inasema ile Ofisi ya Kilindi, yale mabati yaliyoko pale juu, CAG anafanya kazi ngumu sana na nakwambia kama hamatumia ripoti zao kufanya kazi aliyogundua mtawa-*discourage* hawa vijana. CAG anafanya kazi katika mazingira magumu, anakuletea ripoti, ameandika kwenye taarifa yake yale mabati yaliyowekwa pale, yule mkandarasi yale mabati aliyoyasema kwenye mkataba sio hayo yaliyowekwa pale juu. Ameenda kununua mabati sijui *gauge* namba ngapi kwa sababu CAG

alikwenda mpaka *TBS* kwenda kutathmini hayo mabati ni ya aina gani, akagundua sio yale lakini mabati yamekwenda ya shilingi milioni 44. Shilingi milioni 44 halafu unasema upelelezi? Kama ningekuwa mimi Mrema si napanda pale juu naenda kuyaangalia au kuyakagua? Ni kazi ya dakika tano (5) tu. Yule mkandarasi angekwishakamatwa na kushtakiwa, angeshafungwa, ushahidi ni yale mabati na ripoti ya CAG lakini *we are not doing that*, hatufai! Kwa hiyo, tutagombana na wananchi bure, tutagombana na Wabunge bure, mtatuona wabaya lakini hatuna sababu ya kugombana na ninyi kama mtafanya kazi yenu kisawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni mfano wa Kishapu lakini tumekwenda Rombo ufisadi uko palepale hakuna kilichotokea. Kilindi ndio tuiseme, Misungwi, Kilosa Bagamoyo lakini tungekuta hatua zinachukuliwa na hatua hizo zitangazwe, zifulikane, washikadau wenu wajue hatua hizo, hakuna mtu angekuwa na ugomvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni la kwanza ambalo nimeona Wabunge wengi wamelipigia kelele juu ya wizi, wahusika hawakamatwi, kama Waziri anaweza katuonyesha hilo faili kwamba kweli wanakamatwa, wahusika hawachukuliwi hatua za kisheria na nikwambie *seriousness* ya jambo hili, mimi nimeona pendekezo hapa watu wamefikia hatua wanasema wewe Waziri unayehusika na TAMISEMI ushtakiwe, ufunguliwe mashtaka, uunganishwe na hawa watuhumiwa, sio jambo jema! *It is not healthy*, lakini tumewafikisha Wabunge kufikia hatua hiyo. Sio vizuri! Wahusika wote kwenye Halmashauri zote 134 wasakwe, fanyeni operesheni na hiyo operesheni ijulikane. Mkifanya kazi hiyo, Watanzania wote na wananchi wote, ndio mimi nakwambia tangu jana watu wanashangilia Bunge hili, wanafikiri labda leo tutatoka na dawa ya kusaidia kupambana na wizi uliokithiri katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zilizopo, kanuni zilizopo Wabunge wanasema zitumike. Walikuwa wanasema Serikali ipewe muda maalum wa kutekeleza haya waliyosema. Wapewe muda na pengine hili lisituondoe kwenye yale maazimio yetu. Tuliandika maazimio jana, tukayapitisha na leo nitaendelea kuomba Serikali, kuomba Bunge hili yale maazimio yabaki palepale yasiondolew kwa maneno tu hapa.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana ni kengele ya pili.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Ya pili? Bado!

**NAIBU SPIKA:** Ya pili Mheshimiwa Mwenyekiti.

(*Hapa Mhe. Dkt. Augustine L. Mrema alirudi kwenye kitichake*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema. Tunatambua kwamba yeye ana-cover eneo kubwa sana na kwa kweli alikuwa anahitaji muda mwingi zaidi, lakini muda wetu ni mdogo kama ambavyo Waheshimiwa mlivyokuwa mkisema kila wakati.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika hoja hii na kutohakana na muda, sitoweza kuwataja majina wote kwa sababu inahitaji tupate muda wa kutosha kuweza kuzijibu hoja zote pamoja na majibu ambayo baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri wameyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza tuboreshe mapendekezo ya Kamati, pendelezo namba 7.2.7 kuhusiana na ukodishaji wa ndege wa *Air Bus* ambao ulifanywa na ATCL tarehe 27 Oktoba, 2007 na baadaye Serikali ikatoa guarantee kinyume na Sheria ya Mikopo. Mwezi Aprili 2008 walitoa guarantee baada ya kuwa mkataba umeshaingiwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge watatu waliochangia kwa maneno na wanne waliochangia kwa maandishi wamependekeza kwamba Bunge liunde Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza mazingira ya kuingia mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaendelea na michango, nimepata taarifa, tulitoa taarifa kwanza Serikali haijaanza kulipa fedha zile kwenye Kampuni ya *Wales Trading* ya Lebanon lakini nimepata nyaraka ambazo zinaonyesha kwamba Serikali imeanza kulipa. Mpaka sasa tumeshawalipa shilingi bilioni 2.5, tumewatengenezea *schedule* ya malipo mpaka watakapokuwa wamekamilisha kuyalipa na ninayo hapa nitampatia Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini linalonisikitisha ni kwamba tarehe 27 Machi, 2012, Maafisa wa Wizara ya Fedha walikutana na wawakilishi au wamiliki wa Kampuni hii ya *Wales Trading* ambayo walitukodishia ndege ambayo haikuruka na ambayo imetuingizia madeni makubwa sana na

Waheshimiwa Wabunge na hasa Wabunge wa Mikoa ya Kusini, naomba wanisikilize kwa makini, watu hawa sasa katika nia ya kulipa deni hili wanapewa bandari ya Mtwara. Nina nyaraka hizi, nitaziweka Mezani na kuweza kumpatia Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na mambo haya, nakubaliana na mapendekezo ambayo Waheshimiwa Wabunge ambayo wameyatao kwamba tuboreshe pendekezo namba 7.2.7 kwamba Bunge liunde Kamati Teule ili kuchunguza mazingira ya mkataba huu na mazongezonge mengine yote. Niwaambie tu kwamba Waziri wa Miundombinu aliishauri Wizara ya Fedha kwamba Wales wasilipwe, lakini Wizara ya Fedha imewalipa Wales, hii inaonyesha mkanganyiko ambao uko Serikalini mionganoni mwa Wizara. Kwa hiyo, pendekezo hilo naomba lirekebishwe na litakuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kuhusiana na suala la *Special Audit* ya *Consolidated Holdings*. *Special Audit* ya *Consolidated Holdings Corporation* iko ndani ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwanza, nimeshauriana na Wajumbe wenzangu wa Kamati tumekubaliana kwamba taarifa nzima ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ule Ukaguzi Maalum ufanyiwe kazi na Kamati na kwa ruhusa ya Wajumbe wa Kamati nimeunda timu ya Wajumbe watatu ambao watashughulikia suala hili ambaye ni Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Murtaza Mangungu na timu hii itaongozwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu na nitataka wamalize kazi hii ndani ya muda mfupi iwezekanavyo kwa ajili ya kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, ushauri wangu ni kwamba kwa Mawaziri wote namna ya kuendesha Mashirika ya Umma, naomba tufanye *eyes on hands off* kwa sababu ya kuweza kuepuka kuingilia Mashirika haya. Mheshimiwa Nundu amesema kwamba yeye ataingilia tu hata chooni, sisi tutamwambia hapana, kwa sababu ya kutaka kuhakikisha kwamba Mashirika yetu yanaendeshwa kwa misingi inayotakiwa lakini lazima iwe *eyes on hands off* pasipokuwa na *eyes on madudu* ya Mashirika yatakuwa makubwa sana. Kwa hiyo, lazima ku-*balance eyes on hands off*, msifanye *micro-managing*, kwa sababu *micro-managing* ndiyo ambayo inatuletea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Waziri wa Fedha ambaye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imemuonyesha dhahiri kwamba aliingilia na kufanya maamuzi kuhusiana na Shirika la CHC, ajipime, ajione kama bado anastahili kuendelea kushikilia fedha za nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Bodi ya Pamba na maelezo, Waziri wa Kilimo ameyazungumza na napenda nitofautiane naye Mheshimiwa Maghembe kwa sababu tarehe 17 Novemba, 2011 nilisema mmiliki mwenye Mashirika kwa niaba yetu Msajili wa Hazina aliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya kuivunja Bodi ya Pamba ambayo ilikula fedha za wananchi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameshaonyesha kwamba fedha za wananchi zimeliwa. Waziri anasema kwamba anaomba mamlaka ya uteuzi iteue Mwenyekiti mwiningine na hili ni kwa Mawaziri wote, tabia ya kumsingizia Mheshimiwa Rais kila jambo ambalo wanapaswa kulifanya, ikome. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Rais hayuko humu ndani ni rahisi sana kusema kwamba Rais hajafanya, Rais hajateua, suala la kuvunja Bodi ni mamlaka ya Waziri, uteuzi ni mamlaka ya Rais, Waziri anayo mamlaka ya kuweza kuvunja Bodi na kumtaarifu Mheshimiwa Rais ateuue Mwenyekiti mwiningine na ateuue Wajumbe wengine na hatua zingine ziweze kuchukuliwa. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe aliyoyazungumza ni maelezo ambayo si sahihi. Mimi kama Mwenyekiti wa Kamati sijayakubali na Bunge lichukulie tu kwamba yalikuwa yanapita tu kwa sababu ilikuwa ni lazima Wizara ichukue hatua, fedha za wakulima zimeliwa na tusifanye mchezo kabisa na hawa wananchi wa kawaida, wa chini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *TBS* limezungumzwa kwa kina sana lakini majibu hayajatosheleza. Hayajatosheleza kwa sababu kuna hatua ambazo ni lazima zichukuliwe. Sisi tulitoa taarifa, tukampelekea Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika akatoa taarifa akampelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa sisi hatufahamu kama Ofisi ya Waziri Mkuu, haikupeleka taarifa ile kwa Waziri wa Viwanda na Biashara maana Waziri wa Viwanda na Biashara anasema kwamba hakuwa na taarifa. Kwa hiyo, anachokisema ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, haikumpelekea taarifa na nyaraka zote ziko hapa kwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa yetu tulishauri kwenye uchunguzi, Mkurugenzi Mkuu wa *TBS* asimamishwe kazi, apishe uchunguzi. Mbona ilikuwa ni rahisi sana kwa Mkurugenzi Mkuu wa *CHC* kusimamishwa tena bila kufuata taratibu lakini inakuwa ni vigumu sana kwa Mkurugenzi Mkuu wa *TBS* anayewafanya wakulima wetu watumie mbolea ambayo haina ubora, anayewalisha watoto wetu *Blue Band fake*, anayeingiza matairi nchini ambayo yanasaababisha ajali, inakuwa ngumu sana, lakini inakuwa rahisi kwa watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichokuwa nakiomba ni kwamba, maelekezo ya Mheshimiwa Spika, kwa Waziri Mkuu kuhusiana na *TBS* yatekelezwe na yatolewe taarifa Bungeni kwa sababu maelezo haya Mheshimiwa Spika ameshayatoa muda mrefu sana na ni zaidi ya miezi miwili sasa imepita toka Mheshimiwa Spika, ayatoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho. Tatizo kubwa la Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokutekelezwa ni ukosefu wa uwajibikaji na kama nchi hii tunataka tuendele, kama tunataka tupigane kwa dhati kabisa dhidi ya ubadhirifu, dhidi ya udokozi, dhidi ya uzembe, dhidi ya uvivu, ni kuhakikisha tuna misingi sahihi ya uwajibikaji (*accountability*). Niliwahi kuwaambia vijana fulani kwamba kama kutakuwa kuna neno moja linalotakiwa liandikwe kwenye Katiba mpya, neno moja; ni ‘*accountability*,’ uwajibikaji, ndicho kinachokosekana. Taarifa hizi zinatolewa kila mwaka, nashukuru sana safari hii Wabunge mmekuwa wakali sana lakini bila kuhakikisha *Executive* inawajibika katika haya mwaka kesho tatarudia hayahaya na tutakuwa wakali hivihivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba; mimi na Bunge hili halina mamlaka ya Mkurugenzi wa Shirika, Katibu Mkuu wa Wizara au Mkurugenzi wa Halmashauri. Mawaziri ambao wametajwa kwa njia moja au nyagine kutokuwajibika ipasavyo na kuliingizia hasara Taifa wamekuwa wagumu sana kuwajibika, wanampa kazi Rais ya kuwafukuza lakini sisi hatuwezi kuwaazimia hapa ila sisi tuna mamlaka na mtu mmoja tu humu ndani ya Bunge na naomba mnisikilize kwa makini sana. Tuna mamlaka na mtu mmoja tu, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kumwajibisha Waziri Mkuu, hawa Mawaziri waliotajwa hawatatoka na wasipotoka madudu haya yatarudia. Kwa hiyo, Mbunge yeyote mwenye uchungu na ubadhirifu, Mbunge yeyote ambaye anakereka na watoto kwenye Jimbo lake kukaa chini, Mbunge yeyote anayekereka na dawa kuharibiwa na *MSD* na *MSD* kushindwa kupeleka dawa kwenye vijiji vyetu, nampa taarifa kwamba kuanzia kesho tunakusanya saini za Wabunge 70, ili siku ya Jumatatu tutoe hoja hapa Bungeni ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu na kipindi hiki tunakitoa Mawaziri wote ambao wapo *implicated* kwenye taarifa hizi waweze kuona ama wao au wamtoe rehani Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge wote wenye uchungu, kuanzia kesho tutakuwa pale mlangoni, saini zinazohitajika ni 70 tu, kwa ajili ya kuleta hapa Bungeni na Wabunge wanahitajika kupitisha hilo Azimio ni nusu tu ya Wabunge, *50 plus one*. Tukifanya hivyo tutakuwa

tumewapa heshima wananchi wetu, wataona kweli tumewatendea haki badala ya kupiga kelele bila ya kuchukua *action*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wenyeverti wenzangu wote, Mheshimiwa Cheyo na Mheshimiwa Dkt. Mrema, nitoe hoja sasa kwamba Bunge lako lipokee taarifa za Kamati zote hizi tatu na mapendelekezo yake na kuweza kuyapitisha. Naomba kutoa Hoja. (*Makofii*)

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Wenyeverti wote watatu ambao wanasi mamia Kamati za Mahesabu ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika yetu ya Umma kwa niaba ya Kamati zenu kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya.

Nitoe ufanuzi kabla ya kuwahoji kuhusiana na ninawahoji jambo gani. Mimi nitakachowahoji ni yale ambayo yaliwekwa Mezani hapa Bungeni na ambayo yameandikwa katika vitabu hivi kama ndiyo ripoti za Kamati tangu mwanzoni. Ndiyo ambayo nitayahoji kama mnayaafiki kwamba sasa tuyapeleke Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wake wote. Yale ya kuhusu Bunge kuunda Kamati Teule yanabidi yafuate utaratibu wa kawaida wa maandishi kumfikia Katibu katika muda mwafaka kabla ya hoja kama hizo hazijaingia yaani ifuatwe ile Kanuni ya 117 ipasavyo. Yale mengine ya Waziri Mkuu na kadhalika, hayo nayo yana utaratibu wake kama zilivyo, Kanuni zetu zina utaratibu wote. Namna ya kumwondoa Naibu Spika imo humu, namna ya kumwondoa Waziri Mkuu imo humu. Kwa hiyo na yenyewe Kanuni zake zifuatwe inavyopasa. Siwahoji hilo, maana tusije tukachanganyana hapa ikaenda message nytingine kabisa. Kwa hiyo, nitakachowahoji mimi ni mapendelekezo yaliyoletwa na Kamati zote tatu ambazo ripoti zake mmezipata, mmezipokea, mmezisoma.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki Mapendelekezo ya Kamati Tatu (*Oversight Committees*)  
yapelekwe Serikalini kwa hatua zilizopendekezwa)

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, mapendelekezo haya tunayapeleka Serikalini na ni matumaini yangu makubwa kwamba Serikali itayaangalia kipekee mambo haya, ikizingatia kwamba mjadala huu wa jana na leo kwa kweli umekuwa mjadala wa moto sana. Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya wananchi wameonyesha kwa uchungu mkubwa sana kutaka kuona

mabadiliko katika usimamizi na matumizi ya fedha za umma na tumeishauri Serikali yetu vizuri. Mimi naamini kabisa Serikali yetu imesikia na kama nilivyochangia kidogo kwa upande wa Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri zetu kuhusu namna ya upatikanaji wa wataalam wetu, kwa kweli ni jambo la kulitazama sana. (*Makofi*)

Wakati ule Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa Waziri wa TAMISEMI, ilikuwa nafasi za Wakurugenzi zinatangazwa si kama sasa. Yupo rafiki yangu mmoja, msomi mzuri tu, akawa ameomba kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Siku hizi utaratibu huo haupo tena. Basi wakawa wamekuja wengi tu hapa Dodoma kuja kufanya *interview*. Nikakutana naye hapa *Stand anazunguka*, nikamuuliza vipi ndugu yangu? Akasema aisee acha tu ndugu yangu. Nikamuuliza vipi kwani hukuja na gari? Akaniambia, kweli bwana, nimesahau nilipoli-park. Amechanganyikiwa, kwa nini amechanganyikiwa? Alikuwa kwenye *interview* ya Wakurugenzi wakati huo, amefika kwenye chumba kile, kwanza ile *interview* yenyewe imemchanganya, *graduate* mzima na kitambi chake na nini, lakini kubwa zaidi kukawa na *computer* na *laptops* ziko pale, wakapewa zoezi fulani, wakaambiya haya nendeni muandae chapuchapu dakika ishirini kila mmoja aje afanye *presentation* kwa *PowerPoint*. Sasa bwana mkubwa *computer* na yeye ni mbali kabisa. Wakati wenzake wanahangaika kule, yeye anasema ikabidi atafute *flipchart*, zunguka na kitambi chake kutafuta *flipchart* akaipata, akaanza kuandika na *marker pen*, haionekani. Akaandikaandika pale, ilipofika kwenye *presentation* akaenda kwenye ubao ule, kubandika yale ma-*flipchart* hata *pin* za kubandikia hazipo, mara *flipchart* inadondoka chini, jasho limemtoka. Anasema kwa kweli ule Ukurugenzi kwa vyovoyote vile yeye hatakuwepo. Kwa kweli majibu yaliviyotoka wala hakuwemo. Vinasaidia kidogo viji-process hivi, mtu mwiningine anaridhika kwamba nimeshiriki na sikufanikiwa.

Kwa hiyo, ni ushauri tu kwamba tuangalie namna ya kuwapata watu wetu wa Halmashauri, itatusaidia kabisa. Sisi tunaoshi nao huko na ninyi Wabunge wote ni Madiwani mnanielewa, ninachokizungumza na Kamati hasa ya LAAC mnaziona zile timu zinazokuja za Wakuu wetu wa Idara nchi nzima mnakutana nazo, kama mngekuwa mnafanya *assessment* ya wakuu wetu wa Idara mtaona jinsi ambavyo kwa kweli tunahitaji kuzimarisha kwa kiwango kikubwa lakini ndiyo kazi yetu kama Wabunge.

Nawashukuru tena kwa kushiriki kwa uchangamfu mkubwa na muda wetu unakaribia kwisha. Kesho tutaendelea na ratiba yetu ya kuzisikiliza zile Kamati ambazo ndiyo zimeweka ripoti zake Mezani ambazo ni Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini na tutawaomba wale watakaopenda kuchangia kuhusu Nishati na Madini wa-*indicate*

19 APRILI, 2012

mapema kwa Makatibu kusudi wapate nafasi hiyo kuchangia mwanzo kwa sababu wengi wa Wajumbe hao watasafiri kwenda Norway, wana mwaliko maalum, kwa hiyo, kabla hawajaondoka ni vizuri kuwa wameshasikia mambo mengi yanayohusu Kamati yao. Vilevile Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Miundombinu, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Hizo ndizo ambazo kesho zitapata nafasi ya kushughulikiwa.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa niahirishé shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.12 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 20 Aprili, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*